

**LUGHA KAMA RASILIMALI YA JAMII: UCHUNGUZI WA REDIO ZA FM
ZINAZOTUMIA KIBUKUSU KATIKA KAUNTI YA BUNGOMA**

**WASIKE DAVID MISIKO
(SASS/DPHIL/06/2009)**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI
YA SHAHADA YA UZAMIFU(PhD) KATIKA KISWAHILI KATIKA IDARA
YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA**

**CHUO KIKUU CHA MOI
ELDORET**

NOVEMBA, 2017

IKIRARI**IKIRARI YA MTAHINIWA**

Hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu chochote ili kutimiza mahitaji ya shahada yoyote. Sehemu yoyote ya tasnifu hii hairuhusiwi kutoleshwa bila kibali cha mwandishi na /au Chuo Kikuu cha Moi.

David Misiko Wasike.

SASS/DPHIL/06/2009

Sahihi..... Tarehe:.....

IKIRARI YA WASIMAMIZI

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa idhini na ridhaa yetu kama washauri na wasimamizi wa mzamifu walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Moi.

Prof. Nathan O. Ogechi,

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,

Chuo Kikuu Cha Moi,

Sahihi..... Tarehe:.....

Dkt. Mosol Kandagor,

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,

Chuo Kikuu cha Moi,

Sahihi..... Tarehe:.....

TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa wanangu Mercy, Mike, Eugene na Peter. Ninawapokezeni mwanga huu wa elimu ambao ni hazina kuu maishani mwenu. Kwa marehemu mamangu Julia Wasike, Mungu ailaze roho yako mahali pema peponi. Ulikuwa nguzo kuu katika maisha yangu. Ulinipa msingi thabiti kielimu, kidini na kimaisha kwa jumla.

IKISIRI

Matumizi ya lugha za kiasili yameshutumiwa na watu wengi kwa kukuza ukabila haswa nchini Kenya. Hata hivyo, lugha hizi zinaweza kuwa rasilimali kwa wazungumzaji zikitumiwa vyema. Utafiti huu ulilenga kuchunguza lugha za kiasili zinavyojitokeza kama rasilimali kwa wazungumzaji wake zinapotumika katika redio za FM. Aidha, utafiti ulinua kujadili jinsi matumizi ya lugha za kiasili katika redio za FM yanavyoweza jamii husika kupata habari zinazoweza kuboresha hali zao za maisha kwa njia mbalimbali. Uchunguzi ulidhamiria hususan: Kuhakiki yaliyomo katika vipindi vya jamii, uchumi, siasa na afya vinavyowasilishwa kwa kutumia Kibukusu katika redio za FM, zinazosikika katika kaunti ya Bungoma; Kutathmini Kibukusu kinavyojitokeza kama rasilimali kuangazia masuala ya jamii, uchumi, siasa na afya kwa wazungumzaji wake kinapotumika katika redio za FM, kisha kutambua changamoto za matumizi ya Kibukusu kama rasilimali kwa wakaazi wa Bungoma kupitia vituo vya redio za FM. Utafiti ulitumia mbinu za ustahilivu na kikiasi. Lahaja ya Kibukusu ilitafitiwa katika mazingira halisi ambapo lugha hiyo hutumika na wazungumzaji wake. Mikadha ya matumizi ya Kibukusu ilichunguzwa, hususan kama rasilimali kwa wazungumzaji wake. Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili; Sarufi Amilifu ya Halliday na ya Uanzilishi wa Ajenda iliyoasisiwa na McCombs na Show. Sarufi Amilifu ilihusishwa katika uchanganuzi wa vipindi vinavyopeperushwa kwa kutumia lugha za kiasili. Nadharia ya Uanzilishi wa Ajenda ilitumika kuhakiki uteuzi wa vipindi vinavyopeperushwa na vituo hivyo viwili vya redio. Uchunguzi ulifanywa katika vituo vya Sulwe na West FM vinavyopeperusha matangazo kwa Kibukusu katika kaunti ya Bungoma. Utafiti ulihusisha mhariri mmoja, watangazaji wawili na wataalamu wanne; mmoja kwa kila mojawapo ya masuala haya; jamii, uchumi, afya na siasa ambao hualikwa kwa kila mojawapo ya vituo hivyo. Vilevile, wasikilizaji 70 kutoka kila mojawapo ya vituo hivyo viwili vya redio walihusishwa. Kwa jumla, utafiti uliuhusisha watu 154. Wasikilizaji hao waliteuliwa kutoka kwa kaunti ndogo sita za kaunti ya Bungoma na walihusisha jinsia zote. Wasikilizaji waliteuliwa kwa kutumia usampulishaji kimakusudi ambao huwezesha idadi ya wahojiwa kuongezeka kadiri utafiti unavyoendelea. Vipindi vya redio vya vituo vyote viwili vilivyohusiana na masuala ya jamii, afya, uchumi na siasa vilisikilizwa. Mbinu ya ujazaji wa hojaji kwa watangazaji na wasikilizaji, usaili wa wahariri, watangazaji na wataalamu na kurekodi vipindi mahususi zilitumika. Vifaa vifuatavyo vilitumiwa kukusanya data: hojaji kwa wanahabari, hohaji kwa wasikilizaji, mwongozo wa usaili kwa wahariri, watangazaji na wataalamu na kinas sauti kunasia vipindi vilivyoteuliwa kisha vikachanganuliwa kwa kutumia nadharia ya Sarufi Amilifu. Data ifuatayo ilikusanywa: vipindi vya redio vinavyotumia lahaja ya Kibukusu, yaliyomo katika vipindi hivyo, Kibukusu kinavyojitokeza kama rasilimali kwa wazungumzaji wake na changamoto za matumizi ya lahaja hiyo katika redio za FM. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kutumia maudhui yaliyomo kisha matokeo yakawasilishwa kwa maelezo na takwimu. Matokeo ya utafiti huu yalikuwa yafuatayo: Matumizi ya lugha za kiasili katika redio za FM yalijaza pengo liliokuwepo katika upashaji habari kwa watu walioko mashinani; Matumizi ya lugha za kiasili katika redio za FM yaliwezesha wazungumzaji kufikia maamuzi faafu kuhusiana na masuala ya afya, siasa, uchumi na jamii; ukosefu wa taasisi ya kudhibiti uundaji wa istilahi ni mojawapo ya changamoto zinazokumba matumizi ya lugha za kiasili katika redio za FM. Matokeo ya utafiti huu yalitoa picha halisi ya mchango wa lugha za kiasili katika redio za FM nchini Kenya kwa maendeleo ya jamii husika. Matokeo ya uchunguzi huu yatakuwa mchango kwa tafiti ambazo zimefanywa kuhusu matumizi ya lugha za Kiafrika katika vyombo vya habari. Utafiti huu vilevile utawafaidi wapangaji lugha kitaifa na katika viwango vya kaunti. Utafiti huu pia unatarajiwa kutoa mchango kwa uhifadhi na makuzi ya lugha za Kiafrika kichanya. Utafiti unapendekeza yafuatayo: Kuundwa kwa taasisi za kutafiti, kuunda na kudhibiti istilahi zinazotumika katika lugha za kiasili; Vyuo vikuu kufundisha baadhi ya lugha hizi za kiasili ili kubadilisha mtazamo hasi kuzihusu; Serikali za kaunti kuanzisha sera za lugha katika viwango vya kaunti na hatimaye, kufufuliwa kwa ufundishaji wa lugha za kiasili mbali na Kiingereza, Kiswahili na lugha zingine za kigeni kama vile Kifaransa na Kijerumani katika sera ya lugha nchini Kenya.

ABSTRACT

Use of vernacular languages has been blamed by many people for promoting tribalism, especially in Kenya. However, these languages can be a great asset to speakers if properly used. This research sought to find out how use of vernacular languages in FM radio stations are an asset for development to speakers. The study specifically sought to: Evaluate the content in social, economic political and health programmes aired through Bukusu dialect on FM radio stations that are listened to in Bungoma County; assess how Bukusu dialect is an asset to its speakers in addressing social, economic, political and health issues and finally identify challenges experienced by Bukusu dialect speakers residing in Bungoma when the language is used on FM radio stations. Both qualitative and quantitative approaches were used to carry out the study. The research studied Bukusu dialect in its natural environment, where the dialect was used by its speakers. The study looked at the context of use of the dialect as an asset to its speakers. This research utilized two theories to analyze the data collected; Halliday's Functional Grammar Theory and McCombs and Snow's Agenda Setting Theory. The Functional Grammar theory was used in the analysis of programmes aired on FM stations using vernacular languages. The Agenda Setting theory was used to choose programmes aired on the two radio stations using vernacular languages. The research was conducted in two FM radio stations; Sulwe and West FM that air their programmes in Bungoma County. One editor, two broadcasters and four specialists from each of the radio stations, with one in each of the following fields were involved: social, economic, health and political. It also involved 70 listeners from each of the two radio stations. In total it involved 154 people. The listeners were sampled from 6 sub-counties and involved both gender. The listeners were sampled using snowball sampling method. The researcher listened to programmes from the two radio stations that addresses social, health, economic and political issues. The following tools were used to collect data: questionnaires for broadcasters, specialists in the fields who are normally invited to the radio stations and listeners. Interview schedules for editors, broadcasters and specialists who were invited to the radio stations. A recorder was used to record chosen programmes before analysing the data using Functional Grammar Theory. Data for the study was as follows: programmes that use Bukusu dialect, content of the programmes, how the dialect is an asset to users and challenges facing the use of Bukusu dialect when used on FM radio stations. Collected data was analysed by use of thematic analysis and presented in form of explanations and figures. The findings of this research were: Use of vernacular on FM stations filled the gap that was in existence on disseminating information to people at the grassroots; Use of vernacular language made the speakers make informed decisions on matters of health, politics, economic and social issues; Lack of an institute that controls creation of terminologies is one of the challenges facing use vernacular languages in FM radio stations. The findings of this research gave a clear picture of the role of vernacular languages on FM radio stations in Kenya and their role in development of the respective communities. The findings of this research will be a contribution to researches done on use of African Languages in media. The research could be useful to language planners, both nationally and at the county level. This research is also expected to contribute towards conservation and development of vernacular languages positively. The research recommends the following: Formation of institutes to do research, create and control terminologies used in vernacular languages; Universities to teach some of these vernacular languages so as to change their negative publicity; County governments to initiate language policies at the county level and revival of teaching of vernacular languages apart from English, Kiswahili and foreign languages such as French and German in the Kenyan language policy.

YALIYOMO

IKIRARI	i
TABARUKU	ii
IKISIRI	iii
ABSTRACT.....	iv
YALIYOMO.....	v
TAFSIRI YA MANENO	x
MAELEZO YA AKRONIMU.....	xi
SHUKURANI.....	xii
SURA YA KWANZA	1
MISINGI YA UTAFITI.....	1
1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Usuli wa Suala la Utafiti	1
1.2 Suala la Utafiti	7
1.3 Malengo ya Utafiti	9
1.4 Nadharia Tete za Utafiti.....	9
1.5 Upeo wa Utafiti.....	9
1.6 Umuhimu wa Utafiti	11
1.7 Hitimisho.....	12
SURA YA PILI.....	13
MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA KINADHARIA.....	13
2.0 Utangulizi.....	13
2.1 Mapitio ya Maandishi	13
2.1.1 Matumizi ya Lugha za Kiasili kwa Jumla.....	13
2.1.2 Sera ya Lugha Nchini Kenya	19
2.1.2.1 Tume ya Ominde (1964).....	20
2.1.2.2 Tume ya Gachathi (1974)	21
2.1.2.3 Ripoti ya Mackay (1981)	22
2.1.2.4 Tume ya Koech (1999)	23
2.1.3 Matumizi ya Lugha za Kiasili Nchini Kenya	25
2.1.4 Majukumu ya Vyombo vya Habari.....	26
2.1.5 Lugha za Kiasili katika Vyombo vya Habari.....	29
2.1.6 Hadhi ya Lugha za Kiasili.....	37
2.1.7 Lugha za Kiasili kama Rasilimali	41
2.2 Misingi ya Kinadharia.....	47

2.3 Hitimisho.....	52
SURA YA TATU	53
MBINU ZA UTAFITI	53
3.0 Utangulizi.....	53
3.1 Eneo la Utafiti.....	53
Ramani ya Kaunti Ndogo za Bungoma	54
3.2 Usampulishaji	57
3.3 Ukusanyaji wa Data	62
3.3.1 Usikilizaji Vipindi.....	63
3.3.2 Usaili	63
3.3.3 Ujazaji Hojaji.....	64
3.3.4 Kurekodi Vipindi	66
3.4 Vifaa vya Kukusanyia Data	66
3.4.1 Hojaji.....	66
3.4.2 Mwongozo wa Usaili	68
3.5 Utafiti Mwigo.....	69
3.6 Unukuzi wa Data.....	71
3.7 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data	71
3.8 Itikeli	72
3.9 Hitimisho.....	73
SURA YA NNE.....	74
KIBUKUSU KAMA RASILIMALI INAYOANGAZIA MASUALA YA JAMII NA UCHUMI	74
4.0 Utangulizi.....	74
4.1. Masuala Yanayoangaziwa katika Vipindi vya Jamii	74
4.1.1. Uwajibikaji.....	74
4.1.2 Maadili	79
4.1.3. Tamaduni za Wabukusu.....	85
4.1.4 Matukio ya Kaunti ya Bungoma	92
4.1.5 Kibukusu ni Rasilimali kupitia Taarifa za Masuala ya Jamii	97
4.2 Masuala Yanayoangaziwa katika Vipindi vya Uchumi.....	99
4.2.1 Uchumi wa Mtu Binafsi.....	99
4.2.2 Uchumi wa Kaunti ya Bungoma.....	106
4.2.3 Habari Kuhusu Uchumi wa Kaunti Jirani na Ule wa Kenya.....	111
4.3 Kibukusu kama Rasilimali Inayoangazia wa Masuala ya Uchumi.....	115

4.4 Hitimisho.....	117
SURA YA TANO	118
KIBUKUSU KAMA RASILIMALI INAYOANGAZIA MASUALA YA SIASA NA AFYA.....	118
5.0. Utangulizi.....	118
5.1. Masuala Yanayoangaziwa katika Vipindi vya Siasa	118
5.1.1. Vipindi vya Siasa za Kaunti ya Bungoma	118
5.1.2. Siasa za Kaunti za Kaunti Jirani na Zile za Kenya	125
5.2. Kibukusu kama Rasilimali Inayoangazia Masuala ya Siasa.....	130
5.3. Masuala Yanayoangaziwa katika Vipindi vya Afya.....	132
5.3.1. Masuala ya Afya kwa Wakaazi wa Kaunti ya Bungoma.....	132
5.3.2. Masuala ya Afya ya Wakaazi wa Kaunti Jirani	137
5.3.3 Masuala ya Afya ya Wakenya kwa Jumla	142
5.4 Kibukusu kama Rasilimali Inayoangazia Masuala ya Afya	145
5.5. Changamoto za Matumizi ya Lugha ya Kibukusu kama Rasilimali kwa Wakaazi wa Bungoma, Kupitia Vituo vya Redio za FM.	146
5.6. Hitimisho.....	153
SURA YA SITA	154
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	154
6.0 Utangulizi.....	154
6.1. Muhtasari wa Tasnifu	155
6.2 Matokeo ya Utafiti	155
6.2.1 Vipindi vya Jamii, Uchumi, Siasa na Afya Vinavyowasilishwa kwa Kutumia Kibukusu katika Sulwe na West FM.....	156
6.2.2 Kibukusu kama Rasilimali Inayoangazia Masuala ya Jamii, Uchumi, Siasa na Afya kwa Wazungumzji Wake katika Redio za FM.....	164
6.3 Mchango wa Utafiti	169
6.4 Mapendekezo ya Utafiti.....	170
6.5 Mapendekezo kuhusu Tafiti za Baadaye	172
MAREJELEO	173
VIAMBATISHO.....	180
KIAMBATISHO I: Hojaji kwa Wasikilizaji	180
KIAMBATISHO II: Hojaji kwa Watangazaji	186
KIAMBATISHO III: Mwongozo wa Usaili kwa Mhariri	190
KIAMBATISHO IV: Mwongozo wa Usaili kwa Mtangazaji	192

KIAMBATISHO V: Mwongozo wa Usaili kwa Magalacha.....	193
KIAMBATISHO VI:Baadhi ya Data Iliyochanganuliwa.....	194
KIAMBATISHO VII: Idhini ya Kufanya Utafiti	197

UFAFANUZI WA ISTILAHU

Data ghafi	Data ambayo haijachanganuliwa
Lugha asili/kiasili	Lugha ya mama au lugha ya kwanza. Katika tasnifu hii, imetumika kwa kubadilishana na lugha ya wenyeji.
Lugha ya wenyeji	Lugha ya asili inayozungumzwa na wakaazi wa asili wa eneo fulani.
Lugha ya kwanza	Lugha ambayo alilelewa na kukua nayo msemaji ambaye anajua na kutumia lugha mbili au zaidi.
Lugha ya jamii	Katika tasnifu hii, imetumika kama lugha asili.
Magalacha	Wataalamu katika nyanja mbalimbali.
Masuala	Mambo yanayojadiliwa na kutolewa maamuzi.
Nasuri	Ni shimo linalotokana na kujeruhiwa ambalo si la kawaida na hutokea kwa mwanamke aliyepata shida wakati wa kujifungua na huwa linapitisha mkojo na kinyesi kwa pamoja
Ngariba	Ni mtu ambaye hupasha vijana wa kiume tohara katika jamii za Kiafrika.
Rasilimali	Jumla ya mali aliyo nayo mtu au nchi
Redio ya jamii	Kituo cha redio kinachojikita katika kuangazia masuala ya jamii hiyo na huwa hakina lengo la kupata faida.

TAFSIRI YA MANENO**KIINGEREZA****Agenda Setting Theory****Fistula****Functional Grammar Theory****Media Council of Kenya****National Council of Science and Technology****Qualitative Method****Quantitative Method****Vernacular languages****KISWAHILI**

Nadharia ya Uteuzi wa Ajenda

Nasuri

Nadharia ya Sarufi Amilifu

Baraza la Habari nchini Kenya

Baraza la Kitaifa la Sayansi na
Teknolojia

Mbinu ya Kiustahimilifu.

Mbinu ya Kikiasi

Lugha za Kiasili

MAELEZO YA AKRONIMU

BAT	British American Tobacco
IEBC	Independent Electoral and Boundaries Commission
KNBS	Kenya National Bureau of Statistics
MCK	Media Council of Kenya
Mh	Mhariri
RMS	Royal Media Services
ROK	Republic of Kenya
TUKI	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
Wh	Wahariri

SHUKURANI

Kazi hii haiengeweza kukamilika na kuwasilishwa katika hali iliyomo bila ya msaada kutoka watu mbalimbali. Shukrani zangu za dhata zawaendea wote waliohusika kuwezesha kazi hii kukamilika. Kwanza namshukuru Maulana kwa kinipa siha njema, nguvu, amani na kuniletea wasaidizi walionifaa nilipokuwa nimetamauka. Nawashukuru vilevile wasimamizi wangu Prof. Nathan Ogechi na Dkt. Mark Kandagor kwa kunielekeza kuikamilisha kazi hii. Laiti isingekuwa uvumilivu wao na kujitolea kwao kuzisoma kazi zangu, nisingeikamilisha kazi hii.

Ningependa vilevile kuwashukuru wahadhiri wengine katika Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Moi. Sitasahau kuwashukuru wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Kibabii katika Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika hususan Prof. Isaac Ipara na Mkuu wa Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika ndugu Eric Wamalwa. Aidha, nawashukuru wazamifu wenzangu Dkt. Eucabeth On'gau, ndugu Charlse Wasike na Bi. Harriet Ibala. Tuliweza kufaana hususan mawimbi ya safari hii yalipokuwa mazito.

Ningependa vilevile kuishukuru familia yangu. Mke wangu Dkt. Julia Situma Misiko, ulinifaa sana kwa hali na mali. Kila uliponikumbusha kuikamilisha kazi hii nilipata mhemko wa kuikamilisha. Kwa wanangu Mercy, Mike, Eugene na Peter nawashukuru kwa kuwa wavumilivu wakati ambapo niliwatenga kwa lengo la kuikamilisha kazi hii. Kwa babangu mzazi Peter Wasike na marehemu mamangu Julia Wasike, shukrani zangu za dhata kwa kuthamini masomo na kuniwekea msingi bora. Hatimaye, nawashukuru ndugu zangu Mary, marehemu Getrude, Grace, marehemu Betty, Ken na John kwa mapenzi yenu na kunipa matumaini mawimbi ya safari hii yalipokuwa mazito. Mungu awape nyote baraka zisizo kifani.

SURA YA KWANZA

MISINGI YA UTAFITI

1.0 Utangulizi

Katika sura hii nimebainisha misingi ya utafiti ambapo nimeangazia vipengele vifuatavyo: usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti na malengo ya utafiti huu. Aidha, nimeorodhesha nadharia tete zilizoongoza utafiti huu, upeo wake na umuhimu wa utafiti.

1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Lugha za kiasili katika mataifa mengi barani Afrika zimepuuzwa huku lugha za kigeni zikitukuzwa (Ongarora, 2002). Ithibati ya hali hiyo ya kusikitisha hujitokeza bayana kupitia kwa sera za lugha zilizoibuka mwongo wa baada ya ukoloni (Prah, 2005). Sera hizi zilitukuza lugha za kigeni huku zikipuuzwa lugha za Kiafrika.

Hata hivyo, mataifa ya Afrika yanahitaji kuchukulia kwa umakini zaidi changamoto za kukuza lugha zao za Kiafrika na kuziinua hadi kiwango cha kuwa lugha za sayansi na uvumbuzi wa kiteknolojia (Mugambi, 2007). Hali hii hutokana na kuwepo haja ya kutumia ama lugha inayowawezesha au zinazowawezesha kuelewa na kufanya maamuzi yanayohusiana na afya, kilimo, elimu yao, uraia, maslahi yao kiuchumi na pia mambo yanayohusiana na vipengele vingine vya kijamii.

Ingawa mataifa mengi ya Afrika hutukuza zaidi lugha za kigeni, hasa kupitia mifumo ya elimu, ni vigumu kwa watu kuwa wabunifu katika lugha inayowatatiza wanapojieleza (Prah, 1998, akinukuliwa na Muthwii, 2002). Maoni haya yanaoana na ya Wolff (2006). Wolff (2006) anadahili kwamba ithibati zote kutoka Afrika zinaonyesha kwamba matumizi ya lugha za kigeni yamekosesha kufikiwa kwa

malengo ya kufundisha lugha hizo. Inasemekana walimu na wanafunzi hawafikii viwango vinavyokubalika vya umilisi wa lugha hizo za kigeni zinazofundishwa.

Wolff (2006) anazidi kusema kwamba, kusoma lugha rasmi za wenyeji katika kiwango cha shule za msingi, licha ya kuboresha umilisi katika lugha za kiasili, hukuza stadi za ueledi, ufahamu na ubunifu na kuwezesha wanaokamilisha masomo ya shule za msingi kuhusika zaidi katika masuala ya kimaeneo na kitaifa na kuwasiliana na taifa kupitia matumizi ya lingua franka moja au mbili. Hivyo basi, lugha za kiasili ni muhimu kwa mawasiliano hasa mashinani. Kwa wale walio mashinani, lugha za kiasili zinaweza kutumika kuwawezesha kujieleza kikamilifu na kutatua mambo mengi wanayokumbana nayo katika shughuli za kila siku.

Bara la Afrika limekuwa likijitahidi kuinua kiwango chake cha maendeleo. Hata hivyo, maendeleo ya Afrika na juhudi zake zinazolenga kufikia ufanisi yanategemea matumizi ya lugha za kiasili hasa iwapo juhudi hizo zinawalenga wakaazi wa mashambani (Prah, 2008). Ingawa maendeleo haya yanategemea matumizi ya lugha za kiasili, kuna wale wanaopinga matumizi ya lugha hizo. Watu hawa wanadai kwamba wasikilizaji wa lugha za kiasili ni wachache. Kwa mfano, Wole Soyinka akiwa kati ya wanaopinga matumizi ya lugha za kiasili, anamshutumu mwandishi Ngugi wa Thiongo kwa kuandika vitabu vyake kwa lugha ya Kikikuyu. Kwa mujibu wa Wole Soyinka, hali hiyo inapunguza idadi ya wasomaji ambao huenda wasielewe lugha hizo za kiasili (Ongarora, 2002).

Mitazamo hasi kama hiyo ya Wole Soyinka ni ya kusikitisha kwani, maendeleo katika uandishi wa habari, uchapishaji, utalii na kadhalika yatapanuka zaidi ikiwa lugha za Kiafrika na tamaduni zitapewa nafasi kukua na kuchangia maendeleo (Muthwii, 2002). Maendeleo hayo yatafikiwa, iwapo lugha za kiasili zitatumika zaidi si tu katika

uandishi bali pia katika vyombo vya habari. Kutokana na matumizi ya lugha za kiasili katika vyombo vya habari, idadi kubwa zaidi ya walengwa wa habari zinazohusiana na jamii husika zitaweza kufikiwa. Hivyo basi, habari zinazowasilishwa kupitia kwa vyombo vya habari zitakuwa za manufaa zaidi hususan kwa wananchi walioko mashinani iwapo lugha za Kiafrika zitatumika.

Hapa nchini Kenya, redio imetumika kama kifaa cha kushughulikia mahitaji ya watu mbalimbali kama vile upashaji habari na burudani. Kwa miaka mingi, mbinu zinazolenga mawasiliano zimetumika kama njia ya kushughulikia masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi (Gathigi, 2009). Kuhusu masuala ya kijamii, redio inadaiwa kuleta ukruha mkubwa miongoni mwa wasikilizaji. Redio imewaleta pamoja wasikilizaji kupitia vipindi kama vile vya kutumiana salamu redioni.

Lugha ya matumizi katika redio ni mojawapo ya sababu kuu za uteuzi wa vituo vya redio ambavyo wasikilizaji husikiliza (Gathigi, 2009). Wakati uo huo, uteuzi wa usikilizaji wa redio za lugha za kiasili hutokana na ufahamu wa yaliyomo. Kwa hivyo, mada inayoshughulikiwa katika kipindi cha redio huenda itachangia katika maamuzi ya usikilizaji wa kituo hicho. Wakati uo huo, kuibuka kwa vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili huenda kumewapa wazee nafasi ya kusikiliza redio kwa mara ya kwanza bila kuhitaji usaidizi wa wakalimani. Hali hiyo ya usikilizaji inatokana na matumizi ya lugha wanazozielewa moja kwa moja (lugha za kiasili).

Vituo vya redio vya lugha za kiasili huvutia wasikilizaji wengi wa mashambani, kwa sababu lugha za kiasili huzungumzwa na watu wengi katika maeneo hayo ya mashambani (Gathigi, 2009). Kwa hivyo, utangazaji kwa kutumia lugha za kiasili ni muhimu sana, hasa inapozingatiwa kwamba idadi kubwa ya wasikilizaji ni watu walioko mashambani na ambao hawawezi kupuuzwa, hususan katika nchi

zinazoendelea kama vile Kenya. Vilevile, kuna wasikilizaji wa mijini, ambao husikiliza vituo vya lugha za kiasili, ingawa inadaiwa ni hadhira iyo hiyo (ya wasikilizaji kwa jumla wa lugha za kiasili), ambayo vituo vikuu vya redio visivyotumia lugha za kiasili hulenga kushughulikia (Gathigi, 2009).

Ili kupanua zaidi matumizi ya lugha za kiasili katika vyombo vya habari, pana haja ya kutafitia matumizi ya lugha za kiasili katika vyombo vya habari na mchango vinaoutoa katika kuifahamisha jamii husika kuhusu masuala ya jamii. Masuala haya ni kama vile: siasa, jamii, afya, na uchumi. Anavyohoji Miguda–Atyang (2002), lugha za kiasili hutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya jamii husika kwa kuwezesha wazungumzaji wake kuelewa masuala yahusianayo na maendeleo vizuri zaidi.

Nchini Kenya, nafasi kwa wakaazi wa mashambani ya kujieleza na kutatua matatizo yao imeongezwa na vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili. Hali hiyo inatokana na umilisi zaidi walio nao katika lugha zao za kwanza ikilinganishwa na Kiswahili na Kiingereza; lugha ambazo zimekuwa zikitumika zaidi katika redio (Prah, 1998 akinukuliwa na Muthwii, 2002).

Wakati uo huo, teknolojia mpya ya mawasiliano imeweza kuhusishwa katika vyombo vya habari mathalan, matumizi ya simu ambapo watangazaji na wasikilizaji huwasiliana moja kwa moja hususan kujadili masuala ibuka katika jamii kupitia upigaji wa simu na kwa kutumia jumbe fupi. Kupitia teknolojia hii, utangazaji na ubadilishanaji mawazo baina ya watangazaji na wasikilizaji umeweza kuboreshwa. Ongezeko la matumizi ya simu mashambani limesababisha watangazaji na wasikilizaji kutumia simu za mkono kuanzisha na kuendeleza mazungumzo kwenye redio. Hali hiyo vilevile imewezesha wasikilizaji kutoa maoni yao kuhusu ubora na uwasilishaji wa vipindi kwa watangazaji (Gathigi, 2009).

Aidha, Kamau (2011), anadahili kwamba vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili ni njia bora zaidi ya upashaji habari mashinani huku akiziita “rafiki” atoaye habari wanazotumia kufikia maamuzi kuhusu masuala mbalimbali. Kupitia kwa mijadala ya redioni, masuala ya kijamii na kisiasa vilevile yameweza kujadiliwa huku wananchi wakitoa maoni na misimamo yao. Swali la kujiuliza hapa ni, je lugha za kiasili huweza kuwasilisha masuala hayo kikamilifu? Je, lugha hizi zinajitosheleza, hivi kwamba wasikilizaji wake huweza kufikiwa na habari tondoti, masuala yoyote yanayohusiana na jamii husika yanapoangaziwa?

Lugha za kiasili pia zimeshutumiwa kwa kusababisha mgongano miongoni mwa Wakenya na hata kusababisha maafa (Orao, 2009; Mbeke & Mshindi, 2008; Kriegler, 2008). Inasemekana machafuko yaliyoshuhudiwa nchini Kenya baada ya uchaguzi wa 2007 yalitokana na matumizi ya lugha za kiasili hasa katika vyombo vya habari. Inadaiwa kwamba vyombo hivyo vilitumika visivyo na wanasiasa ili kuchochea makabila kuangamizana kwa misingi ya kikabila.

Ingawa nchini Kenya matumizi ya lugha za kiasili yameshutumiwa hasa katika vyombo vya habari kwa kuchochea vita vya kikabila (Mbeke & Mshindi, 2008; Kriegler, 2008; Orao, 2009), wasomi wa isimu jamii barani Afrika wana mtazamo mpya kuzihusu. Wanaisimu jamii kwa sasa huangalia wazungumzaji na watumiaji wa lugha hizi wanavyozitumia au kutozitumia lugha hizo kama malighafi ya maisha yao ya kila siku (Wolff, 2006).

Kwa upande mwingine, mataifa mengi ya mashariki yaliyostawi kiviwanda na kiuchumi kama vile Japan, Hong Kong na Korea yamepiga hatua kimaendeleo kwa kutumia lugha zao za kiasili (Mudhune, 2002). Hali hii inatuacha kwa njia panda na

kutufanya tujiulize maswali yafuatayo: Je, tushutumu matumizi ya lugha za kiasili kwa jumla au matumizi yake mabaya?

Nchini Kenya, katiba mpya (ROK, 2010) imewapa Wakenya matumaini ya kubadilisha hali iliyokuwa ikipuuza lugha za kiasili na kuleta sera madhubuti kuhusiana na matumizi ya lugha hizo. Katiba mpya ya nchi ya Kenya imeangazia umuhimu wa lugha za kiasili kwa kusema:

Jamhuri; (a) itakuza na kulinda wingi lugha wa watu wa Kenya na (b) kukuza maendeleo na matumizi ya lugha za kiasili. (uk.15).

Katiba ya Kenya (ROK, 2010) vilevile inapendekeza, ugatuzi wa mamlaka na kufikiwa kwa huduma mbalimbali kwa viwango nafuu katika maeneo yote ya jamhuri. Ili kuweza kufikia hayo, pana haja ya matumizi ya lugha inayoeleweka mashinani (Prah, 2008). Anavyodahili Mutahi (2006), matumizi ya lugha zote za Kenya katika maendeleo yamesababisha kuhusika kikamiifu kwa Wakenya katika shughuli za taifa.

Matokeo ya utafiti wa Kamau (2011), Gathigi (2009) na tafiti zingine zinazohimiza matumizi ya lugha za kiasili kwa upande mmoja na madhara yanayosababishwa na vituo vya lugha za kiasili yanayodaiwa na Orao (2009), Mbeke & Mshindi (2008) na Kriegler (2008 kwa upande mwingine yanatuacha katika hali ya mtanziko. Ni bayana kwamba ingawa matumizi ya lugha za kiasili yanapongezwa kwa upande mmoja, yanashutumiwa kwa upande mwingine. Kwa hivyo, suluhu kwa hali hiyo ni ipi? Je, matumizi ya lugha za kiasili katika vituo vinavyozitumia yaharamishwe, kumaanisha kuharamisha lugha hizo kwa jumla au matumizi yaruhusiwe lakini vituo vidhibitiwe? Je, watumiaji wote wa lugha za kiasili washutumiwe au wanaozitumia kwa nia mbaya ndio wanaostahili hizo shutuma? Na je, matumizi yakiharamishwa kuna faida gani au

hasara gani hasa ikizingatiwa kwamba katiba ya Kenya (ROK, 2010) inahimiza kukuzwa kwa lugha zote za kiasili? Je, turuhusu matumizi yake lakini kwa kudhibiti uchochezi?

Kwa mujibu wa Wolff (2006), tafiti za wanaisimu zinafaa kuangazia kile lugha hizi zinafaa kufanyia wazungumzaji wake. Hivyo basi, tunajiuliza je, lahaja ya Kibukusu imewafanyia nini wazungumzaji wake hasa tunaporejelea masuala ya kijamii, kiafya, kiuchumi na kisiasa? Je, lahaja hii imewawezesha kwa njia yoyote wazungumzaji na wasikilizaji wake kupata fahamu zaidi kuhusu masuala ya jamii, afya, uchumi na siasa hasa kupitia kwa redio maadamu ni mojawapo ya njia za kufikia watu wengi kwa haraka (Mohochi, 2007)?

Wakati uo huo, hata kama tafiti nyingi zimefanywa kuhusiana na lugha za kiasili zikiwemo tafiti kuhusu manufaa ya lugha hizo, ni chache ambazo zimefanywa kuhusu matumizi ya lugha hizo katika redio za FM. Nyingi za tafiti hizi zimeangazia lugha za kiasili zinavyotumika kwa jumla. Utafiti wa hivi karibuni miongoni mwa tafiti katika redio za FM ni ule wa Okoth (2015). Mtafiti huyu alichunguza kuhusu makuzi ya lugha za kiasili katika redio ya Ramogi FM. Maswali ambayo yamejitokeza hapo juu na tafiti za hivi karibuni kuhusu matumizi ya lugha za kiasili katika vyombo vya habari kama ule wa Okoth (2015) yalituelekeza kwa suala la utafiti.

1.2 Suala la Utafiti

Lugha za kiasili zimeshutumiwa kwa kusababisha mgongano miongoni mwa Wakenya na hata kusababisha maafa. Wakati uo huo, lugha hizi zimepongezwa kwa kuwawezesha wazungumzaji wake kupata habari ambazo zimewawezesha kujistawisha. Wasomi wa isimu jamii barani Afrika wana mtazamo mpya kuzihusu lugha za kiasili. Wanaisimu jamii kwa sasa huangalia wazungumzaji na watumiaji wa

lugha hizi wanavyozitumia au kutozitumia lugha hizo kama malighafi ya maisha yao ya kila siku. Ingawa kuna tafiti nyingi ambazo zimefanyiwa lugha ya Kibukusu, hakuna utafiti ambao umelenga kuhakiki matumizi ya lugha hiyo katika redio za FM na jinsi matumizi hayo yamewafaidi wasikilizaji wake wanaoishi katika kaunti ya Bungoma. Hivyo basi, pana haja ya utafiti kufanywa ili kuchunguza yale ambayo Kibukusu kimewafanyia wazungumzaji wake kinapotumika katika redio.

Wakati uo huo, katiba ya Kenya iliyoidhinishwa mwaka wa 2010 inahimiza makuzi ya lugha za kiasili. Vyombo vya habari vimechangia pakubwa katika kukuza matumizi ya lugha hizi za kiasili. Mchango huo umeweza kushuhudiwa na ongezeko la matumizi ya lugha za kiasili hususan katika redio za FM, ambapo kufikia 2014, kulikuwa na vituo 54 vilivyotumia lugha za kiasili 19 katika kutoa matangazo yake. Mtafiti alikisia kwamba ongezeko hilo linatokana na lugha hizi kuwawezesha wazungumzaji wake kuelewa zaidi masuala wanayokumbana nayo kila siku. Mtafiti alikisia kwamba matumizi ya Kibukusu katika redio za FM katika uangaziaji wa masuala ya jamii, uchumi, afya na siasa yamewapa uwezo na ueledi zaidi wazungumzaji wake. Uwezo huo umewapa nafasi nzuri wazungumzaji wa lugha hiyo, kuelewa zaidi masuala hayo na kutoa michango ambayo imesaidia kuboresha hali ya maisha ya wakaazi wa kaunti ya Bungoma. Ni kwa misingi hii ambapo utafiti huu umefanywa ili kuchunguza matumizi ya lugha hii katika redio za FM yanavyojitokeza kama rasilimali kwa wazungumzaji wake na kutambua changamoto zinazoikumba katika matumizi hayo.

1.3 Malengo ya Utafiti

Katika utafiti huu, tulilenga kuchunguza Kibukusu kinavyotumika kama rasilimali kwa jamii inayokizungumza kupitia kwa redio za FM zinazosikika katika kaunti ya Bungoma. Tulidhamiria hususan:

1. Kuhakiki yaliyomo katika vipindi kuhusu masuala ya jamii, uchumi, siasa na afya vinavyowasilishwa katika redio za FM.
2. Kutathmini Kibukusu kinavyojitokeza kama rasilimali katika kuangazia masuala ya jamii, uchumi, siasa na afya kwa wazungumzaji wake kinapotumika katika redio za FM.
3. Kupambanua changamoto za matumizi ya Kibukusu kama rasilimali kwa wakaazi wa Bungoma.

1.4 Nadharia Tete za Utafiti

Katika utafiti huu, tuliongozwa na nadharia tete zifuatazo:

1. Mambo mengi huangaziwa katika vipindi vya masuala ya jamii, uchumi, siasa na afya vinavyowasilishwa katika redio za FM, kwa kutumia Kibukusu.
2. Matumizi ya Kibukusu katika redio za FM yana manufaa mengi kwa wazungumzaji wake kupitia masuala ya jamii, uchumi, siasa na afya.
3. Kuna changamoto zinazokumba matumizi ya Kibukusu katika redio za FM.

1.5 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika vituo vya redio vya Sulwe na West FM vinavyopeperusha matangazo katika kaunti ya Bungoma. Redio ya Sulwe FM huwafikia wasikilizaji kupitia masafa ya 89.6. huku West FM ikiwafikia wasikilizaji kwa masafa ya 96.7. Uteuzi wa vituo hivyo viwili ulitokana na vituo hivyo kuwepo kwa zaidi ya miaka mitano vikipeperusha matangazo kwa kutumia Kibukusu. Kituo

cha West FM hutumia Kiswahili na baadhi ya lugha za kiasili zinazozungumzwa katika kaunti ya Bungoma kama vile Kiteso, Kisabaoti na Kibukusu huku Sulwe FM ikitumia lahaja ya Kibukusu pekee. Mtafiti vilevile aliviteua vituo hivyo kwa sababu, kati ya lugha vinazotumia vituo hivyo viwili ni Kibukusu, lahaja anayozungumza mtafiti. Kwa hivyo, hali hiyo ilipunguza dhiki za kumtafuta mkalimani kwa kusudi la kumfanyia ukalimani wa data aliyokusanya. Anavyohoji Crowley (2007), umilisi wa mtafiti katika lugha ya watafitiwa ni mojawapo ya vigezo muhimu vya uteuzi wa eneo la utafiti.

Mtafiti aliteua lahaja ya Kibukusu ambayo ni mojawapo ya lahaja 17 za Kiluyia (Were, 2014). Ni lahaja ambayo hususan huzungumzwa na wakazi wengi wa kaunti ya Bungoma na baadhi ya wakaazi wa kaunti ya Trans Nzoia. Katika Sulwe FM, vipindi vilisikilizwa kuanzia asubuhi; tangu saa kumi na mbili za asubuhi hadi saa tano za usiku kwa miezi miwili ingawa niliteua tu vile vilivyoangazia masuala ya jamii, afya, uchumi na siasa. Sababu za kuteua vipindi kuanzia saa kumi na mbili za asubuhi ni kwa vile vipindi kabla wakati huo huwa vya burudani tu na salamu. Iitarajiwa kwamba miezi miwili ingetosha kubainisha na kurekodi vipindi ambavyo vingewezesha kupata data aliyolenga kupata mtafiti. Kwa mujibu wa Onyebadi (2008), utafiti wa aina hii; uliotumia nadharia ya Uteuzi wa Ajenda, muda wa mwezi mmoja ulitosha kukusanya na kuchanganua data.

Kwa upande mwingine, West FM ilisikilizwa usiku tu kati ya saa tatu hadi saa tano za usiku kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa kwa miezi miwili kwani vipindi vyake katika lahaja ya Kibukusu huwasilishwa tu usiku katika hizo siku za juma. Siku za Jumamosi na Jumapili vipindi vya West FM vilisikilizwa wakati wa aduhuri kwa majuma manane kuanzia saa nane hadi saa kumi kwani ndizo saa ambapo vipindi

huwasilishwa kwa Kibukusu. Iitarajiwa kwamba, kufikia mwisho wa majuma hayo manane, data ambayo ingewezesha kufikia uamuzi jarabati ingekuwa imepatikana. Uteuzi wa muda huo ulitokana na tafiti zingine za awali zinazohusisha nadharia ya Uteuzi wa Ajenda. Kwa mujibu wa Onyebadi (2008) akinukuu tafiti zingine zilizoongozwa na nadharia ya Uteuzi wa Ajenda zilizofanywa na wasomi kama vile, McCombs, Llamas, Lopez-Escobar na Rey, muda wa mwezi mmoja ulitosha kutafiti kwa kutumia nadharia hiyo. Hata hivyo, utafiti huu ulitumia miezi miwili ukiongozwa na nadharia hiyo pamoja na ile ya Sarufi Amilifu.

Wanahabari waliohusishwa ni: wahariri na watangazaji wa vipindi ambao hutangaza kwa kutumia lahaja ya Kibukusu kutoka vituo vya redio vya Sulwe na West F.M. Pia wasikilizaji wa vituo hivyo viwili vya redio walihusishwa. Wasikilizaji waliohusishwa walikuwa wenyeji wa kaunti ya Bungoma. Wasikilizaji waliolengwa ni wanaosikiliza vipindi vya Kibukusu, vya West na Sulwe FM. Mtafiti aliwaomba watangazaji kumwelekeza kwa wasikilizaji kwa kumjulisha kwao hususan wale ambao huhusishwa katika vipindi kupitia upigaji simu kwa vituo vya redio. Mtafiti aliteua kaunti ya Bungoma kwa sababu inahudumiwa na vituo vyote viwili vya redio (Sulwe na West FM).

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unatarajiwa kuwa na manufaa yafuatayo:

1. Kutoa taswira ya nafasi ya lugha za kiasili kama rasilimali kwa watumiaji wake.
2. Kuchangia uhifadhi na makuzi ya lugha za kiasili kichanya.
3. Utakuwa mchango kwa tafiti za isimu jamii zilizofanywa kuhusu matumizi ya lugha za Kiafrika katika vyombo vya habari.

4. Umependekeza suluhisho kwa changamoto zinazokabili matumizi ya lugha za kiasili katika redio za FM.
5. Utatoa mapendekezo kwa wapangaji sera za lugha katika kaunti ya Bungoma na Kenya kwa jumla kuhusu kukuza lugha za kiasili na wakati uo huo kupeleka maendeleo mashinani.
6. Kutoa taswira kamili ya majukumu yanayotekelezwa na lugha za kiasili nchini Kenya hususan kwa wazungumzaji wake kupitia vyombo vya habari hususan redio.

1.7 Hitimisho

Katika sura hii tumetoa msingi kwa utafiti huu kwa kuangazia masuala mbalimbali. Miongoni mwa yale ambayo yamezungumziwa katika sehemu hii ni usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti na azma ya utafiti. Vilevile, tumeorodhesha nadharia tete zilizoongoza utafiti huu, tukatoa upeo wake na hatimaye kuangazia umuhimu wa utafiti. Kwenye sura inayofuata tunaangazia mapitio ya maandishi na misingi ya kinadharia ambapo nadharia zilizoongoza utafiti huu zimezungumziwa kwa kina.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA KINADHARIA

2.0 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia tumeshughulikia usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti na malengo ya utafiti. Vilevile tumeorodhesha nadharia tete zilizoongoza utafiti huu na tukaweka upeo na kuorodhesha umuhimu wa utafiti huu. Katika sura hii, tunaangazia yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti na hatimaye tutazungumzia nadharia zilizoongoza utafiti.

2.1 Mapitio ya Maandishi

Sehemu hii inaangazia mapitio mbalimbali kuhusu mada ya utafiti. Imeshughulikia maandishi hayo chini ya mada zifuatazo: Matumizi ya lugha za kiasili kwa jumla, sera ya lugha nchini Kenya na matumizi ya lugha za kiasili nchini Kenya. Vilevile, imeshughulikia majukumu ya vyombo vya habari na lugha za kiasili katika vyombo vya habari. Hatimaye, sehemu hii imepitia hadhi ya lugha za kiasili kama rasilimali kwa wazungumzaji.

2.1.1 Matumizi ya Lugha za Kiasili kwa Jumla

Tuko katika ulimwengu ambao urasimishaji na utambuzi wa lugha za kiasili na tamaduni umekuwa kaida. Shauku mpya katika lugha hizi lazima ijitokeze kupitia kujitolea bayana katika kampeni kuzifunza na kutoa kazi za kifasihi kwa kuzitumia (Chabata, 2001). Msomi huyu anahoji, kupigiwa chuku tofauti zilizopo kati ya makabila ya Kiafrika kumechangia pakubwa katika kutenganisha makabila hayo badala ya kuyaunganisha. Hali hiyo inabainika, hata katika vituo vya redio za kiasili. Vituo hivi vimeshutumiwa kwa kueneza chuki miongoni mwa Wakenya mwaka 2007 (Kriegler, 2008, Mbeke & Mshindi, 2008 na Orao, 2009).

Chabata (2001) anadahili kwamba, vita miongoni mwa jamii huweza kutokea hata miongoni mwa makabila yaliyo na asili na historia moja. Anahoji, migawanyiko miongoni mwa jamii zetu iliyoanzishwa enzi ya Wakoloni imewafanya watu wajitambulisha na makundi ya kikabila na kufanya ushirika kati ya makabila hayo ukosekane. Migawanyiko hii vilevile imezifanya juhudi za wanaojitahidi kuunganisha jamii mbalimbali ziwe ngumu. Swali hapa ni je, mikakati gani inayoweza kutekelezwa ili lugha nyingi za kikabila ziwe nguvu za umoja badala ya udhaifu? Iwapo zitakuwa na nguvu za umoja, zitakuwa rasilimali badala ya kuwa kikwazo kwa jamii husika. Wakati uo huo tunajiuliza, ni mikakati gani inayoweza kuwekwa ili kutatua changamoto ya lugha za kiasili kuwa rasilimali ya jamii? Utafiti huu umejibu baadhi ya maswali hayo.

Khamisi (2008:1) anasema kwamba, fikra za ukuzaji wa lugha za Kiafrika zimetawaliwa sana na maendeleo ya kisiasa na kiuchumi ya nchi zetu za Afrika. Anasema:

...ni jambo la miujiza na kinyume cha taratibu kupata sera ya ukuzaji wa lugha inatofautiana na kuachana na hatua ya uchumi iliyopo.

Hii inamaanisha kwamba ili lugha za Kiafrika zikubalike kama “zilizoendelea”, zinafaa kuwa na uwezo wa kuwasilisha masuala ya kisiasa na kiuchumi. Maoni ya msomi huyu yanadhihirisha kupuuzwa kwa maendeleo ya lugha za kiasili. Mapuuza hayo yapo licha ya kwamba nchi nyingi za Kiafrika zinajivunia maendeleo, hasa baada ya kujinyakulia uhuru. Kama lugha hizi zitapewa nafasi ya kukua, hususan kupitia vyombo vya habari, zitaweza kuwa rasilimali kuu ya maendeleo ya jamii zinazozitumia.

Hali ya matumizi ya lugha za kiasili kwa mapana itawezekana tu iwapo lugha hizo zitapewa majukumu fulani katika jamii na majukumu hayo yalindwe ili kutoa haki kwa wazungumzaji kuzitumia kama wapendavyo (Msanjila, 2002). Mojawapo ya njia za utekelezaji wa haki hizi ni ufunguzi wa vituo vya redio vya lugha za kiasili kama tunavyoshuhudia sasa. Hata hivyo, ili lugha hizo ziwe na manufaa zinapotumika katika vyombo hivyo, zinafaa zitumike kwa uangalifu ili zisiwe vyombo vya kutenganisha jamii. Wakati uo huo nchini Kenya, lugha za kiasili zimepewa majukumu ya kufundishia katika madarasa ya chini katika shule za msingi sehemu za mashambani. Hata hivyo, katika hali halisi, sera hiyo haitekelezwi.

Shitemi (2002), anahoji, wingilugha na hali mbaya ya tafiti katika lugha za Kiafrika imeathiri sana maendeleo ya kitaifa kwa mtazamo wa kilugha. Tathmini ya uanuwai wa lugha imepigwa chuku kupitia kupuuzwa kwa tafiti za kiisimu jamii. Anauliza:

Wanaisimu jamii watawezaje kutathmini wingi lugha na hali hii itawezaje kutumika kuleta maendeleo ya taifa? (uk.17).

Kwa mujibu wa msomi huyu, lugha za kiasili zinafaa kuchangia katika kuleta maendeleo ya taifa. Haya maendeleo yataweza kufikiwa tu iwapo lugha za kiasili zinatumika kichanya, hivyo basi kuzifanya kuwa si rasilimali ya jamii zinazozizunguma tu, bali taifa lote kwa jumla. Hii ni kwa vile, jamii kadhaa zinaposhuhudia maendeleo, kiwango cha maendeleo ya nchi vilevile huinuka.

Naye Mwita (2002: 125), akishadidia umuhimu wa lugha za kiasili anasema kwamba, maendeleo katika jamii hulenga kuboresha maisha ya binadamu kwa njia zote lakini lengo hili haliwezi kufikiwa bila ya lugha. Anadai:

Maendeleo katika sehemu za mashambani yanalenga kuwezesha watu wengi waishio mashambani kupata huduma muhimu kama vile, huduma za afya, elimu, maji na utaratibu wa kuweka mifereji ya maji chafu.

Akionyesha upungufu ulioko katika lugha za kiasili, Mukuria (2002) anadahili kwamba, Wakenya wengi hawawezi kusoma na kuandika kwa lugha zao za kiasili. Anasema, mara nyingi fasihi inayopatikana katika lugha za kiasili ni Biblia na nyimbo za dini. Hali hii imechangiwa pakubwa na upuuzaji wa lugha za kiasili. Laiti mkazo wa kuzithamini lugha za kiasili ungewekwa, huenda hali isingekuwa hivyo. Hata hivyo, tangu kuanzishwa kwa vituo vya redio vya FM vinavyotumia lugha za kiasili, juhudi za kukuza lugha hizo ni za kujivunia. Kama mchango wa kukuza lugha za kiasili, utafiti huu ulilenga kuchunguza lugha hizi zinavyotumika kama rasilimali kwa wazungumzaji kupitia matumizi yake katika redio za FM. Urasilimali huu ulitokana na upekee wa habari ambazo watumizi lugha walipata, habari ambazo hawangepata kama lugha za kiasili hazingetumika.

Hata hivyo, matumizi ya lugha za kiasili yanakumbwa na changamoto kadhaa. Tisho kubwa la kufufuliwa upya kwa lugha za Kiafrika ni utandaridhi (Ongarora, 2002). Hali hii imesababisha ukinzani baina ya familia kubwa na ndogo za kimataifa. Kwa mfano, iwapo eneo fulani la kibiashara litateua lugha moja kwa mawasiliano mapana badala ya lugha ya wachache, lugha hiyo ya wachache huenda ikafa. Hali hiyo inaweza kudhihirika hasa katika baadhi ya lugha za kiasili zinazozungumzwa na watu wachache kama vile Kisuba na Kinjemp. Kwa hivyo, kuteuliwa na kuendelezwa kwa lugha mahususi huathiri kihasi kukua kwa lugha zingine. Kwa mfano, kuteuliwa kwa Kiswahili kama lingua franca ya Afrika Mashariki, kuna athari hasi kwa nyingi za lugha za kiasili. Swali tunalojiuliza ni, je, changamoto hii ina athari yoyote kwa lugha za kiasili kama rasilimali kwa watumiaji wake kupitia redio za FM ?

Kwa mujibu wa Kanana (2013: 17), mojawapo ya changamoto za makuzi ya lugha za kiasili ni kutotambuliwa kwa haki za lugha hizo. Kanana anasema kwamba:

Kutotambuliwa kwa haki za lugha za makundi yaliyo machache kunamaanisha kwamba lugha za kiasili hazitakuzwa na kupewa uwezo. Kutokana na hilo, wazungumzaji hawatapata huduma za serikali, mipango, maarifa na habari. Wazungumzaji wa hizi lugha mara nyingi huwa hawaelewi sera, malengo na mipangilio ya maendeleo hivyo basi hawawezi kuchangia kwa njia ifaayo katika mchakato huo.

Hapa tunaona kwamba, lugha za makundi machache ambazo katika muktadha huu ni lugha za kiasili zinakosa kukua na kupata uwezo kutokana na haki zake kupuuzwa. Matokeo ya kupuuzwa kwa haki hizo ni, wazungumzaji wa lugha hizo kutonufaika na huduma za serikali kwa vile, maarifa na habari zinazotolewa huwa kwa lugha wasiyoielewa. Wazungumzaji watanufaika pindi lugha hizo zitakapotambuliwa kupitia kwa utekelezaji wa haki za lugha. Utafiti huu uliweza kutathmini iwapo kuna huduma ambazo wazungumzaji wa Kibukusu wangekosa kupata, laiti lahaja hiyo isingetumika kuwasilisha huduma hizo.

Naye Prah (2005) anahoji, maendeleo yaliyodumishwa katika nchi huhusisha jamii za mashinani. Anasema, kufikiwa kwa jamii za mashinani, kutawezekana tu iwapo jamii-lugha hizo zitaweza kupewa mawazo ya ubunifu na yawasilishwe kwa lugha zao za kiasili ambazo hufikia watu wa mashambani kwa haraka zaidi na moja kwa moja. Kwa kuzingatia maoni ya msomi huyu, utafiti ulilenga kuchunguza iwapo matumizi ya Kibukusu kupitia kwa redio za FM yatawasilisha mawazo ya ubunifu kwa wakaazi wa Bungoma kwa haraka zaidi ikilinganishwa na lugha zingine. Iwapo hali hiyo inadhihirika, basi Kibukusu ni rasilimali kwa wazungumzaji wake kinapotumika katika redio za FM.

Ili kuweza kufikia maendeleo, sera na mipango ya serikali katika nyanja kama vile za siasa, utamaduni, uchumi, elimu na afya zinapaswa kuwasilishwa kwa watu kwa kutumia lugha watakayoelewa (Mohochi, 2007). Hali hii inatokana na uhalisia wa

mambo kwamba lugha za kiasili zinapotumika hutuwezesha kuwafikia watu wengi zaidi hata wale wasiofahamu Kiingereza na Kiswahili kwani takriban kila mtu anajua lugha yake ya kiasili. Iwapo kuna wasiojua lugha zao za kiasii, ni wachache tu wanaotokana na ndoa za wazazi wa makabila tofauti na hasa huwa ni vijana waliozaliwa na kukulia mijini. Tukirejelea jamii iliyoko mashinani katika kaunti ya Bungoma, utafiti huu ulitaka kuchunguza jinsi jamii ya Wabukusu inavyopata mawazo mbalimbali mapya, Kibukusu kinapotumika katika redio za FM.

Mtu huweza kuyaeleza maoni yake kwa njia bora zaidi kwa kutumia lugha yake au ya umilisi (Kachale, 2008). Kwa Waafrika wengi, lugha zao za umilisi ni lugha mama ambazo aghalabu huwa ni lugha za kiasili za Kiafrika. Ikiwa Waafrika wote watashiriki katika mchakato wa maamuzi, lazima wawe na wingi wa fahamu kuhusu yanayotendeka ulimwenguni. Ili kupata hiyo fahamu, pana haja ya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA). Ni kupitia kwa TEKNOHAMA ndipo wataweza kubadilishana mawazo na watu wengine wa ulimwengu. Swali la kujiuliza hapa ni je, lugha za kiasili zina istilahi zinazoweza kutumika katika TEKNOHAMA? Utafiti ulichunguza iwapo Kibukusu kimeweza kuibua istilahi zinazoweza kutumika katika TEKNOHAMA. Na kama istilahi hizo hazipo, je, lugha za kiasili zipuuzwe kutokana na udhaifu huu ama suluhu itafutwe na wasomi kupitia kuanzishwa kwa taasisi za kushughulikia changamoto hizo?

Changamoto kuu ya matumizi ya lugha za kiasili katika vyombo vya habari ni, madai kwamba vinaongeza chuki miongoni mwa Wakenya (Gathigi, 2009). Lugha za kiasili zinapotumika katika vyombo vya habari, mara nyingi zimeshutumiwa na kuhusishwa na uchochezi pamoja na vita vya kikabila (Mbeke & Mshindi; 2008, Kriegler; 2008 na O'rao, 2009). Ingawa shutuma hizo zipo, tunajiuliza je, iwapo patakuwa na udhibiti wa

namna fulani kwa matumizi ya lugha hizi hususan katika redio za FM, si lugha hizi zitaweza kuwa rasilimali kwa watumiaji? Hayo ni baadhi ya maswali yaliyolengwa kujibiwa na utafiti huu.

Kanana (2013) anadahili kwamba, maendeleo ya Afrika yamejikokota kwa vile mawasiliano muhimu hutegemea lugha za kigeni huku wahusika katika mchakato wa maendeleo wakikosa kuwasiliana kikamilifu. Kwa hivyo, si ajabu upate afisa wa serikali kule nyanjani akiwasiliana na watu mashinani ama kwa Kiingereza au Kiswahili na mwishowe asifikie lengo alilonuia. Kukosa kufikiwa kwa lengo la afisa husika hutokana na mawasiliano kamili kukosekana kutokana na hadhira yake kutokuwa na umilisi katika hizo lugha. Maoni haya ya Kanana yanaonyesha kwamba, pana haja ya kutambua lugha za kiasili ili wale wasio na umilisi katika Kiingereza na Kiswahili waweze vilevile kuhusika katika masuala muhimu yanayowahusu.

Msomi huyo anazidi kuhoji kwamba, Waafrika wengi hununua bidhaa kutoka Uchina, Korea na Japan mathalan simu, magari, bidhaa za nyumbani na kadhalika. Anahoji, vijitabu vya maelekezo ya jinsi ya kuzitumia bidhaa hizo huwa kwa lugha hizo. Ajabu ni kwamba ingawa vijitabu hivyo vimeandikwa kwa hizo lugha za Kichina na Kijapani, wanunuzi bado wanazinunua bidhaa hizo bila kutilia maanani lugha zilizotumika. Ni bayana kwamba siri ya maendeleo ni kuweka mikakati ya maendeleo kwa lugha za kiasili, jambo ambalo linakosekana katika nchi nyingi za Kiafrika.

2.1.2 Sera ya Lugha Nchini Kenya

Sera za lugha nchini Kenya zinadhihirika zaidi katika taasisi kama vile elimu, bunge, vyombo vya habari na mahakama, sehemu ambapo lugha mahususi zinatengewa majukumu mahususi (Muaka, 2011). Tangu Kenya ipate uhuru mwaka wa 1963, kumekuwa na tume kadhaa za elimu ambazo zimekuwa zikibuniwa kuunda upya sera

za elimu na kuunda upya sera za lugha zinazounganisha ufahamu wa kiisimu katika ujenzi wa taifa.

Kihistoria, Kenya inajulikana kuwa na tume mbalimbali za elimu ambazo zimetokana na mahitaji ya mabadiliko ya kitaifa. Kutokana na hayo, mapendekezo na sera za lugha zifuatazo zilianzishwa na kuendelezwa:

2.1.2.1 Tume ya Ominde (1964)

Ndiyo tume ya kwanza ya elimu katika Kenya huru. Tume hii ilijukumiwa miongoni mwa mambo mengine, kuchunguza vifaa vilivyokuwepo vya elimu. Vilevile ilitarajiwa kutoa ushauri kwa serikali kuhusu kuundwa na kutekelezwa kwa sera za kitaifa za elimu, zinazoonyesha thamani za tamaduni na kile nchi ya Kenya ililenga kufikia.

Kwa upande wa lugha, tume hii ilipendekeza yafuatayo:

- i). Matumizi ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia kuanzia darasa la kwanza.
- ii). Lugha za kiasili zitumike kila siku wakati wa kipindi cha masimulizi ya ngano katika darasa la kwanza, pili na tatu. Hili lingeweza lugha za kiasili kutekeleza majukumu yake ya kihistoria ya kuendeleza mawasiliano kitaifa.
- iii). Kiswahili kiwe lugha ya kuunganisha Wakenya na kuhimiza mawasiliano kimataifa. Hii ilitokana na usambazi wa Kiswahili nchini.
- iv). Kiswahili kiwe somo la lazima katika viwango vya shule za msingi ila pale ambapo Kiswahili na Kiingereza zilikuwa lugha ngeni (kwa jamii za Kihindi na zisizo na asili ya Kibantu). Miongoni mwa jamii hizo, Kiswahili kifundishwe kutoka darasa la tatu ili kuepuka na hali ya wanafunzi kusoma lugha ngeni mbili kwa wakati mmoja. Hata hivyo, Kiswahili hakikutahiniwa katika darasa la saba.

- v). Lugha ya Kiarabu kufundishwa katika shule za waislamu na za pwani kuanzia darasa la tatu.
- vi). Kiswahili kuwa somo la lazima katika shule za upili huku Kiingereza kikibaki kuwa lugha ya kufundishia. Hata hivyo, Kiswahili hakikutahiniwa katika kidato cha nne.
- vii). Kifaransa, kama lugha ya ziada katika shule ya upili kuwa bora zaidi ikilinganishwa na Kijerumani, Kirusi, Kilatini na Kiarabu kwa vile kilitumika katika nchi nyingi barani Afrika. Kijerumani na Kirusi kufundishwa kule ambako kulikuwa na vifaa huku Kilatini kikifundishwa katika kidato cha 6 kule kilikotumika.

2.1.2.2 Tume ya Gachathi (1974)

Ilikuwa tume ya pili ya elimu nchini Kenya. Iliundwa kuangalia upya malengo ya elimu nchini Kenya na kupendekeza sera mahususi na zinazogusia muundo wa mfumo wa elimu ikiwepo idadi ya miaka wanafunzi wanafaa kuwa shuleni, yaliyomo katika silabasi na utahini katika viwango vyote vya elimu. Tume hii ilitoa mapendekezo yafuatayo:

- i). Kutumia lugha inayozungumzwa zaidi katika eneo la shule kuwa lugha ya kufundishia kuanzia darasa la kwanza hadi tatu.
- ii). Kuanzisha Kiingereza kama somo, kuanzia darasa la kwanza na kukifanya kipiku lugha za kimaeneo kwa kukifanya kama lugha ya kufundishia katika darasa la 4.
- iii). Kufundisha kwa Kiswahili na Kiingereza kuanzia darasa la 4 hadi 7.
- iv). Kuhimiza kukuzwa kwa stadi za ufahamu katika lugha na uwezo wa kuwasilisha mawazo katika maandishi na mazungumzo.

- v). Kiswahili kuwa somo la lazima katika darasa la 3 (ama wakati Kiingereza kinapoanza kutumika kama lugha ya kufundishia). Hapa ni, pindi lugha za kiasili ziachapo kuwa lugha za kufundishia. Hili lingepusha wanafunzi kusoma lugha mbili ngeni; Kiswahili na Kiingereza kwa wakati mmoja.
- vi). Kukifanya Kiswahili lugha kuu na ya kutahiniwa katika shule za upili na kuchukua hatua madhubuti kuandaa walimu wa kutosha.
- vii). Kukifanya Kiswahili lugha ya taifa ya Kenya, inayopatikana katika shule kwa njia faafu ili kukuza ufundishaji wake katika vyuo vikuu.
- viii). Kufundisha kusoma na kuandika katika lugha za kiasili huku ikitiliwa maanani, matatizo yanayotokana na jitihada za kufunza lugha za kiasili pamoja na lugha mpya kama Kiswahili.

2.1.2.3 Ripoti ya Mackay (1981)

Lengo la Tume ya Mackay lilikuwa ni kupitia mfumo wa elimu ya juu uliokuwepo na kuanzishwa kwa chuo kikuu cha pili nchini Kenya. Kuhusu lugha, tume hii ilipendekeza yafuatayo:

- i). Kiswahili kiwe somo la lazima katika chuo kikuu cha pili nchini Kenya. Lengo la pendekezo hilo lilikuwa kukuza maendeleo ya Kiswahili kama lugha ya umoja si tu nchini bali pia katika Afrika Mashariki. Hata hivyo, pendekezo hilo halikutekelwa na chuo kikuu cha pili nchini Kenya, ila tu Chuo Kikuu cha Baraton. Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Baraton hutakiwa kuchagua kati ya Kiswahili na Kifaransa na wengi huteua Kiswahili.
- ii). Kiswahili kuwa somo la lazima na kutahiniwa katika darasa la nane na kidato cha nne.

2.1.2.4 Tume ya Koech (1999)

Ni tume ya mwisho ya elimu iliyo na ripoti iliyoandikwa. Lengo kuu la tume hiyo lilikuwa ni kuandaa jamii ya Wakenya kukumbana na changamoto za karne ya 21 na milenia ya 3. Hayo yalifaa kufikiwa kupitia kwa elimu, utafiti na kufundishwa. Tume hiyo ilikuwa na mapendekezo yafuatayo, yaliyogawika katika kiwango cha shule za msingi na za upili:

- i). Masomo katika shule za msingi yanayokuza umoja wa kitaifa. Kwa mfano, Kiswahili, fasihi, muziki na michezo ya kuigiza iendelezwe kama mojawapo ya njia za kuhifadhi tamaduni za Kenya, uzalendo na urithi wa kimataifa katika mtaala wa elimu.
- ii). Mtaala wa shule za msingi uwe na muundo unaowezesha mwanafunzi kupata maarifa yafuatayo:
 - a) Stadi za mawasiliano (Kuandika, Kusoma, Kusikiliza na Kuongea) anapokuwa shule za chekechea (miaka 5-6).
 - b) Stadi za lugha (Kuandika, Kusoma, Kusikiliza na Kuongea) katika lugha za kiasili, Kiswahili na Kiingereza katika darasa la 1 hadi 3.
 - c) Kiingereza na Kiswahili kufundishwa katika darasa la 4 hadi 7.
- iv). Lugha ya kufundishia katika darasa la 1 hadi 3 iwe lugha ya kiasili au inayozungumzwa na wengi katika eneo kunakopatikana shule. Katika jiji la Nairobi, manispaa na maeneo ya miji ambako idadi kubwa ya watu ni kutoka makabila mbalimbali, Kiswahili kiwe lugha ya kufundishia kuanzia darasa la 4 hadi 7, Kiingereza kitumike kama lugha ya kufundishia nchini kote.
- v). Wizara ya elimu ipendekeze mbinu za kuhakikisha kuchapishwa kwa vifaa vya kufundishia kwa lugha zote za kiasili nchini. Katika elimu ya shule za upili, tume hii ilipendekeza yafuatayo:

- a) Kutenganishwa kwa Lugha ya Kiswahili na Fasihi ya Kiswahili ili yawe masomo mawili kinyume na ilivyokuwa pale awali. Vivyo hivyo, Kiingereza kitenganishwe ili tuwe na masomo mawili: Lugha ya Kiingereza na Fasihi kwa Kiingereza.
- b) Kiswahili na Kiingereza kufanywa masomo ya lazima huku lugha za kigeni kama vile Kijerumani, Kifaransa na Kiarabu yakiwa masomo ya hiari.

Ripoti hii ilitazama sera ya lugha kupitia kwa mtaala, hivyo basi kupendekeza mabadiliko; badala ya ufundishaji, iwe utekelezaji. Katika viwango vya shule za msingi, ripoti hii ilisisitiza sera za lugha zinazokuza tamaduni za Kenya, uzalendo na urithi wa kimataifa kama sura mpya katika sera ya lugha.

Kutokana na mapendekezo ya ripoti za tume nne ambazo zimebuniwa tangu Kenya ipate uhuru mwaka wa 1963, ni bayana kwamba sera ya lugha kupitia kwa mitaala ya elimu haijatoa mchango mkubwa kwa makuzi ya lugha za kiasili. Kati ya ripoti hizo nne, Tume ya Mackay haitoi mchango wowote kuhusu lugha za kiasili.

Tume ya Mackay ilitilia mkazo makuzi ya Kiswahili kwa kupendekeza kufundishwa kwa lugha hiyo na kutahiniwa katika darasa la nane na kidato cha nne. Vilevile, tume hiyo ilipendekeza Kiswahili kiwe somo la lazima katika chuo kikuu cha pili nchini Kenya. Lengo la pendekezo hilo lilikuwa kukuza maendeleo ya Kiswahili kama lugha ya umoja, si tu nchini bali pia katika Afrika Mashariki. Kutokana na mkazo kutiliwa kwa Kiswahili, makuzi ya lugha za kiasili yaliweza kuathirika kihasi.

Kwa jumla, ripoti hizo nne zinatoa mwanga kwa misingi ya baadhi ya changamoto za matumizi mapana ya lugha za kiasili miongoni mwa wazungumzaji wake. Kwa hivyo, pana haja ya juhudi kufanywa kusudi kuiwekea misingi madhubuti matumizi ya lugha

za kiasili. Hilo litawezekana tu kama tafiti zitafanywa kuhusu umuhimu wa lugha za kiasili na majukumu zinayotekeleza zaidi ya majukumu ya kihistoria na mawasiliano iliyopendekeza Tume ya Ominde.

2.1.3 Matumizi ya Lugha za Kiasili Nchini Kenya

Kuna kiasili kilichokita mizizi miongoni mwa Wakenya wengi hasa wapangaji wa lugha kwamba matumizi ya lugha za kiasili ni ya kikabila, ya kutenganisha na kurudisha nyuma maendeleo (Luoch na Ogutu, 2002). Hata hivyo, tunapotathmini vita vya kikabila nchini Kenya vya 1992 na Disemba 2007 hadi Februari 2008, tunaona kwamba madai ya vita hivyo kusababishwa na tofauti za lugha hayana mashiko. Wanasiasa wamekuwa wakiwachochea Wakenya kwa misingi ya kikabila ili kufanya tofauti za kikabila zionekane kama msingi wa vita vya kikabila ilhali vita hivyo vilitokana hasa na katiba iliyokuwepo iliyompa rais mamlaka mengi kupita kiasi na matumizi mabaya ya hayo mamlaka (Roberts, 2009, Kriegler 2008 na Iraki, 2010).

Lugha hizi zimetumika katika nyimbo mbalimbali na kupendwa hata na watu wasio wazungumzaji wa lugha hizo. Kwa mfano kuna nyimbo kama vile “*Ategesi*” (na msanii Emmy Kosgei), “*Jo Kristo Duto*”(na kwaya ya St. Josephs Rapogi) na “*Umbolela Si*”(na msanii David Barasa) ambazo zinasikizwa na watu wengi wakiwemo hata wasio wazungumzaji wa lugha hizo. Kutokana na hali hiyo, ni bayana kwamba lugha hizo si mbaya ila matumizi mabaya ndiyo yanayofaa kushutumiwa. Utafiti huu unatoa mapendekezo ya njia mbalimbali ambazo zinaweza kutumika kuzifanya lugha hizo ziwe rasilimali si tu kwa wazungumzaji wake, bali pia kwa wasio wazungumzaji wake.

Akisisitiza umuhimu wa lugha za kiasili, Mugambi (2007: 67) anasema hivi:

Miradi ya kisasa inayokusudiwa kuelimisha umma nchini Kenya haiwezi kueleweka katika lugha nyingine yoyote isipokuwa lugha ya wananchi hao wa vijijini, ambao wengi wao hawajui kusoma wala kuandika.

Kusoma na kuandika anakorejelea msomi huyu ni kwa lugha za kigeni ambazo hasa ndizo lugha zinazotumika katika mfumo wa elimu. Miradi hii ni pamoja na, kampeni za kuhamasisha umma kuhusu katiba ya elimu ya uraia, tohara ya wanawake, marekebisho ya mfumo wa elimu na utetezi wa haki za wanawake. Kwa mujibu wa Mugambi (2007), kutokana na hali hiyo, mashirika ya serikali na wadau wengine wanastahili kutumia lugha za kiasili au lugha za wenyeji vijijini kadiri wawezavyo, ikiwa wanataka kupata matokeo yenye manufaa. Utafiti wetu ulinuia kutathmini madai haya kwa kutumia kigezo cha lugha za kiasili zinavyojitokeza kama rasilimali kwa wazungumzaji wake.

2.1.4 Majukumu ya Vyombo vya Habari

Miongoni mwa majukumu yanayotekelezwa na vyombo vya habari ni kutambua, kufuata na kueleza matukio mbalimbali katika mazingira yetu, hasa kwa kuyahusisha na hali ya kisiasa na kiuchumi inayotawala maisha yetu (Mohochi, 2006). Akiwanukuu McQuail (1987) na Wood (1983), Mohochi (2006) anasema kwamba vyombo vya habari hutoa fursa kwa watu kujihusisha na kushiriki katika maamuzi na majadiliano kuhusu masuala tofauti yanayoathiri maisha yao kitaifa na kimataifa. Tukirejelea vituo vya redio vinavyowasilisha baadhi ya matangazo kwa lugha za kiasili katika kaunti ya Bungoma, Sulwe FM na West FM, mtafiti alilenga kuchunguza jinsi vituo hivi hutekeleza majukumu haya hususan Kibukusu kinapotumika na changamoto zake katika utekelezaji huo.

Naye Makunja (1995) anahoji kwamba, redio na televisheni zina uwezo wa kuwafikia mamilioni ya watu katika muda uleule. Ni wazi kuwa vyombo hivi viwili vina uwezo mkubwa upande wa kutekeleza mawasiliano, hivi kwamba vinaweza kutegemewa kwa mawasiliano yanayohitaji kufikia umati mkubwa wa watu. Mtafiti alilenga

kuhakiki uwezo huu unavyojitokeza katika redio za Sulwe na West FM. Alilenga kuhakiki uwezo huo Kibukusu kinapotumika katika mawasiliano yanayolenga kuangazia masuala ya jamii, afya, uchumi na siasa kwa wasikilizaji wake. Hivyo basi, matumizi hayo yalizifanya rasilimali kwa wakaazi wa kaunti ya Bungoma wanaozungumza Kibukusu.

Mawazo haya ni sawa na ya Mlacha (1995), anayesema kwamba vyombo vya habari vina nafasi kubwa sana katika kukidhi lengo la mawasiliano katika jamii. Aidha, hii ndiyo njia mojawapo ya kuwafanya wanajamii waweze kuyafahamu matukio tofauti ya kila siku katika jamii yao, waifahamu na kuelewa jamii yao na mazingira yao kwa upana na undani zaidi. Iwapo wanajamii watapata ufahamu huu, hasa kwa kutumia lugha za kiasili, basi vyombo hivyo na lugha zitakuwa zimejitokeza kama rasilimali. Utafiti wetu ulijifunga katika kuchunguza iwapo matumizi ya Kibukusu katika Sulwe na West FM yanatimiza jukumu la kufanya jamii ya wakaazi wa kaunti ya Bungoma inayozungumza Kibukusu iyaelewe mazingira yake kwa upana na undani.

Akiwarejelea Haji Konde (1984) na Igbenedion (1985), Mlacha (1995) anadai kwamba ingawa vyombo vya habari vinaweza kuwa na athari mbaya kwa hadhira, baadhi ya vyombo hivi vinaweza kuwa silaha ya kulinda hadhi ya binadamu hasa tunapozingatia kipengele cha kuelimisha jamii. Swali alilojiuliza mtafiti ni, je vituo vya West na Sulwe FM vimejitokeza vipi kama silaha ya kulinda jamii inayozungumza Kibukusu kwa kuelimisha kuhusu masuala ya jamii, afya, uchumi na siasa kupitia vipindi vinavyopeperushwa?

Mdee (1999) anahoji, mawasiliano huathirika itokeapo kuwa baadhi ya wanajamii hawaelewi maana ya msamiati unaotumiwa katika mazungumzo. Mawasiliano yanapotumia lugha ya kitaalamu vilevile huathirika hususan iwapo istilahi

zinazotumika hazifahamiki kwa wazungumzaji wote. Ikikisiwa, kwamba matumizi ya istilahi za kitaaluma ni baadhi ya changamoto za lugha za kiasili kujitokeza kama rasilimali kwa wazungumzaji, utafiti ulilenga kuchunguza mikakati iliyoandaliwa na redio za FM kukabiliana na changamoto hiyo.

Musau (2002), akimnukuu Wardhaugh (1987) anasema, vyombo vya habari vinaweza kukuza lugha fulani kwa kuamua kuitumia kimakusudi. Hali hiyo huweza kuchukuliwa kama njia makusudi ya kuingilia masuala ya lugha; hali inayoweza kuathiri mwelekeo wa lugha. Katika muktadha huu, vyombo vya habari huwa vimetoa ajenda kwa matumizi ya lugha kwa kuelekeza lugha ya matumizi katika mawasiliano. Maadamu Sulwe na West FM vinatumia Kibukusu kupeperushia matangazo, mtafiti alikisia kwamba vituo hivyo viliamua kutumia Kibukusu kwa vile vilitambua ni rasilimali kwa wazungumzaji. Kwa hivyo, utafiti ulilenga kuchunguza Kibukusu kinavyojitokeza kama rasilimali kuangazia masuala ya jamii, uchumi, siasa na afya kwa wakaazi wa Bungoma kitumikapo katika redio za FM.

Kutokana na upana wa hadhira yake, vyombo vya habari vina nafasi kubwa kuliko mwalimu yeyote ya kuwafikia watu wengi zaidi kwa wakati mmoja (Mohochi, 2006). Maadamu vyombo hivyo vina uwezo wa kuwafikia watu wengi, mtafiti alitaka kutathmini iwapo Kibukusu kinapotumika katika redio za FM katika kaunti ya Bungoma zinatekeleza majukumu ya kupasha habari zinazostahili kupashwa wakaazi hao. Hususan, utafiti ulilenga kuchunguza iwapo vituo hivyo viliwapasha habari muhimu kuhusu masuala ya jamii, afya, uchumi na siasa.

Ni muhimu kutambua hapa kwamba, ili lengo la mawasiliano liweze kufikiwa, pana haja ya kutumia lugha inayoeleweka vizuri zaidi na jamii husika (Muluka, 2010). Hii ndiyo sababu kuu ya matumizi ya lugha za kiasili hasa katika vyombo vya habari

kama vile redio sehemu za mashambani. Utafiti ulilenga kuhakiki yaliyomo katika vipindi vya masuala ya jamii, uchumi, siasa na afya vinavyowasilishwa kwa kutumia Kibukusu katika redio za FM zinazosikika katika kaunti ya Bungoma. Vilevile, utafiti ulitaka kutambua manufaa ya matumizi ya lugha hiyo ya kiasili ikilinganishwa na lugha zingine kama vile Kiswahili.

Nyika (2015) anahoji kwamba, licha ya vyombo vya habari kuongeza nafasi za ajira, husaidia kuhifadhi na kukuza lugha za tamaduni mbalimbali. Iwapo ukuzaji lugha za tamaduni mbalimbali ni kati ya majukumu ya vyombo vya habari, utafiti ulitaka kuchunguza jinsi jukumu hilo linavyoendelezwa na vituo vya redio vya West na Sulwe FM ambapo kwa kufanya hivyo vinajidhihirisha kama rasilimali kwa wasikilizaji.

2.1.5 Lugha za Kiasili katika Vyombo vya Habari

Baada ya uchaguzi wa 1992 nchini Kenya, kulitokea uhuru wa vyombo vya habari na kuvifanya viwe na nguvu zaidi katika eneo hili. Kama kifaa cha kupasha habari, vyombo vya habari vina athari kubwa kwa wananchi. Shirika la Utangazaji la Kenya (KBC) hutumia Kiingereza na Kiswahili katika matangazo yake. Vipindi vyake vingi ni vya Kiingereza vikifuatiwa na Kiswahili huku vituo vya redio zinazotumia lugha za kiasili 17 vikitengewa saa nne kwa siku.

Kwa mujibu wa Muaka (2011), watangazaji katika redio za FM zinazotumia lugha za kiasili hawaajiriwi kutokana na elimu yao katika taaluma ya uanahabari, bali umaarufu wao kwa umma. Hata hivyo, hali hiyo imeweza kubadilika kutokana na hatua ambazo zimepigwa na vituo hivi vya redio vinavyotoa matangazo kwa lugha za kiasili. Kwa mujibu wa MCK (2012), kiwango cha chini cha kuajiriwa kama mwanahabari katika vingi vya vituo hivi vya redio vinavyotumia lugha za kiasili ni

stahhada katika taaluma ya mawasiliano. Hilo ni jambo ambalo tuliweza kudhihirisha katika utafiti huu. Baadhi ya wanahabari hao hata walikuwa na shahada za uzamili katika mawasiliano huku wengine wakiwa wamejisajili kama wanafunzi wa uzamifu. Katika uandishi wa habari za magazeti, Kiingereza kimetumika zaidi huku tukiwa na gazeti moja tu la Kiswahili (Taifa Leo).

Lugha za kiasili hazitumiki katika uandishi wa magazeti ya kitaaluma. Serikali ya Kenya haiungi mkono lugha za kiasili kama njia ya kupasha habari kwa umma kwa hofu ya kusababisha tofauti za kikabila. Kutokana na msimamo huo, serikali nchini Kenya imekuwa ikiviza ukuaji wa matumizi ya lugha za kiasili. Hata hivyo, uhuru wa vyombo vya habari umeweza kusaidia katika ongezeko la vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili huku vituo hivyo vikifikia 54 mwaka wa 2014 (Okoth, 2015).

Ingawa vituo vya redio za kibinafsi vya FM vimechangia pakubwa kueneza matumizi ya lugha za kiasili, sera ya lugha katika vyombo vya habari kama vile KBC inahimiza zaidi matumizi ya Kiingereza na Kiswahili. Hata hivyo, kufikia mwaka wa 2015, tumeshuhudia ongezeko la vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili huku *Royal Media Services* ikiongoza kwa idadi ya vituo vinavyotumia lugha za kiasili kwa kuwa na vituo 12 vya lugha za kiasili (Okoth, 2015).

Maendeleo katika uandishi wa habari na uchapishaji yatawezekana tu iwapo lugha za Kiafrika na tamaduni zake zitapewa nafasi kukua na kuchangia maendeleo (Muthwii, 2002). Lugha za Kiafrika zinapotumika, hadhira ya uandishi habari na uchapishaji itaongezeka kwa vile jamii isiyo na umilisi wa lugha za kigeni itaweza vilevile kuhusishwa. Kuanzishwa kwa vituo vya redio vya FM vinavyotumia lugha za kiasili kunaweza pia kuchangia maendeleo hayo kwa vile, hadhira isiyo na umilisi katika

lugha zingine kama vile Kiswahili na Kiingereza itahusishwa katika maamuzi yanayohusu jamii hizo. Matumizi ya lugha hizi za kiasili yatawezesha wakaazi hasa wa mashambani kupata maarifa kwa lugha wanazoelewa. Utafiti huu ulichunguza mchango wa redio za Sulwe na West FM katika kukipa Kibukusu na tamaduni zake nafasi ya kukua na kuchangia maendeleo ya wenyeji, hivyo basi kujitokeza kama rasilimali ya jamii inayozisikiza.

Naye Prah (2005) anadai, bila matumizi ya lugha za Kiafrika katika mfumo wote wa elimu na jamii kwa jumla, maendeleo katika bara la Afrika hayawezi kufikiwa. Anazidi kusema kwamba, hatua ya vyombo vya habari kuamua kwa njia ya makusudi kuingilia masuala ya lugha kama njia inayoweza kuathiri mwelekeo wa lugha kwa kuongeza idadi ya vituo vinavyotumia lugha za kiasili inafaa kupongezwa. Ni wazi kwamba, vituo hivi vinapongezeka, vinakumbana na changamoto mbalimbali. Utafiti huu ulilenga kupambanua na kujadili changamoto zinazokumba vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili hususan lugha za wenyeji zinapotumika huku ukijikita katika Kibukusu, lahaja inayozungumzwa na wengi katika kaunti ya Bungoma.

Nchini Kenya, ingawa Kiswahili ndiyo lugha ya Kiafrika inayotumika zaidi, matumizi yake katika redio hayashughulikii kikamilifu wasikilizaji wake (Gathigi, 2009). Hivyo basi, kumekuwa na haja vilevile ya kutumia lugha za kiasili ambazo zina uwezo wa kuathiri wenyeji kichanya. Tofauti ya utafiti wa Githigi (2009) na huu ni kwamba, yeye alitafitia usikilizaji wa redio miongoni mwa wakaazi wa mashambani katika eneo la Kyeni ilhali utafiti huu ulitafitia matumizi ya lugha za kiasili katika redio za FM, huku ukijikita katika kaunti ya Bungoma. Hata hivyo, tafiti zote mbili zinaoanisha lugha za kiasili na redio za FM.

Uteuzi wa lugha ya kutumika katika vyombo vya habari hutegemea masuala mengi. Mojawapo ya sababu za uteuzi wa lugha ya kutumika ni, idadi ya wazungumzaji (Kachale, 2008). Ni kutokana na sababu hii ndipo baadhi ya lugha zikatumika katika vituo vya redio zaidi ya zingine. Kwa mfano, lugha za kiasili kama vile Kikikuyu, Kiluyia, Kikalenjin na Kijaluo zina idadi kubwa ya wazungumzaji. Huenda wingi huo wa wazungumzaji ukawa mojawapo ya sababu kuu ya lugha hizo kutumika zaidi katika redio za FM. Vituo hivi vya redio vimekuwa vikilenga hasa wakaazi wa mashambani ambako kuna wazungumzaji wengi zaidi wa lugha za kiasili. Hata hivyo, wingi wa watu hautoshi kuwa msukumo wa ongezeko la vituo hivyo sehemu za mashambani. Tunakisia kwamba katika enzi hii, ongezeko hilo linatokana na vituo hivyo vya redio kuwapasha wazungumzaji habari ambazo hawangepata laiti lugha zingine zingetumika. Kwa hivyo, utafiti huu ulitathmini Kibukusu kinavyojitokeza kama rasilimali kuangazia masuala ya jamii, uchumi, siasa na afya kwa wazungumzaji wake kinapotumika katika redio za FM. Huenda masuala hayo hayangeangaziwa vizuri kwa Kiswahili jinsi Kibukusu kinavyoangazia kwa wazungumzaji wake .

Awali, idhaa za redio zilizotumia lugha za kiasili zilikuwa zikirusha matangazo yake kwa saa chache sana (Mohochi, 2007). Hata hivyo, miaka ya hivi karibuni imeshuhudia ongezeko la matangazo kwa kutumia lugha za kiasili. Hali hiyo imetokana na kuibuka na kuongezeka kwa vituo vya redio vya FM hasa vinavyotangaza kwa kutumia lugha za kiasili. Utafiti huu ulilenga kuchunguza manufaa ya ongezeko la muda uliotengwa na vituo hivi kwa matumizi ya Kibukusu kwa Wabukusu ambao ni wakaazi wa kaunti ya Bungoma. Kwa mfano, kituo cha Sulwe FM hupeperusha matangazo yake yote kwa kutumia Kibukusu.

Kwa mujibu wa Wanjiku (2009), redio za jamii huwa na athari ya moja kwa moja katika ukuzaji wa uwezo wa jamii husika. Hali hii hutokana na lugha inayotumika ambayo ni ya wenyeji na masuala yanayoangaziwa ambayo yanaihusu jamii hiyo. Utafiti huu ulilenga kuchunguza iwapo matumizi ya Kibukusu katika Sulwe na West FM yanakuza uwezo wa jamii inayoitumia lugha hiyo, hivyo basi kujitokeza kama rasilimali kwa watumiaji wake (Wabukusu).

Anavyohoji Shitemi (2010), aina yoyote ya maendeleo huhitaji lugha inayokubalika na kueleweka ili kutumika kwa pamoja baina ya wadau. Hii ndiyo sababu ya ongezeko la vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili, lengo likiwa ni kuweza kuwanufaisha zaidi watu walioko mashambani katika uboreshaji wa hali zao kiuchumi na kijamii. Utafiti huu ulichunguza iwapo Kibukusu kimewanufaisha watumiaji wake kinapotumika katika redio za FM. Iwapo lugha hii inawanufaisha wazungumzaji wake, basi ni rasilimali kwa watumizi wake.

Vita vya kikabila vilivyotokea nchini Kenya baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi ya 2007 vilisababisha mizozo na madhara baina ya baadhi ya jamii, jambo lililosababishwa na uchochezi kwa kutumia lugha za kiasili (Mshindi, 2008). Vita hivyo vya kikabila vilisababisha hasara kubwa kwani, licha ya watu wengi kupoteza maisha, wengine walifanywa kuwa wakimbizi wa ndani kwa ndani huku viwango vya uchumi wa nchi ya Kenya vikishuka chini. Ingawa madai hayo ya uchochezi yalitolewa, ni vituo vichache tu vinavyoshutumiwa kwa madai hayo. Kwa hivyo, hatuwezi kujumlisha kwamba, matumizi ya lugha za kiasili katika vyombo vya habari kama vile redio lazima yachochee chuki miongoni mwa jamii. Kama mojawapo ya njia za kukuza matumizi bora ya lugha za kiasili, utafiti huu umependekeza njia zinazoweza kutumika kudhibiti matumizi mabaya ya lugha za kiasili hususan katika redio za FM zinazotumia lugha za kiasili.

Kwa mujibu wa Seidu Al-hassan na wenzake (2011), wakirejelea manufaa ya mojawapo ya redio za jamii kwa jina “Simli Redio” kilichoko nchini Ghana, wanasema yalikuwa mengi yakiwemo: kuelimisha, kukuza tamaduni za jamii, mawasiliano kwa wasikilizaji, burudani na kukuza mali ya jamii. Utafiti huu ulitaka kuchunguza baadhi ya manufaa waliyopata wasikilizaji wa Sulwe na West FM yakilinganishwa na “Simli Redio.”

Seidu Al-hassan na wenzake (2011) wanahoji, “Simli Redio” inatumika kuboresha ufahamu wa wasikilizaji wake kuhusu masuala mbalimbali yanayowahusu na kutoa suluhisho kwa changamoto zinazowakumba zikiwemo za tamaduni, elimu, afya, kilimo na utawala wa mashinani. Utafiti huu ulilenga kuchunguza mchango wa redio za Sulwe na West FM katika kuboresha ufahamu wa wasikilizaji wake kuhusu masuala mbalimbali Kibukusu kinapotumika.

Utafiti huu vilevile ulichunguza mikakati inayotumika na vituo hivyo vya redio kwa kutumia Kibukusu kushughulikia changamoto zinazowakumba wasikilizaji wake. Tofauti ya utafiti wa Seidu Al-hassan na wenzake (2011) na huu ni kwamba, wao walitafitia jamii zinazopatikana katika wilaya za Tolon-Kumbungu na Savelugu-Nanton kaskazini mwa Ghana huku huu ukitafitia jamii ya Wabukusu, inayopatikana katika kaunti ya Bungoma. Vilevile, kinyume na utafiti huu ambao unatafitia vituo vya redio vya kibinafsi, wao walishughulikia redio za jamii ambazo hushughulikia masuala ya jamii na kusimamiwa na jamii hiyo.

Kulingana na Kamau (2011), vituo vya redio vya lugha za kiasili ni njia bora zaidi ya upashaji habari mashinani. Anazidi kuhoji kwamba, wasikilizaji huziona redio zinazotumia lugha za kiasili kama “rafiki” anayetoa habari wanazotumia kufikia maamuzi kuhusu masuala mbalimbali. Ni bayana kwamba, Kamau anahimiza kuwepo

kwa vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili. Kinyume na utafiti wake uliotafitia redio zinazotumia lugha za kiasili, utafiti huu ulichunguza matumizi ya lugha za kiasili katika redio za FM huku ukilenga kuchunguza lugha hizi zinavyojitokeza kama rasilimali kwa watumiaji wake hususan katika kaunti ya Bungoma.

Kwa mujibu wa Baraza la Wanahabari Nchini Kenya (MCK, 2012), redio zinazotumia lugha za kiasili hutoa mchango mkubwa katika mijadala ya masuala ya umma. Baraza hili linasisitiza kwamba lugha za kiasili katika vyombo vya habari huchangia pakubwa maendeleo mashinani na uhusishwaji wa jamii za mashinani ambapo idadi kubwa ya watu haitumii Kiingereza na Kiswahili katika mawasiliano. Swali tunalojiuliza kutokana na ripoti hiyo ya Baraza la Wanahabari nchini Kenya ni, Je, miaka kadhaa baada ya ripoti hiyo kutolewa, kuna mabadiliko yoyote kuhusu matumizi ya lugha za kiasili katika vyombo vya habari na maendeleo mashinani hususan katika kaunti ya Bungoma, huku upeo wetu ukiwa ni redio za Sulwe na West FM?

Baadhi ya masuala ambayo West FM huangazia ni ya kuelimisha wakulima, ya kijamii na kiuchumi kwa mujibu wa mwenyekiti wa kituo hicho (MCK, 2012). Utafiti ulilenga kuchunguza kwa kina masuala ambayo Sulwe na West FM huangazia kwa kutumia Kibukusu. Utafiti ulitarajia vile vile kuchunguza manufaa wanayopata wasikilizaji wa redio hizo walioko mashinani kutokana na vipindi hivi, Kibukusu kinapotumika.

Kutokana na ripoti ya Halmashauri ya Mawasiliano nchini Kenya, kufikia mwaka wa 2012, kulikuwa na vituo 30 vya utangazaji vilivyotumia lugha za kiasili (MCK, 2012). Makuzi haya yalikuwa ya kasi kwa vile kituo cha kwanza cha lugha za kiasili; Kameme FM kilianzishwa mwaka wa 2000. Hata hivyo, kati ya vituo vya kwanza

barani Afrika kutumia lugha za kiasili, kilikuwa Kituo cha Redio cha Jamii cha Homabay kilichoanzishwa Mei 1982. Ingawa kituo hiki kilitumia lugha ya kiasili, kilikuwa kituo cha redio za jamii (Ngugi na Kinyua, 2014). West na Sulwe FM vikiwa kati ya vituo hivyo 30, utafiti ulitaka kuchunguza yanayowasilishwa na vituo hivi kwa kuzingatia masuala ya jamii, siasa, uchumi na afya.

Kufikia mwaka wa 2014, vituo hivi vilikuwa vimeongezeka hata zaidi na kufikia 54 (Okoth, 2015). Kwa mujibu wa Okoth (2015), kufikia mwaka wa 2014, kati ya vituo 158 vya redio, ni 54 vinavyotangaza kwa lugha za kiasili. Anahoji kwamba, kati ya vituo hivyo 54, 'Royal Media Services' ilimiliki vituo 12 vinavyotoa habari kwa lugha za kiasili. Okoth (2015) alitafitia makuzi ya lugha za kiasili hususan katika Ramogi FM. Utafiti huu ni tofauti na wa Okoth (2015) kwa vile ulitafitia jinsi lugha za kiasili zinavyojitokeza kama rasilimali kinyume na wake uliotafitia makuzi ya lugha za kiasili katika redio za FM.

Ingawa vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili vilishutumiwa kwa kuchochea uwoga na chuki miongoni mwa jamii nchini Kenya 2007, zilipongezwa kwa mchango wake katika kutuliza migogoro (Githethwa, 2008). Vituo hivi viliweza kutuliza migogoro miongoni mwa Wakenya kwa kuhimiza mijadala ya amani ipewe uzito zaidi miongoni mwa jamii zilizokuwa zikizozana (Kamau, 2011).

Katika nchi nyingi na maeneo mbalimbali, vituo vya redio vya jamii hukuza wanajamii na kuamsha hamu yao kushiriki na kuchangia katika usimamizi ulio na uwazi na uwajibikaji hata katika mazingira yaliyo na changamoto za udhibiti (Wabwire, 2013). Usimamizi mzuri na uongozi madhubuti hususan katika jamii zilizo na umaskini ni mchakato unaojumuisha jamii yote na hutegemea jamii iliyo na ufahamu na bidii. Kwa hivyo, redio za jamii zimedhihirisha kwamba zinaweza

kuendelezwa na kuwa njia ya kusikika kwa jamii zilizo maskini na zilizotengwa. Utafiti huu ulilenga kuchunguza matumizi ya Kibukusu yalivyowezesha jamii ya Wabukusu kusikika.

Kwa mujibu wa Castle (2014), lugha za kiasili katika vyombo vya habari ni muhimu sana hususan katika masuala ya maendeleo kwa vile wasikilizaji wengi huweza kupokea ujumbe na kuelewa kwa njia rahisi. Akitaja lugha ya Kisuba kama mfano, anasema kwamba “redio hufufua” lugha zisizozungumzwa sana kutokana na elimu ya kimagharibi. Kwa mujibu wa Castle (2014), Kisuba kimefufuliwa na kusikizwa sana kutokana na kutumika kwa Redio ya EK inayotangaza kwa Kisuba. Utafiti huu ulilenga kutathmini iwapo matumizi ya Kibukusu katika vituo vya redio vya Sulwe na West FM yanachangia kuhakikisha kwamba lugha hiyo inachangia masuala ya maendeleo kupitia ujumbe unaowasilishwa na kueleweka vizuri zaidi ikilinganishwa na matumizi ya lugha zingine kwa wakaazi wa Bungoma. Iwapo Kibukusu kilitoa mchango huo, utafiti ulichunguza ikiwa matumizi hayo ya Kibukusu katika redio za FM ni rasilimali kwa wazungumzaji wake.

2.1.6 Hadhi ya Lugha za Kiasili

Utafiti huu ulitafitia jinsi redio za FM zinavyochangia kuinua hadhi ya Kibukusu kwa kukiimarisha kama rasilimali kwa wazungumzaji wake. Vyombo vya habari vya kielektroniki vimeanzisha majukwaa ya kisasa yanayowezesha wananchi kuchangia masuala yanayoangaziwa katika vyombo hivyo (Mbeke & Mshindi, 2008). Kutokana na maendeleo hayo, redio na televisheni huwa na mahojiano ya moja kwa moja wakati wa kutolewa kwa matangazo, mijadala hewani, pamoja na kuhojiwa kwa washikadau mbalimbali moja kwa moja kwenye vyombo hivyo.

Hata hivyo, kuna mtazamo wa jumla kwamba vituo vingi vya redio havina udhibiti katika mazungumzo ambayo huwepo kati ya watangazaji na wasikilizaji kutokana na watangazaji hao kutoandaliwa kimafunzo (Kamau, 2011). Akinukuu Tume Huru ya Mageuzi ya Katiba nchini Kenya baada ya uchaguzi wa 2007, msomi huyu anahoji kwamba ripoti hiyo ilipendekeza kupigwa marufuku kwa vituo vya redio vinavyopeperusha matangazo kwa lugha za kiasili. Mapendekezo ya tume hiyo yanachangia kurudisha hadhi ya lugha za kiasili chini na kuzifanya zionekane kama zinazorudisha mataifa nyuma ikizingatiwa kwamba zinasababisha machafuko. Swali tunalojiuliza hapa ni je, vituo vyote vinavyotumia lugha za kiasili vifungwe au vile vinavyotumia lugha hizo vibaya? Utafiti huu ulidhamiria kudhihirisha kwamba lugha za kiasili zinaweza kuwa rasilimali, si kwa wazungumzaji wake pekee bali taifa zima zinapotumika redioni kichanya.

Wakati uo huo, mfumo wa uwasilishaji vipindi katika redio umebadilika sana. Kumeibuka mtindo wa mawasiliano yanayowashirikisha wasikilizaji kwa kupiga simu kwa kiasi kikubwa na kuandika jumbe fupi kwa watangazaji kwa kutumia simu za mkono. Hali hiyo inatokana na muungano kati ya teknolojia ya kisasa na ya kale (Ogechi na Bosire, 2010; Gathigi, 2009). Hii teknolojia ya mawasiliano inahusisha tarakilishi, simu tamba, picha na tovuti. Kwa upande mwingine, teknolojia ya kale ya mawasiliano inahusisha redio, televisheni na magazeti. Teknolojia mpya ilimwezesha mtafiti kuwafikia wasikilizaji wengi wa Sulwe na West FM. Kwa kusaidiwa na watangazaji, mtafiti aliweza kupata nambari za simu za viongozi wa baadhi ya vikundi ambavyo husikiliza vituo hivyo. Kutokana na nambari hizo, mtafiti aliweza kuwafikia wasikilizaji wengine kwa urahisi na kuwahoji.

Kuhusu hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuipa lugha hadhi, Evariste (2001) akimnukuu Sadembaou (1990) anatoa mapendekezo kadhaa ya kutekelezwa. Miongoni mwa mapendekezo yake ni, kuifanya lugha hiyo kuwa muhimu katika maisha ya wazungumzaji kijamii na kiuchumi. Swali tunalojiuliza hapa ni, je, Sulwe na West FM zimekipa Kibukusu umuhimu gani katika maisha ya wazungumzaji kijamii, kisiasa, kiafya na kiuchumi, hivyo basi kuchangia katika kuinua hadhi ya mojawapo ya lugha za kiasili?

Buliba (2002) akishadidia umuhimu wa lugha za kiasili anahoji, hapana yeyote anayeweza kufikia ufanisi kwa kutumia lugha asiyoweza kuimudu kikamilifu. Anasema, watu huweza tu kuyaeleza na kuyafafanua mambo ya kimsingi katika utamaduni wao kwa kutumia lugha wanayomudu kikamilifu. Msomi huyu anahoji, lugha hii agahalabu huwa ni ile ya kiasili. Utafiti huu ulilenga kuchunguza ikiwa wataalamu mbalimbali huweza kuyaelezea mambo ya kimsingi kuhusu taaluma zao yanayoangazia masuala ya jamii, afya, uchumi na siasa kupitia vituo ya redio vilivyoteuliwa katika Sulwe na West FM. Iwapo wataalamu hawa huangazia masuala hayo kwa ukamilifu, basi hali hiyo huinua hadhi ya lahaja ya Kibukusu na kuifanya rasilimali kubwa kwa wazungumzaji wake.

Kushirikishwa kwa jamii katika upunguzaji umaskini kunaweza tu kufikiwa kikamilifu iwapo lugha inayotumika mahali kama vile bungeni, katika manispaa na kadhalika haitakuwa ya kigeni (Moto, 2002). Pana haja ya kushirikishwa kwa jamii kupitia matumizi ya lugha za wenyeji kama vile lugha za kiasili katika mawasiliano hayo. Hatua kama hiyo inaweza ikachangia kuinuliwa kwa hadhi ya lugha za kiasili. Maadamu upeo wa utafiti huu ni masuala ya jamii, uchumi, afya na siasa, niliweza kuchunguza iwapo hadhi ya Kibukusu imeinuliwa kutokana na masuala haya

kuangaziwa kupitia redio za FM hivyo basi kukifanya rasilimali kwa wazungumzaji wake.

Kwa mujibu wa Simala (2002), maendeleo barani Afrika hayawezi kufikiwa bila lugha za Kiafrika kupata uwezo wa kuwasiliana. Uwezo huo hauwezi kufikiwa bila ya lugha za Kiafrika kuhusishwa kikamilifu katika uwasilishaji wa masuala muhimu yanayopatikana katika jamii husika. Kwa hivyo, iwapo lugha za kiasili ambazo ni miongoni mwa zile za Kiafrika zitakazohusishwa katika mawanda mapana ya mawasiliano, hadhi ya lugha hizo itainuka. Utafiti ulilenga kutathmini jinsi Kibukusu kinavyojitokeza katika uwasilishaji wa masuala muhimu yanayopatikana katika jamii na hivyo basi kuwa rasilimali kwa wazungumzaji wake na kuinua hadhi yake.

Kulingana na Musau (2002), pana haja ya Waafrika kuzifanya lugha zao ziwe za kisasa licha ya kutambua majukumu ya lugha hizo. Waafrika wanahitaji kuamini uwezo wa lugha zao katika utatuzi wa matatizo yao. Jambo hili litawezekana kwa kuzihusisha katika TEKNOHAMA. Matumizi ya lugha za kiasili katika vyombo vya habari kama vile redio ni mojawapo ya juhudi za kuziingiza katika TEKNOHAMA. Ni matarajio yetu kwamba iwapo Kibukusu kinatumika kuangazia masuala yanayoiathiri jamii kiafya, kiuchumi, kisiasa na kijamii huku kikitatua matatizo yao, basi hadhi yake itakuwa ya kiwango cha juu.

Lugha haiwezi kustawi na kuitwa lugha ya kisasa bila kuwepo mahitaji ya matumizi yake katika shughuli nyingi zaidi (Wolff, 2006). Matumizi hayo yatawezekana tu iwapo lugha hiyo itatumika katika shughuli za kila siku ambazo hatimaye huiinua hadhi yake. Kutokana na kijisababu cha lugha za Kiafrika “kutokuwa za kisasa,” asilimia kubwa ya lugha hizo imetengwa zaidi isipokuwa Kiswahili. Vijisababu ambavyo hutolewa mara kwa mara ni kwamba lugha hizo zina upungufu wa msamiati

unaoweza kutumika katika maendeleo hasa ya kisasa. Utafiti huu ulilenga kubaini kama upungufu wa msamiati ni mojawapo ya changamoto zinazokumba Kibukusu kinapotumika katika redio za Sulwe na West FM.

Kwa mujibu wa Prah (2005), kiasili cha lugha za Kiafrika kukosa uwezo wa kisayansi na teknolojia ya kisasa ni wazo lililoanzishwa na Wakoloni kwa lengo la kuzidhalilisha. Kwa sasa, wazo hilo linaendelezwa na tabaka la wasomi wa Kiafrika hata baada ya mkoloni kuondoka. Swali tunalojiuliza hapa ni je, mawazo haya yameathiri vipi hadhi ya lugha za kiasili? Na je, Kibukusu kama mojawapo ya lugha za kiasili kina uwezo huo wa kisayansi na teknolojia unaozungumziwa pale kinapotumika katika redio za FM?

Naye msomi Ngugi (2014), akihimiza umuhimu wa kuthamini lugha za Kiafrika, anahoji kwamba fasihi ya Kiafrika kuandikwa kwa lugha za Ulaya tayari imestawi. Anauliza, mbona sasa tusianze kuzingatia lugha zetu za Kiafrika? Msomi huyu anazidi kusema kwamba badala ya kuwepo mijadala kuhusu Kiingereza, ambacho kinafanya vyema sana, wakati umefika tuekeze maarifa yetu, ubunifu, muda na pesa kwa lugha zetu. Utafiti huu ni mchango katika uekezaji huo katika lugha za Kiafrika. Kupitia kwa lugha za kiasili, wazungumzaji wanaweza kuelezea ubunifu wao ambao hatimaye unaweza ukaboresha hali zao za uchumi na maarifa.

2.1.7 Lugha za Kiasili kama Rasilimali

Nchi zilizostawi za mashariki ya Asia kama vile Japan, Hong Kong, Malasyia, Taiwan na Korea zimepata ustawi wa maendeleo ya kiviwanda na maendeleo ya kiuchumi kwa kutumia lugha zao za kiasili (Mudhune, 2002). Hiyo ndiyo sababu ya kuwepo majina ya vyombo vya matumizi kama vile Samsung, Sanyo, Fuji, Toyota, Mitsubishi na Nissan. Vyombo hivi vimepewa majina kwa lugha za kiasili za nchi

hizo na wala si lugha nyingine. Nchi hizo zimeweza kudhihirishia ulimwengu kwamba ustawi hauwezi ukafikiwa tu kwa kutumia lugha za kigeni kama vile Kiingereza. Maoni haya yanachochea swali hili, je, matumizi ya Kibukusu katika redio za FM yanaweza kuchangia ustawi wa maendeleo kwa wazungumzaji wake walioko katika kaunti ya Bungoma na hivyo basi kuwa rasilimali ama lazima wategemee lugha nyingine?

Kwa hivyo, iwapo nchi za mashariki ya Asia zimeweza kupiga hatua kimaendeleo bila kuhusisha lugha za kigeni, pana uwezekano wa nchi za Kiafrika vilevile kufuata mkondo huo kwa kuhusisha zaidi lugha zake katika shughuli nyingi. Anavyohoji Prah (2002), Afrika inahitaji lugha zake si tu kwa elimu ya msingi bali pia kwa maendeleo ya jumla ya jamii ya Afrika. Hata hivyo, changamoto za matumizi ya lugha hizi za kiasili ni madai ya kupotosha miongoni mwa baadhi ya watu wanaodai kwamba lugha hizo si za kisasa. Utafiti ulidhamiria kutathmini kama Kibukusu kilichangia maendeleo ya jamii ya wazungumzaji wake walioko katika kaunti ya Bungoma.

Naye Mwita (2002), anahoji kuwa maendeleo ya sehemu za mashambani yatatoa nafasi na uwezo wa kupata rasilimali kwa watu wa mashambani hivyo basi kuboresha uwezo wao kuzalisha mali. Anazidi kusema kwamba, hali hiyo itasababisha nafasi za kazi kwa watu wa mashambani. Anasisitiza kwamba, miongoni mwa sababu za kukosekana kwa maendeleo sehemu za mashambani ni ukosefu wa njia bora za mawasiliano. Wakenya wanaoishi mashambani wanahitaji habari kuhusu teknolojia mpya katika kilimo, elimu, afya na miundo msingi. Kwa jumla ufahamu unahitajika katika biashara ili wajue vitu vilivyoko sokoni, jinsi ya kuvitengeza na athari yake: hasi na chanya. Jambo hilo litakuwa muhali iwapo lugha zinazozungumzwa sehemu za mashambani (za kiasili) zitapuuzwa. Utafiti huu ulidhamiria kutathmini Kibukusu

kilivyotumika kuwapasha wazungumzaji wake habari kuhusu masuala ya jamii, afya, siasa na uchumi.

Kwa mujibu wa Mutahi (2002), uekezaji unaofanywa na familia pamoja na jamii utakuwa wa manufaa iwapo wataalamu wetu watawasiliana kikamilifu na wahudumiwa. Anaendelea kusema kwamba, iwapo watazua mijadala na kuwasiliana kikamilifu na wazalishaji pamoja na wafanyikazi, watatoa mazingira yanayofaa kuleta mabadiliko. Lakini iwapo wataalamu watahindwa kupitisha ujumbe wa maarifa, Kenya itazidi kukosa maendeleo. Anasema:

iwapo hatutaweza kupitisha maarifa kikamilifu, tutaendelea kujaribu kuwafanya watu waendeleo badala ya kuwawezesha wajiendeleze wenyewe (uk.12).

Maoni ya msomi huyu yanashadidia umuhimu wa kuwepo mawasiliano iwapo tunatarajia maendeleo. Mawasiliano haya lazima yawe katika lugha inayoeleweka. Vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili vitaweza kutoa mchango katika kutekeleza mawasiliano hasa kuhusiana na masuala yanayoathiri jamii husika. Utafiti huu ulichunguza Kibukusu kinavyochangia katika mawasiliano kamilifu kwa kupitisha maarifa yanayohitajika mashinani ukijikita katika masuala ya jamii, afya, siasa na uchumi.

Lugha yoyote inaweza kuendelezwa ili iweze kuhudumia mahitaji ya jamii lugha na hakuna lugha ambayo kwa undani haiwezi ikatumika katika mahitaji ya maendeleo ya jamii lugha katika elimu na teknolojia (Luoch na Ogutu, 2002). Kwa hivyo, madai ambayo yamekuwa yakishikiliwa na baadhi ya watu kwamba lugha za Kiafrika hususan za kiasili haziwezi kutumika katika maendeleo hayana mashiko. Utafiti huu ulilenga kutathmini kwa viwango vipi lugha za kiasili zinavyojitokeza kama rasilimali kwa wazungumzaji hasa kupitia redio za FM katika kaunti ya Bungoma.

Lugha za kiasili za Afrika zinaweza kutumika kushughulikia matatizo kadhaa kama vile elimu, ujinga, umaskini, janga la ukimwi, demokrasia na kadhalika (Ongarora, 2002). Lugha hizo zitafaa zaidi maeneo ya mashambani kwa vile zitawezesha wenyeji kuhusishwa zaidi katika kushughulikia masuala yanayowahusu. Uchunguzi huu ulilenga kutathmini jinsi Kibukusu kinavyotumika kuangazia masuala ya jamii, afya, siasa na uchumi kwa wakaazi wa kaunti ya Bungoma.

Kwa mujibu wa Okombo (2014), kupitia kwa lugha zetu huwa tunaweza kueleza tamaduni zetu, ufahamu wetu kuhusu mimea yote, mkusanyiko wa wanyama na mkusanyiko wa maarifa tuliyonayo. Kwa hivyo, ni bayana kwamba lugha tunayotumia katika mazingira yetu ni muhimu sana. Maswali tuliyojiuliza ni: Kibukusu kinapotumika hususan katika redio za FM, kina umuhimu gani? Je, wazungumzaji wake watakosa kupata ufahamu kuhusu mambo gani iwapo lugha nyingine itatumika? Majibu kwa maswali haya yalidhihirisha iwapo Kibukusu ni rasilimali kwa wazungumzaji wake hususan kinapotumika katika redio za FM.

Kulingana na Okombo (2014), ni lazima tuimarisha lugha za kiasili kwa Wakenya walioko mashinani ili kuwawezesha kuwa na maazimio yaliyo na ufahamu kuhusu masuala ya maendeleo. Anazidi kuhoji kwamba ugatuzi wa mamlaka ya serikali unafaa uende hadi mashinani ambapo wavua samaki na wakulima huketi chini ya miti na kujadili masuala ya maendeleo yanayowagusa moja kwa moja. Hili linajitokeza kupitia kwa kuwaelimisha watoto wao, kutafuta soko kwa samaki wao na mazao ya mashamba na uwakilishaji wao katika mabaraza ya machifu. Kutokana na maoni ya msomi huyu, ni bayana kwamba lugha hizi zinaweza kuwa rasilimali kwa jamii. Utafiti wetu ulilenga kuchunguza wasikilizaji wa redio za West na Sulwe FM wanavyoendeleza mijadala ya mambo yanayowahusu kwa kutumia Kibukusu.

Akisisitiza mchango wa lugha katika kupata maarifa, Michieka (2011:8) anadai:

Watu wengi watakubali kwamba uwezo wa kufahamu habari hutegemea kwa kiwango kikubwa lugha itakayotumika. Hata watu werevu sana watahasirika iwapo habari zitawasilishwa kwao kwa lugha wasiyoifahamu au ile wasio na umilisi nayo.

Michieka (2011) anazidi kusema kwamba, iwapo watu hawaelewi lugha ya siasa nchini mwao, hawawezi kushiriki kikamilifu katika siasa za kitaifa. Anadai, Kiingereza na Kiswahili kwa viwango fulani ni lugha za kigeni hususan kwa wale watokao mashambani. Kwa hivyo, pana haja ya matumizi ya lugha za kiasili ambazo si za kigeni ili kuwezesha watu hao washiriki katika masuala ya siasa. Utafiti huu ulichunguza Kibukusu kilivyoboresha ufahamu wa wakaazi wa Bungoma kilipotumika katika redio za Sulwe na West FM hususan katika masuala ya jamii, siasa, uchumi na afya.

Wakirejelea Kongamano la Muungano wa Afrika, Quane na Glanz (2010:6) wanasisitiza kuhusu umuhimu wa lugha za kiasili, kwa kudai:

Lugha za kiasili zinakamilishana na za kimataifa katika viwango tofauti na haziwezi kuepukwa kwa minajili ya mpangilio unaoridhisha na uliokamilifu, wa watu binafsi na jamii.

Hii inamaanisha kwamba lugha za kiasili zinaweza zikatumiwa kutekeleza majukumu ambayo hayawezi kamilishwa na lugha za kimataifa ndiposa lugha hizi kusemekana kukamilishana. Utafiti huu ulilenga kuchunguza masuala yanayoangaziwa kwa kutumia Kibukusu. Utafiti ulidhamiria kuchunguza baadhi ya masuala ambayo yasingewasilishwa kwa wasikilizaji laiti Kibukusu kisingetumiwa katika redio za FM, hivyo basi kukifanya rasilimali kwa jamii.

Quane na Glanz (2010) wanazidi kukariri kwamba Afrika inafaa ithamini kukuza lugha za Kiafrika ili ziwe njia za muhimu zaidi za mawasiliano na za kujitambulisha kwa Waafrika wengi. Kukuza na kuthamini lugha hizi za Kiafrika kumeendelezwa

nchini Kenya na redio za FM. Ingawa hali hiyo inajitokeza, utafiti huu ulilenga kutathmini lugha za kiasili ambazo ni za Kiafrika zinavyojitokeza kama rasilimali hususan kwa wenyeji wa kaunti ya Bungoma zinapotumika katika redio za FM.

Kulingana na ripoti ya MCK (2012), 36% ya habari za vituo vinavyotumia lugha za kiasili huwa za mashinani na kieneo, 31% zikiwa za kitaifa, 7% za Afrika huku 20% zikiwa za kimataifa. Kutokana na takwimu hizo, wazungumzaji wa lugha hizi za kiasili wanaweza kupata habari kuhusu viwango hivi vyote; habari za mashinani na kieneo zikichukua asilimia kubwa. Imedhihirika kwamba, vituo hivyo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili vina wasikilizaji wengi kwa vile huangazia habari na masuala ya jamii husika zaidi kuliko vituo vya taifa (MCK, 2012). Kwa kufanya hivyo, vituo hivi vinajitokeza kama rasilimali inayowawezesha wazungumzaji walio ughaibuni kuchangia katika masuala yanayoathiri jamii kupitia kwa mtandao. Utafiti huu ulilenga kuchunguza, ni kwa kiasi gani kiwango kikubwa cha habari za mashinani ziliwafaidi wasikilizaji wa vituo vya redio vilivyotumia lugha za kiasili.

Mwandishi maarufu wa fasihi, Ngugi wa Thiong'o akinukuliwa na Ochieng (2014) anahoji, ni kupitia tu kwa lugha ambayo ulikua ukiizungumza tangu utoto hadi uwe mtu mzima ndipo unapoweza kuielezea hali ya jamii yako, uwezo wao na malengo yao kwa njia sahihi. Ingawa msomi huyu alikuwa akichangia katika mjadala kuhusu ufundishaji wa lugha za kiasili, anasisitiza kuhusu umuhimu wa lugha za kiasili. Utafiti huu kinyume na suala alilokuwa akichangia Ochieng (2014) ulichunguza lugha za kiasili katika redio za FM na hususan zinavyojitokeza kama rasilimali kwa jamii husika.

Akimrejelea mwandishi Kithaka wa Mberia, Thatiah (2014) anadahili kuwa ujifunzaji wa lugha za kiasili husaidia watoto kujifunza mambo mengine. Watoto wanapokuwa

na msingi thabiti katika lugha za kiasili unaohusisha kuandika na kusoma, stadi hizi huweza vilevile kujitokeza katika Kiingereza. Kutokana na madai haya, ni bayana kwamba lugha za kiasili ni muhimu. Pana uhusiano mdogo kati ya maoni ya msomi Kithaka wa Mberia na msisitizo tunaowekea lugha za kiasili. Hata hivyo, utafiti huu ulilenga kuchunguza lugha za kiasili zinavyojitokeza kama rasilimali kwa jamii husika kupitia kwa redio za FM zinazotumia lahaja ya Kibukusu.

Naye Okoth (2015) anadahili, vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili licha ya kupata idadi kubwa ya wasikilizaji kila uchao, vilevile vinazidi kupanua mawanda yake hadi viwango vya kimataifa kupitia kwa mtandao. Iwapo lugha hizi zinawafikia hata wale walio ughaibuni, basi ni rasilimali kwa wazungumzaji. Utafiti huu ulidhamiria kutathmini urasilimali huu unavyojitokeza Kibukusu kinapotumika katika redio za West na Sulwe FM kuangazia masuala ya jamii, afya, siasa na uchumi.

2.2 Misingi ya Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili: Nadharia ya Uanzilishi wa Ajenda ya McCombs na Show (McCombs & Show, 1993) kuhakiki aina ya vipindi vinavyopeperushwa pamoja na ile ya Nadharia ya Uamilifu wa Lugha katika kuhakiki matini za vipindi vya redio vilivyoteuliwa.

Nadharia ya Uanzilishi wa Ajenda inahoji kwamba vyombo vya habari huandaa ajenda kwa maoni ya umma kwa kusisitiza mada fulani. Tangu kuasisiwa kwa nadharia hii (1972), imekua na kupitia ushawishi wa vyombo vya habari, kwa mtazamo wa umma, upande wa masuala muhimu kwa wagombezi wa kisiasa na sifa za mashirika. Nadharia hii ina mihimili minne:

- i) Ajenda ya vyombo vya habari, ambayo ni masuala yanayojadiliwa katika vyombo kama vile magazeti, runinga na redio.

- ii) Ajenda ya umma ambayo inajadiliwa kibinafsi na umma.
- iii) Ajenda ya sera ambayo ni masuala ambayo wapangaji sera huchukulia kuwa ya muhimu.
- iv) Ajenda ya mashirika ambayo ni masuala yanayothaminiwa na wafanyibiashara na mashirika kama ya muhimu.

Utafiti uliteua na kutumia mhimili wa (i) na (iii) pekee kutoka kwa Nadharia ya Uanzilishi wa Ajenda ya McCombs na Show. Mhimili wa (i) unaangazia jinsi vyombo vya habari huteua masuala ambayo vyombo hivyo huyaangazia. Hapa vyombo vya habari huteua mada na vipindi vya kupeperushwa. Kutokana na uteuzi huo, vyombo vya habari huipa uzito mada maalum na kuwafanya wasikilizaji wawe makini zaidi kuhusu mada hiyo. Uteuzi wa mada unaofanywa na vyombo vya habari huwafanya wasikilizaji wazungumzie na hata kuchangia huku wakipuuza mada zingine zilizopo.

Nao mhimili wa tatu unaohusu masuala yanayoteuliwa na wapangaji sera na kutiliwa uzito. Katika mhimili huu, kuwepo sera hudhibiti masuala ya kuangaziwa na vyombo vya habari. Katika mhimili huu, udhibiti wa aina ya matangazo ambayo hupeperushwa na vyombo vya habari unajitokeza. Kwa mfano, marufuku ya matangazo yanayoweza kuibua chuki miongoni mwa jamii yanazingatiwa.

Sera za serikali zinaweza zikaweka nyakati ambapo vipindi fulani vinaruhusiwa kupeperushwa. Kwa mfano, nyakati ambazo masuala kama vile ya mapenzi huruhusiwa kupeperushwa hewani. Hapa vyombo vya habari vinapaswa kuzingatia muda huo ambao umependekezwa kusudi matangazo hayo yasiwe na athari hasi kwa vijana wa umri mdogo. Vyombo hivyo vinapokwenda kinyume cha muda huo, basi pana uwezekano wa ama kutozwa faini au kutoruhusiwa kufanya biashara

(kufungwa). Kutokana na hali hiyo, panatokea udhibiti wa masuala ya kuangaziwa na vyombo vya habari. Kwa hivyo, hata vyombo vya habari vinapoangazia masuala ya mapenzi vinachunga visije vikayapeperusha nje ya saa zilizowekwa na sera za serikali. Swali ni, je, mikakati gani imewekwa kudhibiti matumizi mabaya ya lugha za kiasili kupitia redio za FM zinazotumia lugha za kiasili? Na je, mikakati hiyo imefaulu?

Hapa utafiti ulichunguza jinsi vipindi vinavyopeperushwa hewani vinavyoweza kuchangiwa na washikadau kama vile wapangaji sera mbalimbali, mathalan sera za lugha, kisiasa, kiuchumi na kadhalika. Kwa mfano, serikali inapolenga kuboresha viwango vya afya, vyombo vya habari vinaweza vikatumiwa kama njia ya kuifikia umma. Hapa baadhi ya maswali ambayo utafiti, utajibu kuhusiana na sera ni kama vile je, kuna sera yoyote katika serikali kuhusu matumizi ya lugha za kiasili kuwezesha masuala muhimu kuwafikia wasio na umilisi katika Kiingereza na Kiswahili? Na ni mikakati gani imewekwa kuweza kufikia lengo hilo; wasio na umilisi wa Kiingereza kuwezesha kupata habari za muhimu kupitia lugha za kiasili?

Utafiti ulitangulia kwa kutumia nadharia ya Uteuzi wa Ajenda kuteua vipindi vya kuangaziwa. Matumizi ya nadharia ya Uteuzi wa Ajenda yalisaidia katika uteuzi wa vipindi vya kuchanganuliwa. Ingawa wasikilizaji husikiliza vipindi husika, uteuzi wa vipindi vya kupeperushwa na mada huwa mikononi mwa waratibu wa vipindi katika vituo vya redio. Baada ya kuteua vipindi, utafiti ulitumia nadharia ya Sarufi Amilifu kuchanganua vipindi vilivyoteuliwa.

Nadharia ya Sarufi Amilifu huchanganua jinsi lugha inavyotumika kwa lengo la mawasiliano. Nadharia ya Sarufi Amilifu ya Halliday 1994 (Halliday na Matthiessen, 2004) inahoji kwamba, sarufi amilifu ni maelekezo ya mazingira kuhusu uchunguzi

wa lugha ambapo tunachunguza watu wanavyotumia lugha katika mawasiliano. Hulenga kuchunguza data kisarufi inayotokana na mtagusano kijamii (Dik, 1980, Halliday, 1994).

Haya maelekezo ya mazingira hutokana na hulenga hususan kuchunguza lugha katika muktadha halisi wa matumizi. Katika nadharia hii, kila elementi huelezwa kwa kurejelea dhima yake katika mfumo kamilifu wa kiisimu. Sarufi Amilifu hutazama lugha kama mfumo bayana ulio na maana na kategoria zingine za kisarufi na kisha hutekeleza wajibu wa ruwaza za semantiki. Kwa hivyo, Sarufi Amilifu huwasilishwa kama mfumo wa kisemantiki unaoambatana na maumbo ya kiisimu ambapo maana mbalimbali hufikiwa.

Sarufi Amilifu hujumuisha sarufi pamoja na mbinu za ufasiri wa maana kama njia ya kuelewa kinachoitwa na Halliday uamilifu halisi wa lugha. Uhalisi katika muktadha huu ni ufundi mzima wa matumizi ya lugha, yaani umilisi na utendaji katika lugha husika. Thamani ya uhalisi huu wa lugha ni uamilifu tendi wa lugha. Kwa mujibu wa Halliday, uamilifu tendi una mihimili mitatu:

- i) Mhimili unaotambua uhusiano kati ya wanajamii. Katika mhimili huu, huwa tunatumia lugha kuanzisha, kudhibiti na kuhifadhi uhusiano kati yetu na watu wengine. Hapa lugha huwa ni kitendo, huiga na kuonyesha uhusiano wa kibinafsi na wa kijamii.
- ii) Mhimili wa kiutambuzi ambapo lugha hutuwezesha kuelewa mazingira yetu. Mhimili huu hutuwezesha kupata maarifa, kuelewa ulimwengu unaotuzunguka kisha kuwasiliana kuhusu tajriba zetu kwa mambo mbalimbali. Hapa kipengele cha lugha kama mfumo hurejelea uwezo wa kuingiliana na mazingira halisi ambamo mazungumzo husika hutokea na mazingira ya jamii.

Hapa mazungumzo huwa na uwezo wa kuunda mazingira yake. Uwezo huu hutokana na mfumo wa lugha kukua na kuzalisha maana kutokana na mazingira yalivyo.

- iii) Mhimili wa ki-umatini ambao huipa uhai mihimili hiyo mingine miwili. Mhimili huu hutoa vifaa vya kupanga habari ili ziwe na muwala, uhusiano na ziwe za kuvutia. Vinginevyo, mhimili huu hupatia habari matini katika diskosi. Katika mhimili huu, namna ya kueleza maarifa na kuingiza mahusiano mbalimbali kijamii au kibinafsi hutegemea uwezo wa kujenga mfululizo na mfuatano fulani wa mazungumzo, kuhusisha mazungumzo moja na nyingine, kupanga na kuwa na mshikamano wa mwendelezo wa mazungumzo mbalimbali yanayohusiana.

Cha msingi katika mhimili wa (i) na wa (ii) ni kwamba katika matumizi ya lugha pana haja ya kuelewa mazingira na kutekeleza majukumu kwa watu wengine. Halliday (2004) anajumuisha mihimili hii yote mitatu na kueleza thamani ya uamilifu tendi wa lugha ambapo lazima sarufi iingiliane na hali tofauti za ulimwengu na mifanyiko ya kijamii wanamoshiriki watumizi wa lugha (Halliday na Matthiessen, 2004).

Utafiti huu ulitumia mihimili yote mitatu ya nadharia ya Sarufi Amilifu ya Halliday. Mhimili wa kwanza ulituwezesha kupima jinsi mahusiano mema yalidhibitiwa katika jamii kwa uhifadhi wa maadili. Mhimili wa pili ulitumika kutathmini maarifa yaliyopitishwa na Kibukusu kuhusu mambo mbalimbali mathalan elimu kuhusu magonjwa anuai. Nao mhimili wa tatu ambao ni wa ki-umatini uliwezesha kutathmini athari za habari zilizowasilishwa kutumia Kibukusu kwa wasikilizaji wa vituo vya redio vya Sulwe na West FM.

2.3 Hitimisho

Sura hii imehakiki yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti. Katika uhakiki huo, imeangalia matumizi ya lugha za kiasili kwa jumla, lugha za kiasili katika vyombo vya habari, hadhi ya lugha za kiasili na lugha za kiasili kama rasilimali. Aidha, imezungumzia sera ya lugha nchini Kenya, matumizi ya lugha za kiasili nchini Kenya na majukumu ya vyombo vya habari. Hatimaye sura imeangazia mwelekeo wa kinadharia. Sura imeelezea nadharia zote mbili ambazo zimeongoza utafiti huu. Sura inayofuata inazungumzia mbinu zilizotumika katika utafiti huu.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.0 Utangulizi


Sura iliyotangulia imejadili mapitio ya maandishi kuhusu mada ya utafiti na mielekeo ya kinadharia. Sura hii imezungumzia yafuatayo: eneo la utafiti, usampulishaji, ukusanyaji data na vifaa vya kukusanya data. Aidha, utafiti mwingi, unukuzi wa data iliyokusanywa na uwasilishaji na uchambuzi wa data zimeshughulikiwa. Hatimaye, imezungumzia itikeli ambapo masuala ya maadili katika utafiti yamezungumziwa. Aidha sura inaelezea mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu.

3.1 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika kaunti ya Bungoma. Bungoma inapatikana magharibi mwa Kenya karibu na mpaka wa nchi ya Uganda. Kaunti ya Bungoma inapakana na kaunti za Busia, Kakamenga na Trans Nzoia. Kaunti hii ina eneo la kilomita 3032.2 mraba. Viwango vyake vya joto ni kati ya sentigredi 15⁰-20⁰ kwa viwango vya chini hadi kati ya 22⁰-30⁰ kwa viwango vya juu. Kaunti hii ina misimu miwili ya mvua, iliyo na wastani ya mvua kati ya milimita 1200 hadi milimita 1800 kwa mwaka (First Bungoma County Integrated Development Plan 2013- 2017). Kaunti ya Bungoma ni kaunti kubwa ya tatu nchini Kenya, baada ya Nairobi na Kakamega kwa misingi ya wingi wa watu, ikiwa na watu 1,630,934 (Ndi, 2010).

Kaunti ya Bungoma ina kaunti ndogo tisa, ambazo ni: Kanduyi, Bumula, Kabuchai, Webuye Magharibi, Webuye Mashariki, Tongaren, Kimilili na Mlima Elgon (tazama ramani).

Ramani ya Kaunti Ndogo za Bungoma



Asili (First Bungoma County Integrated Development Plan 2013- 2017)

Kwa upande wa viwango vya umaskini, asilimia 53% ya wakaazi wake huishi katika viwango vya umaskini. Mali asili kuu ni kama vile Msitu wa Mlima Elgon, Mito ya Nzoia na Malakisi. Vivutio vya watalii katika kaunti ya Bungoma ni kama vile Hifadhi ya Wanyama ya Mlima Elgon, Hifadhi ya Msitu wa Mlima Elgon, Msitu wa

Chepkitale, maporomoko ya maji ya Nabuyole na Malakisi, Vilima ya Sang'alo, Musikoma na Kabuchai, Mapango ya Kitum, Mackingeny, Chepnyali na Kiptoro. Viwanda vinavyopatikana katika kaunti hii ni: Kampuni ya sukari ya Nzoia na kampuni za kusaga tumbaku ya BAT Mastermind inayopatikana Malakisi. Mazao yanayopatikana katika kaunti hii ni hususan sukari, kahawa, maziwa, mahindi, tumbaku, ndizi, viazi vitamu na viazi vya kizungu.

Kwa upande wa vituo vya redio vilivyoko katika jimbo ni: West FM, Redio Mambo, Nyota FM na BK Redio. Kati ya hivi vituo, West FM na Redio Mambo zimetenga asilimia ndogo ya saa zake za kutangazia kwa kutumia Kibukusu, ambacho ni kati ya lahaja zinazotumika katika kaunti hii. Lahaja zingine za Kiluyia katika kaunti hii ni Kitachoni na Kitura. Lugha zingine zinazozungumzwa katika kaunti ya Bungoma ni Kisabaoti na Kiteso. Mbali na vituo hivi vya redio, kuna vituo vingine vya redio ambavyo hutumia Kiluyia ambavyo ingawa havina makao katika kaunti ya Bungoma, husikika na wakaazi hao. Baadhi ya vituo hivyo ni Mulembe FM, Vuka FM na Sulwe FM.

Kwa mujibu wa MCK (2012), Sulwe FM ni kati ya vituo vya redio vya Royal Media Services (RMS) kinachopeperusha matangazo kwa Kibukusu. Habari za vituo vyote 12 vya Royal Media Services vinavyotumia lugha za kiasili huandaliwa mahali pamoja (meza moja). Hata hivyo kuna habari 2 au 3 za ziada za mashinani kwa kila mojawapo ya vituo hivyo 12 vinavyotumia lugha za kiasili (MCK, 2012).

Bungoma ilituliwa kama eneo la utafiti kwa vile ingeweza kufikiwa kwa urahisi. Kama anavyohoji Singleton (1993), uwezo wa kufikia kwa urahisi mahali pa kutafitiwa ni miongoni mwa mambo ya kuzingatiwa katika kuteua mahali pa kufanya utafiti. Kwa hivyo, kaunti ya Bungoma ilifaa sana kwa mtafiti. Vilevile, mtafiti aliliteua eneo hili kwa vile hakuna utafiti mwingine wa aina hii ambao umefanywa

katika kaunti hiyo hususan, utafiti kuhusu vituo vya redio vinavyotumia Kibukusu. Sababu nyingine ya uteuzi wa kaunti hii ni kwamba, vituo vyote viwili; Sulwe FM na West FM husikika katika kaunti ya Bungoma.

Pia mtafiti aliteua kaunti ya Bungoma kwa sababu inaendeleza kilimo kwa kiwango kikubwa kutokana na tabia ya nchi katika kaunti hiyo. Tabia ya nchi ya kaunti ya Bungoma ni nzuri kwa kilimo hivyo basi ni miongoni mwa sehemu ambazo huendeleza kilimo kwa kiwango kikubwa. Eneo hili hukuza vyakula kama vile mahindi, maharagwe na miwa kwa wingi. Lina viwanda viwili; Nzoia-cha kusaga sukari na kiwanda cha tumbaku cha Malakisi. Kiwanda kilichokuwa cha tatu cha Panpaper na kilichokuwa kikitengeneza karatasi kilifungwa kwa sababu ya kufilisika na madeni mengi. Ingawa kiwanda hicho kilifunguliwa upya mwaka jana, anayefanya biashara katika kiwanda hicho ni mwekezaji wa kibinafsi. Kutokana na kuwepo kwa viwanda na kuendelezwa kwa kilimo, shughuli ambazo huathiri masuala anayotafitia mtafiti; siasa, uchumi afya na jamii, palikuwa na uwezekano wa mtafiti kupata data aliyolenga kupata na kutoa maamuzi kuhusu lugha za kiasili kama rasilimali zinapotumika katika redio za FM.

Mbali na hayo, mtafiti aliteua kaunti ya Bungoma kwa vile wengi wa wenyeji huzungumza lahaja ya Kibukusu, anayozungumza mtafiti. Kwa hivyo, mtafiti hangehitaji mkalimani alipokuwa akichanganua data. Kwa mujibu wa Crowley (2007), ufanisi wa utafiti nyanjani mara nyingi hutegemea kwa kiwango kikubwa lugha wanayozungumza watafitiwa na mtafiti. Crowley (2007) anahoji kwamba, umilisi wa mtafiti katika lugha ya watafitiwa ni mojawapo ya vigezo vikubwa vya uteuzi wa eneo la utafiti. Kwa hivyo, mtafiti aliteua eneo ambalo wengi wa wakaazi wake huzungumza Kibukusu; lugha anayoimudu mtafiti.

Eneo hili la utafiti vilevile lilitolewa kwa vile, ingawa wengi wa wakaazi wanazungumza Kibukusu, wazungumzaji wa lahaja zingine za Kiluyia kama vile: Kitachoni, Kimaragoli, Kiwanga, Kimarama na Kinyore vilevile wamehamia hapo na kununua mashamba hasa sehemu ambazo awali zilimilikiwa na walowezi. Hata hivyo, mtafiti alijifunga katika lahaja ya Kibukusu. Kutokana na kuwepo kwa wazungumzaji wa lahaja nyingi za Kiluyia, niliweza kupata data inayohusisha maoni ya jamii pana; hivyo basi kuifanya ya kutegemewa. Vilevile, nililiteua eneo hili kwa vile ni kati ya maeneo yaliyo na rutuba nzuri magharibi mwa Kenya.

Kaunti ya Bungoma ni ya tatu kati ya kaunti 47 nchini Kenya kwa kurejelea idadi ya wakaazi (KNBS, 2013). Kaunti hii inafuatia kaunti za Nairobi na Kakamega kwa wingi wa idadi ya watu (KNBS, 2013). Walengwa wa utafiti huu walikuwa wakaazi wa kaunti ya Bungoma, wanaosikiliza vituo vya Sulwe FM na West FM na kuelewa lahaja ya Kibukusu inayotumika katika matangazo.

3.2 Usampulishaji

Usampulishaji ni mbinu ambayo mtafiti hutumia kukusanya watu, mahali au vitu vya kutafitiwa. Ni mbinu ya uteuzi wa idadi ya watu au vifaa kutoka kwa idadi jumla ya watafitiwa hivi kwamba kikundi kilichoteuliwa kiwe na elementi zinazowakilisha sifa zinazopatikana katika kikundi kizima (Tromp & Kombo, 2006).

Kwa mujibu wa Sankoff (2001), sampuli ya wahusika katika isimu jamii huwa kati ya watu 20 na 120, na inapoteuliwa kwa umakini, huwa na uwakilishaji tosha wa mienendo ya jamii lugha. Kwa kuongozwa na ushauri wa Sankoff (2001), utafiti huu uliteua wahusika 156. Jambo kuu lililoongoza uteuzi wa sampuli lilikuwa ni kuteua kikundi ambacho kingeweza kupatikana kwa habari za kina kwa muda mfupi.

Utafiti uliteua kikundi kilichotoa habari zilizohitajika bila kutumia gharama kubwa ya usafiri.

Usampulishaji kimakusudi ulitumika katika uteuzi wa waliohusika kutoka vikundi vifuatavyo: vituo vya redio, vipindi vilivyopeperushwa, wahariri, watangazaji na magalacha. Usampulishaji kimakusudi hutumika hususan kutokana na mahitaji ya utafiti husika (Morse, 1994). Hapa watafiti huteua wahusika ambao hutoa habari zinazohitajika kwa utafiti unaofanywa kwa kina (Patton, 1990). Wahusika waliteuliwa kimakusudi kwa sababu za upekee wa ujuzi wao katika taaluma zao.

Katika usampulishaji kimakusudi, mtafiti huteua sampuli kwa kutilia maanani zaidi sababu kuu za uteuzi wa sampuli (Kothari, 2004). Hapa mtafiti huteua sampuli itakayomsaidia kupata matokeo aliyolenga. Katika utafiti huu lengo lilikuwa, kubainisha Kibukusu kinavyojitokeza kama rasilimali kinapotumika katika redio za FM. Usampuli humhitaji mtafiti asiwe na mapendeleo ndipo matokeo yake yawe ya kutegemewa (Kothari, 2004).

Usampulishaji wa kwanza ulifanyiwa vituo vya redio. Vituo vya redio vya Sulwe na West FM viliteuliwa kimakusudi kutokana na matumizi ya mojawapo ya lugha za kiasili za wenyeji wa kaunti ya Bungoma (Kibukusu). Uteuzi wa vituo hivyo viwili ulitokana na vituo hivyo kuwepo kwa zaidi ya miaka mitano vikipeperusha matangazo kwa kutumia Kibukusu. Vituo hivyo vilevile viliteuliwa kwa sababu vinatumia lahaja anayozungumza mtafiti (Kibukusu), kwa hivyo hali hiyo ilipunguza dhiki za kumtafuta mkalimani.

Baada ya kuteua vituo vya redio, vipindi vinavyowasilishwa kwa Kibukusu viliteuliwa. Palikuwa na haja ya kuteua tu vipindi vinavyowasilishwa kwa Kibukusu kwa vile katika West FM, vipindi vingi viliwasilishwa kwa Kiswahili huku Kibukusu

kikitumika kwa saa chache tu. Vipindi viliteuliwa kimakusudi na vilikuwa vile vilivyoangazia masuala ya jamii, uchumi, siasa na afya.

Usampulishaji kiazma vilevile ulitumika kuwateua wahariri wa vituo hivyo. Mhariri mmoja kutoka kila kituo (Sulwe na West FM) aliteuliwa. Wahariri waliohusishwa walikuwa hasa wale waliohusika na vipindi vinavyohusiana na masuala ya jamii, uchumi, afya na siasa lakini kwa Kibukusu. Utafiti haukutumia wahariri wa vipindi vya Kiswahili katika West FM ambayo vilevile hutumia Kiswahili. Utafiti ulitumia tu wale ambao hutumia Kibukusu. Wahariri walitoa data ya yaliyomo katika vipindi wanavyotayarisha. Wahariri hao waliwezesha kubaini matini ya vipindi vya masuala ya jamii, afya, uchumi na siasa. Vilevile, walitoa habari kuhusu Kibukusu kinavyojitokeza kama rasilimali kwa wazungumzaji wake, changamoto za matumizi ya Kibukusu kama rasilimali na kupendekeza suluhu kwa changamoto hizo.

Watangazaji vilevile waliteuliwa kimakusudi. Maadamu hawa ndio wanaotumika kuwasilisha vipindi, watangazaji wawili kutoka kila kituo cha redio (Sulwe na West FM) waliteuliwa. Wahusika hawa walihusishwa kwani, wao ndio huingiliana na wasikilizaji wakati wa kupeperusha vipindi vya Kibukusu hewani. Watangazaji wa vipindi walitoa habari muhimu kuhusu vipindi vinavyowasilishwa na vituo vyao vya redio. Watangazaji hawa vilevile walitoa habari kuhusu lugha za kiasili, zilivyojitokeza kama rasilimali, kwa kuzingatia yaliyomo katika vipindi walivyowasilisha. Baadhi ya habari walizotoa ni: kufahamisha kuhusu masuala yanayoangaziwa na redio zao za FM kwa kutumia Kibukusu, urasilimali wa Kibukusu kwa watumiaji na changamoto za matumizi ya Kibukusu kama rasilimali. Hatimaye, watangazaji hao walipendekeza suluhu kwa changamoto hizo katika utekelezaji wa majukumu yao.

Magalacha pia waliteuliwa kimakusudi. Utafiti uliwateua wataalamu waliotumika katika uwasilishaji wa vipindi vinavyoangazia masuala hayo ya jamii, uchumi, afya na siasa kwa Kibukusu. Mtaalamu mmoja aliteuliwa kutoka kwa kila mojawapo ya vipindi vya jamii, uchumi, afya na siasa. Wataalamu hawa waliweza kufikiwa kwa kutumia watangazaji wa vipindi husika. Mtaalamu mmoja kwa kila kipindi aliteuliwa. Wataalamu hao walitoa habari zifuatazo: lugha ambazo wao hutumia katika vipindi ambavyo wao hushiriki katika redio za FM, yaliyomo katika vipindi hivyo na changamoto ambazo wao hukumbana nazo wanapotumia Kibukusu kuangazia masuala ya kitaaluma. Magalacha hawa waliweza kutoa mapendekezo ya kutatua changamoto hizo, kisha maoni yao kuhusu uwezo wa lugha za kiasili kama rasilimali huku wakitoa sababu.

Aidha, mbinu ya uteuzi nasibu ilitumika kuteua kaunti ndogo sita zilizohusishwa katika utafiti. Uteuzi nasibu vilevile ulitumika kuwateua wasikilizaji wa vituo hivi, wanaoishi katika kaunti ya Bungoma na ambao husikiliza vituo vya Sulwe na West FM. Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006), uteuzi nasibu ni mbinu ya kuteua watu, maeneo na vitu bila utaratibu maalum. Kila kipengee katika mkusanyiko husika huwa na nafasi sawa ya kuteuliwa (Kothari 2004). Mbinu ya uteuzi nasibu hutoa nafasi sawa kwa sampuli husika kuhusishwa katika utafiti husika.

Uteuzi nasibu uliotumika ulikuwa ule ulio sahili. Katika mbinu hii, kila kipengee kina nafasi sawa ya kuteuliwa kutoka kwa sampuli. Huipa kila elementi katika idadi husika nafasi sawa ya kuwezekana kuhusishwa katika sampuli na kila uteuzi ni huru (Kothari, 2004). Usampulishaji wa wasikilizaji uliotumika ni ule ambao uliwezesha idadi ya watafitiwa kuongezeka kadiri utafiti ulivyoendelea. Usampulishaji huu ulitumika kuwafikia wasikilizaji wa vipindi katika redio zote mbili (Sulwe na West

FM). Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (2003), huu ni usamplishaji ambao watafitiwa wachache huwataja wengine ambao wanajua wana sifa zinazohitajika kwa mtafiti.

Kwa usaidizi wa wanahabari wa Sulwe na West FM, orodha ya majina ya wasikilizaji ambao hasa hupiga simu kwa vituo hivyo viwili vya redio (Sulwe na West FM) kutoa michango yao iliandaliwa. Baadhi ya wasikilizaji hao walitumika kupata orodha zaidi ya wasikilizaji. Hatimaye orodha hiyo ndefu ilitumika kuteua sampuli iliyotumika kinasibu. Kutokana na sampuli jumla hiyo ya wasikilizaji, wasikilizaji 140 waliteuliwa kwa jumla. Wasikilizaji 70 kutoka kwa kila mojawapo ya vituo hivyo vya redio ndio waliohusishwa katika utafiti. Katika kaunti ndogo tano: Bumula, Kabuchai, Webuye Magharibi, Tongaren na Kimilili, wasikilizaji 13 waliteuliwa. Katika kaunti ndogo ya Mlima Elgon, kuliteuliwa wasikilizaji watano kutoka kila kituo cha redio (Sulwe na West FM).

Wasikilizaji wachache waliteuliwa kutoka kaunti ndogo ya Mlima Elgon kwa vile wengi wa wakaazi wake ni Wasabaoti ilhali utafiti ulitafitia Kibukusu. Kwa hivyo, palikuwa na uwezekano wa kuwepo wasikilizaji wachache wanaosikiliza vituo vya redio vinavyotumia Kibukusu ikilinganishwa na kaunti ndogo zingine ambako Kibukusu hutumika. Hao wasikilizaji wachache waliopatikana katika kaunti ndogo ya Mlima Elgon walikuwa ni Wabukusu ama waliohamia huko, wanaofanya kazi huko, wanaofanya biashara au walioingiliana na Wasabaoti kupitia kwa ndoa baina ya jamii za Wabukusu na Wasabaoti.

Mtafiti aliomba nambari za simu za wasikilizaji hao, ambazo wao hutumia katika mtindo wa utangazaji unaowashirikisha wasikilizaji kupitia upigaji simu (Gathigi, 2009, Ogechi na Bosire, 2010). Mtafiti aliwateua kwa kuelekezwa na watangazaji.

Aliomba nambari za simu za wasikilizaji ambao husikiliza vituo hivyo kutoka kwa watangazaji wa vituo vyote viwili vya redio. Watangazaji waliombwa kumwelekeza mtafiti kwa wasikilizaji kwa kutoa nambari za simu za wasikilizaji.

Kwa kuzingatia ushauri wa watangazaji, mtafiti alipewa nambari za simu za viongozi wa vikundi vya wasikilizaji baada ya kubainika kwamba walikuwa na vikundi vya wasikilizaji. Ni viongozi hawa ambao walimsaidia mtafiti kuwapata wasikilizaji wengine. Miadi ya jinsi ya kukutana ilitolewa baina ya mtafiti na wasikilizaji hao kwa kusudi la kuwahoji. Wasikilizaji hawa walikuwa na vikundi mbalimbali vili vyoletwa pamoja na usikilizaji wa vipindi katika vituo hivi vya redio.

Wasikilizaji walitoa data inayohusiana na aina ya vipindi vya jamii, uchumi, afya na siasa ambavyo wao husikiliza. Walitoa habari kuhusu aina ya masuala ambayo huangaziwa na vipindi hivyo. Walitoa habari kuhusu manufaa waliyopata kwa kuvisikiliza vipindi vinavyowasilishwa kwa Kibukusu na kuwezesha kufikia maamuzi kuhusu lugha za kiasili kama rasilimali kwa wazungumzaji. Aidha, walitoa habari kuhusu changamoto zinazokumba matumizi ya Kibukusu katika kuangazia masuala ya jamii, uchumi, afya na siasa. Hatimaye, walipendekeza njia mbalimbali zinazoweza kutumika kutatua changamoto hizo.

3.3 Ukusanyaji wa Data

Ukusanyaji wa data unarejelea kukusanya habari mahususi zinazolenga ama kuthibitisha au kupinga ukweli fulani (Kombo na Tromp, 2006). Mbinu zinazotumika kukusanya data huathiriwa na vifaa vya ukusanyaji data (Kombo na Tromp, 2006). Njia mbalimbali zilitumika katika utafiti huu kukusanya data kutokana na vifaa vilivyoteuliwa. Mbinu zilizotumika ni: usikilizaji wa vipindi, usaili, ujazaji hojaji na kurekodi vipindi.

3.3.1 Usikilizaji Vipindi

Vipindi teule vilisikizwa na mtafiti. Uchunguzi usio shirikishi ulitumika kusikiliza vipindi vinavyowasilishwa na vituo vya redio vya Sulwe na West FM. Vipindi vinavyohusu masuala ya jamii, uchumi, afya na siasa vinavyoandaliwa na vituo hivyo vya redio kwa Kibukusu vilisikilizwa. Usikilizaji ulikuwa wa vipindi vinavyopeperushwa kwa lahaja ya Kibukusu. Usikilizaji wa vipindi ulimwezesha mtafiti kuyakinisha yaliyomo katika vipindi hivyo. Usikilizaji huu vilevile uliwezesha kuyakinishwa kwa baadhi ya changamoto zinazowakumba magalacha na watangazaji katika uwasilishaji wa vipindi kwa kutumia Kibukusu. Aidha, usikilizaji uliwezesha kuyakinishwa kwa baadhi ya habari zilizotolewa na wahariri wa vipindi pamoja na watangazaji. Baadhi ya habari hizi ni kama vile: nyakati za vipindi kuwasilishwa, faida za vipindi na yale waliyowasilisha wasikilizaji kupitia kwa upigaji simu.

Vipindi vya burudani havikushughulikiwa kwa vile, havikuwa katika upeo wa utafiti huu. Vipindi husika viliteuliwa kwa majuma manne. Muda huo ulitosha kunasa angalau vipindi vinne kutoka kila mojawapo ya vitengo vilivyotafitiwa ambavyo ni: jamii, afya, uchumi na siasa. Hatimaye, vipindi vitatu viliteuliwa kutoka kila mojawapo ya vipindi vinavyoangazia masuala ya jamii, afya, uchumi na siasa kisha vikachanganuliwa.

3.3.2 Usaili

Huu ni utolewaji wa hojaji isiyoandikwa au kupata habari kupitia mwongozo wa mahojiano (Mugenda & Mugenda, 2003). Mtafiti humhoji mhojiwa ana kwa ana. Ili kupata habari sahihi, mtafiti huhitaji kupata ushirika kutoka kwa wasailiwa. Ni njia bora ya kupata habari za kina ambazo mtafiti anaweza kutumia (Mugenda na Mugenda, 2003).

Anavyodai Gina (2001), mbinu hii huwezesha kupatikana kwa habari za kina. Vilevile, iliwezesha kupata habari za ziada kuongeza kwa habari zilizokuwa zimepatikana kupitia kwa mbinu zingine zilizotumika kama vile hojaji na usikilizaji wa vipindi kwa redio.

Mbinu hii ilifaa, kwani maswali ambayo hayakuwa yamejibiwa kwa utoshelevu katika hojaji yalifafanuliwa barabara wakati wa kuyajibu katika usaili (Fraenkel na Wallen, 1993). Mbinu hii vilevile iliwezesha kueleweka bayana kwa baadhi ya majibu ya hojaji. Aidha, wakati wa usaili, baadhi ya mambo yaliyoibuka kutoka kwa wadadisiwa yalitambuliwa na kusaidia kufikia maamuzi kuhusu lugha za kiasili kama rasilimali kwa wazungumzaji wake, hususan zinapotumika katika redio za FM.

Vikundi vya watafitiwa vilivyohusishwa ni: wahariri, watangazaji na magalacha. Mhariri mmoja kutoka kila kituo cha redio alisailiwa. Miadi ya kufanya usaili iliwekwa baina ya mtafiti na wahariri hao. Mtafiti alifika katika vituo hivyo siku ambazo walikuwa wamekubaliana katika miadi na kuwasaili wahariri hao. Vivyo hivyo, mtafiti aliweka miadi ya siku za kuwasaili watangazaji na magalacha. Vikundi hivi vyote vilihusisha tu watangazaji na magalacha waliohusika tu na vipindi vya: jamii, uchumi, siasa na afya.

3.3.3 Ujazaji Hojaji

Ujazaji hojaji ulifanywa na watangazaji na wasikilizaji wa vituo vyote viwili vya redio vya Sulwe na West FM. Hojaji hizi ziliwasilishwa moja kwa moja kwa wasailiwa. Lengo la kufanya hivyo lilikuwa, kuhakikisha kwamba hojaji zimewafikia walengwa. Kifaa hiki kilifaa kwa vile kilipunguza muda wa kukusanya data iliyohitajika (Ary na wenzake, 1972). Maagizo sawa yaliyopelekewa wasailiwa wote yaliwezesha kulinganisha na kulinganua majibu ya wasailiwa na kuwepo kwa mtafiti

hakukuingilia majibu yao. Hojaji hizi zilikuwa zimeandaliwa kwa lugha ya Kiswahili. Watangazaji wawili kutoka kila kituo cha redio ambao hutangaza kwa Kibukusu walijaza hojaji. Mtafiti mwenyewe alipeleka hojaji hizo kwa vituo hivyo vya redio.

Ujazaji hojaji vilevile ulitekelezwa na wasikilizaji wa vituo hivyo viwili vya redio. Kwa kusaidiwa na viongozi wa vikundi vya salamu vya vituo hivyo vya redio, mtafiti aliwapa wasikilizaji walioteuliwa kinasibu kujaza hojaji hizo. Aliwapa hojaji baada ya kuwaelezea lengo la utafiti na kuwahakikishia kwamba habari ambazo wangetoa zingehifadhiwa kwa siri wakati na baada ya utafiti. Ingawa taarifa kuhusu lengo la utafiti na hakikisho la uwekaji wa siri zilikuwa katika utangulizi wa hojaji zote, mtafiti alichukua jukumu la kuwafahamisha hayo kupitia kwa mazungumzo. Mtafiti alifanya hivyo kwa lengo la kujenga mlahaka mzuri baina yake na watafitiwa. Mlahaka huo ulisaidia kuwashawishi wahojiwa wasikatae kujaza hizo hojaji. Anavyohoji Peil (1995), hojaji zinapotolewa na mtafiti kwa watafitiwa moja kwa moja, watafitiwa huweza kuhimizwa kushiriki katika utafiti.

Baada ya hojaji kutolewa kwa watafitiwa, miadi iliwekwa kati ya mtafiti na watafitiwa juu ya siku ya kuchukua hojaji hizo. Wahojiwa walipewa juma moja ili kujaza hojaji. Baada ya hilo juma kukamilika, mtafiti alikwenda na kuchukua hizo hojaji. Wakati wa kuzichukua hojaji, mtafiti alizipitia kuhakikisha kwamba zilikuwa zimejazwa zikakamilika. Mtafiti mwenyewe alizichukua hojaji hizo kutoka kwa watafitiwa. Kuzichukua mwenyewe kutoka kwa watafitiwa kulikuwa na manufaa kwa vile anavyosema Peil (1995), mtafiti mwenyewe anapochukua hojaji kutoka kwa watafitiwa, huweza kuwaomba wale ambao hawajazikamilisha inavyostahiki wazikamilishe.

3.3.4 Kurekodi Vipindi

Ni mbinu muhimu kwani mazungumzo yaliyorekodiwa huweza kucheza, kusikizwa upya na kuchunguzwa kwa makini zaidi ikilinganishwa na uandishi wa mazungumzo husika (Mugenda na Mugenda, 2003). Kinasa sauti kilitumika kurekodi vipindi vilivyowasilishwa na vituo hivyo viwili vya redio (Sulwe na West FM), kisha baadaye matini yake ilichanganuliwa kwa kuongozwa na nadharia ya Sarufi Amilifu. Vipindi teule vya Kibukusu vilivyoangazia masuala ya jamii, afya, uchumi na siasa ndivyo vilirekodiwa.

Vipindi hivi vilirekodiwa kwa muda wa majuma manne kwa kila kituo cha redio. Katika redio ya Sulwe, vipindi hivyo vilisikizwa kati ya saa kumi na mbili za asubuhi na saa sita za usiku. Katika redio ya West FM, vipindi vilisikilizwa siku za Jumamosi na Jumapili tu kati ya saa nane na saa kumi za mchana. Ni vipindi vilivyohusu masuala ya jamii, uchumi, siasa na afya vilivyosikilizwa.

3.4 Vifaa vya Kukusanyia Data

Vifaa anuwai vilitumika kukusanya data. Vifaa vifuatavyo vilitumika ili data iliyohitajika ipatikane: hojaji, mwongozo wa usaili na tepurekoda.

3.4.1 Hojaji

Data ilikusanywa kwa kutumia seti mbili za hojaji: hojaji kwa wanahabari na hojaji kwa wasikilizaji (tazama viambatisho I na II). Hojaji za wanahabari ziligawika katika sehemu tano: sehemu ya kwanza ilitafuta habari kuhusu vituo vya redio na lugha za matumizi. Sehemu ya pili ililenga kupata habari kuhusu vipindi vilivyowasilishwa kwa lugha za kiasili. Miongoni mwa habari zilizolengwa kupatikana ni masuala yaliyoangaziwa katika vipindi, vikundi vya wasikilizaji vilivyolengwa na muda uliotengewa vipindi.

Sehemu ya tatu ililenga kupata habari kuhusu lugha za kiasili zinavyojitokeza kama rasilimali kwa wasikilizaji. Sehemu ya nne ya hojaji hiyo ilitoa habari kuhusu uimarishaji wa lugha za kiasili kupitia kwa redio za FM. Sehemu ya mwisho ililenga kupata habari kuhusu changamoto za matumizi ya lugha za kiasili wakati wa kuangazia masuala ya jamii, afya, uchumi na siasa kwa wakaazi wa kaunti ya Bungoma. Hatimaye, sehemu hiyo ililenga kupata mapendekezo kuhusu utatuzi wa changamoto zilizokumba matumizi ya lugha za kiasili katika vituo vya redio vya FM.

Hojaji za wasikilizaji zilizotumika ziligawika katika sehemu nne: sehemu ya kwanza ilikuwa na maswali yaliyolenga habari za kimsingi kama vile kiwango cha elimu, jinsia na umri wa mhojiwa. Sehemu ya pili ilikuwa na vipengele vya maswali yaliyolenga kupata habari kuhusu lugha anazozungumza mhojiwa, kazi anazofanya, usikilizaji wake wa redio, vituo vya redio wanavyosikiliza na vipindi wanavyosikiliza.

Sehemu ya tatu ilikuwa na maswali yaliyolenga kupata habari kuhusu manufaa waliyopata kutokana na usikilizaji wa vipindi vinavyowasilishwa kwa lugha za kiasili. Hatimaye, sehemu ya mwisho ilihusisha maswali yaliyolenga kupata habari kuhusu changamoto zinazokikumba kituo cha redio wakati wa uwasilishwaji wa vipindi vya kitaaluma kwa kutumia lugha za kiasili. Aidha ilihusisha mapendekezo ya msikilizaji kuhusiana na changamoto za lugha zinazojitokeza katika vipindi ambavyo yeye husikiliza lugha za kiasili zinapotumika na mapendekezo ya jinsi ya kuyatatua matatizo hayo.

Katika maandalizi ya hojaji maswali funge na huru yalitumika. Maswali huru yalikuwa ni ya kufafanua zaidi majibu yaliyokuwa yametolewa katika maswali funge. Miadi ya kuwapa wahusika hojaji iliwekwa. Hilo lilifanyika baada ya idhini kutolewa na wasimamizi wa vituo hivyo vya redio na kamishna wa kaunti ya Bungoma kwa

upande wa wakaazi. Baada ya kuwapa hojaji, miadi iliwekwa kuhusu siku za kuzichukua hojaji hizo kutoka kwao.

Hojaji zilifaa kwa vile gharama yake ni ya chini na hazina athari ya mwenye kuhoji kwa mhojiwa (Peil, 1995). Aidha, hutoa muda wa kutosha kutoa majibu yaliyofikiriwa (Kothari, 1993). Kwa hivyo mtafiti aliteua kifaa hiki kukusanyia data kwa vile hakikuhitaji pesa nyingi katika matumizi yake na vilevile kiliwapa watafitiwa muda wa kutosha kutoa majibu.

3.4.2 Mwongozo wa Usaili

Mwongozo wa usaili ulilenga kupata habari sawa na zile zilizokuwa katika hojaji. Hata hivyo, ulilenga kupata ufafanuzi wa ziada. Mwongozo huu vilevile ulilenga kupata habari kutoka kwa wahariri wa vipindi katika vituo hivyo vya redio pamoja na magalacha walioalikwa kuangazia masuala mbalimbali. Seti tatu za maswali ya usaili ziliandaliwa: usaili kwa wahariri, watangazaji na maghalacha wa vituo hivyo vya redio (tazama viambatisho III, IV na V).

Maswali ya usaili kwa wahariri yalilenga kupata habari zifuatazo: masuala ambayo huangaziwa katika vipindi vya jamii, afya, uchumi na siasa. Aidha, yalilenga kuangazia mikakati iliyowekwa na vituo hivyo kuhakikisha kwamba wasikilizaji wanafaidika kutokana na vipindi hivyo na urasilimali wa lugha za kiasili pale zinapotumika katika redio za kiasili kwa jamii husika. Vilevile, mwelekeo wa matumizi ya lugha za kiasili katika kaunti ya Bungoma, changamoto wanazokumbana nazo na mapendekezo ya jinsi ya kutatua changamoto hizo ziliangaziwa.

Mwongozo wa usaili kwa watangazaji ulilenga kupata habari zifuatazo: mbinu wanayotumia kuwezesha jamii inayosikiza vituo vyao kuielewa jamii yao na mazingira yao kwa upana na undani, jinsi vituo vyao vinavyohakikisha kwamba kuna

kushiriki katika maamuzi na majadiliano kuhusu masuala tofauti yanayoathiri maisha ya wasikilizaji kwa kutumia Kibukusu na urasilimali wa Kibukusu kwa wazungumzaji kinapotumika katika redio za FM. Hatimaye changamoto ambazo hukumba matumizi ya Kibukusu katika redio zao na suluhisho kwa changamoto hizo.

Nao mwongozo wa usaili kwa magalacha ulisaidia kupata habari zifuatazo: taaluma za maghalacha hao, lugha ambayo wanataaluma hao walitumia katika uwasilishaji vipindi vya redio na sababu za matumizi ya hiyo lugha. Hatimaye, changamoto wanazokumbana nazo pale wanapotumia Kibukusu kuangazia masuala ya taaluma zao kisha mapendekezo yao kuhusu jinsi ya kutatua changamoto hizo zilizojitokeza.

3.5 Utafiti Mwigo

Utafiti mwigo ulifanywa katika kituo cha Redio Mambo kinachopatikana mjini Webuye. Sababu ya kukiteua kituo cha Redio Mambo kwa utafiti mwigo ni kupatikana kwake katika kaunti ya utafiti (Bungoma), hivyo basi huangazia masuala mengi ya wakaazi licha ya masuala ya kitaifa. Vile vile, kiliteuliwa kwa vile kama West FM, hutumia lugha za Kiswahili na Kibukusu katika uwasilishaji wa vipindi vyake. Kwa hivyo, kilifaa zaidi kuwezesha kupima mbinu za utafiti, watafitiwa na vifaa vya utafiti.

Utafiti ulifanywa katika kituo cha redio cha Redio Mambo kupima maswali yaliyotungwa na mtafiti. Wanahabari na wasikilizaji walitumika kupima vifaa vya utafiti. Upimaji huo ulifanywa ili kuhakikisha kwamba data ambayo ingekusanywa ingekuwa ya manufaa kwa utafiti na ya kutegemewa. Utegemezi wa data uliweza kuhakikishwa kwa kuwapa wasikilizaji hojaji zilezile na kuchunguza walivyojibu maswali.

Utafiti mwigo ulimsaidia mtafiti kukisia changamoto za utafiti na kugundua zaidi mianya iliyofaa kuzuiwa. Vilevile, utafiti awali ulisaidia kutupilia mbali data ambayo haingeusaidia utafiti huu (Denzin & Lincoln, 2005). Aidha, utafiti mwigo uliwezesha kutafuta njia za kuondoa vizuizi vya utafiti kama vile ukosefu wa uaminifu miongoni mwa watafitiwa (Denzin & Lincoln, 2005). Utafiti mwigo ulifanywa kwa lengo la kupima vifaa vya utafiti kisha virekebishwa.

Kutokana na utafiti mwigo, mbinu zilizolengwa kutumika katika utafiti huu zilipimwa. Kwa mfano, uwazi wa maswali na mtiririko wake vilitathminiwa. Maswali ambayo yalionekana kutowezesha kupata data iliyonuiwa yalirekebishwa huku mengine yakibadilishwa kabisa ili kupata data iliyolengwa kupatikana. Vilevile, baadhi ya vipindi vinavyogusia masuala ya afya, uchumi na siasa vilisikilizwa kwa lengo la kurekebisha vifaa vilivyoandaliwa kukusanya data. Hilo lilifanywa kusudi data aliyolenga kupata mtafiti ipatikane. Data lengwa kupitia usikilizaji na kurekodi vipindi ilikuwa ni matini ya vipindi vya jamii, afya, uchumi na siasa.

Muda wa kufanyia utafiti vilevile ulipimwa kwa lengo la kujua iwapo ungetosha kukusanyia data ambayo mtafiti alilenga kupata. Utafiti mwigo uliwezesha kugunduliwa kwamba, muda ulionuiwa kutumika kukusanya data (mwezi mmoja) ulikuwa mfupi. Kwa hivyo, muda huo ulirefushwa baada ya matokeo ya utafiti mwigo. Muda huo ulirefushwa kutoka kwa mwezi mmoja hadi miezi miwili.

Utafiti mwigo vilevile ulisaidia kutambua vitengo muhimu vya watafitiwa vilivyofaa kushirikishwa katika utafiti na vifaa vya kutumika kwa kila mojawapo ya vikundi hivyo. Kwa mfano, baada ya utafiti mwigo, hojaji tulizolenga kutumiwa kwa maghalacha na wahariri zilitupiliwa mbali. Badala ya kutumia hojaji kwa vikundi

hivyo, mwongozo wa usaili ulitumiwa. Utafiti mwigo uliwezesha kushirikishwa kwa vitengo vilivyotoa habari zote zilizolengwa kupatikana.

Vifaa vya kukusanya data mathalan: hojaji, mwongozo wa usaili na tepurekoda iliyokuwa ikifanya kazi viliandaliwa kabla ya kuenda kufanya utafiti mwigo. Utafiti uliwahusisha watu wafuatao: mhariri mmoja na mtangazaji mmoja. Wakati uo huo uliwahusisha wasikilizaji kumi wa kituo cha Redio Mambo. Watangazaji wa kituo hicho cha redio walitumika kuwapata hao wasikilizaji. Wasikilizaji waliotumika ni wale ambao hupiga simu kwa kituo hicho na kuchangia mijadala ya Redio Mambo.

3.6 Unukuzi wa Data

Data ifuatayo ilikusanywa: vipindi vya redio vinavyotumia lugha za kiasili, yaliyomo katika vipindi hivyo vinavyotumia lugha za kiasili, lugha za kiasili zinavyojitokeza kama rasilimali kwa wazungumzaji wake na changamoto za matumizi ya lugha za kiasili katika redio za FM. Data ghafi iliyokusanywa ilihakikiwa kwa kuhusishwa na suala la utafiti ili kuteua tu iliyo ya muhimu. Kabla ya kuichanganua, ilipangwa kwa kuiweka katika maandishi huku mtafiti akizingatia tu ile iliyo na umuhimu kwa utafiti (Kombo na Tromp, 2006). Vipindi vilivyorekodiwa vilichanganuliwa kwa kuongozwa na nadharia ya Sarufi Amilifu.

3.7 Uwasilishaji na Uchambuzi wa Data

Uwasilishaji wa data unarejelea upangaji wa data ili kuifanya ieleweke bayana (Kombo na Tromp, 2006). Data ghafi ilichanganuliwa kikiasi na kiustahilifu. Uchanganuzi wa data kikiasi huhusisha mbinu za kupima matokeo kwa kurejelea upimaji data kwa idadi huku uchanganuzi kiustahilifu ukirejelea upimaji data kwa maelezo (Mugenda na Mugenda, 2003). Maelezo haya huwa katika kategoria mbalimbali. Data iliyokusanywa kwa hojaji ilipangwa kisha ikaingizwa kwenye

programu ya SPSS (Statistical Programme for Social Sciences) na kuchanganuliwa. Data hii ilichanganuliwa kwa kuzingatia maudhui kisha ikawasilishwa kwa kutumia takwimu na maelezo.

Uchanganuzi huu wa kimaudhui ulitumika kutoa muhtasari wa habari zilizotokana na hojaji, usikilizaji wa vipindi na miongozo ya usaili. Matokeo yaliwasilishwa kwa kutumia takwimu zilizoonyesha lugha za kiasili kama rasilimali kwa watumiaji wake kupitia redio za FM kuangazia masuala yanayoathiri jamii moja kwa moja kama vile ya afya, uchumi, jamii na siasa. Data hii ilimwezesha mtafiti kutoa maamuzi juu ya lugha za kiasili kama rasilimali kwa jamii husika na taifa kwa jumla.

3.8 Itikeli

Mtafiti alifanya utafiti huu baada ya kupata idhini ya kufanya utafiti kutoka kwa Baraza la Kitaifa la Kisayansi na Teknolojia (National Council for Science and Technology) kisha kwa kutumia idhini hiyo, akapata idhini kutoka Kamishna wa kaunti ya Bungoma na wasimamizi wa vituo vya redio vya Sulwe na West FM. Vilevile, alipata idhini kutoka kwa watafitiwa kabla ya kuwahusisha katika utafiti huu.

Watafitiwa walihakikishiwa kwamba habari zote walizotoa zilitumika tu kwa utafiti huu wala si kwa sababu zingine zozote. Walishauriwa wasiandike majina yao mahali popote kwenye hojaji na kuhakikishiwa kwamba habari zote walizotoa zingehifadhiwa kwa siri wakati wa utafiti na baada ya utafiti. Kazi zote kutoka kwa tafiti zingine zimetambuliwa na mtafiti.

3.9 Hitimisho

Sura hii imeangazia kuhusu eneo la utafiti. Vilevile, imezungumzia usampulishaji, ukusanyaji data na vifaa vya kukusanya data. Aidha, utafiti mwigo, unukuzi wa data iliyokusanywa na uwasilishaji na uchambuzi wa data umeshughulikiwa. Hatimaye imezungumzia itikeli ambapo masuala ya maadili katika utafiti yamezungumziwa. Sura inayofuata inawasilisha na kuchambua data iliyokusanywa kuhusiana na masuala ya jamii na uchumi.

SURA YA NNE

KIBUKUSU KAMA RASILIMALI INAYOANGAZIA MASUALA YA JAMII NA UCHUMI

4.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia imezungumzia mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Sehemu hii itaangazia Kibukusu kinavyojitokeza kama rasilimali kinaposhughulikia masuala ya jamii na uchumi kupitia redio za FM zinazotumia lugha za kiasili. Mifano ya dondoo zilizotumika kutoka kwa vipindi mbalimbali na ufafanuzi wake imetumika kudhihirisha Kibukusu kinavyojitokeza kama rasilimali. Miongoni mwa yale ambayo yamechanganuliwa katika masuala ya jamii ni uwajibikaji, maadili, na tamaduni za Wabukusu. Kuhusiana na masuala ya uchumi, uchanganuzi umefanywa kuhusiana na uchumi wa mtu binafsi, uchumi wa kaunti ya Bungoma na uchumi wa kaunti zinazopakana na kaunti ya Bungoma pamoja na nchi nzima ya Kenya. Wino mzito umetumika katika mifano ya dondoo kwa ujumbe mkuu. Wakati uo huo, majina yaliyotumika katika dondoo hizi si majina halisi ya wahusika bali ni majina ya kubuni.

4.1. Masuala Yanayoangaziwa katika Vipindi vya Jamii

Kibukusu kimejitokeza kama rasilimali kinapoangazia masuala ya jamii kupitia redio za FM zinazotumia lugha za kiasili. Hili linadhahirika kupitia kwa masuala yanayoangaziwa katika vipindi mbalimbali vinavyowasilishwa na redio za Sulwe na West FM. Ifuatayo ni mifano ya masuala yanayoangaziwa katika vipindi vya jamii:

4.1.1. Uwajibikaji

Uwajibikaji huangaziwa kupitia vipindi kama vile “Bwasia ne Sulwe” (Kumekucha na Sulwe), “Mumilimo” (Katika kazi), “Lotia bakosi” (Rudisha nyumbani wapendwa) na “Lumasaba” (Kibukusu). Wasikilizaji huhimizwa kuwajibika kwa chochote

wanachokifanya pamoja na kuwajibikia familia zao. Wasikilizaji huhimizwa kuamka mapema na kuacha kulaza damu kupitia kwa kipindi cha “Bwasia ne Sulwe”. Hiki ni kipindi cha watu kuamshana na kuhimizana kuchapa kazi. Hili hufikiwa kupitia kwa simu zinazopigwa na jumbe fupi kwa kituo hicho cha redio huku wapigaji simu wakiorodhesha majina ya wale ambao wangependa kuwaamsha, wakiwashauri waende kazini. Ushauri wa kuamka mapema vilevile huwasilishwa kupitia jumbe fupi (burume bubwimbi) ambazo hutumwa kwa vituo hivi vya redio na kusomwa na watangazaji:

1.

Kibukusu

Ninyosia papa we babana, Nekesa we Kibichori, Wafula we Sanandiki nende Joseck we Khuchwele. Burume, embabolela endi bache mumikunda khuraka khubela efula yolile asi.

Kiswahili

Ninamuamsha baba watoto, Nekesa wa Kibichori, Wafula wa Sanandiki na Joseck wa Chwele. Ujumbe kwao, ninawaambia kwamba waende mashambani kwa upanzi kwa vile mvua imenyeshwa ya kutosha.

Uwajibikaji hapa unajitokeza kupitia kwa himizo linalotolewa kwa walengwa wa ujumbe. Msemaji analenga kuwahimiza anaowasiliana nao wawajibike kwa kusema, *ninyosia papa we babana* (ninamuamsha baba watoto) pamoja na hao watu wengine (Wafula na Joseck). Licha ya kuwaamsha, msemaji anawashauri waende kwa upanzi mashambani (*embabolela endi bache mumikunda khuraka*). Hapa *papa we babana* (baba watoto) anayerejelewa ni mume wa msemaji maneno hayo.

Linalobainika katika dondoo hili ni kwamba watu walioorodheshwa hawashauriwi tu kuamka, bali pia kuchapa kazi. Kwa kufanya kazi, watu hawa wanawajibikia kazi kwa vile bila kuchapa kazi hawawezi kujikimu kimaisha. Watu hao wanapokwenda

mashambani, wataweza vilevile kuwajibikia familia zao kwa kukimu mahitaji yao ya chakula, mavazi na malazi.

Kilimo ni uti wa mgongo kwa wakaazi wa kaunti ya Bungoma. Kwa hivyo, wakaazi wengi hutegemea kilimo si kwa chakula tu bali vilevile kama njia ya kupata fedha kupitia uuzaji wa mavuno yao ya mashambani. Kwa hivyo, mawasiliano haya yanalenga kuwahimiza waliotajwa (*baba watoto, Nekesa wa Kibichori, Wafula wa Sanandiki na Joseck wa Chwele.*) kutolaza damu ili waweze kuwajibikia familia zao na kuzikimu kwa kwenda mashambani na kutekeleza kazi ya upanzi. Kupitia kwa Sarufi Amilifu ambapo lugha huanzisha, dhibiti na hifadhi uhusiano miongoni mwa wahusika, tunaona uhusiano bora ukijitokeza kati ya wanaoamshwa na wanaoamsha.

Suala la uwajibikaji vilevile huangaziwa kupitia kwa kipindi cha “Mumilimo” (Katika kazi). Katika kipindi hicho, wasikilizaji huhimizana kuchapa kazi huku wakitumiana salamu. Hilo hufikiwa ama kwa kupiga simu au kutuma jumbe fupi. Ufuatao ni mfano wa mawasiliano hayo ya “Mumilimo”:

2.

Kibukusu

*Ningila mumilimo nende ambano: Maraka, Wanyonyi nende Wafula boosi bafundi be Chinju be Enakalira. Embabolela endi **bachape ekasi ne kamani.***

Kiswahili

*Ninaingia katika kipindi cha “Mumilimo” na wafuatao: Maraka, Wanyonyi na Wafula wote ni mafundi wa nyumba huko Nakalira. Ninawashauri **wachape kazi kwa bidii.***

Hapa msikilizaji huyu anawahimiza ama marafiki au jamaa zake (akina Maraka, Wanyonyi na Wafula) ambao ni waashi wawajibike kazini kwa kufanya kazi nzuri. Uwajibikaji unajitokeza kupitia kwa ushauri unaotolewa na msikilizaji huyo. Anatoa ushauri kwa kuwahimiza jamaa hao wachape kazi kwa bidii pale anaposema, **bachape**

ekasi ne kamani (wachape kazi kwa bidii). Vilevile, mtu anapofanya kazi, huwa anapata riziki ambayo humwezesha kuishughulikia jamii au familia yake. Kwa kuikimu familia, huwa ameiwajibikia.

Uwajibikaji vilevile huweza kuangaziwa kupitia kwa ushauri utolewao kupitia kwa kipindi cha “Lotia bakosi” (Rudisha wapendwa nyumbani). Katika kipindi hiki, kama ilivyo na vipindi vingine, wasikilizaji huwasiliana na wenzao ama kwa kupiga simu au kwa kutuma jumbe fupi kwa redio. Huwa wanawashauri wasikilizaji wenzao warudi nyumbani baada ya kazi ya kutwa. Wakati uo huo, huwa wanawashauri warudi nyumbani angalau na kitu mkononi. Ufuatao ni mfano wa hizo jumbe:

3.

Kibukusu

Endotia bakosi abano nende chipepapak: Wekesa Nyongesa, Simiyu Barasa nende Dorcas Nakhumicha.

Kiswahili

Ninawarudisha nyumbani wafuatao wakiwa wamebeba mifuko ya karatasi: Wekesa Nyongesa, Simiyu Barasa na Dorcas Nakhumicha.

Katika dondoo hili, wasikilizaji wanahimizwa kurudi nyumbani mapema kupitia kwa himizo, *endotia bakosi abano nende chipepapak* (Nawarudisha wapendwa wafuatao nyumbani na mifuko ya plastiki). Kwa kurudi nyumbani mapema wanawajibika, hususan wale walio na familia kusudi wawe na muda wa kujua familia zao zilivyoshinda mchana kutwa. Wakati uo huo, ujumbe unaowasilishwa hapa ni kwamba lazima ushahidi uwepo kuonyesha kwamba mtu amekuwa akienda kazini. Ushahidi huu ni kipato anacholeta nyumbani. Ithibati ya kupata kipato hicho ni kununulia familia mahitaji. Ununuzi wa mahitaji hayo katika dondoo hili ni ule ubebaji wa mifuko ya plastiki (chipepapak). Kwa hivyo, kwa kuwaambia *endotia bakosi abano nende chipepapak* (ninawarudisha nyumbani wafuatao wakiwa

wamebeba mifuko ya plastiki), msikilizaji huyo anahimiza uwajibikaji kwa msikilizaji aliyelengwa na ujumbe huo. Habari hizi za *endotia bakosi abano nende chipepapak* (ninawarudisha nyumbani wafuatao wakiwa wamebeba mifuko ya plastiki) zimepangwa katika muwala na uhusiano huku zikivutia wasikilizaji. Kwa kujitokeza hivyo, habari hizo zinaakisi mhimili wa kiumatini katika Sarufi Amilifu, ambapo vifaa hutolewa na habari kupangwa katika muwala na uhusiano huku zikiwa za kuvutia.

Mfanyikazi yeyote anapokimu mahitaji ya familia yake, tunaweza tukasema kwamba ameiwajibikia. Aghalabu mtu aendapo sokoni au dukani kununua vitu, huwa anafungiwa vitu hivyo alivyonunua katika mfuko wa karatasi. Vitu hivyo huwa vinafungwa kwa lengo la kuvisitiri. Katika jamii tunamoishi, si ajabu kukutana na mtu ambaye huwa harudi kwake nyumbani baada ya kazi, labda kutokana na kushiriki sana katika anasa. Watu wawa hawa, inapotokea kwamba wanarudi nyumbani, mara nyingi hurudi wakiwa wamechelewa hivi kwamba iwapo ni mtu wa familia, basi hurudi nyumbani familia yake ikiwa imelala. Pana uwezekano wa mtu kama huyo kutojua changamoto inazopitia familia yake kwa vile ama hurudi nyumbani amechelewa au huwa harudi kabisa.

Kwa kurejelea habari zilizowasilishwa kupitia kwa vipindi vya “Bwasia ne Sulwe” (Kumekucha na Sulwe), “Mumilimo” (Katika kazi), na “Lotia bakosi” (Rudisha nyumbani wependwa), suala la uwajibikaji lilijitokeza. Uwajibikaji huo ulidhihirika kupitia kwa watu kuamshana mapema, kuchapa kazi na kuzikimu familia zao. Ni bayana kwamba habari zilizowasilishwa kwa Kibukusu zilikuwa na athari chanya kwa wazungumzaji wa lahaja hiyo. Hili linadhihirika tunaporejelea mhimili wa kiumatini

wa nadharia ya Sarufi Amilifu. Katika mhimili huo, habari katika matini hupangwa, zikawa na muwala na mvuto mkubwa.

4.1.2 Maadili

Maadili huangaziwa kwa mapana na vituo hivi vya redio vinavyotumia lugha ya Kibukusu. Maadili huangaziwa kupitia kwa vipindi mbalimbali mathalan “Lumasaba”, (Kibukusu) “Busya bwasya nako” (Kunakucha na matukio yake), “Endekhelo” (Mjadala), “Sina sisinyanga?” (Kipi kinachoudhi?) na “Mbuka busa” (Ninashangaa). Miongoni mwa maadili ambayo huangaziwa ni kama vile tabia na mienendo isiyopendeza katika jamii. Kwa mfano, kupitia kwa kipindi cha “Sina sisinyanga?” (Kipi kinachoudhi?),” wasikilizaji hueleza bayana yale yanayoudhi jamii:

4.

Kibukusu

Ese sisinyanga sili babandu babasima khulosya ke babandu babandi ne kewabwe kabakhaya.

Kiswahili

Kinachonisinya mimi ni watu ambao hupenda kuzungumzia mambo ya watu wengine na ya kwao yamewashinda.

Ujumbe hapa ni kwamba, kuna baadhi ya watu ambao wana mazoea ya kuzungumzia matatizo ya watu wengine ilhali pana uwezekano kwamba ya kwao ni makubwa zaidi. Hilo linajitokeza kupitia kwa maneno, *babandu babasima khulosya ke babandu babandi ne ke wabwe kabakhaya.* (watu ambao hupenda kuzungumzia mambo ya watu wengine na ya kwao yamewashinda). Kuzungumza kuhusu watu wengine wasipokuwepo ni umbeya ambao ni ukosefu wa maadili. Kwa hivyo, tabia hiyo inakashifiwa kupitia kwa kipindi hicho kwa kukaririwa kwamba inaudhi.

Miongoni mwa jamii zetu, kuna watu ambao wana mazoea ya kusambaza maneno hata ambayo hawana uhakika kuyahusu. Watu wa sampuli hiyo huchukiwa katika jamii kwa vile, aghalabu wanapoulizwa kutoa ushahidi kuhusu wanayosambaza, wao hujitetea kwa kusema kuwa pia wao walisikia tu. Ukosefu wa maadili katika mazungumzo hayo ni mtu kuzungumza kumhusu mtu mwingine ambaye hayuko kujitetea kuhusu yale yanayosemwa kumhusu.

Ukosefu wa maadili unajibainisha zaidi pale inaposemekana kwamba huyo mtu ameshindwa kuyatatua matatizo ya kwake nyumbani ilhali anazungumzia ya wengine. Hilo linadhihirika kupitia kwa maneno, *ne ke wabwe kabakhaya* (na ya kwao yamewashinda). Kukosekana kwa maadili hapa ni watu kuwa wasambazi, mwenendo usio mwema katika jamii na ambao husababisha migogoro miongoni mwa watu. Kwa hivyo, watu hawa wanaposababisha migogoro husababisha ukosefu wa amani miongoni mwa jamii kutokana na ukosefu wa maadili miongoni mwa watu hao.

Ukosefu wa maadili miongoni mwa wanasiasa vilevile huangaziwa pale wanasiasa wanapokosa kutimiza ahadi zao kwa watu ambao wao huwawakilisha katika mabunge ya kitaifa na kaunti. Wanasiasa hao hutoa ahadi wasizotimiza na hatimaaye kuwa wajeuri kwa wapiga kura wanaofuatilia hizo ahadi. Hali hiyo inadhihirika katika mfano huu kutoka kwa kipindi “Mbuka busa”

5.

Kibukusu

Ese mbuka busa sikila babandu balala sanasana wanasiasa nebabeanga amilukha kye kamasika! Onyola omundu kenyokha amasika ali, ese enga MCA namwe enga Omubunge we lubeka luno, nakhekombile khusubisya namulekhwa nende bafubi endi, endema nenabo. Omwana wa marehemu wamalile kamasomo ke endererwa oyo ndamubukula emuwe kimilimo kusudi ayete babasie. Mwanasiasa chana alekha khukhola enga ne kalaka. Oba oli namulekhwa namwe omwana wa marehemu amulondakhokhumukhebusia

endakano chana, ne mwanasiasa oyo abarafwilila ne khubatimania. Ese mbuka busa!

Kiswahili

Mimi hushangazwa na watu wengine hasa wanasiasa ambao hudanganya katika sherehe za matanga! Utapata mtu akiamka katika sherehe ya matanga na kusema, mimi kama MCA au kama mbunge wa eneo hili, ningependa kuwahakikishia mjane na mayatima kwamba nitasimama nao. Mtoto wa marehemu ambaye alikamilisha elimu ya juu, nitamtafutia kazi ili awasaidie wenzake. Baadaye huyo mwanasiasa hukosa kutimiza alivyoahidi, na huyo mjane au yatima anapofuatilia hiyo ahadi, mwanasiasa huyo huwa mkali sana kwa hao wafiwa na kuwafukuza. Mimi nashangaa!

Katika dondoo hili, tunafahamishwa kwamba kuna watu hususan wanasiasa ambao husema uwongo katika sherehe za matanga. Hili linadhihirika kupitia kwa maneno, *wanasiasa nebabeyanga amilukhake kamasika!* (*wanasiasa ambao hudanganya katika sherehe za matanga!*) Udanganyifu hujitokeza kwa vile wanasiasa hawa huwa hawatimizi ahadi zao kama anavohoji mlalamishi pale anaposema *alekha khukhola enga ne kalaka* (*hukosa kutimiza alivyoahidi*). Hatimaye, waliopewa ahadi hizo wanapozifuatilia, matokeo huwa ni kukaripiwa pamoja na matusi tunavyoona katika dondoo hili anapohiji, *abarafwilila ne khubatimania* (*huwa mkali sana kwa hao wafiwa na kuwafukuza*).

Mtu anapodanganya, huwa anakwenda kinyume cha maadili ya jamii. Mtayarishi wa kipindi katika dondoo hili anashangazwa na tabia zisizopendeza kutoka kwa viongozi ambazo ni za udanganyifu na ujeuri. Viongozi hawa wa kisiasa hutoa ahadi za uwongo katika hafla kama vile za mazishi kwa lengo la kuufurahisha umati wa watu uliofika. Wanasiasa hawa wanapofuatwa kutimiza ahadi walizotoa, huwa wakali kwa wanaofuata hizo ahadi. Wakati uo huo, mwanasiasa huyo anakosa maadili kwa kuwakaripia wafiwa pale wanapofuata ahadi alizotoa mwenyewe. Huku kuwakaripia ni kukosa maadili kwa vile wafiwa hao wanastahili huruma kama ishara ya utu wala si kukaripiwa. Pili, kuwakaripia ni ukosefu wa maadili kwa vile wanasiasa hao huwa

wanatoa ahadi hizo kwa hiari. Kwa mujibu wa Halliday (Halliday & Matthiessen, 2004), hapa lugha ya wanasiasa imetumika kuanzisha, kudhibiti na kuhifadhi uhusiano kati ya mwanasiasa na wafiwa. Katika muktadha huu, uhusiano unaoanzishwa na kudhibitiwa na mwanasiasa asiyetimiza ahadi ni mbaya. Uhusiano huo si mzuri kwa vile licha ya kutotimiza ahadi, anawakaripia wale aliowaahidi usaidizi.

Lengo la kipindi “Mbuka busa” huwa ni kubadili mienendo mibaya katika jamii. Kwa hivyo, kinacholengwa kubadilishwa katika dondoo hilo ni mienendo mibaya ya wanasiasa ambayo ni udanganyifu. Wanasiasa hawa hujifanya wakarimu sana huku wakitoa ahadi ambazo hatimaye huwa hawazitimizi. Wanasiasa hao hutonesha vidonda vya wale wanaohitaji usaidizi wao kwa kuwa wakali na kuwafukuza.

Ukosefu wa heshima miongoni mwa vijana kwa wazazi wao vilevile ni suala la maadili ambalo huangaziwa. Kwa mfano, kupitia kwa kipindi cha “Mbuka busa”, shutuma ifuatayo inajitokeza:

6.

Kibukusu

*Kumwima enga kuno kuli kwe embelekeu saana. Onyola omundu akobola engo ne anyola omukhaye wewe karere kumunwa khu kundi. Enga ne amureba ali sina sibi, ne omukhaye oyo aloma ali ese mayi masala wase mungo omuno kakhayile. Omundu oyuno enga ne aulila ario ne **acha khu mawe omusala ne khukhwanja khumurafwilila** ali ewe mayi lekhana nende enju yase kabisa, **oli khowenya khufuna enju yase ne wilemo namwe?** Ese embuka saana embelekeu ye lukano oluno!*

Kiswahili

*Tabia kama hii ni utovu wa nidhamu sana. Uutapata mtu anarudi nyumbani kwake na kumpata mkewe akiwa amenuna. Anapomuuliza nini kibaya, huyo mke atamwambia kwamba mama mkwe amemshinda katika hili boma. Huyo mtu anaposikia hivyo, **atakwenda kwa mama yake mzazi na kuanza kumgombeza** akisema, wewe mama wachana na ndoa yangu kabisa. **Unataka***

kuivunja ili wewe uchukue nafasi ya mke wangu ama? Mimi nashangazwa sana na utovu huu wa nidhamu!

Hapa inasemekana kwamba kijana huyu wa kiume anakosa maadili kwa kumkaripia mamake mzazi anavyosema mtayarishaji kipindi kwamba, ***acha khu mawe omusala ne khukhwanja khumurafwilila*** (*atakwenda kwa mama yake mzazi na kuanza kumgombeza*). Mshutumiwa anazidisha kumkosea mzazi wake maadili kupitia kwa swali analomuuliza mamake mzazi, ***oli khowenya khufuna enju yase ne wilemo namwe?*** (*unataka kuivunja nyumba yangu ili wewe uchukue nafasi ya mke wangu ama?*). Suala la mke kutosikilizana na mavyaa wake si geni. Katika familia nyingi za kisasa jambo hilo hutokea. Hata hivyo, ni utovu wa nidhamu kwa mtu kumkaripia mama aliyemzaa na kumuuliza iwapo huyo mamake mzazi alikuwa anamvuruga mke wake kwa lengo la kutaka aolewe kwa mwanawe kama inavyojitokeza katika dondoo hilo, ***oli khowenya khufuna enju yase ne wilemo namwe?*** (*unataka kuivunja nyumba yangu ili wewe uchukue nafasi ya mke wangu ama?*).

Katika nukuu hiyo, tunaona ukosefu wa maadili ukiendelezwa na huyo mtu ambaye anamkaripia mamake eti kwa vile amekosana na mkewe. Ukosefu wa maadili vilevile unadhihirika kupitia kwa madai yasiyo na chembe cha heshima, anayotoa mtu huyo kwamba mamake angependa mkewe aondoke kusudi mamake aolewe kwake! Ujumbe unaojitokeza hapa ni kwamba, kuna baadhi ya watu ambao huwa hawaheshimu wazazi wao kiasi cha kuwakosea adabu kabisa. Watu kama hao hudhalilisha wazazi wao hususan wa kike kiasi cha hata kuwaambia hao wazazi wanawasumbua wake zao. Ukosefu wa nidhamu hufikia kiasi cha kudai mama zao walikuwa na nia ya kuolewa kwa hao watoto wao kama inavyojitokeza katika dondoo hilo! Mazungumzo ya aina hiyo ni ithibati ya ukosefu wa maadili miongoni mwa

vijana. Huo ukosefu wa maadili ni baadhi ya mambo ambayo huangaziwa na vituo hivi vya redio vinavyotumia lugha za kiasili.

Kupitia kwa mijadala ya redio, masuala ya maadili yaliweza kuangaziwa na kujadiliwa huku wale wasiofuata maadili ya jamii wakishutumiwa na wasikilizaji pamoja na watangazaji wa vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili. Mijadala hiyo iliafikiana na maoni ya Gathigi (2009) alipohoji kwamba, kupitia kwa mijadala ya redioni katika vituo vya redio vilivyotumia lugha za kiasili, masuala ya kijamii yaliweza kujadiliwa huku jamii ikitoa maoni yake.

Mifano ya ukosefu wa maadili katika jamii iliyotolewa haikutoka kwenye ombwe tupu. Mifano hiyo ilitokana na visa halisi vilivyotokea katika jamii, visa ambavyo watayarishaji wa vipindi hivyo walitumia kukashifu mienendo mibaya. Visa hivyo vinadhihirisha nadharia ya Sarufi Amilifu. Mhimili wa kiutambuzi ya Sarufi Amilifu unaeleza kwamba lugha huwezesha watu kuelewa mazingira yao. Watu hao hupata maarifa, wakaelewa ulimwengu unaowazunguka kisha wakawasiliana kuhusu tajriba zao kwa mambo mbalimbali (Halliday & Matthiessen, 2004). Kwa mfano, mtayarishaji wa kipindi cha “Mbuka busa” anawashutumu wanasisia waongo ambao hudanganya katika ghafla za mazishi. Udanganyifu huo ni tukio ambalo hushuhudiwa mara kwa mara katika jamii.

Kutokana na mifano hiyo, maadili yameweza kuangaziwa kwa njia mbalimbali. Tumeweza kuona maadili yakishughulikiwa kupitia kwa mienendo mibaya miongoni mwa baadhi ya watu. Watu hao ni wale ambao wana mazoea ya kuzungumzia matatizo ya watu wengine badala ya kushughulikia mambo yao. Vilevile, tumeweza kuona wanasisia wasiozingatia maadili. Wanasisia hao wana mazoea ya kutoa ahadi

za uwongo kwa wananchi. Kilele cha ukosefu wa maadili ni pale ambapo wanasiasa hao huwakaripia watu waliofuatilia ahadi walizopewa na wanasiasa hao.

4.1.3. Tamaduni za Wabukusu

Tamaduni ziliweza kuangaziwa kwa njia mbalimbali mathalan, upashaji tohara miongoni mwa jamii ya Wabukusu na wasikilizaji kukumbushwa kuhusu miiko ya jamii hiyo. Hili lilifikiwa kupitia kwa kipindi cha “Lumasaba” (Kibukusu) na “Embalu yefwe” (Tohara yetu). Aidha, utamaduni ulijitokeza kupitia kwa misemo ya Kibukusu ambayo huangaziwa kupitia kwa vipindi kama vile “Lusimo lwe endalo.”

Tohara huthaminiwa sana na Wabukusu na hufanyiwa watoto wote wa kiume wanapofikia umri wa kubaleghe. Wabukusu huifanya sherehe hii wakiwa wamejawa na hisia huku wakiirejelea kama “Embalu yefwe”. Uteuzi wa kipindi cha “Embalu yefwe” ulifanywa makusudi na kituo cha redio kilichokipeperusha. Kipindi hicho kiliteliwa na kupeperushwa mwezi ambao jamii ya Wabukusu ilikuwa ikipasha vijana wa kiume tohara. Kwa kuteua mada hiyo wakati huo, mhimili wa vyombo vya habari kuteua ajenda unajitokeza wanavyohoji Mcombs & Show (1993) katika nadharia ya Uteuzi wa Ajenda. Kupitia kwa “Embalu yefwe” na “Lumasaba,” vipindi vilivyoangazia tohara katika jamii ya Wabukusu, wasikilizaji walifahamishwa kuhusu yale wanayopaswa kuzingatia wakati wa sherehe za upashaji tohara:

7.

Kibukusu

Enda yo omwana Mubukusu, manya muli omukhebi wafwisya omukhasi, omueyi, owayaba eng'ani namwe wakheba omufu sakhoya kakheba babana ta.

Kiswahili

Jamii ya Wabukusu fahamu kwamba, ngariba aliyefisha mke, mkware, aliyewahi chimba kaburi au aliyetahiri mfu hapaswi kupasha watoto tohara.

Dondoo hili linatufahamisha kuhusu hulka ambazo ngariba hafai kuwa nazo msimu wa upashaji tohara miongoni mwa jamii ya Wabukusu. Hulka hizo ni zifuatazo kwa mujibu wa dondoo: ***omukhebi wafwisya omukhasi, omueyi, owayaba eng'ani namwe wakheba omufu.*** (ngariba aliyefisha mke, mkware, aliyewahi chimba kaburi au aliyetahiri mfu). Wasikilizaji waliosikiliza kipindi hiki walitarajiwa kuwachunguza ngariba ambao wangewapasha watoto wao tohara kabla ya kuwapa kazi hiyo. Ngariba yeyote aliyekuwa na mojawapo ya hulka hizi zilizoordheshwa, hakustahili kupewa kazi ya kuwapasha tohara vijana. Iwapo angepewa kazi hiyo, ingekuwa ni kwenda kinyume na tamaduni za jamii ya Wabukusu.

Miongoni mwa Wabukusu, inaaminika kwamba ngariba aliye na hizo sifa huenda akaleta kijana anayepashwa tohara mkosi. Mkosi huo huenda ukawa miongoni mwa mengine, kijana huyo kutokwa na damu hadi afe au asistahimili uchungu wakati wa kupashwa tohara. Kwa hivyo, kupitia kwa mafundisho hayo, jamii iliweza kuhifadhi baadhi ya tamaduni zake ambazo huenda zimesahaulika kutokana na athari za miji.

Utamaduni unaoendelezwa hapa ni upashaji tohara kwa vijana wa kiume miongoni mwa Wabukusu kwa njia iliyo salama. Usalama huo unatokana na sheria zilizowekwa na jamii kwamba ngariba aliyejihusisha na mambo kama vile ***kufisha mke, mkware, aliyewahi chimba kaburi au aliyetahiri mfu*** kutopewa nafasi ya kuwapasha vijana tohara. Kutokana na vikwazo hivyo, ngariba waliotarajia kupewa kazi ya upashaji tohara walijitunza na kuhakikisha hawafanyi mambo ambayo yangewakosesha kazi hiyo kwa kuenda kinyume cha tamaduni za jamii. Katika upashaji tohara huo, kuna mambo kadhaa yasiyohitaji kupuuzwa kwa hofu kwamba yanapopuuzwa, pana uwezekano wa msiba kutokea. Mifano ambayo tumepewa ni kama vile ukware na ngariba aliyetahiri mfu kumpasha tohara kijana wa Kibukusu.

Katika jamii nyingi za Kiafrika, ni mwiko kwa mtu kufanya mapenzi kabla ya kwenda vitani. Huwa inaaminika kwamba akifanya mapenzi kabla kwenda vitani, huenda akafikwa na mkosi wa ama kushindwa vitani au hata kuuawa. Tohara pia ilichukuliwa kama “vita”. Kwa hivyo ngariba aliyelala na mkewe au mwanamke mwingine yeyote yule angekosa kutekeleza kazi yake vizuri ama kwa kutahiri kijana huyo vibaya na kusababisha umwagikaji wa damu nyingi au hata kijana huyo anayepashwa tohara kutoonyesha ushujaa kwa kuogopa wakati wa kupashwa tohara.

Wazazi wa kijana aliyetarajia kupashwa tohara vilvile walionywa dhidi ya kufanya mapenzi kusudi wasimletee mwana wao mkosi. Hii ndiyo sababu kuu ya kuwepo mkazo miongoni mwa jamii ya Wabukusu kwamba watu wote ambao walitarajiwa kutagusana na kijana aliyetarajiwa kupashwa tohara wadumishe utakaso wa kimwili kupitia kwa vitendo vyao. Kwa upande mwingine, kwamba yule aliyetahiri mfu, anapothubutu kumpasha tohara kijana, angesababisha mizimu imletee kijana huyo maafa kama vile kifo kutokana na kutokwa na damu nyingi.

Kutokana na mfao huo, wasikilizaji wa kipindi hicho walipata maarifa kuhusu umuhimu wa kuwakagua ngariba kabla kuwapa kazi. Wawasilishaji kipindi waliweza kutoa tahadhari hiyo kutokana na tajriba yao kuhusu upashaji tohara. Ushauri huo unaoana na mhimili wa kiutambozi katika Sarufi Amilifu unaotilia uzito umuhimu wa lugha katika kuwezesha mtu apate maarifa na kuwasiliana kuhusu tajriba yake kuhusu mambo mbalimbali (Halliday & Matthiessen, 2004). Katika muktadha huu, lugha ya Kibukusu imetumika kuwafahamisha wasikilizaji kuhusu tahadhari wanayopaswa kuchukua. Ushauri huo unatokana na tajriba ambayo Wabukusu wamekuwa nayo kuhusiana na suala la upashaji tohara.

Tamaduni vilevile zinaendelezwa kupitia kwa miiko inayothaminiwa katika jamii ya Wabukusu. Kupitia kwa kipindi cha “Lumasaba” (Kibukusu), wasikilizaji walikumbushwa kuhusu baadhi ya hizi tamaduni. Wasikilizaji walifundishwa baadhi ya miiko ya jamii na umuhimu wake. Baadhi ya miiko hiyo ni, mtu kutoruhusiwa kumsalimu mama mkwe wake na baba mkwe kutoruhusiwa kumsalimu mkaza mwana kwa mkono inavyodhihirika katika mfano huu:

8.

Kibukusu

Papa wo omwana sokhoya wakhesya mkha omwana mukhono ta. Wamukhesia mukhono bukhwe bukhwosia.

Kiswahili

Baba ya mtoto hustahili kumsalimu mkaza mwana mkononi. Ukimsalimia kwa mkono, utachomwa na ukwe.

Kwa mujibu wa mwiko huu, baba mtu haruhusiwi kumsalimia mkaza mwana kwa mkono inavyodhihirika katika maneno, *papa wo omwana sokhoya wakhesya mkha omwana mukhono ta. (baba ya mtoto hustahili kumsalimu mkaza mwana mkononi)*. Kwa kufanya hivyo, utakuwa unakwenda kinyume cha tamaduni za jamii ya Wabukusu. Ili kuhakikisha watu walizingatia mwiko huo, walitishwa kwamba iwapo wangepanya hivyo, “**ukwe ungewachoma.**” Kuchomwa na ukwe ni hali ya rangi ya ngozi ya mtu kubadilika na kuwa hudhurungi kutokana na kwenda kinyume cha tamaduni. Iliaminika kwamba yeyote aliyefanya hivyo angejulikana kutokana na kubadilika kwa rangi ya ngozi yake. Kwa kuhofia kuaibika kutokana na rangi ya mwili kugeuka na kuwa ya hudhurungi, Wabukusu walijiepusha na salamu hizo. Kwa hivyo, Wabukusu wengi huchukua tahaadhari ya “kutochomwa na ukwe” kwa kutokaribia wakwe zao wa jinsia nyingine.

Lengo la kuwepo mwiko huu ni kudumisha heshima kati ya wakwe wa jinsia zote. Katika jamii ya Wabukusu, kutosalimiana kwa mkono kati ya mtu na wakwe zake ni jambo ambalo limekuwepo kwa miaka na mikaka. Hali hiyo inatokana na kuhakikisha kwamba pande hizo mbili hazizoeani kisha hatimaye zikoseane heshima. Inaaminika kwamba hawa watu (wa jinsia ya kiume na kike) wakizoea kusalimiana kwa mikono huenda hatimaye wakakosa kudumisha heshima inayostahili kuwepo kati yao.

Kwa mfano, kumekuwa na visa vya baadhi ya wanaume ambao wamekuwa wapenzi wa wake za watoto wao wa kiume kutokana na kuzoeana ambako huanzia kwa salamu za mkononi jambo ambalo ni la aibu. Ili kuhakikisha heshima inadumishwa kati ya mtu wa kiume na mkazamwana au mtu wa kike na mume wa binti yake, mwiko huu umekuwa ukisisitizwa kupitia kwa vipindi kama vile “Lumasaba.” Kwa kufanya hivyo, jamii imezingatia na kuendeleza tamaduni za kale zilizodumisha heshima miongoni mwa watu walioletwa pamoja na ndoa.

Kutokana na mfano huo, Kibukusu kinatumika kuanzisha, kudhibiti na kuhifadhi uhusiano miongoni mwa wazungumzaji wake kama inavyojitokeza katika sarufi Amilifu (Halliday & Matthiessen, 2004). Katika muktadha huu, uhusiano unaoanzishwa, thibitiwa na hifadhiwa ni ule wa kudumisha heshima. Heshima hiyo inadumishwa kupitia kwa kuzingatiwa kwa miiko na kwa kufanya hivyo, tamaduni zinadumishwa.

Kupitia kwa masuala ya jamii utamaduni vilevile hujitokeza kwa misemo na methali za Kibukusu. Kwa mfano, kupitia kwa “Lusimo lwe endalo” (Msemo wa siku), wasikilizaji huulizwa kufafanua maana ya msemo ambao hutolewa na mwasilishaji kipindi mathalan:

9.

Kibukusu*Kumwikule kukwoo ne kumwikale kwabene.***Kiswahili***Mlango uliofunguliwa ni wako na uliofungwa ni wa wenyewe.*

Maana isiyo batini ya msemu huu ni kwamba, mlango uliofunguliwa ni wako na uliofungwa ni wa wenyewe. Maana batini ya msemu huu ni kwamba mke wa mtu hastahili kutongozwa na mtu mwingine. Katika muktadha huu mke huyo amerejelewa kama *kumwikale* (mlango uliofungwa). Kijana wa Kibukusu anapopashwa tohara, vilevile hupewa ushauri nasaha wa jinsi ya kuishi katika jamii huku akijiepusha na mambo ambayo huenda yakamletea maafa. Miongoni mwa mambo ambayo yangeweza kumletea maafa ni kuwatongoza wake za watu ambao hurejelewa kama *kumuliango kumwikale* (mlango uliofungwa).

Katika jamii ya Wabukusu, baada ya upashaji tohara, kijana wa kiume alikuwa tayari kuo na kuanzisha familia. Kwa hivyo, msemu huu ambao unatumika hadi wa leo ulimtahadharisha dhidi ya mambo yanayoweza kuhatarisha maisha yake pale anapoanza maisha ya familia. Ngariba aliyempasha kijana ndiye huwa wa kwanza kutoa ushauri huo. Ushauri huo vilevile hurejelewa kwa huyo kijana aliyepashwa tohara anapotoka jandoni.

Mlango uliofunguliwa inamaanisha msichana ambaye hajaolewa huku mlango uliofungwa ukiashiria mwanamke aliyeolewa. Kwa hivyo, vijana hawa walishauriwa kwamba walipomtafuta mke wa kuo, walifaa kutafuta wasichana ambao walilinganishwa na mlango uliofunguliwa. Kwa hivyo, vijana hawa walionywa wajiepushe na kuwatongoza wake za watu ambao ni sawa na mlango uliofungwa. Onyo hapa ni kwamba, kwa kumtongoza mke wa mtu, pana uwezekano wa kufikwa

na maafa yanayoweza hata yakawa kifo. Kwa hivyo, msemu huu ulisaidia kuendeleza utamaduni na kudumisha heshima kati ya watu walioolewa na vijana ambao hawajaoa. Msemu huo unapotumiwa katika jamii ya kisasa unaweza kuwa na maana zaidi ya hiyo ya hapo awali. Kwa sasa, kutokana na umuhimu unaowekeka elimu vijana hawaoi pindi wanapopashwa tohara kwa vile wanaendeleza masomo yao. Kwa hivyo, kwa sasa mlango uliofungwa unajumuisha vilevile vitu vya watu. Hapa vijana wanaonywa kuheshimu vitu vya watu wengine. Kwa mfano, huwezi ukaingia kwa shamba la mtu na kuvuna mahindi yake. Kwa kufanya hivyo, huenda ukaadhibiwa kwa kukosa kuheshimu vitu vya watu. Kwa hivyo, kwa jumla msemu huu unahimiza heshima kwa vitu vya watu.

Mifano hiyo inaonyesha jinsi matumizi ya Kibukusu katika redio za FM yalivyotumika kueleza utamaduni wa Wabukusu. Kwa hivyo, wasikilizaji wananufaika na matumizi ya Kibukusu katika vituo hivi vya redio. Anavyohoji Okombo (2014), kupitia kwa lugha zetu za kiasili, tunaweza kueleza tamaduni zetu.

Kupitia kwa mifano hii, tumeweza kuona Kibukusu kinavyotumika nyakati mbalimbali kuendeleza tamaduni za Wabukusu. Jambo hilo limeweza kufikiwa kupitia kwa vipindi kama vile “Lumasaba”, “Embalu yefwe” na “Lusimo lwe endalo.” Kupitia kwa vipindi hivi, jamii ilifundishwa tamaduni kadha wa kadha ambazo zinapaswa kuzingatiwa na vilevile kuendelezwa mathalan, uendelezaji wa utamaduni wa upashaji tohara kwa vijana wa kiume. Wakati uo huo, tumeona tamaduni zikiendelezwa kupitia kwa uzingatiaji wa miiko katika jamii na hatimaye kupitia kwa misemo ambayo huchambuliwa kwa wasilikizaji.

Kutokana na mifano hiyo, ni bayana kwamba baadhi ya tamaduni zilipitishwa kwa njia fiche. Kwa mfano jumbe katika “kuchomwa na ukwe” na “mlango uliofungwa”

zikuwa kama mafumbo. Hata hivyo, kwa kuzingatia Sarufi Amilifu, ufasiri wa maana aliourejelea Halliday (Halliday & Matthiessen, 2004) kama uamilifu halisi wa lugha uliweza kujitokeza. Ufundi mzima wa matumizi ya lugha uliweza kutoa maana iliyolengwa kufikiwa na jamii ya Wabukusu.

4.1.4 Matukio ya Kaunti ya Bungoma

Matukio katika kaunti ya Bungoma ambayo ni ya kijamii vilevile huangaziwa hususan kupitia kwa “Kamakeni” (Taarifa za habari). Aidha, matukio hayo huangaziwa kupitia kwa “Busya bwasia nako” (Kumekucha na matukio yake). Baadhi ya matukio ya kijamii ambayo huweza kuangaziwa ni kama vile mizozo ya kifamilia ambayo huvunja hizo familia. Kwa mfano, unywaji wa pombe kupita kiasi miongoni mwa wakaazi, ukosefu wa uaminifu kati ya wanandoa, mizozo kati ya wanandoa na dhuluma dhidi ya watoto. Kwa mfano, katika mojawapo ya vipindi vya “Kamakeni,” mwakilishi wa wanawake katika kaunti ya Bungoma anashutumu ongezeko la visa vya watoto wadogo kunajisiwa kwa kusema:

10.

Kibukusu

Nesindukhile basecha balala khukonia babana babwe besikhana ne khubakubhega abo be sisoreli!

Kiswahili

Nimeshtushwa na visa vya baadhi ya wanaume kufanya mapenzi na mabinti zao huku wakiwapiga watoto wao wa kiume!

Kisa cha baba mzazi kufanya mapenzi na binti wake ni jambo lisilokubalika katika jamii zetu, kwa hivyo ni jambo la kushangaza. Kama wanavyofundishwa wanahabari katika vyuo vya uanahabari, mbwa anapomuuma mtu si habari lakini mtu anapomuuma mbwa, hizo huwa ni habari. Kumaanisha habari ni tukio lisilo la kawaida. Katika muktadha huu, kitendo cha mzazi kufanya mapenzi na binti wake ni

habari au tukio kwa vile, mtu hastahili kufanya mapenzi na binti wake. Kitendo hiki ni tukio kwa vile mtoto huyo wa kike anapofanyiwa dhuluma ya kimapenzi, anapaswa kumkimbilia babake ili apate hifadhi. Lakini kinaya hapa ni kwamba, yule mtu anayepaswa kumpa hifadhi ndiye anayemdhulumu. Hii ndiyo sababu mwakilishi wa wanawake katika kaunti anashangazwa na kisa hicho pale anaposema, ***nesindukhile basecha balala khukonia babana babwe besikhana.*** (*nimeshtushwa na visa vya baadhi ya wanaume kufanya mapenzi na mabinti zao!*)

Habari hizi zikijitokeza kama tukio vilevile pale wazazi wawa hawa wa kiume wanapozidi kuendeleza dhuluma hata kwa watoto wao wakiume anavyolalama mwakilishi huyu kwamba, ***ne khubakubega abo be sisoreli!*** (*huku wakiwapiga watoto wao wakiume*). Tukio hili ni la kushangaza kwa vile mtoto yeyote yule anapaswa kutafuta hifadhi kwa wazazi wake anapogundua kwamba maisha yake yako hatarini. Lakini katika kisa hiki, ni baba mzazi ndiye anayetishia maisha ya wanawe wote (wa kike na wa kiume).

Mbunge huyo alishutumu matukio hayo alipokuwa katika ziara katika mojawapo ya maeneo bunge aliyozuru katika kaunti ya Bungoma. Anashutumu kitendo hicho kutokana na ripoti zilizokuwa katika vyombo vya habari kuhusu dhuluma hizo. Ripoti hizo zilidai kwamba wasichana wengi katika eneo hilo walikuwa wameacha masomo kutokana na kupachikwa mimba na watu wazima. Kwa mujibu wa mbunge huyu, dhuluma hizo zilichangia wengi wa vijana kutofanya vyema masomoni. Wakati uo huo, visa kama hivi viliwafanya watoto hao kuogopa kurudi kwao nyumbani. Kutokana na matukio hayo yaliyokuwa yameenea katika baadhi ya maeneo ya kaunti ya Bungoma, mbunge huyu alihimiza kwamba kuongezwe shule za bweni ili kuwasetiri vijana kama hao dhidi ya dhuluma za wazazi wa kiume. Hili lingesaidia

vijana hao kuwa na muda mfupi nyumbani, hivyo basi kuwaepushia madhila ya wazazi wa aina hiyo.

Visa vya dhuluma zinazofanyiwa watoto na watu wazima zimeongezeka nchini Kenya. Miongoni mwa dhuluma hizo ni akina baba kuwapachika mimba mabinti wao. Vitendo hivyo vinafanya hao wasichana waache masomo na kutengwa na jamii kwa kuonekana kama watoto wa mkosi. Visa hivyo huwa ni matukio katika jamii zetu za Kiafrika, kwa vile haiwezekani mtu wa akili razini kufanya mapenzi na mwanawe. Huwa ni jambo la aibu sana na ambalo hatimaye humwathiri huyo mtoto hivi kwamba huenda hata akakosa mtu wa kumuoa kutokana na doa hilo. Baadhi ya waathiriwa hukosa thamani ya maisha na kuingilia ama ukahaba au hata kujitia kitanzi. Wakati uo huo, baadhi ya wasichana ambao hufanyiwa unyama huu hufanyiwa mizaha na wenzao kwa kuitwa “wake za baba zao,” jambo ambalo huwaathiri kihasi kisaikolojia.

Kupitia kwa matukio ya kaunti yaliyowasilishwa kupitia kwa “Kamakeni,” wasikilizaji waliweza vilevile kufahamishwa kuhusu ukosefu wa usalama ulioathiri jamii za sehemu mbalimbali katika kaunti ya Bungoma. Miongoni mwa mambo haya yanayoweza kujitokeza kama ukosefu wa usalama ni watu wanaposhambuliwa na magenge ya watu. Kwa mfano, kwa wakati mmoja, mwalimu wa shule ya msingi katika maeneo ya Tongaren alishambuliwa na kuuawa alipokuwa akirejea nyumbani. Kutokana na kisa hicho, habari ziliendelezwa hivi katika “Kamakeni”;

11.

Kibukusu

Bamenywa be Embakalo, Naitiri besindukhile lifwa lya mwalimu niye berire silo sye likoloba mala ne bara kumubili kwewe khumwanda kumubofu kucha Enaitiri. Bamenywa abo balikhebekicha babemelesi be bulindi ne alimo omwimelesi we bapolisi mbo batile khangu babandu baberire mwalimu

oyoo enga ta bacha khukhwimurukunya kukhwenya babemelesi abo bauyisibwe.

Kiswahili

Wakaazi wa Mbakalo, Naitiri wamegutushwa na kifo cha mwalimu ambaye aliuawa jana usiku na mwili wake ukawekwa kwa barabara kuu ya kwenda Naitiri. Wakaazi hao wanawauliza wasimamizi wa usalama akiwemo mkuu wa polisi wawakamate watu waliotekeleza uhalifu huo haraka la sivyoy, watafanya maandamano ya kushurutisha hao wasimamizi wa usalama kuhamishwa.

Tunachoona hapa ni, kisa cha mojawapo wa wakaazi ambaye ni mwalimu akiuawa na kisha mwili wake kurushwa barabarani kama inavyojitokeza katika maneno haya, *lifwa lya mwalimu niye berire silo sye likoloba mala ne bara kumubili kwewe khumwanda kumubofu kucha Naitiri.* (Kifo cha mwalimu ambaye aliuawa jana usiku na mwili wake ukawekwa kwa barabara kuu ya kwenda Naitiri), tukio ambalo linawagutusha wakaazi hivi kwamba walikuwa wanatishia kufanya maandamano iwapo taasisi zilizojukumiwa usalama hazingewahakikishia usalama inavyodhihirika katika maelezo, *enga ta bacha khukhwimurukunya kukhwenya babemelesi abo bauyisibwe.* (La sivyoy, watafanya maandamano ya kushurutisha hao wasimamizi wa usalama kuhamishwa.). Kifo cha mwalimu huyo hakikuwa cha kawaida na waliotekeleza mauaji hayo waliuweka mwili wake kwenye barabara kuu ya kuelekea mji mdogo wa Naitiri jambo ambalo liliripotiwa na vyombo vya habari kama tukio.

Kati ya majukumu ya vyombo vya habari ni kuelimisha, kuburudisha na kufahamisha (Mohochi 2006). Kwa kuelezea kisa cha mauaji yaliyofanywa katika kaunti ya Bungoma, kituo hicho cha redio kinachotumia Kibukusu kilikuwa kinawafahamisha wasikilizaji kuhusu tukio hilo. Habari hizi zinajitokeza kama tukio katika kaunti na ziliwafikia wenyeji mapema kwa vile redio za FM zinazotumia lugha za kiasili huangazia zaidi habari za mashinani kunakozungumzwa hizo lugha. Ingawa habari

hizo baadaye zilisikika katika redio ya Citizen, ziliweza kuwafikia mapema zaidi wasikilizaji wa Sulwe FM katika habari za saa moja za asubuhi.

Wakaazi wa Bungoma wanafahamishwa kuhusu tukio hili kama ithibati ya kuzorota kwa usalama katika kaunti. Wakaazi wanajulishwa kuhusu kifo cha huyo mwalimu ambaye huenda aliuawa na majambazi au maadui zake. Kutokana na habari hizo kuwekwa hewani, utendakazi wa wale wanaohusika na usalama ulikuwa unaangaziwa. Kutokana na matangazo hayo, viongozi mbalimbali hususan wa kisiasa waliweza kupata ufahamu kuhusu kudorora kwa usalama na kuwahimiza waliohusika na usalama kuuboresha.

Tukio hili linaakisi maoni ya Kamau (2011) anapohoji kwamba, vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili ni njia bora zaidi ya upashaji habari mashinani. Hali hiyo inadhihirika bayana katika habari za kuuawa kwa mwalimu inavyojitokeza hapo juu. Ni bayana kwamba Kibukusu kinaweza kutumika katika redio za FM kuwapasha wazungumzaji wake kuhusu matukio yanayotokea katika kaunti ya Bungoma. Baadhi ya matukio hayo ni dhuluma zinazofanyiwa watoto wa kike na kiume pamoja na visa vya uhalifu kama vile mauuaji yanayofanyiwa baadhi ya wakaazi. Kutokana na habari hizo kupeperushwa hewani kwa lugha ya wengi wa wakaazi (Kibukusu), habari hizo ziliweza kuwafikia wazungumzaji wengi wa lugha hiyo. Ufanisi wa habari kuwafikia wazungumzaji wa Kibukusu unadhihirisha nadharia ya Sarufi Amilifu. Hapa tunaona Kibukusu kikiwezesha wazungumzaji wake kuuelewa ulimwengu uliowazunguka (Halliday & Matthiessen, 2004). Hilo linaafikiwa kupitia kwa vipindi vya “Kamakeni” (Habari).

4.1.5 Kibukusu ni Rasilimali kupitia Taarifa za Masuala ya Jamii

Kutokana na masuala ambayo huangaziwa yanayoihusu jamii kwa kutumia Kibukusu, tunaweza kusema kwamba Kibukusu ni rasilimali kwa wazungumzaji wake. Ilibainika kwamba wengi wa wasikilizaji, 89% (N=125) kati ya 140 waliohojiwa katika vituo vyote viwili waliungama kwamba, laiti Kibukusu kisingetumika katika redio za FM kuangazia masuala kama vile maadili, lugha zingine zisingeyafafanua bayana. Mfano ni, usisitizaji wa kuwepo maadili ya heshima kati ya mtu na mkaza mwana wake kutokana na kuwepo imani kwamba watu hao wakisalimiana kwa mkono, “wangechomwa na ukwe.”

Mojawapo ya wahariri waliohusishwa katika utafiti huu alisisitiza kwamba kuna baadhi ya dhana za Kibukusu zisizo na visawe katika Kiswahili. Kwa hivyo, dhana hizo haziwezi kueleweka bayana bila matumizi ya Kibukusu. Kwa mfano, dhana ya *bukhwe khukhwoosia* (ukwe kukuchoma) huweza kuelezwa na kueleweka vizuri zaidi Kibukusu kinapotumika. Na ni Wabukusu tu ndio walio na ufahamu bora kuhusu *bukhwe khukhwosia* (ukwe kukuchoma). Mawazo ya mhariri huyo kuhusu lugha ya Kibukusu kuelezea vyema zaidi baadhi ya masuala yanayoiathiri jamii yalioana na maoni ya Okombo (2014) kuhusu umuhimu wa lugha za kiasili katika kuelezea tamaduni zetu.

Kwa kutumia mhimili wa pili wa nadharia ya Sarufi Amilifu (Halliday & Matthiessen, 2004), tunaona kwamba lugha ya Kibukusu inawawezesha wazungumzaji wake kupata maarifa na kuuelewa zaidi ulimwengu unaowazunguka. Hili liliafikiwa kupitia kwa vipindi kama vile “Kamakeni” (Habari). Kutokana na hali hiyo, Kibukusu kilifaa zaidi kutumika kuangazia masuala hayo. Kwa mfano, itikadi za jamii ya Wabukusu zilieleweka vizuri zaidi Kibukusu kilipotumika. Maoni hayo yanakubaliana na yale ya Kachale (2008) aliyehoji kwamba, mtu huweza kuyaeleza

maoni yake kwa njia bora zaidi anapotumia lugha aliyo na umilisi. Lugha ya umilisi katika muktadha huu ni lugha ya kiasili.

Aidha, ilibainika kwamba kupitia kwa vipindi kama vile “Kamakeni”, wasikilizaji waliweza kupata ufahamu kuhusu masuala ibuka. Wengi wa wasikilizaji wa Sulwe, 97% (N=68) kati ya 70 na 60% (N=42) kati ya 70 wa West FM waliohusishwa katika utafiti huu walihoji kwamba kipindi hicho kiliwafaa sana kwani kilijadilia masuala ibuka yaliyoathiri jamii. Kwa mfano, ongezeko la ukosefu wa usalama katika kaunti ya Bungoma liliweza kuangaziwa katika mojawapo ya vipindi vya “Kamakeni” (Habari). Mfano wa habari hizo ni kile kisa cha mwalimu aliyeuawa na mwili wake kutupwa barabarani katika maeneo ya Naitiri. Baada ya habari kama hizo kuwasilishwa, wasikilizaji walishirikishwa katika mijadala iliyoangazia mambo hayo katika redio hizo. Katika mijadala hiyo, wasikilizaji waliulizwa na watangazaji kutoa maoni yao kuhusu walivyokadiria viwango vya usalama katika kaunti ya Bungoma. Mijadala hiyo ilizua hisia mbalimbali huku wasikilizaji wakitoa mapendekezo yao kuhusu usalama unavyopaswa kuboreshwa.

Mijadala hiyo iliwezesha lugha ya Kibukusu kuingiliana na mazingira halisi ambamo mazungumzo na mijadala hiyo hutokea, mazingira ya jamii husika yanayorejelewa katika nadharia ya Sarufi Amilifu (Halliday & Matthiessen, 2004). Hali hiyo ilioana na mtazamo wa Wanjiku (2009), kwamba, lugha za wenyeji kutumika katika redio na masuala yanayozungumziwa kuhusu jamii zimekuwa na athari ya moja kwa moja katika ukuzaji wa uwezo wa jamii husika.

Ingawa redio zingine zinazotumia lugha rasmi na ya taifa kama vile Kiswahili zilikuwa na mijadala kuhusu masuala ibuka hususan yaliyoathiri taifa kwa jumla, ilibainika kwamba vituo vya redio vya West na Sulwe FM viliegemea zaidi masuala yaliyoathiri jamii za Waluyia na hususan yale ya kaunti ya Bungoma. Matokeo hayo

yanakubaliana na ripoti ya Halmashauri ya Vyombo vya Habari nchini Kenya (MCK, 2012) kwamba sababu kuu ya kusikilizwa zaidi kwa vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili ni asilimia kubwa ya habari (36%) kuwa habari za mashinani na kieneo.

Ingawa mada za mijadala zilihusu sanasana masuala yanayoathiri kaunti ya Bungoma, uteuzi wa mada za mijadala ulitokana na masuala ibuka. Vituo hivyo ndivyo vilivyoamua mada za mijadala kama inavyojitokeza katika nadharia ya Uteuzi wa Ajenda (McCombs & Snow, 1993) kwamba, vyombo vya habari huteua masuala ya kujadiliwa katika vyombo kama vile magazeti runinga na redio. Hata hivyo, kupitia kwa mijadala hiyo, masuala yaliyoathiri wazungumzaji wa Kibukusu yaliweza kuangaziwa.

4.2 Masuala Yanayoangaziwa katika Vipindi vya Uchumi

Kibukusu vilevile kimejitokeza kama rasilimali kinapoangazia masuala ya uchumi kupitia redio za FM zinazotumia lugha za kiasili. Hali hiyo imeweza kudhihirika kupitia kwa masuala yanayoangaziwa katika vipindi mbalimbali vinavyowasilishwa na redio za Sulwe na West FM. Habari hizi zinahusu uchumi wa mtu binafsi, uchumi wa kaunti ya Bungoma, kaunti zinazopakana na Bungoma na kisha nchi ya Kenya kwa jumla.

4.2.1 Uchumi wa Mtu Binafsi

Habari kuhusu uchumi wa mtu binafsi huweza kuwafikia wasikilizaji kupitia kwa vipindi kama vile “Bukusi ne bukulani” (Uuzaji na ununuzi) na “Kamakeni” (Habari). Habari hizi huweza kuwa zinazohusu bei ya mazao na bidhaa za sokoni au mifugo. Kupitia kwa vipindi hivi, wakulima na wafanyibiashara huweza kujua bei ya mazao, bidhaa za sokoni na mifugo katika masoko mbalimbali kwenye kaunti ya Bungoma.

Kwa mfano, kupitia kwa kipindi cha “Bukusi ne bukulani,” mazungumzo yafuatayo yaliweza kurekodiwa:

13.

Kibukusu

Engokho etwaya khu soko ye Kimilili luno eli khekula chisilingi chimia saba, sisonga chimia chirano ne chinywinywi chisilingi chimia chibili. Chikhafu nacho, chiunwa chakhakulikha khusilingi chielefu salasini, che kamabele chielefu salasina tano ne chimosoti chielefu ishirina nane.

Kiswahili

Jogoo leo ameuzwa kwa shilingi mia saba katika soko ya Kimilili, kuku wa kike mia tano na vifaranga shilingi mia mbili. Nao fahali wameuzwa elfu thelathini, ng'ombe wa maziwa elfu thelathini na tano, na wa kike lakini wasio wa maziwa shilingi ishirini na nane.

Hizi ni bei za mifugo mbalimbali katika soko ya Kimilili. Wasikilizaji wanafahamishwa kuhusu bei ya hao mifugo katika soko hiyo. Kwa mfano, wanafahamishwa kwamba, *etwaya elikhekula chisilingi chimia saba* (Jogoo anauzwa shilingi mia saba). Habari kuhusu bei hizi ziliwanufaisha wasikilizaji kwa vile, walipata ufahamu kuhusu bei ya mifugo hao. Kwa kufahamu bei ya mifugo, msikilizaji angeweza kufikia maamuzi bora ambayo yangemwezesha kuboresha uchumi wake alipouza hao mifugo sokoni bila kutapeliwa.

Habari hizi ziliwafaa wakulima waliotaka kuuza mifugo wao sokoni. Ziliwapa fununu ya bei ya mifugo hao hivyo basi kuwaepusha na matapeli ambao huwalaghai. Matapeli hawa waliwatapeli kwa kuwaambia kwamba bei ya mifugo iko chini pale walipotaka kuuza mifugo wao huku wakidai bei ya mifugo imepanda pale waliponua kununua. Kwa hivyo, huku kuwaepusha wakulima dhidi ya wafanyibiashara laghai kuliwasaidia kuinua hali zao za uchumi kwa vile walifaidi na kilimo chao moja kwa moja bila kupoteza pesa kwa wafanyibiashara wa katikati.

Kwa wale ambao walitaka kuboresha hali zao za uchumi kwa kununua kwa mfano ng'ombe wa maziwa, walikwenda sokoni wakiwa na pesa zisizo chini ya elfu thelathini na tano baada ya kusikiliza kipindi hicho cha “Bukusi ne bukulani” (Uuzaji na ununuzi). Kwa mujibu wa kipindi hicho, *chikhafu che kamabele chielefu salasina tano* (ng'ombe wa maziwa anauzwa elfu thelathini na tano). Kwa kununua ng'ombe hao wa maziwa, mtu anaweza kuboresha uchumi wake kwa kuuza sehemu ya maziwa hayo. Kwa kuuza hayo maziwa, mtu huyo angeweza kupata pesa za matumizi hivyo basi kuinua uchumi wake.

Kwa mujibu wa mojawapo wa wakulima waliohojiwa, hapo awali alipunjwa na wachuuzi ama waliompelekea mifugo sokoni kuuza au alioalika kwake nyumbani kununua mifugo alipotaka kuuza. Alihoji kwamba, pale alipotaka kuuza mifugo wake, wachuuzi wangemwambia kwamba bei ya mifugo iko chini. Hata hivyo, alipowauliza watu waliokuwa wamekwenda sokoni siku hiyo, alifahamishwa kwamba bei ya mifugo ilikuwa juu.

Alizidi kusema kwamba, kilikuwa kinaya kwa bei kupanda tu kila alipotaka kununua mifugo lakini alipotaka kuuza, bei hiyo ilishuka chini! Alisema kwamba kutokana na kusikiliza vipindi vya “Bukusi ne bukulani,” (Uuzaji na ununuzi) vinavyowasilishwa na Sulwe na West FM alinufaika kutokana na habari alizopata. Alizidi kusema kuwa alipokwenda sokoni ama kuuza au kununua mifugo, huwa tayari ana fununu ya bei anayostahili ama kuuza au kununua. Alisema vivyo hivyo alipomwita mchuuzi kununua mifugo kwake, alikuwa na fununu ya bei ya mwisho ya kuwauza mifugo hao. Kutokana na habari hizo alizopata kupitia kwa usikilizaji wa vipindi vya redio zinazotumia lugha za kiasili, mkulima huyo huwa hapunjwi alivyokuwa akifanyiwa

pale mbeleni. Akisifia kuzinduliwa kwa matumizi ya lugha za kiasili katika redio za FM anasema:

14.

Kibukusu

Chiredio chefwe chino che Lubukusu ne chikhecha ta napanga siibi! Bachurusi abele bamenya khukhubeya alubeka lwe ebeyi ye bukusi bwe bibiayo. Lelo naona kaakila ndekeresyanga kachilila khu chisoko, emanya bukusi bwe bibiayo ne ekhacha khukula namwe khukusya ta.

Kiswahili

Kabla kuja kwa redio zetu za Kibukusu, nilikuwa nikipata matatizo! Wachuuzi walikuwa wamezoea kunidanganya upande wa bei ya mifugo. Siku hizi nimebahatika kwa vile huwa ninasikiliza yanayoendelea katika soko nikijua ununuzi wa mifugo kabla niende ama kununua au kuuza mifugo hiyo.

Ujumbe unaojitokeza hapa ni, matumizi ya lugha ya Kibukusu katika redio yamewanufaisha wakulima wa kaunti ya Bungoma. Wakulima hawa wamewezeshwa kuwa na ufahamu kuhusu bei ya mifugo na mazao ya mashambani katika masoko mbalimbali. Hali hiyo iliwaepushia dhiki ya kulaghaiwa na wafanyibiashara walaghai, hivyo basi kuboresha hali zao za uchumi.

Mkulima huyu anaelezea manufaa aliyopata kutokana na kuanzishwa kwa vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili anahoji, *ndekeresyanga kachililila khu chisoko, emanya bukusi bwe bibiayo ne ekhacha khukula namwe khukusya ta.* (huwa ninasikiliza yanayoendelea katika soko nikijua ununuzi wa mifugo kabla niende ama kununua au kuuza mifugo hiyo). Ujumbe unaojitokeza hapa kupitia kwa maneno ya msikilizaji huyu ni kwamba yeye husikiliza biashara inavyoendelezwa sokoni huku akipata ufahamu kuhusu bei ya mifugo (ununuzi wa mifugo hao).

Bei hiyo humwezesha kufanya maamuzi yanayofaa kuhusu uuzaji na ununuzi wa mifugo. Kwa hivyo, kuanzishwa kwa vituo hivi vya redio kumekuwa kwa manufaa kwake kwa vile anaungama kwamba, *Chiredio chefwe chino che Lubukusu ne*

chikhecha ta napanga siibi! (Kabla kuja kwa redio zetu za Kibukusu, nilikuwa nikipata matatizo!) Hata hivyo, baada ya vituo hivi kuanzishwa, yeye husikiliza biashara inavyoendelezwa sokoni na kujua bei ya mifugo kabla aende ama kuuza au kuwanunua.

Kutokana na ufahamu huo, mkulima huyo anajiepusha na hasara ambayo angesababishiwa na matapeli ambao ni wafanyibiashara wa kati ya mkulima na mfanyibiashara huyo. Kwa kujiepusha na hasara hizo, tunaweza tukafikia uamuzi wa kusema kwamba uchumi wake kama mtu binafsi umeboreka. Kuboreka huko kunatokana na faida anayoipata. Faida hiyo anayopata bila kupunguzwa na wafanyibiashara wa katikati inatokana na kuanzishwa kwa vituo vya redio vinavyotumia Kibukusu kwa matangazo.

Aidha, ushauri kuhusu kuboresha kilimo chao uligusiwa, hivyo basi kuboresha hali zao za uchumi. Jambo hilo lilitokana na kilimo kuwa ndiyo shughuli ya muhimu zaidi inayotekelezwa na wakaazi wa kaunti ya Bungoma kujipatia riziki. Ushauri huo ulifikiwa kupitia kwa vipindi vilivyowasilishwa na kampuni za dawa za kuuza wadudu kama vile viwavi na kampuni za kutengeneza mbegu mbalimbali za upanzi hususan zilizotengeza mbegu za mahindi.

Habari hizi za muhimu ziliwasilishwa kwa njia ya matangazo maalum na ya biashara. Ushauri wa kilimo bora uliwasilishwa na kampuni za mbegu kwa kuangazia utayarishaji bora wa mashamba, wakati ufaao kwa upanzi na mbegu bora za kupandwa katika sehemu mbalimbali kulingana na angahewa. Ushauri huo ulilenga kuhakikisha wakaazi wanapata mazao bora. Kampuni za dawa za kuuza na kuzuia kuenea kwa wadudu vilevile zilitoa ushauri kwa wakulima kupitia kwa matangazo ya

biashara maalum. Matangazo hayo yaliwasilishwa kwa wakulima kufahamishwa kuhusu aina mbalimbali za dawa za kuangamiza wadudu mbalimbali.

Kwa mujibu wa mojawapo wa wasikilizaji wa vituo hivi vya redio, matangazo hayo yalikuwa ya manufaa kwao. Msikilizaji huyo anaeleza:

15.

Kibukusu

Kamatangasio ke ekampuni ya Syngenta kanjetile lukali po. Esese abele bhiukha khebimalila kamaindi. Lakini enga nenautila kamalesi kamaya ka Actelic Gold khubirira kumuinda kwa West FM, nacha nakakula mala kanjetile lukali. Kamalile bhiukha mumaindi kase. Andi kamakunia kase emia ke kamaindi kosi bufu busa.

Kiswahili

Matangazo ya kampuni ya “Syngenta” yamenisaidia sana. Viwavi walikuwa wananimalizia mahindi yangu. Lakini niliposikia dawa mpya ya “Actelic gold” kupitia kwa redio ya West FM, nilienda nikanunua dawa hiyo na imenisaidia sana. Imewamaliza viwavi katika mahindi yangu. Magunia yangu mia moja ya mahindi yangekuwa unga mtupu.

Mkulima huyu anatumfahamisha kuhusu faida aliyopata kutokana na usikilizaji wa mojawapo ya vituo hivi vya redio (West FM). Anatumfahamisha kwamba kutokana na kusikiliza kituo hicho cha redio, alipata kujua kuhusu dawa ya kuhifadhi mahindi kutoka kampuni ya “Syngenta” anaposema, *kamatangasio ke ekampuni ya Syngenta kanjetile lukali po* (matangazo ya kampuni ya “Syngenta” yamenisaidia sana). Anatumfahamisha kwamba viwavi walikuwa wakimletea hasara kubwa baada ya yeye kuvuna mahindi yake. Viwavi wanapovamia mahindi, huyatafuna na kuyasaga hadi yakawa unga. Mahindi yanapotafunwa hadi kiwango hicho huwa hayawezi kuuzwa kwa vile wanunuzi hutaka mahindi ambayo ni mazuri. Kwa hivyo, viwavi wanapoyavamia mahindi, humletea hasara mkulima kwa vile hawezi akayauza tena. Hali hiyo inapotokea, hali ya uchumi wa mkulima kama huyo hurudi chini.

Hata hivyo, kwa mujibu wa mkulima huyu, aliweza kupata suluhu kutoka kwa kampuni ya “Syngenta.” Anadhihirisha hilo anaposema yafuatayo kuhusu dawa mpya ya kampuni hiyo, *kamalile bhiukha mumaindi kase. Andi kamakunia kase emia ke kamaindi kosi bufu busa* (imewamaliza viwavi katika mahindi yangu. Magunia yangu mia moja ya mahindi yangekuwa unga mtupu). Kwa kuokoa mahindi yake, ameboresha hali yake ya uchumi kwa vile anaweza kuuza baadhi ya hayo mahindi kisha atumie hizo pesa kwa mahitaji yake mengine. Wakati uo huo, kutokana na kuwepo kwa mahindi hayo, hatapunguza pesa zake alizopata kwa njia zingine kwa kununua mahindi kama chakula, kwa hivyo uwezo wake wa uchumi utaboreka kwa vile hizo pesa anaweza kuzitumia kwa mahitaji mengine .

Kwa hivyo, tunaona kwamba habari hizi ni za muhimu kwa mkulima huyu kwa vile, kutokana na usikilizaji kipindi hiki, mkulima huyu alinunua dawa ya “Actelic Gold” ambayo ilimuangamizia viwavi na kuokoa magunia yake mia moja ya mahindi. Kwa kuokoa hayo mahindi, mkulima huyo alikuwa anaboresha uwezo wake wa kiuchumi. Mahindi yaliyookolewa yanapouzwa, pana uwezekano mkubwa wa mkulima huyo kuinua uwezo wake kiuchumi kutokana na hela anazopata.

Kutokana na mifano hiyo, matumizi ya Kibukusu katika redio za FM yanamfaidi msikilizaji kwa upande wa uchumi wa mtu binafsi. Manufaa hayo yalitokana na habari wanazopata wasikilizaji kwa kuvisikiliza vipindi mbalimbali vilivyowasilishwa kwa Kibukusu. Miongoni mwa vipindi hivi vilikuwa ni vile vya biashara (Bukusi ne bukulani), na vile vya matangazo maalum. Licha ya vipindi hivi kuwapa mafundisho wasikilizaji kwa lengo la kuinua hali zao za uchumi kibinafsi, kupitia kwa matangazo ya kampuni mbalimbali, walijifunza kutokana na tajriba za wasikilizaji wengine wa

vituo hivi vya redio. Hatimaye, mafundisho hayo yaliweza kuboresha hali zao za uchumi.

Mafundisho waliyopata wakulima yaliakisi mhimili wa kiutambuzi katika Sarufi Amilifu unaotilia uzito umuhimu wa lugha katika kuwezesha mtu apate maarifa na kuwasiliana kuhusu tajriba yake kuhusu mambo mbalimbali (Halliday & Matthiessen, 2004). Katika muktadha huu, lugha ya Kibukusu ilitumika kuwafahamisha wasikilizaji kuhusu mbinu wanazoweza kutumia kuimarisha kilimo chao.

4.2.2 Uchumi wa Kaunti ya Bungoma

Kupitia kwa vituo vya redio vinavyotumia Kibukusu, wakaazi waliweza kupata habari muhimu kuhusu hali ya uchumi katika kaunti ya Bungoma. Habari hizo ziliweza kupitishwa kupitia kwa vipindi kama vile “Endekhelo”, “Kamakeni” na “Bukusi ne bukulani.” Kwa mfano kupitia kwa mijadala ya “Endekhelo,” kampuni ya kusaga sukari ya Nzoia ilianguzia mikakati inayoifanya ihakikishe kwamba wakulima wa miwa wananufaika na kampuni. Manufaa hayo yangetokana na kampuni kuinua maisha yao kiuchumi hivyo basi kuinua uchumi wa kaunti ya Bungoma kwa jumla.

Baadhi ya mikakati hiyo ni kuwalipa wakulima kwa wakati ili waweze kukeza pesa wanazopata kutokana na malipo hayo. Kampuni hiyo ya sukari inapochelewa kuwalipa wakulima kwa wakati, wakulima hao hulalamika kupitia kwa redio za Sulwe na West FM. Kwa mfano, wakati malipo ya wakulima wa miwa yalipocheleweshwa, malalamishi yafuatayo yalinakiliwa katika kipindi cha “Endekhelo” (Mjadala):

16.

Kibukusu

Efwe balimi be Nzoia sekhehubona bukhala bwe khuraka kimiiba ta ne sikila ekampuni selakhurunganga ta enyuma we khurema kimiiba! Nzoia

seyakhurungile kamapesa kefwе khu miesi sita ta. Sisyuma sye Nzoia esino syakhulerere kumtambo saana ne khubela efwe khweyikina kimiiba kyong'ene. Bona babana benyekhana khucha ebikuli mala sebakhurungile ta. Khokhusaba wanasiasa befwе bengilile akari khubona mbo khwarungilwe chisendi chefwе chili Nzoia.

Kiswahili

Sisi wakulima wa Nzoia hatuoni manufaa ya kupanda miwa kwa vile kampuni imekuwa haitulipi baada ya kukata miwa yetu. Nzoia haijatulipa pesa zetu kwa miezi sita. Hiki kiwanda cha Nzoia kimetuletea umaskini sana kwa vile sisi hutegemea miwa pekee. Ona watoto wetu wanafaa kwenda shuleni ilihali hatujalipwa. Tunaomba wanasiasa wetu waingilie kati na kuona kwamba tumelipwa pesa zetu zilizoko Nzoia.

Huu ni mfano wa malalamishi ya mojawapo wa wakulima wa miwa katika kaunti ya Bungoma. Mkulima huyo anahoji kwamba, yeye na wakulima wenzake hawaoni manufaa ya kupanda miwa kwavile hawajalipwa kwa muda mrefu inavyodhihirika katika maneno yake, *Nzoia seyakhurungile kamapesa kefwе khu miesi sita ta* (*Nzoia haijatulipa pesa zetu kwa miezi sita*). Hii ni licha ya miwa yao kukatwa. Kwa kampuni hiyo kutowalipa wakulima, inarudisha uwezo wa kiuchumi wa wakulima hao chini. Uwezo wa kiuchumi wa wakulima hawa unaporudi chini, unaathiri moja kwa moja uwezo wa kiuchumi wa kaunti ya Bungoma.

Kwa mfano, mkulima huyu anahoji kwamba watoto wao hawaendi shule kwa kukosa karo, tatizo linalotokana na kampuni ya Nzoia kutowalipa madeni yao kama inavyodhihirika katika maneno, *bona babana benyekhana khucha ebikuli mala sebakhurungile ta* (*tazama watoto wetu wanafaa kwenda shuleni ilihali hatujalipwa*).

Watoto wa wakulima hawa wanapokosa kwenda shuleni, hawawezi kupata ajira ambazo zingewawezesha kuboresha hali zao za uchumi. Hali zao za uchumi zinapokosa kuboreka, huathiri kaunti ya Bungoma moja kwa moja. Ni bayana kwamba, iwapo kiwanda kitawalipa wakulima kwa wakati, hali zao za uchumi zitaboreka na wakati uo huo kuboresha hali ya uchumi ya kaunti. Lakini iwapo

kiwanda hakiwalipi wakulima kwa wakati, hali yao ya uchumi itakuwa dhaifu na wakati uo huo kuathiri hali ya uchumi ya kaunti ya Bungoma kwa jumla. Kwa hivyo, kupitia kwa matumizi ya Kibukusu katika redio za FM, uchumi wa kaunti ya Bungoma huweza kuangaziwa kupitia uangaziaji wa hali ya uchumi ya wakulima kama vile wale wa miwa.

Wakulima wameweza vilevile kunufaika na kuanzishwa kwa vituo hivi vya redio ambavyo vimewapa jukwaa la kujadili changamoto zinazowakumba kiuchumi na ambazo vilevile huathiri uchumi wa kaunti ya Bungoma. Juhudi za serikali ya kaunti ya Bungoma kuboresha viwango vya uchumi pia huangaziwa kupitia kwa redio za Sulwe na West FM. Haya huweza kufikiwa kupitia kwa “Kamakeni.” Baadhi ya mikakati ambayo kaunti imetekeleza ili kuinua uchumi wa kaunti ni kurekebisha barabara ambazo zimeharibika kusudi wakulima waweze kufikisha mazao yao sokoni kwa wakati. Wakulima wanapofikisha mazao sokoni kwa wepesi, kaunti pia inapata pesa kupitia kwa ushuru wanaotozwa hao wafanyibiashara. Nayo serikali ya kaunti inapopata huo ushuru, inautumia kuinua uchumi wa kaunti kwa kuweka miundo msingi itakayoboresha biashara. Habari kuhusu maendeleo yanayofanywa na serikali za kaunti katika juhudi za kuinua uchumi wake zimeweza kuwafikia wakaazi kwa upesi zaidi kupitia kwa redio zinazotumia lugha za kiasili kama anavyohoji Castle (2014). Kwa mujibu wa Castle (2014), matumizi ya lugha za kiasili katika vyombo vya habari huwezesha wasikilizaji wengi kupokea ujumbe na kuuelewa kwa urahisi.

Vilevile, kupitia kwa “Kamakeni” wakaazi waliweza kupata habari kuhusu maamuzi yaliyofanywa na serikali ya kaunti ya Bungoma. Maamuzi haya yanaweza kuwa yanayoathiri kaunti kihasi au kichana. Mifano ya maamuzi hayo ni kama vile kaunti iliponunua troli kumi kwa kima cha zaidi ya milioni moja. Vilevile, kaunti

ilisemekana kunuia kununua kiti na kigoda kutumika na gavana wa kaunti ya Bungoma kwa sherehe mbalimbali kwa zaidi ya milioni mbili!

Visa hivyo vilizua malalamishi na mijadala miongoni mwa wakaazi wa Bungoma. Kupitia kwa maoni ambayo wasikilizaji hao hutoa kupitia upigaji simu na utumaji jumbe fupi, wakaazi walilalamikia ubadhirifu wa pesa za kaunti. Ubadhirifu ulioendelezwa na viongozi wa serikali ya kaunti ya Bungoma. Kwa mujibu wa mmoja wa wasikilizaji wa Sulwe, serikali hiyo ya kaunti haikuwa na nia njema kwa wakaazi kwani badala ya kutumia pesa walizopata kutoka kwa serikali kuu na utozaji ushuru kuinua uchumi wa kaunti, walijishughulisha zaidi na ubadhirifu. Alihoji:

17.

Kibukusu

Serikali yefwe ye ekaunti ye Ebungoma eli kherumikhila chisendi chefwe bubu. Patala ye khuchirumikhila khurusyayo bumanani, kheyonaka busa chisendi chefwe! Chiredio chefwe enchino che Lubukusu cha khuyetile khura abuwanga bikholwa bye bukhalukha bibikholekha mukaunti ye Ebungoma.

Kiswahili

Serikali yetu ya kaunti ya Bungoma inatumia pesa zetu vibaya. Badala ya kutumia hizo pesa kuondoa umaskini, wanatumia vibaya pesa zetu. Redio hizi zetu za Kibukusu zimetusaidia kuweka wazi vitendo vya ufisadi vinavyofanyika katika kaunti ya Bungoma.

Ni bayana kwamba msikilizaji huyu hafurahishwi na ubadhirifu unavyoendeshwa katika kaunti ya Bungoma. Anaonyesha kutofurahia pale anaposema, *Serikali yefwe ye ekaunti ye Ebungoma eli kherumikhila chisendi chefwe bubu. Badala ye khuchirumikhila khurusyayo bumanani, khebonaka busa chisendi chefwe!* (Serikali yetu ya kaunti ya Bungoma inatumia pesa zetu vibaya. Badala ya kutumia pesa hizo kuondoa umaskini, wanatumia vibaya pesa zetu). Ubadhirifu huu wa pesa kutoka kwa serikali ya kaunti, unaathiri uchumi wa kaunti ya Bungoma. Badala ya

uchumi wa kaunti kuinuliwa, ama unabaki palepale au unarudi chini. Hii inatokana na matumizi mabaya ya fedha zinazotoka kwa serikali kuu pamoja na zile zinazotokana na ukusanyaji ushuru katika serikali ya kaunti. Hizi pesa za ushuru zinazokusanywa katika kaunti hutolewa na wakaazi. Hiyo ndiyo sababu wakaazi wana haki ya kulalamika pesa zao zinapotumika vibaya.

Kwa mfano, badala ya serikali ya kaunti ya Bungoma kuanzisha mradi ambao utaboresha uchumi wa kaunti, ilitaka kutumia kitita cha milioni mbili kununua meza na kigoda cha kutumika na gavana. Vifaa hivyo vilikuwa vitumike katika sherehe mbalimbali za kaunti! Habari hizo ziliweza kuwafikia wakaazi kwa haraka kupitia kwa redio zinazotumia Kibukusu. Wakaazi walipopokea habari hizo, walizua malalamishi na kuwatia hofu wale waliokuwa na nia ya kufuja pesa zao za serikali ya kaunti. Matokeo ya habari hizi kuwafikia wakaazi kwa haraka inaakisi maoni ya Mohochi (2007). Msomi huyo anasema kwamba, ili kufikia maendeleo, sera na mipango ya serikali katika nyanja za siasa, tamaduni, uchumi, elimu, afya na kadhalika zinapaswa kuwasilishwa kwa lugha watakayoelewa walengwa. Katika muktadha huu walengwa ni wakaazi wa kaunti ya Bungoma na lugha ni Kibukusu.

Bila shaka, matumizi ya Kibukusu katika kuangazia ubadhirifu huu yaliwezesha wakaazi kujua maovu yaliyofanywa katika kaunti ya Bungoma. Maovu haya yalikuwa na athari kwa ukuaji wa uchumi wa kaunti. Kutokana na athari hasi hiyo, wakaazi walijihusisha katika mjadala wa kushutumu maovu hayo. Kutokana na shutuma hizo, kaunti ilisitisha ununuzi wa kiti na kigoda cha gavana kilichokisiwa kuigharimu kaunti zaidi ya milioni mbili.

Ni bayana kwamba matumizi ya Kibukusu katika redio za FM yamewawezesha wasikilizaji kupata ufahamu kuhusu hali ya uchumi wa kaunti ya Bungoma. Hili

lilijitokeza kupitia kwa kipindi cha “Endekhelo” (Mjadala) na “Kamakeni” (Habari). Kupitia kwa vipindi hivyo, wasikilizaji waliweza kupata habari kuhusu ubadhirifu ulioendelezwa katika kaunti na kutoa maoni yao. Kutokana na habari hizi kuwafikia wakaazi kupitia redio za FM, shutuma kuhusu ubadhirifu wa mali ya umma zilitolewa na wakaazi na kusaidia kwa vile serikali ya kaunti iliweza kughairi baadhi ya mipango ya ufujaji wa pesa za serikali ya kaunti kutokana na shutuma za wakaazi. Kwa kurejelea nadharia ya Sarufi Amilifu, (Halliday & Matthiessen, 2004), ni bayana kwamba lugha huwezesha watu kuelewa yale yanayotendeka katika mazingira yao. Katika muktadha huu, matumizi ya Kibukusu katika redio za FM yaliwawezesha wakaazi wa kaunti ya Bungoma kujua maovu yaliyoendelezwa na serikali ya kaunti.

4.2.3 Habari Kuhusu Uchumi wa Kaunti Jirani na Ule wa Kenya

Matumizi ya Kibukusu katika Sulwe na West FM yamewezesha wasikilizaji kujua bei za mavuno katika maeneo mengine ya nchi. Hili liliwezekana kupitia kwa kipindi cha “Bukusi ne bukulani” kama inavyojitokeza katika dondoo hili:

18.

Kibukusu

Likunia lye kamakanda khu soko ya Nakuru likulibwe khusilingi chielefu sita, Eldoret chielefu chirano ne chimia chirano, Kisumu chielefu chirano nechimia saba ne Kakamega chielefu chirano.

Kiswahili

Gunia la maharagwe katika mji wa Nakuru lilinunuliwa kwa shilingi elfu sita, Eldoret elfu tano mia tano, Kisumu elfu tano na mia saba huku Kakamega likiuzwa kwa elfu tano.

Tangazo hilo linaonyesha bei ya mavuno katika masoko mbalimbali nchini Kenya. Bei hizi zinatofautiana kutoka mji au kaunti moja hadi nyingine. Kaunti ambazo bei ilikuwa chini ni zile ambazo uchumi wake ulikuwa chini tukilinganisha na zile za uchumi wa juu. Kwa mfano, tunapotazama bei ya maharagwe katika miji hiyo,

Nakuru iko juu. Tunaambiwa, *likunia lye kamakanda khu soko ya Nakuru likulibwe khu silingi chielefu sita, Eldoret chielefu chirano ne chimia chirano, Kisumu chielefu chirano ne chimia saba ne Kakamega chielefu chirano.* (gunia la maharagwe katika mji wa Nakuru lilinunuliwa kwa shilingi elfu sita, Eldoret elfu tano mia tano, Kisumu elfu tano na mia saba huku Kakamega likiuzwa kwa elfu tano). Mji wa Nakuru una uchumi wa juu ikilinganishwa na miji ya Kisumu na Eldoret kwa vile gharama ya maisha iko juu ukilinganisha na hiyo miji mingine. Kutokana na gharama ya maisha kuwa juu katika mji huo, bei ya vitu kama vile vyakula iko juu vilevile.

Ufahamu kuhusu bei ya mavuno katika maeneo mengi lilikuwa jambo la manufaa hususan kwa wakulima na wafanyibiashara kutoka kaunti ya Bungoma. Habari hizo ziliwawezesha kufikia uamuzi bora kuhusu mahali pa kupeleka mavuno yao kwa lengo la kunufaika zaidi. Habari hizi ni za muhimu kiuchumi kwa vile baada ya wasikilizaji kuzipata, waliweza kukata maamuzi kuhusu mahali pa kupeleka mazao yao lengo la kuyauza. Walipopeleka mazao hayo katika kaunti hizo, walitozwa ushuru katika masoko ya kaunti hizo na kuzifanya zipate pesa ambazo ziliweza kutumika kuboresha miundo msingi katika kaunti hizo.

Suala la uchumi vilevile liliangaziwa kupitia kwa kipindi cha ubadilishaji sarafu. Ubadilishaji sarafu uliangaziwa kupitia kwa “Bukusi ne bukulani” (Uuzaji na ununuzi). Katika kipindi hicho, wasikilizaji walipata habari kuhusu thamani ya shilingi ya Kenya dhidi ya sarafu zingine. Ufuatao ni mfano wa matangazo hayo:

19.

Kibukusu

Chisilingi emia na ishirini cha Kenya chichenjebwe khudola endala ya Amerika, esilingi endala ya Kenya khu chisilingi salasini na tano che Ebuganda ne esilingiendala ya Kenya khu silingi ishirini na tano cha Tanzania.

Kiswahili

Shilingi mia moja za Kenya zilibadilishwa kwa dola moja ya Marekani, shilingi moja ya Kenya ikibadilishwa kwa shilingi thelathini na tano za Uganda huku shilingi moja ya Kenya ikibadilishwa kwa shilingi ishirini na tano za Tanzania.

Katika mfano huu sarafu ya Kenya ilibadilishana na sarafu za nchi zingine kwa viwango mbalimbali. Sarafu hii ilionekana kuwa na thamani dhidi ya sarafu za Tanzania na Uganda ikilinganishwa na dola ya Marekani. Hili linaonekana pale tunapofahamishwa, *chisilingi emia na ishirini cha Kenya chichenjebwe khudola endala ya Amerika, esilingi endala ya Kenya khu chisilingi salasini na tano che Ebuganda ne esilingi endala ya Kenya khu silingi ishirini na tano cha Tanzania.* (shilingi mia moja za Kenya zilibadilishwa kwa dola moja ya Marekani, shilingi moja ya Kenya ikibadilishwa kwa shilingi thelathini na tano za Uganda huku shilingi moja ya Kenya ikibadilishwa kwa shilingi ishirini na tano za Tanzania). Kwa vile uchumi wa Kenya ni bora zaidi ukilinganishwa na wa Tanzania na Uganda, sarafu yake ilikuwa na thamani zaidi ikilinganishwa na nchi jirani zake. Wakati uo huo, uchumi wa Marekani uko juu ukilinganishwa na Wakenya. Hiyo ndiyo sababu ya dola moja ya Marekani kubadilishwa kwa shilingi mia moja na ishirini za Kenya. Mfano huu unaonyesha ubora wa thamani ya shilingi ya Kenya dhidi ya sarafu kadhaa za kigeni. Thamani ya shilingi ya Kenya ikilinganishwa na za nchi zingine ni mojawapo ya vigezo vya kupima uchumi wa nchi.

Kupitia kwa huu ubadilishaji wa sarafu, tunaweza kukisia viwango vya uchumi vya nchi ya Kenya. Habari hizo ziliweza kuwafikia wasikilizaji kupitia kwa vituo vya redio vya lugha za kiasili. Mabadiliko ya thamani ya sarafu ya Kenya hutegemea na kuboreka ama kuzorota kwa uchumi wa nchi. Kwa vile kaunti ya Bungoma inapakana na nchi ya Uganda mpakani Malaba, kwa mujibu wa msikilizaji mmoja aliyehusika

katika utafiti huu, habari hizi zilimwezesha kujua jinsi pesa zilivyobadilishwa mpakani. Alisema:

20.

Kibukusu

Sipindi esyo sinjetanga khumanya enga enja khuchenja chisendi khumupaka. Ne okhmanyile bachenjela esilingi ya Kenya khu chinga che Ebukanda banyalabakhulia.

Kiswahili

Kipindi hicho hunisidia kujua jinsi nitakavyobadilisha pesa mpakani. Kama hujui wanabadilishia pesa ngapi za Kenya kwa za Uganda, huenda wakakulaghai.

Mfanyibiashara huyu anelezea manufaa ya kipindi cha “Bukusi ne bukulani” (Uuzaji na ununuzi), kwamba humpatia mwanga kuhusu jinsi sarafu ya Kenya inavyobadilishana na ya Uganda. Anasema yafuatayo kuhusu kipindi hicho, *sipindi esyo sinjetanga khumanya enga enja khuchenja chisendi khumupaka* (kipindi hicho *hunisidia kujua jinsi nitakavyobadilisha pesa mpakani*). Anatumfahamisha kwamba habari hizo humnufaisha kujua jinsi ambavyo angebadilisha pesa za Kenya kule mpakani. Hili lilikuwa la manufaa kwake kwa vile lilimuepusha na kutapeliwa.

Kuna wakaazi wa kaunti ya Bungoma ambao hufanya biashara ya kununua bidhaa kutoka nchi ya Uganda na kuuza hapa nchini Kenya. Hali hiyo hutokana na bidhaa hizo kuunzwa kwa bei ya chini nchini Uganda ikilinganishwa na Kenya. Kwa wafanyibiashara hawa, habari kuhusu ubadilishaji sarafu zilikuwa za manufaa kwao. Kwa hivyo, kipindi cha “Bukusi ne bukulani” kilichoangazia ubadilishaji sarafu kiliwanufaisha kwa kuwapa mwanga kuhusu ubora wa sarafu ya Kenya. Kwa kupata hizo habari, wafanyibiashara hawa waliweza kukisia natija wanayoweza kupata wanapofanya biashara hiyo. Kutokana na ushuhuda unaotolewa na wakaazi waliohusishwa katika utafiti huu, matumizi ya Kibukusu katika redio za FM

yaliwanufaisha wasikilizaji kwa kuwapa ufahamu kuhusu ubadilishaji wa sarafu ya Kenya dhidi ya sarafu zingine. Kiwango cha ubadilishaji huo kilitegemea uchumi wa nchi ya Kenya.

Ilibainika kwamba vituo vya redio za FM vinavyotumia Kibukusu viliwafahamisha wasikilizaji kuhusu bei za bidhaa hususan mazao ya shambani katika kaunti zingine. Wakati uo huo, vituo hivi viliwafahamisha wasikilizaji kuhusu sarafu ya Kenya inavyobadilishwa na zile za nchi zingine. Habari hizi zilikuwa za muhimu kwa vile zinawasaidia wafanyibiashara kujua thamani ya sarafu ya Kenya kusudi wasipunjwe na wafanyibiashara wa ubadilishaji wa pesa kule mpakani. Kutokana na wasikilizaji kufahamu kuhusu bei ya bidhaa mbalimabali, ufahamu huo unawaweka katika hali njema ya kufanya biashara. Wasikilizaji hawa wanapokuwa na ufahamu kuhusu thamani ya shilingi ya Kenya dhidi ya sarafu zingine, wanakuwa na mpangilio bora wa kuagizia bidhaa kutoka nchi zingine. Ufanisi wa kupata hizi habari za muhimu unatokana na umuhimu wa lugha ya Kibukusu kwa wazungumzaji wake. Umuhimu huu unatokana na lugha hiyo kuwawezesha wazungumzaji wake kupata maarifa na kuyaelewa mazingira yao inavyodhihirika katika Sarufi Amilifu.

4.3 Kibukusu kama Rasilimali Inayoangazia wa Masuala ya Uchumi

Kutokana na mifano, kuanzia ule wa **13** hadi **20**, tunaweza tukasema kwamba Kibukusu kama rasilimali huwezesha wasikilizaji kujiboresha kiuchumi. Wasikilizaji wa vituo hivi vya redio vya Sulwe na West FM wameweza kuboresha hali zao za maisha kiuchumi kupitia kwa vipindi kama vile “Bukusi ne bukulani.” Kupitia kipindi hicho, wasikilizaji wanaotaka kuuza vitu, waliweza kulinganisha bei za bidhaa hizo katika masoko mbalimbali hivi kwamba wanapopeleka bidhaa zao sokoni wasipunjwe na walaghai.

Ilibainika kwamba, wengi wa wasikilizaji, 78% (N=109) kati ya 140 waliohojiwa waliamini kwamba matangazo ya biashara hususan kupitia kwa “Bukusi ne bukulani,” yaliyowasilishwa kwa Kibukusu kupitia kwa redio za FM yaliwafaa sana. Matangazo hayo yaliwawezesha wafanyibiashara na wakulima kufanya biashara zao bila kupunjwa na matapeli ambao hujitokeza kama wafanyibiashara kati yao na soko hususan wakulima. Ili kuhakikisha hawatapeliwi, wakaazi hawa walitumia habari walizopata kupitia kwa redio hizi mbili zilizowasilisha matangazo kwa Kibukusu kufikia maamuzi yaliyowafaa. Kwa hivyo, wenyeji walipata uwezo huo kutokana na wao kupewa nafasi kuyaelewa masuala ya masoko waliyofanyia biashara vizuri zaidi. Waliyaelewa masuala ya masoko hayo kutokana na lugha inayotumiwa ambayo ni Kibukusu. Hali hiyo inakisi maoni ya Miguda-Atyang (2002) anaposema kwamba lugha za kiasili hutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya jamii husika kwa kuwezesha wazungumzaji kuelewa masuala yanayohusu maendeleo vizuri zaidi.

Wakati uo huo, wale waliotaka kununua bidhaa waliweza kwenda sokoni wakiwa na mwanga kuhusu bei ya bidhaa, hivyo basi kujiepusha na walaghai. Walaghai hao hununua bidhaa kutoka kwa wakulima kwa bei ya chini huku wakiwauzia wanunuzi kwa bei ghali. Kinyume na vituo vingine vya redio vinavyotumia Kiswahili, ambavyo hata vinapowafahamisha bei za bidhaa haviangazii zaidi masoko yanayopatikana katika kaunti ya Bungoma, Sulwe FM hujikita zaidi katika masoko yanayopatikana katika maeneo ambapo Kibukusu huzungumzwa, hivyo basi kuwafaidi zaidi wasikilizaji wake.

Ziara za sokoni mara kadhaa baada ya kusikiliza bei hizo redioni, zilidhihirisha kwamba bei zilizotangazwa ndizo zilizotumika sokoni. Ili kuhakikisha wanahabari wa nyanjani wanatoa habari za kweli, mara kwa mara watangazaji waliwaomba hao

wanahabari wa nyanjani kuwaweka hewani ama wafanyi biashara au wanunuzi waliokuwa sokoni ili wazungumze na watangazaji pamoja na wasikilizaji.

4.4 Hitimisho

Sura hii imezungumzia masuala yanayoangaziwa katika vipindi vya jamii katika Sulwe FM na West FM na Kibukusu kama rasilimali katika uangazaji wa masuala ya jamii kwa wasikilizaji wa Sulwe na West FM. Chini ya masuala ya jamii, tumeweza kuzungumzia tamaduni za Wabukusu, maadili katika jamii na uwajibikaji. Vilevile, sura imeangazia masuala yanayoangaziwa katika vipindi vya uchumi katika Sulwe pamoja na West FM ambapo tumeweza kuona uchumi wa mtu binafsi, uchumi wa kaunti ya Bungoma na uchumi wa kaunti zinazopakana na Bungoma na Kenya kwa jumla. Sura inayofuata itajadili kuhusu Kibukusu kama rasilimali katika uangazaji wa masuala ya siasa na afya.

SURA YA TANO

KIBUKUSU KAMA RASILIMALI INAYOANGAZIA MASUALA YA SIASA NA AFYA

5.0. Utangulizi

Kibukusu kama rasilimali inayoangazia masuala ya jamii na uchumi kimezungumziwa katika sura iliyotangulia. Sura hii itaonyesha jinsi Kibukusu kinavyojitokeza kama rasilimali katika uangaziaji masuala ya siasa na afya. Katika masuala ya siasa, vipindi vya siasa za kaunti ya Bungoma, za siasa za kaunti za Trans-Nzoia, Busia, Kakamega na Busia kisha Kenya kwa jumla zimeangaziwa. Vilevile sura inajadili kuhusu afya ya wakaazi wa Bungoma, Trans Nzoia, Busia, Kakamega na hatimaye nchi ya Kenya kwa ujumla.

5.1. Masuala Yanayoangaziwa katika Vipindi vya Siasa

Licha ya masuala ya jamii na uchumi yanayoangaziwa na Kibukusu huku kikijitokeza kama rasilimali kinapoyaangazia, lugha hii imeweza vilevile kuangazia masuala ya siasa kupitia kwa redio za FM zinaizotumia. Hali hiyo inajidhihirisha kupitia kuangaziwa kwa masuala yanayowasilishwa kupitia vipindi mbalimbali vinavyopeperushwa na redio za Sulwe na West FM mathalan:

5.1.1. Vipindi vya Siasa za Kaunti ya Bungoma

Siasa za kaunti huangaziwa kupitia kwa vipindi vya “Kamakeni” (Habari) na “Endekhelo” (Mjadala). Siasa ambazo huangaziwa katika “Kamakeni” zilikuwa hususan za kaunti ya Bungoma. Kinyume cha redio zingine ambazo aghalabu huangazia masuala yanayotokea katika kaunti ya Bungoma siku moja baada ya matukio hayo kutokea, vituo vya Sulwe na West FM viliweka hewani masuala hayo siku iyo hiyo. Hali hiyo ilitokana na vituo hivyo kuwa na wanahabari wa nyanjani kule mashinani hususan katika kaunti ya Bungoma ambao huripoti visa hivyo pindi

vinapotokea. Kwa mujibu wa mojawapo wa washiriki katika utafiti huu, wasikilizaji wanavipenda vituo hivi kwa vile hupeperusha habari kwa wakati. Kwa mfano, msikilizaji huyo anasema:

21.

Kibukusu

Khunyolanga kamakeni ka siasa kakekholekhangha mukaunti ya Bungoma khubirira khu miinda kya Sulwe nende West FM. Anyuma awo abele sonyola kamakeni kenako esiku eng'ene ta, ne aandi hata sekhwanyolanga kamakeni kenako khubirira kimiinda kikyabao ta. Nono kimiinda ekino kyakhuyetile khumanya ka siasa kakekholekha mkaunti mapema.

Kiswahili

Huwa tunapata matukio ya siasa yanayotendeka katika kaunti ya Bungoma kupitia vituo vya redio vya Sulwe na West FM. Hapo awali, hatukuwa tukipata matukio hayo siku yenyewe, na hata saa zingine tulikuwa hatuyapati kupitia kwa redio zilizokuwepo. Kwa hivyo, hizi redio zimetusaidia kujua matukio ya siasa yanayotendeka katika kaunti mapema.

Kwa mujibu wa msikilizaji huyu, kuanzishwa kwa vituo hivi vya redio vinavyotumia Kibukusu, ni kwa manufaa sana kwa wazungumzaji wake. Alisema kwamba vituo hivyo vimewasaidia kupata habari kwa wakati unaofaa. Hili lilidhihirika kupitia kwa maelezo anayotoa kwamba, *khunyolanga kamakeni ka siasa kakekholekhangha mukaunti ya Bungoma khubirirakhu miinda kya Sulwe nende West FM (huwa tunapata matukio ya siasa yanayotendeka katika kaunti ya Bungoma kupitia vituo vya redio vya Sulwe na West FM)*. Ili kusesitiza umuhimu wa wakati ambao wao hupata habari hizo, msikilizaji huyo anahoji, *chiredio echinokhuyetile khumanya kiasiasa chichikholekha mkaunti mapema (hizi redio zimetusaidia kujua matukio ya siasa yanayotendeka katika kaunti mapema)*.

Kupitia kwa dondoo hili, tunafahamishwa kwamba kuanzishwa kwa vituo hivi vinavyotumia Kibukusu kumewanufaisha wazungumzaji wake. Mshiriki katika utafiti huu ambaye amenukuliwa hapo juu anaungama kwamba kabla kuanzishwa kwa vituo hivi vya redio, yeye na wenzake hawakuwa wakipata habari za siasa za kaunti ya

Bungoma siku yenyewe. Anazidi kusema nyakati zingine walikuwa hawazipati kabisa anaposema, *anyuma awo abele sonyola kamakeni kenako esiku eng'ene ta, ne aandi hata sekhwanyolanga kamakeni kenako khubirira kimiinda kikyabao ta (hapo awali, hatukuwa tukipata matukio hayo siku yenyewe, na hata nyakati zingine tulikuwa hatuyapati kupitia kwa redio zilizokuwepo)*. Anatufahamisha kwamba, tangu vituo hivi vya redio vianzishwe, wamekuwa wakipata habari za siasa zilizohusu kaunti ya Bungoma kwa uketo. Hili linadhihirika pale anaposema kwamba kabla kuanzishwa kwa vituo hivyo vya Sulwe na West FM, walikuwa hawapati habari kwa wakati ufaao.

Lile linalobainika hapa ni kwamba, vituo hivi vinavyotumia lugha ya Kibukusu vimewafaidi wasikilizaji wake kwa kuwasilisha masuala yanayoathiri wasikilizaji wake na kuhakikisha kwamba masuala hayo yanawasilishwa kwa wakati. Vituo vya redio za Kiswahili kama vile Citizen, Redio Maisha, Kenya Broadcasting Corporation (KBC) na Milele ziliangazia vilevile masuala ya siasa. Hata hivyo, kinyume na West na Sulwe FM, vituo hivi havikuelezea masuala hayo kwa uketo hususan yaliyohusu kaunti ya Bungoma. Maelezo haya ya kijuujuu yaliyotokea katika redio zilizotumia Kiswahili yalihusu siasa za nchi nzima kwa kifupi. Sulwe na West FM ziliangazia siasa za kaunti zaidi kwa vile hadhira yake kubwa ni ya wasikilizaji wanaozungumza Kibukusu. Kutokana na hali hiyo, vituo hivyo hulenga zaidi kuangazia siasa za maeneo kunakozungumzwa Kibukusu. Msisitizo kuhusu siasa za kaunti vilevile unatokana na 36% ya habari katika vituo hivi kuwa za mashinani na kieneo (MCK, 2012).

Vilevile, kutokana na matumizi ya Kibukusu katika vituo hivi vya redio vya FM, wakaazi wameweza kutathmini utendakazi wa wanasiasa waliowachagua mwaka wa

2013. Kupitia kwa kipindi cha “Endekhelo” (Mjadala), mijadala baina ya wanahabari na viongozi waalikwa iliweza kuendelezwa. Nao wasikilizaji hushiriki katika mijadala hiyo ama kwa kupiga simu au kutuma jumbe fupi kwa kituo cha redio. Kwa mujibu wa Wekesa, mojawapo wa wasikilizaji wa vituo hivi vya redio na ambaye ni mwendesaji wa “bodaboda”:

22.

Kibukusu

Sulwe yakhuyetile lukali khulosia nende wanasiasa befwe ne khubareba kamarebo khulondekhana nende niko bakhulaka kumwaka kwa 2013 enga khwabarobola khucha mubunge. Sulwe yakhuyetile khubanyola, ne kakila khunyala khwabareba kamarebo yakhaba neli muredio. Baaheshimiwa bano enga nekhwamala khwabapila chikura, sebaambikhanga ta. Khusima kumuinda kwa Sulwe khumilimo nikyo kulakholanga khukhulerera babeshimiwa abo khubarebe kamarebo khulondekhana nende ekasi niyo bakhukholele.

Kiswahili

Sulwe imetusaidia sana kuzungumza na wanasiasa wetuna kuwauliza maswali kuhusiana na yale waliyotuahidi mwaka wa 2013 tulipowachagua kwenda bungeni. Sulwe imetusaidia kuwapata kwa vile tunaweza kuwauliza maswali hata kama ni kwa redio. Hawa waheshimiwa tangu tuwapigie kura, huwa hawapatikani. Tunashukuru redio ya Sulwe kwa kazi inayotufanyia kwa kutuletea hao waheshimiwa ili tuwaulize maswali kuhusiana na utendakazi wao.

Bila shaka kupitia kwa maoni ya huyu msikilizaji, redio zinazotumia Kibukusu zimewafaa wasikilizaji kwa kuwawezesha kuzungumzia na kutathmini utendakazi wa wanasiasa baada ya kuwapigia kura. Jambo hilo lilikuwa halifanyiki katika vituo vya redio vinavyopeperusha matangazo kwa Kiingereza na vile vya Kiswahili. Hili linadhihirika pale msikilizaji huyu anaposema, *Sulwe yakhuyetile lukali khulosia nende wanasiasa befwe ne khubareba kamarebo khulondekhana nende ekasi niyo bakhukholele* (Sulwe imetusaidia sana kuzungumza na wanasiasa wetu na kuwauliza maswali kuhusiana na yale waliyotuahidi mwaka wa 2013). Anazidi kusema ya kwamba, *Sulwe yakhuyetile lukali khulosia nende wanasiasa befwe ne khubareba*

kamarebo khulondekhana nende niko bakhulaka kumwaka kwa 2013. (tunashukuru redio ya Sulwe kwa kazi inayotufanyia kwa kutuletea hao waheshimiwa ili tuwaulize maswali kuhusiana na ahadi zao za 2013).

Hili linadhihirisha kwamba vituo hivi vinavyotumia lugha za kiasili vimewanufaisha wasikilizaji kwa kuwawezesha kuwafikia wanasiasa wao. Kutokana na uwezo wa kuwafikia hao wanasiasa japo si kwa macho, wasikilizaji waliweza kuelezea matatizo waliyokumbana nayo kusudi yatatuliwe na hao wanasiasa. Kutokana na mchango unaotolewa na vituo hivi, vinapendwa sana na wasikilizaji hivi kwamba yaliyodhihirishwa katika utafiti huu yaliakisi maoni ya Kamau (2011) anapoviita “rafiki” wa wasikilizaji kwa vile vinawasaidia wasikilizaji kuyatatua baadhi ya matatizo yanayowakumba.

Kupitia kwa kipindi cha “Endekhelo” (Mjadala) ambacho kiliwasilishwa na kituo cha Sulwe kila siku kati ya saa moja unusu na saa tatu za asubuhi; kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa, siasa za kaunti ya Bungoma ziliweza kuangaziwa. Kwa wasikilizaji ambao hukosa kusikiliza hiyo mijadala wakati huo, walifahamishwa kuhusu maudhui ya mijadala hiyo kupitia kwa matangazo ya habari (Kamakeni). Hilo liliwezekana kwa vile vituo hivyo viliandaa baadhi ya habari kutoka kwa mijadala hiyo. Kwa hivyo, matumizi ya Kibukusu katika vituo hivi vya redio yamekuwa rasilimali kwa wanaokizungumza kwa vile huangazia siasa za kaunti ya Bungoma.

Ilibainika kwamba wasikilizaji waliweza kutoa michango yao kwa njia huru kutokana na lugha ya matumizi (Kachale, 2008). Wasikilizaji walihoji kwamba, vituo hivyo viliwawezesha kushiriki katika mijadala na wawakilishi wao katika bunge la kitaifa na kaunti huku wasikilizaji wakipewa nafasi ya kuwahoji. Uwezekano upo kwamba laiti lugha zingine kama vile Kiswahili au Kiingereza zingetumika, wasikilizaji

wasingeshiriki katika mijadala hiyo kikamilifu. Pana uwezekano kwamba kushiriki huko kulitokana na wasikilizaji kuwa na umilisi zaidi katika Kibukusu kama wanavyoashiria Prah (1998) na Muthwii (2002) wanaposema kwamba ni vigumu kuwa na ubunifu katika lugha ambayo mtu hutatizika nayo katika kujieleza.

Matumizi ya Kibukusu katika redio hizi za FM vilevile yalisaidia kuondoa uvumi wa kisiasa ambao wanasiasa wamezoea kueneza. Jambo hilo liliwezekana kutokana na hao wanasiasa kualikwa kwa vituo hivyo ili kuweka paruwanga baadhi ya masuala ambayo yalikuwa ni propaganda. Kwa mfano, wakati mwenyekiti wa chama cha “FORD Kenya,” ambaye ngome yake ni kaunti ya Bungoma alipozindua azimio lake la kuwania kiti cha urais, kulikuwa na migogoro miongoni mwa wabunge wa kaunti ya Bungoma. Baadhi ya wanasiasa, hasa waliokuwa na uhusiano wa karibu na Seneta huyo wa Bungoma walichukua nafasi hiyo kuwaita wenzao wasaliti ambao hawakutaka Seneta huyo awanie kiti hicho cha urais. Hata hivyo, wale waliodaiwa kuwa wasaliti walipoalikwa kutoa misimamo yao katika mojawapo ya vituo hivi vya redio, waliweka wazi mambo. Mmoja wa hao wabunge alihoji:

23.

Kibukusu

Esese sempinga msheshimiwa khukhwenya khuba omuruki we sibala ta. Ese hata naba mlalako khu abo babakampeinila msheshimiwa 2013 khuba Seneta we kauntiyefwe. Esese, msheshimiwa khulosianga lundi hata khwikhalanga naye lukali. Nono ese khulekha khuba Muliro garden esiku ng'eneyo seamaanisa mbo sendinaye ta. Abo baloma bali ese senenya msheshimiwa enga omwana Mubukusu baenja busa political mileage ili babonekhane mbo nibobong'ene babenyela msheshimiwa kamalayi mala bubeyi busa.

Kiswahili

Mimi simpingi msheshimiwa katika azimio lake la kutaka kuwa rais. Mimi nilikuwa kati ya wale waliomtafutia kura msheshimiwa mwaka wa 2013 ili awe Seneta wa kaunti yetu. Mimi huwa ninazungumza na msheshimiwa mara nyingi sana. Hata huwa tunashinda pamoja mara nyingi. Kwa hivyo mimi kukosa kufika Muliro garden hiyo siku, haimaanishi kwamba simuungi mkono. Hao wanaosema kwamba simtaki msheshimiwa kama mtoto wetu wanajitafutia tu

sifa za kisiasa ili waonekane kwamba ni wao pekee wanaomtakia msheshimiwa mazuri ilhali ni uwongo mtupu.

Hapa mwanasiasa huyu anajitetea na kuondoa propaganda za kisiasa ambazo zilikuwepo miongoni mwao. Anaweka mambo paruwanja kwa kuelezea jinsi ambavyo hampingi Seneta wa kaunti inavyosambazwa na wapinzani wake pale anaposema, *esese sempinga msheshimiwa khukhwenya khuba omuruki we sibala ta (mimi simpingi msheshimiwa katika azimio lake la kuwa rais)*. Katika maelezo hayo, mwanasiasa huyu anawafahamisha wasikilizaji kuwa hakuwa na nia yoyote ya kumpinga Seneta huyo kuwania kiti cha urais. Wakati wa mahojiano hayo, wasikilizaji waliweza kupiga simu na kutuma jumbe fupi kwa lengo la kutaka suala hilo liwekwe wazi. Mwanasiasa husika aliweza kujitetea na hatimaye wasikilizaji walitoa misimamo yao anavyodahili Gathigi (2009) kwamba, kupitia kwa vituo vya redio vilivyotumia lugha za kiasili, masuala ya kijamii yaliweza kujadiliwa huku jamii ikitoa maoni yake.

Wapinzani wa viongozi walioko mamlakani na ambao wanataka kuwania viti katika kura kwa chama ambacho ni maarufu katika kaunti hii hutumia njia zote ili wapate uungwaji mkono wa kiongozi wa chama pamoja na wafuasi wa hicho chama. Katika harakati hizo, baadhi yao huchafuliana majina ili waonekane wao ndio wanaofaa kupewa tikiti ya chama wakati wa kura. Wapigaji kura nao huadhibu viongozi wa kisiasa ambao huonekana kumpinga kiongozi wa chama kilicho maarufu katika eneo fulani kwa kutowapigia kura. Hivyo basi, itokeapo kwamba baadhi ya masuala hayajawekwa wazi, huenda baadhi ya wanasiasa wakaadhibiwa bila kosa lolote kwa kutopigiwa kura na wapigaji kura. Huenda uoga huo ndio uliomfanya mwanasiasa huyu kusema, *esese sempinga msheshimiwa khukhwenya khuba omuruki we sibala ta (mimi simpingi msheshimiwa katika azimio lake la kuwa rais)*. Maadamu eneo la

Bungoma linachukuliwa kuwa ngome ya chama cha kisiasa cha FORD Kenya, alihofia kutorudishwa bungeni na wapiga kura kwa kuonekana kumpinga kiongozi wa chama. Kwa hivyo, vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili vilisaidia kuondoa hizo propaganda kupitia kwa mijadala iliyowekwa hewani katika vituo hivyo vya redio.

Ni bayana kuwa vipindi vya siasa zilizojifunga katika kaunti ya Bungoma viliweza kuangaziwa na vituo hivi vya FM. Baadhi ya masuala yaliyoangaziwa ni wanasiasa kutimiza ahadi za siasa za 2013 kwa wapiga kura na kuondoa propaganda za wanasiasa. Propaganda ziliweza kuondolewa kupitia kwa wanasiasa kualikwa katika redio husika kwa lengo la kuulizwa maswali na kubainisha baadhi ya uvumi. Wanasiasa hao waliweza kukomesha uvumi huo kwa kuweka mambo paruwanja pale walipoalikwa katika vituo hivyo vya redio.

Kinachobainika hapa ni kwamba lugha ya Kibukusu ilitumika katika vituo hivi vya redio kudhibiti uhusiano baina ya wapiga kura na wanasiasa. Lugha hiyo vilevile ilitumika kudhibiti uhusiano baina ya wanasiasa wenyewe. Hilo liliwezekana kupitia kwa Sarufi Amilifu (Halliday & Matthiessen, 2004) ambapo lugha hutumika kuanzisha, kudhibiti na kuhifadhi uhusiano kati yetu na watu wengine.

5.1.2. Siasa za Kaunti za Kaunti Jirani na Zile za Kenya

Siasa hizi ziliangaziwa kupitia kwa “Endekhelo” na “Kamakeni.” Siasa hizo ziliweza kuangaziwa kupitia kwa masuala ibuka kama vile mijadala ya kuondolewa kwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC). Upinzani na serikali zilipokuwa zikizozana kuhusu kuondolewa kwa tume hiyo. Baadhi ya wanasiasa kutoka kaunti ya Bungoma walialikwa katika redio ya Sulwe ili kuwafahamisha wasikilizaji sababu kuu walizoona zilichangia wao kusesitiza kwamba lazima tume ya IEBC iondolewe.

Mijadala hiyo vilevile iliwahusisha mawakili wazaliwa wa kaunti ya Bungoma ambao waliwachambulia wasikilizaji katiba ya Kenya ya 2010 kuhusiana na kuondolewa kwa makamishna hao. Kupitia kwa hiyo mijadala, wasikilizaji waliweza kuelimishwa na kuelewa ni kwa nini kulikuwa na mzozo kati ya upinzani na serikali kuhusu kuondolewa kwa makamishina wa Tume ya IEBC. Kwa mujibu wa mzee mmoja ambaye ni mpenzi wa redio ya Sulwe, mijadala hiyo ilimpa mwanga zaidi kuhusu suala la kuondolewa kwa IEBC. Alisema:

24.

Kibukusu

Endekhelo yaelesile kamakhuwa ka IEBC mpaka nekure. Esese abele ndakhilwanga sikila CORD ne bakhaile khukhola maandamano, lakini nakhaelewa sikila.

Kiswahili

Kipindi cha “Endekhelo” kimeelezea masuala ya IEBC hadi “nimeshiba” (nimeridhika). Mimi nimekuwa nikishindwa sababu za CORD kukazania kufanya maandamano, lakini nimeelewa.

Mzee huyu alimaanisha kwamba kupitia kwa kipindi cha “Endekhelo” (Mjadala), ambacho huwasilishwa kwa Kibukusu, aliweza kuelewa sababu za kushutumiwa kwa IEBC. Anasema, *endekhelo yaelesile kamakhuwa ka IEBC mpaka nekure* (kipindi cha “Endekhelo” kimeelezea masuala ya IEBC hadi nimeridhika). Hili lilitokana na maelezo waliyotoa wanasiasa waalikwa na maswali waliyoulizwa na msimamizi pamoja na mwelekezi wa kipindi cha “Endekhelo”. Mzee huyu anadai kuwa aliweza “kushiba” (nekure) kumaanisha aliridhika na maelezo aliyopata. Miongoni mwa jamii ya Wabukusu, mtu anaposema ameshiba na maelezo yako inamaanisha kwamba ameridhika na maelezo uliyompa. Kwa hivyo, kwa mujibu wa msikilizaji huyu, maelezo kuhusu Tume ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) yaliyojadiliwa katika redio

kwa Kibukusu yalimwezesha kufahamu vizuri zaidi kuhusu siasa zilizoizingira tume hiyo hadi akaridhika.

Kipindi cha “Endekhelo,” kilialika wataalamu mbalimbali waliozamia mijadala iliyoshughulikiwa kwa kina. Katika mijadala hiyo, wanahabari na wasikilizaji waliwauliza maswali mbalimbali kuhusiana na hiyo mada ya kuwaondoa Makamishina wa IEBC. Wataalamu hawa walikabiliana na maswali hayo huku wakirejelea vifungu mbalimbali vya katiba ya Kenya. Kufikia mwisho wa mjadala, wasikilizaji walikuwa na ufahamu bora kuhusiana na suala lililojadiliwa.

Hatimaye, kupitia kwa mijadala hiyo, wananchi waliweza kubaini iwapo siasa zilizokuwa zikiendelezwa zilikuwa za kweli au porojo. Anavyohoji Castle (2014), ilibainika kwamba, matumizi ya Kibukusu kuangazia suala la kuondolewa kwa Tume ya IEBC yalifanya suala hilo lieleweke vizuri zaidi. Hilo linadhihirishwa na mshiriki mmoja katika utafiti huu “aliyeshiba” (nekure) na maelezo yaliyotokana na mjadala huo.

Vilevile, kupitia kwa kipindi cha “Kamakeni,” wasikilizaji walipata habari kuhusu matukio ya kisiasa yaliyotendeka nje ya kaunti ya Bungoma. Mifano ya matukio hayo ni, hotuba za kisiasa zilizotolewa na rais wa Jamhuri ya Kenya, naibu wake na viongozi wengine wa kisiasa wakiwemo wale wa upinzani. Kwa mujibu wa msimamizi wa kituo cha Sulwe FM, habari zao za kitaifa zilikuwa sawa na za kituo chao cha redio cha Kiswahili (Redio ya Citizen). Habari za kitaifa za Sulwe kuwa sawa na za Redio ya Citizen ilimaanisha kwamba habari hizo ziliandaliwa kwa meza moja inavyodaiwa na Halmashauri ya Wanahabari ya Kenya (MCK, 2012). Kwa hivyo, kutokana na maandalizi hayo, wasikilizaji wa Sulwe waliweza kupata habari za siasa za kitaifa kwa lugha walioifahamu vizuri zaidi:

25.

Kibukusu

Omulongela we Omuruki we lirambo Omwami abolele Bakenya bosi ali burobosi bwe sisiyama siya sya Jubilee bucha khuba bwe bulekhule ne lundi bwe abuwanga. Asayile Bakenya boosi khukhwituba mu sisiyama sya Jubilee nebarusyeo bubwabukhana akari we Bakenya

Kiswahili

Naibu wa Rais wa Kenya amewaambia Wakenya wote kwamba uchaguzi katika chama kipya cha Jubilee utakuwa wa uhuru na uwazi. Aliwaomba Wakenya wote kujiunga na chama cha Jubilee ili waondoe tofauti zilizopo miongoni mwa Wakenya.

Tangazo hili la Naibu wa Rais, ni mfano wa siasa za kitaifa ambazo ziliangaziwa na vituo hivi vya redio vilivyopeperusha matangazo kwa lugha ya Kibukusu. Ujumbe huu haukuwacha nje wakaazi wa Bungoma pale inaposemekana, *Omulongela we Omuruki we lirambo abolele Bakenya bosi ali burobosi bwe sisiyama siya sya Jubilee bucha khuba bwe bulekhule ne lundi bwe abuwanga* (Naibu wa Rais wa Kenya, amewaambia Wakenya wote kwamba uchaguzi katika chama kipya cha Jubilee utakuwa wa uhuru na uwazi). Ujumbe unaojitokeza hapa ni kwamba hakutakuwa na upendeleo wa aina yoyote katika uchaguzi wa wagombezi katika chama cha Jubilee. Lengo la tangazo hilo lilikuwa ni kuondoa hofu miongoni mwa wanachama. Baadhi ya wanachama waliotaka kugombea viti kwa kutumia tikiti ya Jubilee walikuwa na hofu kwamba huenda wapinzani wao wanaojipendeleza kwa viongozi wa chama wateuliwe kwa njia zisizo za halali.

Ili kusisitiza umuhimu wa kutotenganishwa kwa misingi ya siasa, Naibu wa Rais anawashauri Wakenya kujiunga na chama kimoja pale anaposisitiza, *Bakenya boosi khukhwituba mu sisiyama sya Jubilee nebarusyeo bubwaukhana akari we Bakenya* (Wakenya wote kujiunga na chama cha Jubilee ili waondoe tofauti zilizopo miongoni mwa Wakenya). Kwa mujibu wa dondoo hili, Naibu wa Rais aliamini kwamba kwa

Wakenya kuwa katika chama kimoja cha kisiasa, tofauti za kikabila hazingekuwepo. Hii ndiyo maana anahoji kwamba kwa kujiunga na chama kipya cha Jubilee, tofauti zilizopo miongoni mwa Wakenya hazitakuwepo. Hata hivyo, hilo ni suala la mjadala kwa vile hata watu wakiwa katika chama kimoja pana uwezekano wa kutofautiana kimawazo.

Kutokana na mifano hiyo, tunaona kwamba matumizi ya Kibukusu katika redio yaliwawezesha wasikilizaji kupata habari kuhusu siasa za nchi nzima. Matokeo ya matumizi ya lugha hiyo katika vituo hivi vya redio ni, wasikilizaji kuweza kufafanuliwa baadhi ya masuala ambayo hawakuwa wakiyaelewa hivi kwamba ufahamu wao kuhusu masuala haya uliimarishwa. Mfano wa masuala haya ni wakati ambapo upinzani ulikuwa ukifanya maandamano kuhusiana na Tume Huru ya Mipaka na Uchaguzi (IEBC) kuondolewa. Wakati uo huo, tumeona masuala ya siasa za kitaifa yakiangaziwa kupitia kwa hotuba ya Naibu wa Rais wa Kenya.

Kinachobainika hapa ni kwamba, masuala ya kisiasa yanayojitokeza nchini Kenya yalieleweka vyema zaidi kwa wazungumzaji wa Kibukusu lugha hiyo inapotumika. Kibukusu kinapotekeleza jukumu la kuwawezesha wazungumzaji kuelewa kinachozungumziwa, kinaakisi nadharia ya Sarufi Amilifu kuhusu umuhimu wa lugha katika kuwezesha watu kupata maarifa. Kwa mujibu wa Sarufi Amilifu (Halliday & Matthiessen, 2004), licha ya kupata maarifa, lugha hutuwezesha kuuelewa ulimwengu unaotuzunguka. Katika muktadha huu, ulimwengu unaozunguka wazungumzaji wa Kibukusu ni siasa za nchi. Kwa hivyo, Kibukusu kinawawezesha wazungumzaji kuelewa siasa za nchi.

5.2. Kibukusu kama Rasilimali Inayoangazia Masuala ya Siasa

Kutokana na mifano inayojitokeza katika dondoo la **24** na **25**, tunaweza kusema kwamba Kibukusu ni rasilimali katika uangazaji wa masuala ya siasa kwa wasikilizaji wa Sulwe na West FM. Kupitia kwa Kibukusu, wasikilizaji hupata habari kuhusu siasa za kaunti ya Bungoma na kaunti zingine kwa kina hususan kupitia kwa redio ya Sulwe FM. Kwa mfano, wanasiasa mbalimbali wa kaunti ya Bungoma waliweza kualikwa katika Sulwe FM na kujadilia kwa kina kuhusu siasa za uliokuwa hapo awali mkoa wa magharibi kwa jumla na kaunti ya Trans Nzoia.

Ilibainika kwamba kutokana na msisitizo na muda uliotengewa siasa za kaunti ya Bungoma, Kibukusu kilijitokeza kama rasilimali kwa wasikilizaji wake. Wasikilizaji waliweza kuchangia sana kwa njia huru ama kwa kutoa maoni au kuuliza maswali katika mijadala hiyo ya kisiasa kupitia kwa simu zao za mkono. Kwa mujibu wa wasikilizaji waliotoa data kwa kutumia hojaji, hawakuwa na tatizo lolote la kutoa michango yao katika mijadala kwa vile lugha iliyotumika ilikuwa lugha yao ya kwanza amabayo walikuwa na umilisi nayo anavyohoji Kachale (2008).

Huku kushiriki kikamilifu kulioana na msimamo wa Muthwii (2002), aliyehoji kwamba vituo vya redio za kiasili vimeongeza nafasi kwa wakaazi wa mshambani kujieleza na kutatua matatizo yao kutokana na wao kuwa na umilisi zaidi katika lugha hizo. Ilibainika kwamba matumizi ya Kibukusu katika redio za FM yaliyojitokeza kama rasilimali kwa wazungumzaji wa lugha hiyo. Kwa mujibu wa wasikilizaji wengi, 80% (N=113) kati ya 140 waliohojiwa, Kibukusu kilifaa zaidi ingawa lugha kama Kiswahili iliweza vilevile kutumika kuangazia masuala ya siasa. Aidha, redio zilizotumia Kiswahili ziliegemea zaidi siasa za nchi nzima huku muda uliotengewa siasa za kaunti ya Bungoma ukiwa mfupi. Kutokana na hali hiyo, wakaazi walinufaika zaidi Kibukusu kilipotumika kuangazia masuala hayo.

Kwa hivyo, wasikilizaji walichangamkia zaidi matumizi ya Kibukusu katika redio za FM. Wasikilizaji walikuwa huru zaidi kuchangia mijadala hiyo ya siasa kwa vile hiyo ndiyo lugha waliyokuwa na umilisi zaidi nayo. Hilo lilioana na maoni ya Muthwii (2002), asemapo kwamba redio za lugha za kiasili zimeongeza nafasi kwa wakaazi wa mashambani kujieleza na kutatua matatizo yao kutokana na umilisi wao katika lugha za kiasili.

Kituo cha West FM kilitenga muda mrefu zaidi kuangazia siasa za uliokuwa mkoa wa magharibi kwa jumla kupitia kipindi cha “Crossfire”. Hata hivyo, kipindi hicho kiliwasilishwa kwa Kiswahili. Kipindi cha “Crossfire” kilipeperushwa hewani mara moja tu kwa juma, siku ya Jumapili. 68% (N=95) kati ya 140 ya wasikilizaji wa vituo vyote (Sulwe na West FM) walidai kwamba walinufaika zaidi na vipindi vilivyowasilishwa kwa Kibukusu. Walisema kwamba, kwa juma moja, masuala ya siasa yaliangaziwa mara nyingi kutegemea na yalivyotokea kama masuala ibuka na yalivyoratibiwa na waratibu wa vipindi.

Ilibainika vilevile kwamba, wanasiasa walitegemea sana vituo hivi kuwafikia wananchi walioko mashinani kutokana na matumizi ya Kibukusu. Hili lilidhihirika kutokana na himizo lililotolewa na baadhi ya hao wanasiasa ambao waliwasihi wasikilizaji kusikiza zaidi redio za Sulwe na West FM:

26.

Kibukusu

Efwe khusima kimiinda kyefwe kya Sulwe nende West FM khubamanyisya babandu befwe kachililia mukaunti yefwe. Khusaba bamenywa be Ebungoma nende Trans Nzoia khuli barekelesye kimiinda ekino nyo banyole bubweyangu bwe khumanya kachililia mukaunti chefwe.

Kiswahili

Tunashukuru vituo vyetu vya redio vya Sulwe na West FM kwa kuwafahamisha watu wetu kuhusu yanayoendelea katika kaunti yetu. Tunawaomba wakaazi wa Bungoma na Trans Nzoia wasikilize hizi redio ili wapate nafasi ya kujua yanayoendelea katika kaunti zetu

Katika dondoo hili, mwanasiasa huyu anasifia vituo vya redio vya Sulwe na West FM kwa kazi nzuri zinayofanya ya kuwafahamisha wasikilizaji kuhusu yanayoendelea katika kaunti yao. Hatimaye anawahimiza wakaazi kusikiliza vituo hivyo pale anaposema, ***Khusaba bamenywa be Ebungoma nende Trans Nzoia khuli barekelesye kimiinda ekino*** (Tunawaomba wakaazi wa Bungoma na Trans Nzoia wasikilize hizi radio). Kwa kuwahimiza wasikilizaji kusikiliza vituo hivi vya redio, mwanasiasa huyo alionyesha kwamba walivitegemea vituo hivyo kuwafikia wakaazi.

Maelezo haya yanadhihirisha kwamba vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili husaidia wazungumzaji kuelewa yanayotendeka katika kaunti zao. Katika mfano huu, Kibukusu kina manufaa kwa wazungumzaji walioko katika kaunti ya Bungoma.

5.3. Masuala Yanayoangaziwa katika Vipindi vya Afya

Kibukusu vilevile kimeangazia masuala ya afya kupitia redio za FM zinazokitumia. Masuala ya afya yameangaziwa katika vipengele vifuatavyo: afya kwa wakaazi wa kaunti ya Bungoma, afya kwa kaunti zinazopakana na Bungoma na afya ya nchi ya Kenya kwa jumla. Hilo lilijitokeza kupitia kwa masuala yanayoangaziwa katika vipindi mbalimbali vinavyowasilishwa na redio za Sulwe na West FM.

5.3.1. Masuala ya Afya kwa Wakaazi wa Kaunti ya Bungoma

Vituo hivi vya redio viliangazia masuala ya afya ya wakaazi wa Bungoma kupitia kwa habari mbalimbali. Miongoni mwa habari ambazo ziliwasilishwa ni, magonjwa mbalimbali ambayo huathiri wakaazi endapo hawazingatii usafi wa mwili na mazingira. Kwa mfano, kupitia kwa kipindi cha “Kamakeni,” wakaazi walishauriwa

kuzingatia usafi kwa kunywa maji ambayo ama yametibiwa au kuchemshwa kunapokuwa na mvua nyingi katika kaunti ya Bungoma. Ushauri huo ulitokana na visa vingi vya magonjwa ya kuhara kuripotiwa msimu wa mvua nyingi. Ufuatao ni mfano uliorekodiwa katika mojawapo ya vituo hivi vya redio:

27.

Kibukusu

*Omwimelesi we busilikhi mwikangilo lye Webuye abasaya bamenywa be ekaunti ye Ebungoma ali **khulondekhana ne buluale bwe khunyalala chimbeka echo, bahakikisye bali bakhasya kamechi kabwe ke khunywa.** Lundi abasayile ali basingenge kamatunda nebakhakalia ta, ne chinyenyi ne bakhatekha ta.*

Kiswahili

*Msimamizi wa hospitali ya Webuye anawaomba wakaazi wa kaunti ya Bungoma kwamba **kutokana na mkurupuko wa maradhi ya kuhara maeneo hayo, wahakikishe kwamba wanachemsha maji yao ya kunywa.** Vilevile, anawaomba wawe wakiosha matunda kabla ya kuyala, na mboga kabla ya kupika.*

Tangazo hilo ingawa lilitolewa na daktari msimamizi wa hospitali ya Webuye, linatolewa kwa wakaazi wote wa kaunti ya Bungoma. Tunapata kufahamu kutokana na tangazo hilo kwamba kumezuka ugonjwa wa kuhara katika maeneo ya Webuye anaposema, **khulondekhana ne buluale bwe khunyalala chimbeka echo, bahakikisye bali bakhasya kamechi kabwe ke khunywa** (kutokana na mkurupuko wa maradhi ya kuhara maeneo hayo, wahakikishe kwamba wanachemsha maji yao ya kunywa). Kwa kuchemsha maji yao ya kunywa, wakaazi wangejjepusha na magonjwa hayo ya kuhara ambayo hutokana na kutozingatia usafi wa vyakula vinavyoliwa na vinywaji kama vile maji.

Kutokana na tangazo hilo, wakaazi wa kaunti ya Bungoma ambao hawakuwa wakitilia maanani usafi wa maji waliyokuwa wakinywa walitarajiwa kuchukua tahadhari kusudi wasishikwe na magonjwa yanayotokana na matumizi ya maji chafu.

Wasikilizaji wanapochukua tahadhari hiyo, wanazilinda afya zao. Kutokana na tangazo hilo kuwekwa katika vyombo vya habari, wasikilizaji wengi waliweza kufikiwa. Anavyohoji Mohochi (2007), mawasiliano ya vyombo vya habari “hututembeza” kwingi na kutupatia habari za siasa, dini na elimu habari hizo ziliweza kuwafikia watu wengi. Kwa wale ambao hawakuwa karibu kusikiliza habari hizo, waliweza kuzisikia kupitia kwa wenzao.

Kuhusiana na vifaa vya matibabu, kupitia kwa redio zinazotumia Kibukusu, serikali ya kaunti ya Bungoma iliweza kuwafahamisha wakaazi kuhusu zahanati na hosipitali ambazo zimenunuliwa vifaa na serikali ya kaunti. Wakaazi walifahamishwa kuhusu juhudi za serikali ya kaunti kuboresha vifaa vya matibabu. Hilo liliweza kufikiwa kupitia kwa kipindi cha “Kamakeni” (Habari) na kile cha “Endekhelo” (Mjadala). Kwa mfano, katika mojawapo ya taarifa za habari hizo kulidondolewa yafuatayo:

28.

Kibukusu

Serikali ye ekaunti ye Ebungoma yakulile kamakangilo koosi ke mukaunti chiambulensi che khumema baluale. Gavana we kaunti ye Ebungoma aanile chiambulesi echo luno nealoma ali chicha khuyeta khutimisya baluale mumakangilo kamabofu ne lilimo Iya Moi Referral.

Kiswahili

Serikali ya kaunti ya Bungoma imenunulia hospitali zote katika kaunti magari yakubebea wagonjwa. Gavana wa kaunti ya Bungoma alitoa magari hayo leo na kusema yatasaidia kupeleka wagonjwa kwa hospitali ambazo ni kubwa ikiwemo ile ya Rufaa ya Moi.

Kupitia kwa kipindi cha habari (kamakeni), wakaazi walifahamishwa kwamba magari ya kubebea wagonjwa yalikuwa yamenunuliwa kwa hospitali zote za kaunti ya Bungoma. Tunaambiwa katika habari hizo kwamba, *serikali ye ekaunti ye Ebungoma yakulile kamakangilo koosi ke mukaunti chiambulensi che khumema baluale* (Serikali ya kaunti ya Bungoma imenunulia hospitali zote katika kaunti

magari yakubebea wagonjwa). Hili lilitokeleza na serikali ya kaunti hiyo kama mojawapo ya mikakati ya kuwapa wakaazi huduma bora za afya. Hilo liliweza kufahamishwa wakaazi wa kaunti wakati wa uzinduzi wa magari hayo uliofanywa na gavana. Habari hizi ni za muhimu kwa afya ya wakaazi wa Bungoma kwa vile usafirishaji wa wagonjwa uliweza kurahisishwa. Wagonjwa waliokuwa katika hali mbaya waliweza kusafirishwa kutoka katika vituo vidogo vya afya na kufikishwa kwa hospitali kuu ya Webuye, Bungoma na hata ya Rufaa ya Moi, mjini Eldoret kwa haraka hivyo basi kuokoa maisha ya hao wagonjwa.

Kilichobainika hapa ni kwamba, wengi wa wakaazi walikuwa wakiyapoteza maisha yao kutokana na ukosefu wa magari ya kuwasafirisha haraka kwenye hospitali zingine zilizo na vifaa kama vile vya upasuaji . Walioathirika zaidi ni wale waliokuwa wakitafuta matibabu katika zahanati mbalimbali katika kaunti ya Bungoma. Kuzinduliwa kwa magari haya ya kuwasafirisha wagonjwa, kulitarajiwa kupunguza visa vya wagonjwa waliopoteza maisha yao ama kwa kukosa huduma bora zaidi za matibabu au kucheleweshwa kusafirishwa na kufikishwa kwa hospitali zilizokuwa na vifaa bora zaidi, hususan waliotolewa kwa zahanati za kaunti ndogo mbalimbali.

Vilevile, kupitia kwa kipindi cha “Endekhelo,” mijadala huwepo kuhusu matatizo yanayowakumba wakaazi kwa upande wa kupata afya bora. Matatizo hayo hutokana na upungufu wa vifaa vya afya. Mijadala hii ilihusisha maafisa wa wizara ya afya katika serikali ya kaunti ya Bungoma na waandalizi wa vipindi. Katika mijadala hiyo, wasikilizaji huweza kuuliza hao maafisa waalikwa maswali na kujibiwa. Ufuatao ni mfano wa malamishi kuhusu matatizo yaliyowakumba wakaazi katika baadhi ya zahanati hizo na yakajitokeza katika mojawapo ya mijadala hiyo:

29.

Kibukusu

Efwe khusaba serikali ye ekaunti ye Ebungoma khuli ekule kamalesi mumakangilo koosi. Badala ye khukula chiambulensi, andi bakhakulile kamalesi ne kakila balwale bakalikhebaumia khubela khutakha kamalesi. Chiambulensi chili che khumema balwale batiti bakhililwe lakini kamalesi kayeta buli omulwale.

Kiswahili

Sisi tunaomba serikali ya kaunti ya Bungoma ya kwamba inunulie hospitali zote dawa. Badala ya kununua magari ya kubebea wagonjwa, wangetunulia dawa kwa vile wagonjwa wengi wanaumia kutokana na ukosefu wa dawa. Magari ya kubebea wagonjwa yanawafaa wagonjwa wachache waliolemewa lakini dawa zinafaidi kila mgonjwa.

Mjadala huu uliweza kuandaliwa na mojawapo ya vituo vya redio vinavyotumia lugha ya Kibukusu baada ya kuzinduliwa kwa magari ya kuwabebea wagonjwa katika kaunti ya Bungoma. Lililobainika katika mjadala huo ni kwamba, ingawa serikali ya kaunti ilikuwa imejaribu kuwatatulia wagonjwa tatizo la kutafuta matibabu zaidi kwa kuwanunulia vifaa vya kuwasafirisha, wakaazi walikuwa na tatizo lililoonekana kuwa kubwa zaidi na ambalo lilikuwa ni ukosefu wa dawa.

Kwa mujibu wa dondoo hilo, msikilizaji huyo anasema kwamba serikali ya kaunti ilipaswa kulipa kipaumbele tatizo la dawa.. Kulingana na msikilizaji huyo, ingawa serikali ya kaunti ilikuwa imewanunulia magari ya kubeba wagonjwa, kipaumbele kilipaswa kuwa ununuzi wa dawa. Hii ni kwa vile magari hayo hayangewafaidi wagonjwa wote isipokuwa wale waliohitaji kuhamishiwa hospitali zingine. Kwa hivyo, hata kama serikali ya kaunti ilikuwa imeangazia suala la afya ya wakaazi kwa kuyanunua hayo magari, palikuwa na haja ya dharura zaidi ya kununua dawa kwa hospitali maadamu matibabu ni kati ya huduma zilizogatuliwa.

Matumizi ya Kibukusu katika redio hizi yamewanufaisha wasikilizaji kwa upande wa afya kwa vile, wameweza kupata habari kuhusu vifaa vya afya vinavyopatikana katika

zahanati mbalimbali katika kaunti ya Bungoma. Wakati uo huo, wasikilizaji wameweza kuifahamisha serikali ya kaunti kuhusu matatizo wanayokumbana nayo wanapotafuta huduma za afya. Hilo limewezekana kupitia kwa mijadala ambayo huandaliwa na vituo hivi vya redio.

Kutokana na mifano ambayo imeangaziwa, ni bayana kwamba magonjwa mbalimbali yanaweza yakaathiri wakaazi endapo hawazingatii usafi wa mwili na mazingira kama inavyojitokeza katika “Kamakeni” (Habari). Tumeona afya ya wakaazi ikizungumziwa kupitia kwa matangazo yanayowasilishwa kwa wakaazi kupitia kwa redio za FM zinazotumia Kibukusu. Juhudi za serikali ya kaunti kuboresha vifaa vya matibabu kupitia kwa ununuzi wa vifaa vya matibabu vilevile zimezungumziwa katika sehemu hii kupitia kwa kipindi cha “Endekhelo”. Mambo haya yote yameweza kufikiwa kupitia matumizi ya Kibukusu katika redio za FM.

Vilevile, habari kuhusu kuzuka kwa magonjwa na juhudi za serikali ya kaunti ya Bungoma kuboresha afya ya wakaazi ziliwafikia kupitia kwa Kibukusu. Ufanisi huu wote wa mawasiliano unatokana na matumizi ya Kibukusu na kuthibitisha nadharia ya Sarufi Amilifu. Sarufi Amilifu inahoji kwamba, lugha huwawezesha watu kupata maarifa na kuelewa ulimwengu unaowazunguka (Halliday & Matthiessen, 2004).

5.3.2. Masuala ya Afya ya Wakaazi wa Kaunti Jirani

Kaunti jirani zilizo karibu na Bungoma ni: TransNzoia, Busia, Kakamega na Vihiga. Tatu kati ya kaunti hizo ni uliokuwa mkoa wa magharibi kabla kutekelezwa kwa ugatuzi. Ni kaunti ya TransNzoia tu ndiyo iliyokuwa katika mkoa wa bonde la ufa kabla ugatuzi. Pana uwezekano wa yale yanayotendeka katika kaunti hizo kuathiri wakaazi wa Bungoma.

Masuala ya afya katika kaunti jirani huangaziwa kupitia vituo hivi vya redio. Mfano ni ushauri kuhusu matibabu yanayofanywa na ama wizara ya afya au mashirika ya afya yasiyo ya kiserikali ambayo huwasilishwa kupitia kwa matangazo maalum yanayofadhiliwa na serikali kuu. Mfano wa magonjwa haya ni ugonjwa wa saratani za aina mbalimbali na mahali pa kupata matibabu.

Hili sanasana husikika katika matangazo maalumu siku za kuadhimisha magonjwa hayo. Wakati uo huo, huweza kutokana na matangazo ya serikali za kaunti kwa wakaazi kupitia kwa vyombo vya habari. Kwa hivyo, kupitia kwa matumizi ya Kibukusu katika redio za FM, wasikilizaji wameweza kupata ufahamu kuhusu magonjwa mbalimbali. Wakati uo huo wasikilizaji wamepata kujua juhudi zinazofanywa na serikali za kaunti hizo ili kuyadhibiti kama inavyojitokeza katika mfano huu:

30.

Kibukusu

*Omwimelesi we busilikhi mukaunti ya Trans Nzoia **abasayile babandu be sikhaye ali, bapimenge kamaturu kabwe buli khase** enga engila endala ya khupungusia kamalwale ka **kansa ye kamaturu ebonekhana khutasa mu bandu be sikhaye chimbeka echo**. Apile kumulasi okwo ne ali chimbeka che Saboti mwisiikha lyo omumenywa mulala niye bayabile chimbekaecho. Alomile ali bulwale obwo ne bunyolekha mapema, bunyala bwasilikhwa.*

Kiswahili

*Msimamizi wa matibabu katika kaunti ya Trans Nzoia **amewasihi akina mama kwamba wawe wakipima kila wakati matiti yao** kama njia mojawapo za kupunguza saratani ya **matiti ambayo inaonekana kuongezeka miongoni mwa wanawake maeneo hayo**. Alitoa ushauri huo akiwa maeneo ya Saboti katika mazishi ya mojawapo wa wakaazi wa huko. Alisema kwamba ugonjwa huo unapogunduliwa mapema, huweza kutibiwa.*

Tangazo hili lilihusu umuhimu wa wakaazi kujua hali zao za afya. Tangazo hilo linatolewa na afisa wa afya katika kaunti hiyo ya Trans Nzoia akiwa katika hafla ya mazishi. Habari hizi ni za muhimu kwa wakaazi hao hususan wa kike kwa vile

wanapata ufahamu kwamba ugonjwa wa saratani umeongezeka katika kaunti yao na ni vyema kwao kuchukua tahadhari ya mapema. Hili linajitokeza pale afisa huyo anaposema, *abasayile babandu be sikhaye ali, bapimenge kamaturu kabwe buli khase enga engila endala ya khupungusia kamalwale ka kansa ye kamaturu (aliwasihi akina mama wawe wakipima matiti yao kila wakati kama njia mojawapo za kupunguza saratani ya matiti)*. Ili kuonyesha umuhimu wa wakaazi wa kike kwenda kupimwa mara kwa mara, afisa huyu anasema, *kansa eyo ebonekhana khutasa mu bandu be sikhaye chibeka echo (kansa hiyo inaonekana kuongezeka miongoni mwa wanawake maeneo hayo)*.

Habari hizi ni muhimu kwa wakaazi na zinasisitizwa wakati wa matanga ya mojawapo wa wakaazi aliyekuwa amefariki kutokana na ugonjwa huo wa saratani. Pia aliwafahamisha wakaazi hao ya kwamba ugonjwa wa saratani unaweza ukatibiwa iwapo utagunduliwa mapema. Habari hizi zinasaidia kuondoa imani potofu miongoni mwa baadhi ya wasikilizaji ambao huchukulia kwamba mtu anapougua ugonjwa wowote usiotibiwa, huwa amerogwa.

Aidha, tahadhari kuhusu mkurupuko wa magonjwa kama vile yale ya kipindupindu huweza kutolewa kwa wasikilizaji kupitia kwa matangazo maalum ambayo huwa yametolewa na wizara ya afya. Matangazo haya sanasana hufadhiliwa na wizara ya afya katika serikali kuu. Huwa yanalenga kuwaonya wasikilizaji kuhusu magonjwa hatari kama inavyojitokeza katika mfano huu:

31.

Kibukusu

Bubwimelesi bwe busilikhi mwirambo, bubolela bamenywa be kaunti ya Busia buli khulondekhana nende bulwale bwe khuyara buli mukaunti eyo, bakhakusia byakhulya khumianda ta. Balikhebasaya bamenywa khukhasia kamechi kabwe ke khunywa enga engila endala ye khulekha khunyola

bulwale obwo. *Bamenywa lundi basaywa khuenja busilikhi ao ne babona dalili che khuyara.*

Kiswahili

*Wizara ya afya ya serikali ya kitaifa inawafahamisha wakaazi wa kaunti ya Busia ya kwamba, **kutokana na kuzuka kwa maradhi ya kuhara katika kaunti hiyo, waache kuuza vyakula barabarani. Wananawaomba wakaazi kuchemsha maji ya kunywa kama njia mojawapo ya kujiepusha na magonjwa hayo.** Wakaazi vilevile, wanaombwa kutafuta matibabu pindi wanapoona dalili za kuhara.*

Hapa wakaazi wa kaunti ya Busia wanafahamishwa kuhusu kuzuka kwa magonjwa ya kuhara maeneo hayo. Kutokana na kuzuka kwa magonjwa hayo, wakaazi wanaonywa dhidi ya kula vyakula vinavyouzwa barabarani kwa kuambiwa, **khulondekhana nende bulwale bwe khuyara buli mukaunti eyo, bakhakusia byakhulia khumianda ta.** (*kutokana na kuzuka kwa maradhi ya kuhara katika kaunti hiyo, waache kuuza vyakula barabarani*). Ushauri vilevile unatolewa kuhusu, kujikinga dhidi ya maambukizi. Miongoni mwa hatua ambazo wakaazi wanaombwa kuchukua ni, **khukhasia kamechi kabwe ke khunywa** (*kuchemsha maji yao ya kunywa*). Hatimaye, wakaazi wanaombwa, **khuenja busilikhi ao ne babona dalili che khuyara.** (*kutafuta matibabu pindi wanapoona dalili za kuhara*).

Habari hizi zilizotolewa kwa wakaazi wa kaunti ya Busia zilikuwa za muhimu vilevile kwa wakaazi wa kaunti ya Bungoma kwa vile, waliweza kuchukua tahadhari baada ya kusikia yaliyokuwa yakitendeka katika kaunti jirani. Kutokana na mkurupuko wa magonjwa katika kaunti jirani, wakaazi wa Bungoma wanapata ufahamu kuhusu matukio hayo na kuchukua tahadhari mapema kusudi wasiweze vilevile kuathirika na mkurupuko huo. Habari hizi zilikuwa za muhimu kwa vile, ugonjwa wa kipindupindu ni wa kuambukizana na huenea kwa haraka. Ni bayana kwamba, matangazo yaliyohusu kaunti zilizopakana na Bungoma kuhusu masuala ya afya yalikuwa vilevile ya muhimu kwa wakaazi hawa. Yalikuwa ya muhimu kwa vile, wengi

walisafiri katika kaunti hizo. Kutokana na safari hizo, huenda vilevile wangeathirika na yale magonjwa yanayoathiri kaunti hizo. Kwa mfano, iwapo wakaazi hao hawatajua ya kwamba kuna mkurupuko wa ugonjwa wa kuhara katika kaunti ya Busia, huenda wasichukue tahadhari ya kutokula vyakula vinavyouzwa barabarani. Kwa hivyo onyo hilo ni la manufaa kwa wasikilizaji wa vituo vya redio vinavyotumia Kibukusu kwa vile, wale waliopanga kuzuru kaunti ya Busia wangechukua tahadhari dhidi ya kuambukizwa ugonjwa wa kipindupindu kwa kutokula vyakula ovyo ovyo.

Ni bayana kuwa, habari kuhusu afya ya wakaazi wa kaunti kama vile Busia, Trans Nzoia na Busia zina umuhimu kwa wakaazi wa kaunti ya Bungoma. Ushauri unaotolewa kwa wakaazi wa kaunti zinazopakana na kaunti ya Bungoma uliweza kuwanufaisha vilevile wakaazi hao. Kwa mfano, ingawa wanawake wa kaunti ya Trans Nzoia wanashauriwa kuhusu umuhimu wa kupima ugonjwa wa saratani katika mojawapo ya mifano iliyotolewa hapo juu, kupitia kwa ushauri huo, wale wa kaunti ya Bungoma waliweza vilevile kuchukua tahadhari kwa kupimwa ugonjwa huo na kutafuta matibabu ya mapema. Aidha, kutokana na usafiri wa watu kutoka kaunti moja hadi nyingine, wakaazi wa kaunti ya Bungoma waliweza kuchukua tahadhari kunapokuwa na mkurupuko wa magonjwa ya kuambukiza kama vile kipindupindu katika kaunti jirani. Waliweza kuchukua tahadhari hiyo pindi walipopata ufahamu kwamba kaunti jirani zimeathirika. Kama inavyojitokeza katika Sarufi Amilifu, wakaazi wa Bungoma walitumia Kibukusu kupata habari za muhimu kuhusu afya zao. Habari hizi zilihusu kuchukua tahadhari kabla hawajaambukizwa magonjwa. Hilo lilifanyika kwa Kibukusu kupitia redio za FM kuwafahamisha kuhusu mazingira yaliyowazunguka. Mazingira yaliyowazunguka katika muktadha huu ni kaunti zinazopakana na kunti ya Bungoma kama vile Busia na Trans Nzoia.

5.3.3 Masuala ya Afya ya Wakenya kwa Jumla

Serikali ya kitaifa inapotoa aina mbalimbali za chanjo sanasana kwa watoto kama vile ile ya ugonjwa wa kupooza, habari hizo huweza kutolewa kupitia kwa matangazo maalum kutoka kwa wizara ya afya. Matangazo hayo hutolewa na serikali ya kitaifa. Kwa vile habari hizo hulenga kuwafikia watu walioko mashinani, hutolewa vilevile kwa Kibukusu kupitia redio za Sulwe na West FM. Baadhi ya matangazo hayo ni, tangazo hili kuhusu chanjo dhidi ya ugonjwa wa ukambi na kupooza:

32

Kibukusu

Bulwale bwe liunya butilanga bakhaye babebulanga babana ne basili nende kimiaka mkekhe. Serikali ye lirambo ne buambani bwe likangilo la Medihil, lireba balwale boosi be bulwale bwe liunya mbo bache busilikhi mumakangilo ka Medihil khukhwanjila tarehe 12 mpaka 17 ye kumwesi kwa munane kumwiko kuno.

Kiswahili

Ugonjwa wa nasuri ni ugonjwa ambao huwashika wanawake ambao huzaa wakiwa na umri mdogo. Serikali ya kitaifa ikishirikiana na hospitali ya Medihil zinawaomba wote walio na ugonjwa wa nasuri waende kwa matibabu katika hospitali za Medihil kati ya tarehe 12 na 17 ya mwezi wa nane mwaka huu.

Tangazo hili lililenga kuwafikia wagonjwa wanaougua ugonjwa wa nasuri waliopatikana katika kaunti ya Bungoma. Ingawa tangazo lilitoka kwa serikali ya kitaifa, lililenga kuwanufaisha wakaazi wa mashinani, kaunti ya Bungoma ikiwemo. Wagonjwa na jamaa zilizoathirika na ugonjwa wa nasuri wanaambiwa, *Serikali ye lirambo ne buambani bwe likangilo la Medihil, lireba balwale boosi be bulwale bwe liunya mbo bache busilikhi mumakangilo ka Medihil khukhwanjila tarehe 12 mpaka 17 ye kumwesi kwa munane kumwiko kuno.* (Serikali ya kitaifa ikishirikiana na hospitali ya Medihil inawaomba wote walio na ugonjwa wa nasuri waende kwa matibabu katika hospitali za Medihil kati ya tarehe 12 na 17 ya mwezi wa nane

mwaka huu). Kutokana na tangazo hili, wagonjwa waliweza kupata nafasi ya kwenda kwa matibabu katika hospitali ya Medihil inayopatikana katika mji wa Eldoret.

Kupitia kwa matangazo hayo, wakaazi waliweza kuwapeleka watu wa jamii zao kwa matibabu. Kwa hivyo, matumizi ya Kibukusu katika redio za FM yaliwanufaisha wazungumzaji wa lugha hiyo kwa kuwawezesha kupata habari kuhusu matibabu ya magonjwa kutoka kwa serikali kuu kwa wepesi. Serikali kuu iliteua matumizi ya lugha za kiasili ili iweze kuwafikia wasikilizaji wengi zaidi.

Aidha, tahadhari kuhusu mkurupuko wa magonjwa kama vile kipindupindu na ugonjwa wa saratani iliweza kutolewa kwa wasikilizaji kupitia kwa matangazo maalum ambayo yalitolewa na wizara ya afya. Matangazo haya sanasana hufadhiliwa na wizara ya afya katika serikali kuu. Mfano wa matangazo hayo ni:

33.

Kibukusu

Bulwale bwe embunda ye lusaye butilanga bakhaye. Bulwale obwo bwamanana nende abo bali basinde. Kumukanda kwe bulamu mwiloba limufu kwamenyelesia kwanyola ombo likhoba le omusinde lisutanga buchafu bukali bubisibwa mumukhaye, mungonelo ne lumalilisi onyola ombo omukhaye oyo ali nende libunda lye lusaye. Kumukanda okwo kwanyolile ombo khukhebwa khuli nende bukhala ne kakila khupungusia kamalwale ako.

Kiswahili

Ugonjwa wa saratani ya njia ya uzazi huwashika akina mama. Ugonjwa huo husambazwa hususan na wanaume ambao hawajatahiri. Shirika la Afya Ulimwenguni limechunguza na kugundua kwamba govi la mtu ambaye hajatahiri hubeba uchafu mwingi ambao hupitishwa kwa akina mama wakati wa kufanya mapenzi na hatimaye utapata mwanamke huyo akiwa na saratani ya njia ya uzazi. Shirika hilo limegundua kwamba upashaji tohara una manufaa kwa vile unapunguza magonjwa hayo.

Habari hizi ambazo ni za wizara ya afya ya serikali ya kitaifa, zililenga kuwanufaisha Wakenya wote kwa jumla. Kwa mujibu wa tangazo hili, *bulwale bwe embunda ye lusaye butilanga bakhaye. Bulwale obwo bwamanana nende abo bali basinde.*

(ugonjwa wa saratani ya njia ya uzazi huwashika akina mama. Ugonjwa huo husambazwa hususan na wanaume ambao hawajatahiri). Ugonjwa husambazwa kutokana na uchafu ambao hupatikana katika govi. Uchafu huo husambazwa wakati wa tendo la ndoa.

Kupitia kwa tangazo hili, wasikilizaji walishauriwa kutilia maanani upashaji tohara. Hili lilidhihirika tunapoambiwa kwamba, ***kumukanda okwo kwanyolile ombo khukhebwa khuli nende bukhala ne kakila khupungusia kamalwale ako*** (Shirika hilo limegundua kwamba upashaji tohara una manufaa kwa vile unapunguza magonjwa hayo). Habari hizi ni za muhimu kwa wasikilizaji kwa vile, waliweza kuelewa chanzo cha kusambaa kwa ugonjwa wa saratani ya njia ya uzazi miongoni mwa akina mama. Ujumbe huo ulipitishwa kwa wakaazi kwa kutumia Kibukusu; lugha waliyokuwa na umilisi kwayo. Kwa kupata ushauri huo, wasikilizaji waliweza kuchukua tahadhari dhidi ya kusambazwa kwa saratani ya njia ya uzazi kwa akina mama.

Kutokana na mifano hii, suala la afya nchini Kenya kwa jumla lilizungumziwa. Matangazo ya wizara ya afya katika serikali ya kitaifa yaliyowasilishwa kwa wakaazi wa kaunti ya Bungoma ambao huzungumza Kibukusu ni ithibati ya suala la afya inayowaathiri Wakenya wote kwa jumla lilizungumziwa. Matangazo hayo yaliwawezesha wasikilizaji kupeleka wagonjwa wao kwa matibabu katika vituo vya afya vilivyokuwa vimeteuliwa na kupendekezwa na serikali kuu. Wakati uo huo, wasikilizaji wa vituo hivi vya redio vinavyotumia Kibukusu waliweza kupata habari kuhusu tahadhari ambazo walipaswa kuchukua dhidi ya magonjwa mbalimbali mathalan ugonjwa wa saratani ya njia ya uzazi kwa akina mama. Wakaazi

walifahamishwa na Wizara ya Afya kwamba maenezi ya saratani hiyo yangeweza kudhibitiwa kupitia upashaji tohara kwa wanaume.

Habari hizi za muhimu kuhusu afya zinaakisi maoni ya Mohochi (2007) kwamba, ili kufikia maendeleo, sera na mipango ya serikali katika nyanja za siasa, tamaduni, uchumi, elimu, afya na kadhalika zinapaswa kuwasilishwa kwa lugha watakayoelewa watu. Wakati uo huo, tunaona Kibukusu kinavyotumika kutekeleza mawasiliano ya masuala ya afya. Kwa kupata ufahamu kuhusu magonjwa mbalimbali, maarifa yanayorejelewa katika Sarufi Amilifu yanawasilishwa.

5.4 Kibukusu kama Rasilimali Inayoangazia Masuala ya Afya

Kibukusu kinajitokeza kama rasilimali katika uangazaji wa masuala ya afya kwa wasikilizaji wa Sulwe na West FM kwa njia mbalimbali. Urasilimali huo unatokana na kuwafahamisha wasikilizaji kuhusu dalili za baadhi ya magonjwa ambayo yakigunduliwa mapema, yanaweza kudhibitiwa. Kwa mujibu wa wasikilizaji 57% (N=80) kati ya wasikilizaji 140 waliohojiwa, kwa kusikiliza vipindi vya afya hususan vilivyohusu magonjwa ya kuambukizana, waliweza kunufaika sana. Walinufaika kwa ama kuchukua kinga au kutafuta matibabu kuhusiana na magonjwa mbalimbali kutokana na maarifa waliyopata kupitia redio za FM zilizotumia Kibukusu.

Vipindi vingi vilivyoangazia masuala ya afya vilijikita kwa shughuli za afya katika kaunti ya Bungoma. Kutokana na hali hiyo, vipindi hivi viliweza kuangazia masuala hayo kwa uketo. Jumla ya 93% (N=130) ya wasikilizaji kati ya 140 waliohusika katika utafiti walikiri kwamba matumizi ya Kibukusu kuangazia masuala ya afya yalikuwa na mvuto mkubwa. Kwao hivyo walipendelea kuvisikiliza vituo hivyo vya redio. Maoni hayo yanaafikiana na madai ya Mugambi (2007) kwamba, miradi ya

kisasa inayokusudiwa kuelimisha umma nchini Kenya haiwezi kueleweka zaidi katika lugha nyingine yoyote isipokuwa lugha ya wananchi wa vijijini.

Ilibainika kwamba, matumizi ya Kibukusu kuangazia masuala ya afya yaliwanufaisha sana wasikilizaji. Jumla ya 86% (N=120) ya wasikilizaji kati ya 140 walisema matumizi ya Kibukusu katika kuangazia masuala ya afya yalikuwa bora zaidi kuliko lugha zingine. Matokeo hayo yaliakisi maoni ya Castle (2014), anaposema kwamba, lugha za kiasili zinapotumika, wasikilizaji wengi huweza kuupokea na kuelewa ujumbe kwa njia rahisi. Kwa mujibu wa wasikilizaji hao, matumizi ya Kibukusu yaliwawezesha kuelewa vizuri zaidi, yale yaliyokuwa yakizungumziwa kuhusiana na masuala ya afya. Wakati uo huo, watafitiwa walihoji kwamba, kutokana na matumizi ya Kibukusu katika mijadala iliyowahusu kiafya, waliweza kutoa michango yao bila matatizo yoyote kwa upande wa lugha. Hilo liliwezekana kwa vile, mijadala ilifanywa kwa lugha waliyokuwa na umilisi kwayo. Maoni yao yalioana na yale ya Kachale (2008) aliposema kwamba, mtu huweza kuyaeleza maoni yake kwa njia bora zaidi anapotumia lugha ya umilisi. Kwa Waafrika wengi, lugha hiyo ya umilisi ni ile ya kiasili. Kwa hivyo, Kibukusu kimejitokeza hapa kama rasilimali katika uangazaji wa masuala ya afya kinapotumika katika redio za FM zinazotumia lugha za kiasili.

5.5. Changamoto za Matumizi ya Lugha ya Kibukusu kama Rasilimali kwa Wakaazi wa Bungoma, Kupitia Vituo vya Redio za FM.

Ingawa Kibukusu ni rasilimali kinapotumika katika redio za FM, ilibainika kwamba kinakumbana na changamoto kadhaa. Miongoni mwa changamoto zinazokikumba ni upungufu wa istilahi, baadhi ya vijana kutokifahamu na mitazamo hasi miongoni mwa watu kukihusu. Aidha, kuna ukosefu wa taasisi za kudhibiti uundaji wa istilahi za kutumiwa.

Kuna upungufu wa istilahi kwa baadhi ya vitu, dhana na matukio, hivyo basi vituo hivyo vimekuwa vikibuni istilahi ili kukidhi mahitaji yake. Vituo hivi vimebuni maneno kadhaa kwa kusudi la kuwasilisha jumbe, kwa mfano “esokho” (simu ya mkononi), “nakhalondo” na “kumuinda” (redio) na “khukhwikhunara” (kunajisi), istilahi ambazo awali hazikuwepo. Kwa mujibu wa msimamizi wa mojawapo ya vituo hivyo vya redio, wamekuwa wakibuni istilahi nyingi wao wenyewe ili kukidhi mahitaji yaliyopo kama inavyojitokeza katika maelezo yake:

34

Kibukusu

Eretio yefwe eyino yanjisia kamakhuwa kamakali karumikhanga hata nende bituo bibindi birumikhilanga Lubukusu. Kamakhuwa enga esokho, nakhalondo khukhunara, nifwe khukhwanjisy.

Kiswahili

Kituo chetu cha redio ndicho kilichoanzisha istilahi nyingi hata zinazotumika katika vituo vingine vinavyotumia Kibukusu. Istilahi kama vile simu ya mkono, redio na kunajisi, ni sisi ndio tuliozianzisha

Ni bayana kwamba ingawa vituo hivi vilikuwa na changamoto ya kupata istilahi za kutumika, vilijikakamua kuunda istilahi za kutumika. Viliunda hizo istilahi kusudi vikimu mahitaji yaliyokuwepo. Anavyosema msimamizi huyu, *Eretio yefwe eyino yanjisia kamakhuwa kamakali karumikhanga hata nende bituo bibindi birumikhilanga Lubukusu* (*Kituo chetu cha redio ndicho kilichoanzisha istilahi nyingi hata zinazotumika katika vituo vingine vinavyotumia Kibukusu.*), waliweza kubuni maneno mapya kwa lengo la matumizi. Kubuni huko kwa istilahi mpya kuliwawezesha kujaza pengo lililokuwepo la ukosefu wa istilahi. Hata hivyo, haikubainika vigezo walivyotumia kubuni hizo istilahi, ingawa ilibainika kwamba zilitumika, hivyo basi kukubalika na wasikilizaji. Anavyohoji Mdee (1999), mawasiliano huathirika itokeapo kwamba baadhi ya wanajamii hawaelewi maana ya

msamiati unaotumika katika mazungumzo, istilahi hizi zinapobuniwa zinahitaji kutumika kwa muda ndipo wazungumzaji lugha hiyo wazizoe.

Juhudi zilizofanywa na vituo hivyo kuhakikisha wasikilizaji wanafahamu maana ya istilahi zilikuwa ni matumizi ya istilahi hizo mara kwa mara. Kutokana na hayo matumizi ya mara kwa mara ya istilahi hizo, wasikilizaji waliweza kupata maana kutokana na miktadha ya matumizi. Kwa mfano kutokana na matumizi ya maneno “nakhalondo” na “kumuinda” mfululizo katika vituo hivi, wasikilizaji waliweza kubaini kuwa maneno hayo yalirejelea redio kama inavyojitokeza katika mifano ifuatayo:

35.

Kibukusu

Rekelesia Sulwe, nakhalondo yefwe

Kiswahili

Sikiliza Sulwe, redio yetu

36.

Kibukusu

Kamakhuwa akano khekakhwichila mubuterefu khubirira kumuinda kwoo kwa West FM.

Kiswahili

Habari hizi unazipokea kwa njia laini kupitia kwa redio yako ya West FM.

Kilichobainika hapa ni, neno ***nakhalondo*** lilitumika na kituo cha Sulwe huku ***kumuinda*** likitumika na West FM. Hata hivyo maneno yote mawili yalirejelea kifaa kimoja (redio). Kutokana na matumizi ya kila wakati ya maneno hayo, wasikilizaji walianza vilevile kuyatumia na kuwa istilahi zinazokubalika miongoni mwa wazungumzaji. Wazungumzaji wa Kibukusu walizitumia istilahi hizo kama sinonimu.

Changamoto nyingine ni wengi wa vijana kutofahamu Kibukusu. Kutokana na athari za miji, familia nyingi zinaelekea kutumia Kiswahili badala ya Kibukusu kule nyumbani. Kutokana na hali hiyo, wengi wa hawa vijana hawapendi kusikiliza vituo vya redio zinazotangaza kwa lugha za kiasili. Kwa hivyo, ingawa vituo hivi vina vipindi vingi vinavyoelimisha, kikundi kikubwa cha vijana hakivisikizi kwa vile wengi wao hupenda kusikiliza muziki badala ya vipindi vya mazungumzo na mafundisho.

Msimamizi wa mojawapo ya vituo hivyo vya redio hizo alipoulizwa walivyokabiliana na changamoto hiyo, alifahamisha mtafiti kwamba, ili kujaribu kuwafanya vijana wasikilize kituo chao cha redio, wana kipindi mahususi cha vijana kwa jina “Banjuka.” “Banjuka” ni istilahi ya “Sheng” ambayo humaanisha kucheza muziki. Kwa mujibu wa msimamizi huyo, “Banjuka” ni kipindi kilichowalenga vijana (*baraka*). Mwandalizi wa kipindi hicho alikuwa mtangazaji barobaro ambaye aliweza kuzungumza lugha ya vijana na kuhusisha mada zilizopendwa na vijana kama njia mojawapo ya kuwafanya wasikilize vipindi katika kituo hicho cha redio ilivyobainika katika dondoo hili:

37.

Kibukusu

*Nakhalondo yefwe eino eli nende bipindi bye chirika choosi khukhwanjila khubaraka mpaka basakhulu. **Khuli nende sipindi sye baraka khwisina banjuka.** Sipindi esio simelelwa nende omuraka omanyile niko baraka basima*

Kiswahili

*Redio yetu ina vipindi vya rika zote kuanzia kwa vijana hadi kwa wazee. **Tuna kipindi cha vijana kwa jina banjuka.** Hicho kipindi huwasilishwa na kijana anayeelewa wanayopenda vijana*

Kwa mujibu wa msimamizi huyu wa kituo cha redio, walikuwa na fahamu kwamba kupata wasikilizaji ambapo ni vijana halikuwa jambo rahisi. Hiyo ndiyo sababu kuu ya kuanzishwa kwa kipindi banjuka. Na kusudi wasiwape vijana yale ambayo hawahitaji katika kipindi hicho, waliteua mtangazaji ambaye vilevile ni kijana ili awasilishe kipindi hicho. Mwasilishi kipindi hicho ambaye ni **omuraka** (kijana) aliteua mambo na mada ambazo zingewafanya vijana wasikilize kituo hicho cha redio.

Ili kuwafanya vijana hawa wasikilize kipindi hicho, miziki ya kizazi kipya ilichezwa na mwandalizi kipindi. Usikilizaji wa kipindi hicho, ulibaini kwamba, licha ya huo muziki wa kizazi kipya, kulikuwa na mada mbalimbali zilizojadiliwa kuwahusu vijana. Baadhi ya mada hizo ni kama vile, jinsi vijana wanavyoweza kujipatia mapato badala ya kujiingiza katika visa vya uhalifu na unywaji pombe. Ushauri huu ukitolewa na mwasilishaji kipindi pamoja na wasikilizaji wengine hususan vijana. Baadhi ya vijana waliweza kupiga simu katika kituo hiki cha redio na kuwashauri vijana wenzao kuhusu jinsi ya kuboresha hali zao za maisha kama inavyojitokeza katika mfano ufuatao:

38.

Kibukusu

Esese esaya baraka basyange endi bakhhalinda kimilimo kya serikali ne bamalile ebikuli ta. Ebasaya endi badala banje khunya kamalwa ne bekofusia banje bibiasara binyala byabayeta. Kwa mfano, esese nanjila khukwoosia ne khukusia kamanda mala luno luri endi nende binyosi byase bitaru. Silala samwene embekelamo ne bibindi naandikamo vijana babakholela ekasi. Nono khu siku sengosanga chisilingi eelefu na mia tano enga faida ta.

Kiswahili

Mimi nawaomba vijana wenzangu ya kwamba wasingoje kuajiriwa na serikali wakimaliza masomo. Ninawaomba kwamba badala ya kunywa pombe na kujizeesha, wanafaa waanzishe biashara ya kuwasaidia. Kwa mfano, mimi

*nilianza kwa kuchoma na kuuza makaa lakini kwa sasa nina vinyozi vyangu vitatu. Mojawapo ya vinyozi hivyo mwenyewe huwa ninanyoa na vile vingine nimewaajiri vijana ambao wananifanyia kazi. **Kwa siku huwa sikosi kupata elfu moja na mia tano kama faida.***

Kutokana na kifungu hiki, ni bayana kwamba kupitia kwa kipindi hiki, vijana walihimizwa kutafuta suluhu kwa baadhi ya matatizo yanayowakabili. Vijana hawa wanaombwa kutokata tamaa na kujiingiza katika vitendo ambavyo vitawaangamiza. Hilo linajitokeza kupitia kwa maneno, ***Ebasaya endi badala banje khunywa kamalwa ne bekofusia banje bibiasara binyala babayeta*** (Ninawaomba kwamba badala ya kunywa pombe na kujizeesha, wanafaa waanzishe biashara ya kuwasaidia). Kijana huyo anaelezea manufaa ambayo amepata kutokana na bidii yake anaposema, ***Nono khusiku sengosanga chisilingi eelefu na mia tano enga faida ta.*** (Kwa siku huwa sikosi kupata elfu moja na mia tano kama faida). Kutokana na maelezo hayo, vijana wengine wangufaika kwa kujifunza manufaa ya kutia bidii.

Vilevile, vijana waliweza kujadili changamoto mbalimbali zinazowakumba maishani. Mijadala hiyo ilihusisha upigaji simu kwa kituo hicho cha redio na utumaji jumbe fupi. Vijana hawa sanasana walipata tatizo la kupata ajira baada ya wao kijiunga na vyuo mbalimbali, kisha hatimaye kukosa kazi. Waajiri wengi walitaka wahojiwa kuwa na tajriba huku vijana hao wakinyimwa nafasi ya kupata tajriba hiyo.

Mitazamo hasi miongoni mwa baadhi ya watu kwamba watu wote wanaosikiliza redio za lugha za kiasili ni watu ambao ama hawana elimu au ni wazee pia ilijitokeza kama changamoto inayokumba matumizi ya Kibukusu katika redio za FM. Mitazamo hiyo hususan ilijitokeza miongoni mwa vijana. Baadhi ya vijana waliohusishwa katika utafiti huu walikuwa na mitazamo hasi ya matumizi ya Kibukusu katika vyombo vya habari kama anavyohoji mojawapo wa vijana hao katika dondoo hili:

39.

Kibukusu

Esese sendekeresyanga chiredio che Lubukusu echo ta. Sulwe nende West FM ni chiredio che basakhulu. Nibo barekelesyanga chiredio echo ne kakila sebaelewa Luswahili bulai ta.

Kiswahili

Mimi huwa sisikilizi hizo redio zinazotumia Kibukusu. Sulwe na West FM ni redio za wazee. Ni wao husikiliza hizo redio kwa vile hawaelewi Kiswahili vizuri.

Ujumbe unaojitokeza hapa ni kwamba msemaji huwa hasikilizi vituo vya redio vinavyotumia Kibukusu kwa vile vituo hivyo vinawalenga wazee ambao hawaelewi Kiswahili anaposema, ***nibo barekelesyanga chiredio echo ne kakila sebaelewa Luswahili bulai ta.*** (ni wao husikiliza hizo redio kwa vile hawaelewi Kiswahili vizuri). Ni bayana kwamba maneno hayo yanadunisha usikilizaji wa lugha za kiasili unaojitokeza katika vituo vya redio vinavyoitumia. Udunishaji huo unatokana na mtazamo hasi kuhusiana na lugha za kiasili miongoni mwa baadhi ya watu.

Kinaya ni kwamba, watu hawa huwa hata hawana umilisi katika lugha hizo wanazojivunia; Kiingereza na Kiswahili. Hali hiyo inatokana na kukosa ufahamu kuhusiana na umuhimu wa lugha za kiasili ambapo, kupitia lugha zetu tunaweza kueleza tamaduni zetu, ufahamu wetu kuhusu mimea yote, mkusanyiko wa wanyama na maarifa tuliyo nayo (Okombo, 2014).

Ukosefu wa taasisi inayodhibiti uundaji wa istilahi za Kibukusu pia ni changamoto kubwa. Kutokana na ukosefu wa taasisi hiyo, vituo hivyo vinajitungia tu istilahi bila mwongozo. Kwa hivyo ingawa vituo hivi vinabuni istilahi ambazo zinatumiwa vigezo vya ubunifu huu ni suala linaloweza kutiliwa shaka.

Baadhi ya wataalamu ambao huhusishwa katika uwasilishaji wa vipindi vya kitaaluma kama vile vya afya hawana umilisi wa Kibukusu. Kutokana na ukosefu huo wa umilisi, baadhi yao hulazimika kuhamisha msimbo ama kwa Kiswahili au Kiingereza ili waweze kupitisha ujumbe lengwa.

Pana uwezekano vilevile wa wataalamu wengi kutohusishwa katika vipindi vinavyowasilishwa kutokana na wao kukosa umilisi wa lugha za kiasili. Hii inatokana na kutokuwepo kwa kazi nyingi zilizochapishwa kwa lugha za kiasili mathalan makamusi.

5.6. Hitimisho

Sura hii imeanza kwa kuzungumzia masuala yanayoangaziwa katika vipindi vya siasa na afya katika redio za West na Sulwe FM. Wakati uo huo, imedhihirisha Kibukusu kinavyojitokeza kama rasilimali katika uangazaji masuala ya siasa na afya kwa kutoloea mifano jinsi kinavyofanya hivyo pindi kinapotumika katika redio za lugha za kiasili. Hatimaye sura hii imehitimisha kwa kuelezea changamoto zinazokumba lugha za kiasili zinapotumika katika redio za FM zinazotumia lugha za kiasili.

SURA YA SITA

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

6.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia imezungumzia masuala yanayoangaziwa katika vipindi vya siasa na afya. Wakati uo huo imedhihirisha Kibukusu kinavyojitokeza kama rasilimali katika uangazaji wa masuala ya siasa na afya huku ikitolea mifano ya jinsi kinavyotekeleza hali hiyo. Sura hii inahitimisha tasnifu na kutoa mapendekezo kwa kazi yote kwa jumla.

Tasnifu hii ililenga kuchunguza lugha za kiasili zinavyoathiri maisha ya wazungumzaji zinavyotumika katika redio za FM. Ililenga kujadili jinsi matumizi ya Kibukusu katika redio za FM yanavyoweza jamii husika kupata habari zinazoiwezesha kuboresha hali yake kwa njia mbalimbali, hivyo basi kuwa rasilimali yake. Vilevile, changamoto zinazokumba matumizi ya Kibukusu kupitia vituo vya redio vya FM zimeangaziwa. Utafiti ulililenga kuonyesha matumizi chanya ya lugha za kiasili katika redio za FM yanavyoweza kuwa ya manufaa kwa jamii husika.

Utafiti ulidhamiria hususan: kuhakiki yaliyomo katika vipindi vya jamii, uchumi, siasa na afya vinavyowasilishwa kwa kutumia Kibukusu katika redio za FM zinazosikika katika kaunti ya Bungoma; kutathmini Kibukusu kinavyojitokeza kama rasilimali kuangazia masuala ya jamii, uchumi, siasa na afya kwa wazungumzaji wake kinapotumika katika redio za FM; kutambua changamoto za matumizi ya Kibukusu kama rasilimali kwa wakaazi wa Bungoma kupitia vituo vya redio za FM, kisha kupendekeza mbinu zinazoweza kutumika kuimarisha lugha za kiasili ziwe rasilimali kwa watumiaji kupitia kwa redio za FM.

6.1. Muhtasari wa Tasnifu

Sura ya kwanza inaelezea kuhusu usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti na malengo ya utafiti huu. Aidha, sura hiyo imeangazia nadharia tete zilizoongoza utafiti huu, upeo wake na umuhimu wa utafiti.

Mapitio ya maandishi na misingi ya kinadharia yameshughulikiwa katika sura ya pili. Sura ya tatu imezungumzia mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Nao mjadala kuhusu masuala yanayojitokeza katika vipindi vya jamii na uchumi katika Sulwe na West FM umeangaziwa katika sura ya nne. Aidha, Kibukusu kinavyojitokeza kama rasilimali katika uangaziaji wa masuala ya jamii na uchumi kwa wasikilizaji wa vituo hivyo vya redio imeelezwa katika sura hiyo.

Nayo sura ya tano imeanza kwa kuzungumzia masuala yanayoangaziwa katika vipindi vya siasa na afya katika West na Sulwe FM. Wakati uo huo, imejadili kuhusu Kibukusu kinavyojitokeza kama rasilimali katika uangaziaji wa masuala ya siasa na afya huku ikitolea mifano jinsi kinavyofanya hivyo. Hatimaye, sura ya sita imeelezea matokeo ya utafiti huu na kutoa mapendekezo. Sura hiyo imehitimisha kwa kutoa mapendekezo kwa tafiti za baadaye.

6.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti uliweza kugundua kwamba kuna masuala mengi yanayoangaziwa katika redio za FM hususan Sulwe FM kwa kutumia lugha za kiasili. Ilibainika kwamba, masuala hayo yaliangaziwa kupitia vipindi vya jamii, uchumi, siasa na afya. Kutokana na kuwepo masuala hayo, wasikilizaji wa vituo hivyo walivifurahia huku wakiwa na imani sana na vituo hivyo vya redio.

Vituo hivi viliwapa habari tosha wasikilizaji. Wasikilizaji walisema kuanzishwa kwa vituo hivi kuliwanufaisha sana kwa kuwapasha habari ambazo walizikosa kwa muda

mrefu sana pale walipotegemea vituo vya redio vya kitaifa. Maoni ya wasikilizaji hawa yalioana na yale ya Ripoti ya Vyombo vya Habari nchini Kenya (MCK, 2012), kwamba kuanzishwa kwa redio za FM zinazotumia lugha za kiasili ilikuwa ni kujaza pengo lililoachwa na vituo vya redio vya kitaifa vilivyopeperusha matangazo kwa Kiswahili na Kiingereza.

Matokeo ya utafiti huu yameweza kujadiliwa chini ya kila mojawapo ya malengo ya utafiti kama ifuatavyo:

6.2.1 Vipindi vya Jamii, Uchumi, Siasa na Afya Vinavyowasilishwa kwa Kutumia Kibukusu katika Sulwe na West FM

Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa kuhakiki yaliyomo katika vipindi vya jamii, uchumi, siasa na afya vinavyowasilishwa kwa kutumia Kibukusu katika redio za FM, zinazosikika katika kaunti ya Bungoma. Ilibainika kwamba, matini ya vipindi vya masuala ya jamii, uchumi, afya na siasa ilikuwa na masuala mengi yaliyoweza kujitokeza.

Baadhi ya masuala yaliyojitokeza katika vipindi vya jamii ni: uwajibikaji, maadili, tamaduni na matukio katika kaunti ya Bungoma. Uwajibikaji uliangaziwa kupitia kwa vipindi kama vile “Bwasia ne Sulwe” (Kumekucha na Sulwe), “Mumilimo” (Katika kazi), “Lotia bakosi” (Rudisha nyumbani wapendwa) na “Lumasaba” (Kibukusu). Kupitia kwa vipindi hivi, wasikilizaji walihimizwa kuwajibika kwa chochote wanachokifanya pamoja na kuwajibikia familia zao. Wasikilizaji walihimizana kuamka mapema na kuacha kulaza damu kupitia kwa kipindi cha “Bwasia ne Sulwe”. Hiki ni kipindi cha watu kuamshana na kuhimizana kuchapa kazi. Hili lilitokelezwa kupitia kwa upigaji simu kwa kituo cha redio cha Sulwe FM. Wapigaji simu waliorodhesha majina ya wale ambao wangependa kuwaamsha na kuwashauri waende kazini. Ushauri wa kuamka mapema vilevile uliwasilishwa kupitia jumbe fupi

(burume bubwimbi) ambazo zilitumwa kwa kituo hiki cha redio na kusomwa na watangazaji.

Suala la uwajibikaji vilevile liliangaziwa kupitia kwa kipindi cha “Mumilimo” (Katika kazi). Katika kipindi hicho, wasikilizaji walihimizana kuchapa kazi huku wakitumiana salamu. Hilo lilifikiwa kwa ama kupiga simu au kutuma jumbe fupi. Hapa wasikilizaji walihimizana kuwajibika kazini kwa kufanya kazi nzuri.

Aidha, uwajibikaji uliangaziwa kupitia kwa ushauri uliotolewa kwa wasikilizaji kupitia kwa kipindi cha “Lotia bakosi” (Rudisha wapendwa nyumbani). Katika kipindi hicho, kama ilivyo na vipindi vingine, wasikilizaji waliwasiliana na wenzao kwa ama kupiga simu au kutuma jumbe fupi kwa redio. Upigaji simu na utumaji jumbe fupi ulifanywa kwa kituo cha redio. Wapigaji simu waliwashauri wasikilizaji wenzao warudi nyumbani baada ya kazi ya kutwa. Wakati uo huo, waliwashauri warudi nyumbani angalau na kitu mkononi (wakiwa wamenunulia familia zao kitu).

Maadili vilevile yaliangaziwa kwa mapana na vituo hivi vya redio vinavyotumia lugha ya Kibukusu katika masuala ya jamii. Vipindi mbalimbali, mathalan “Lumasaba”, (Kibukusu) “Busya bwasia nako” (Kunakucha na matukio yake), “Endekhelo” (Mjadala), “Sina sisinyanga” (Kipi kinachoudhi) na “Mbuka busa” (Ninashangaa) viliangazia maadili ya jamii. Miongoni mwa maadili ambayo yaliangaziwa ni kama vile tabia na mienendo isiyopendeza katika jamii. Kwa mfano, kupitia kwa kipindi cha “Sina sisinyanga?” (Kipi kinachoudhi?), wasikilizaji walieleza bayana yale yanayoudhi jamii. Hali hiyo ilijitokeza katika kipindi cha “Mbuka busa” Lengo la kipindi “Mbuka busa” ni kubadili mienendo mibaya katika jamii. Miongoni mwa masuala ya kimaadili yaliyoangaziwa katika kipindi hicho ni tabia ya udanganyifu.

Ukosefu wa heshima miongoni mwa vijana kwa wazazi wao vilevile ni suala la maadili ambalo liliangaziwa chini ya vipindi vya jamii. Kwa mfano, kupitia kwa kipindi cha “Mbuka busa”, tabia mbaya kama vile za vijana kuwakosea heshima wazazi wao zilishutumiwa. Aidha, kupitia kwa kipindi kama vile “Busya bwasia nako” (Kunakucha na matukio), lugha hii ilianguzia tabia ambazo ni kinyume cha maadili ya jamii. Katika kipindi hiki, wasikilizaji ama walipiga simu au kutuma jumbe fupi kwa kituo cha radio na kushutumu mienendo mbaya isiyoambatana na maadili ya jamii. Kwa mfano, mwanamume anayefanya mapenzi na mwanawe.

Aidha, tamaduni zilijitokeza katika matini ya vipindi vya jamii. Tamaduni hizi zilianguziwa kwa njia mbalimbali mathalan, upashaji tohara miongoni mwa jamii ya Wabukusu. Hapa wasikilizaji walikumbushwa kuhusu miiko ya jamii hiyo. Hili liliweza kufikiwa kupitia kwa vipindi “Lumasaba” na “Embalu yefwe.” Pia utamaduni ulijitokeza kupitia kwa misemo ya Kibukusu ambayo ilianguziwa kupitia kwa vipindi kama vile “Lusimo lwe endalo.” Kwa mfano, kupitia kwa “Lusimo lwe endalo” (Msemo wa siku), wasikilizaji waliulizwa kufafanua maana ya msemo wa siku ambao ulitolewa na mwasilishaji kipindi. Baada ya wasikilizaji kufasiri maana ya msemo huo, mtangazaji hatimaye alitoa maelezo sahihi ya msemo husika.

Matukio katika kaunti ya Bungoma ambayo ni ya kijamii vilevile yaliweza kuanguziwa kupitia kwa vipindi vya jamii hususan kupitia kwa “Kamakeni” (Habari). Matukio hayo pia yalianguziwa kupitia kwa “Busya bwasia nako” (Kumekucha na matukio yake). Baadhi ya matukio ya kijamii ambayo yalianguziwa ni mizozo ya kifamilia ambayo huvunja hizo familia. Kwa mfano, unywaji wa pombe kupita kiasi miongoni mwa wakaazi, ukosefu wa uaminifu kati ya wanandoa, mizozo kati ya wanandoa na dhuluma dhidi ya watoto.

Kupitia kwa matukio ya kaunti yaliyowasilishwa kupitia kwa “Kamakeni” (Habari), wasikilizaji waliweza kufahamishwa kuhusu viwango vya usalama katika kaunti ya Bungoma. Miongoni mwa visa vya ukosefu wa usalama vilivyoangaziwa ni watu kushambuliwa na magenge ya watu.

Matini ya uchumi ilijitokeza kupitia kwa vipindi kama vile “Bukusi ne bukulani” (Uuzaji na ununuzi) na “Kamakeni” (Habari). Miongoni mwa masuala yaliyoangaziwa ni bei ya mazao na bidhaa za sokoni au mifugo katika masoko yanayopatikana ndani ya kaunti ya Bungoma na nje ya kaunti hiyo. Kupitia kwa vipindi vya “Bukusi ne bukulani” (Uuzaji na ununuzi), wakulima na wafanyibiashara walifahamishwa kuhusu bei ya mazao, bidhaa za sokoni na mifugo katika masoko mbalimbali kwenye kaunti ya Bungoma.

Aidha, vipindi vya uchumi vilikuwa na ushauri kuhusu kilimo bora. Hilo lilifikiwa kupitia kwa vipindi vilivyowasilishwa na kampuni za dawa za kuua wadudu kama vile viwavi na kampuni za kutengeneza mbegu mbalimbali za upanzi, hususan zilizotengeneza mbegu za mahindi. Habari hizi za muhimu ziliwasilishwa kwa njia ya matangazo ya biashara na matangazo maalum. Ushauri wa kilimo bora uliwasilishwa na kampuni za mbegu kwa kuangazia utayarishaji bora wa mashamba, wakati bora wa kupanda na mbegu bora za kupandwa katika sehemu mbalimbali kulingana na angahewa ya wakaazi ili kupata mazao bora.

Kampuni za dawa za kuua na kuzuia kuenea kwa wadudu vilevile zilitoa ushauri kwa wakulima kupitia kwa matangazo ya biashara na matangazo maalum. Matangazo hayo yaliwasilishwa kwa wakulima kwa kuwafahamisha kuhusu aina mbalimbali za dawa za kuangamiza wadudu mbalimbali. Vipindi hivyo viliwapa mafundisho

wasikilizaji kwa lengo la kuinua hali zao za uchumi kupitia kwa matangazo ya kampuni mbalimbali.

Matini ya vipindi vya uchumi vilevile ilikuwa na habari kuhusu hali ya uchumi katika kaunti ya Bungoma. Habari hizo ziliweza kujitokeza kupitia kwa vipindi kama vile “Endekhelo”, “Kamakeni” na “Bukusi ne bukulani.” Kwa mfano kupitia kwa mijadala ya “Endekhelo”, kampuni ya kusaga sukari ya Nzoia iliweza kuangazia mikakati iliyoifanya kuhakikisha kwamba wakulima wa miwa wananufaika na kampuni kwa kuinua hali yao kiuchumi. Kwa kuinua uchumi wa wakulima, uchumi wa kaunti ya Bungoma kwa jumla uliinuka vilevile. Baadhi ya mikakati hiyo ilikuwa ni kuwalipa wakulima kwa wakati ili waweze kukeza pesa wanazopata kutokana na malipo hayo. Kampuni hiyo ya sukari ilipochelewa kuwalipa wakulima kwa wakati, wakulima hao walilalamika kupitia kwa redio za Sulwe na West FM.

Mijadala kuhusu changamoto zinazowakumba wakulima wa miwa na ambazo huathiri uchumi wa kaunti ya Bungoma moja kwa moja vilevile zilijitokeza katika matini ya vipindi vya uchumi. Licha ya changamoto, juhudi za serikali ya kaunti ya Bungoma kuboresha viwango vya uchumi vilevile ziliangaziwa kupitia kwa redio za Sulwe na West FM. Haya yaliweza kufikiwa kupitia kwa “Kamakeni.” Baadhi ya mikakati ambayo kaunti ilitekelezwa na serikali ya kaunti ili kuinua uchumi wa kaunti ni kurekebisha barabara ambazo zimeharibika kusudi wakulima waweze kufikisha mazao yao sokoni kwa wakati. Wakulima wanapofikisha mazao sokoni kwa wakati, kaunti pia inapata pesa kupitia kwa ushuru wanaotowza hawa wafanyibiashara. Nayoy serikali inapopata huo ushuru, inautumia kuinua uchumi wa kaunti kwa kuweka miundo msingi itakayoboresha biashara.

Aidha, matini ya vipindi vya uchumi ilianguzia ubadilishanaji wa sarafu ya Kenya dhidi ya zile za mataifa mengine. Hapa, wasikilizaji walipata habari kuhusu thamani ya shilingi ya Kenya dhidi ya sarafu zingine kama vile za Tanzania, Uganda na Marekani.

Nayo masuala ya siasa yalijitokeza kupitia kwa vipindi kama vile “Kamakeni” (Habari) na “Endekhelo” (Mjadala). Baadhi ya matini katika vipindi vya kisiasa ilikuwa siasa za kaunti ya Bungoma. Hilo liliweza kufikiwa kupitia kwa vipindi vya “Endekhelo” (Mjadala) na “Kamakeni” (Habari). Siasa hizi za kaunti ya Bungoma zilikuwa kama vile tathmini ya utendakazi wa viongozi mbalimbali wa kisiasa. Tathmini hii iliweza kuangaziwa kupitia kwa hawa wanasiasa kuelezea wasikilizaji kupitia kwa “Endekhelo” maendeleo ambayo walikuwa wametenda tangu wapigiwe kura. Aidha, masuala ibuka yalijitokeza katika matini ya vipindi vya siasa. Kwa mfano, wakati Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) ilipokuwa ikishutumiwa na kuulizwa kung’atuka mamlakani, matini hiyo ilijitokeza katika vipindi vya siasa katika “Endekhelo” na “Kamakeni” kama suala ibuka.

Licha ya masuala ibuka kujitokeza kama matini, kupitia kwa kipindi cha “Kamakeni,” matukio ya kisiasa yaliyotendeka nje ya kaunti ya Bungoma yaliweza vilevile kuangaziwa katika kipindi hicho. Mifano ya matukio hayo ni, hotuba za kisiasa zilizotolewa na rais wa Kenya, naibu wake na viongozi wengine wa kisiasa wakiwemo wale wa upinzani.

Kwa upande wa vipindi vya afya, matini iliyojitokeza ni ya magonjwa mbalimbali ambayo huenda yakawashika wakaazi endapo hawazingatii usafi wa mwili na mazingira. Kwa mfano, kupitia kwa kipindi cha “Kamakeni,” wakaazi walishauriwa kuzingatia usafi kwa kunywa maji ambayo ama yametibiwa au kuchemshwa

kunapokuwa na mvua nyingi katika kaunti ya Bungoma. Ushauri huo ulitokana na ongezeko la visa vya magonjwa ya kuhara vilivyosababishwa mvua nyingi iliyokuwa ikinyesha.

Aidha, vipindi vya afya vilihusisha habari kuhusiana na vifaa vya matibabu ambavyo vilikuwa vimenunuliwa na serikali ya kaunti ya Bungoma kama vile ununuzi wa mashine za eksirei. Vipindi hivyo vilevile vilikuwa na matini kuhusu juhudi za serikali ya kaunti kuboresha vifaa vya matibabu kwa wakaazi. Hilo liliweza kufikiwa kupitia kwa kipindi cha “Kamakeni” (Habari) na kile cha “Endekhelo” (Mjadala). Kwa mfano, kupitia kwa kipindi cha “Kamakeni” (Habari), wakaazi walifahamishwa ya kwamba magari ya kubebea wagonjwa yalikuwa yamenunuliwa kwa hospitali zote za kaunti ya Bungoma ili kurahisisha usafiri wa wagonjwa kutoka kwa hospitali ndogo hadi kubwa.

Aidha, katika vipindi vya afya ambavyo huwasilishwa kupitia kwa “Endekhelo,” (Mjadala), matatizo yanayowakumba wakaazi kwa upande wa kupata afya bora ambayo hutokana na upungufu wa vifaa vya afya yalijitokeza kama matini. Mijadala hii ilihusisha maafisa wa wizara ya afya katika serikali ya kaunti ya Bungoma na waandalizi wa vipindi. Katika mijadala hiyo, wasikilizaji walitoa maoni yao ama kwa kupiga simu au kutuma jumbe fupi kwa vituo hivyo vya redio.

Vipindi vya afya vilikuwa pia na matini ya dalili za magonjwa mbalimbali. Hilo liliweza kujitokeza kupitia kwa kipindi cha “Busilikhi” (Matibabu). Hapa wataalamu wa matibabu lakini ya kiasili waliwaelezea wasikilizaji kuhusu dalili za magonjwa mbalimbali. Wataalamu hao waliwashauri wasikilizaji kutafuta matibabu pindi wanapoona dalili za magonjwa mbalimbali. Mifano ya magonjwa ambayo

yalizungumziwa ni kama vile, ugonjwa wa kisukari, saratani na ugonjwa wa shinikizo la damu.

Licha ya hayo, masuala ya afya yaliangaziwa kupitia kwa matini iliyohusu ushauri wa wizara ya afya na mashirika yasiyo ya kiserikali. Ushauri huu ulihusu matibabu yanayofanywa na ama wizara ya afya au mashirika ya afya yasiyo ya kiserikali. Ushauri huo uliwasilishwa kupitia kwa matangazo maalum yaliyofadhiliwa na serikali kuu. Mfano wa magonjwa hayo ni, ugonjwa wa saratani za aina mbalimbali na mahali pa kupata matibabu. Hayo matangazo maalum ya ushauri yalitokea siku za kuadhimisha magonjwa hayo.

Vipindi vya afya viliweza pia kuwasilishwa kupitia kwa tahadhari zilizotolewa kuhusu mkurupuko wa magonjwa kama vile ya kipindupindu. Tahadhari hizi zilitolewa kwa wasikilizaji kupitia kwa matangazo maalum ambayo yalitolewa na wizara ya afya. Matangazo hayo sana sana yalifadhiliwa na wizara ya afya katika serikali kuu. Mfano wa mikurupuko ya magonjwa ambayo ilitolewa kama tahadhari ni ugonjwa wa kipindupindu.

Licha ya tahadhari kutolewa katika vipindi vya afya, habari kuhusu aina mbalimbali za chanjo kwa watoto kama vile chanjo ya ugonjwa wa kupooza zilitolewa na serikali ya kitaifa. Habari hizo ziliweza kutolewa kupitia kwa matangazo maalum kutoka kwa wizara ya afya. Matangazo hayo yalitolewa na serikali ya kitaifa lakini kwa vile yalilenga kuwafikia watu walioko mashinani, yalitolewa vilevile kwa Kibukusu kupitia redio za Sulwe na West FM. Baadhi ya matangazo hayo ni: chanjo kwa ugonjwa wa ukambi na ugonjwa wa kupooza.

6.2.2 Kibukusu kama Rasilimali Inayoangazia Masuala ya Jamii, Uchumi, Siasa na Afya kwa Wazungumzaji Wake katika Redio za FM

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa ni kutathmini Kibukusu kilivyo rasilimali katika uangazaji masuala ya jamii, uchumi, siasa na afya kwa wazungumzaji wake kupitia kwa redio za FM zinazosikika katika kaunti ya Bungoma. Ilibainika kwamba, Kibukusu ni rasilimali katika uangazaji wa masuala ya jamii, uchumi, afya na siasa. Urasilimali huo uliweza kujibainisha na jinsi lugha hiyo ilivyowawezesha wazungumzaji wake kupata ufahamu zaidi kuhusu masuala mbalimbali.

Miongoni mwa masuala yaliyojitokeza katika vipindi vya jamii ni: maadili uwajibikaji, tamaduni na matukio katika kaunti ya Bungoma. Matokeo ya utafiti yalionyesha kwamba Kibukusu ni lugha faafu kuangazia masuala ya maadili. Ilibainika kwamba wengi wa wasikilizaji; 89% (N=125) kati ya 140 waliohojiwa katika vituo vyote viwili waliungama kwamba laiti Kibukusu kisingetumika katika redio za FM kuangazia maadili, lugha zingine zisingeyafafanua masuala hayo bayana. Hilo liliweza kutimizwa kupitia kwa vipindi kama vile “Lumasaba” na “Sina sisinyanga”,

Mojawapo wa wahariri waliohusishwa katika utafiti huu alihoji, kuna baadhi ya masuala yasiyo na visawe katika Kiswahili. Kwa hivyo mambo hayo hayawezi kueleweka bayana pasipo matumizi ya Kibukusu. Mfano wa “kuchomwa na ukwe” (Bukhwe khukhwosia) ulitumika kama idhibati ya baadhi ya mambo ambayo hueleweka vyema zaidi lugha za kiasili zinapotumika. Maoni hayo yaliafikiana na yale ya Okombo (2014) kuhusu umuhimu wa lugha za kiasili katika kuelezea tamaduni zetu. Okombo (2014) anahoji kwamba, kupitia lugha zetu za kiasili, tunaweza eleza tamaduni zetu na ufahamu wetu kuhusu yote yanayotuzingira. Ilibainika kwamba, Kibukusu kilifaa zaidi kutumika kuangazia masuala hayo. Kwa

mfano, itikadi za jamii ziliangaziwa vyema zaidi Kibukusu kilipotumika. Matokeo hayo yalioana na yale ya Kachale (2008), aliposema kwamba mtu huweza kuyaeleza maoni yake kwa njia bora zaidi kwa kutumia lugha aliyo na umilisi.

Aidha, ilibainika kwamba Kibukusu kiliwafahamisha wasikilizaji kuhusu masuala ibuka. Kupitia kwa vipindi kama vile “Endekhelo”, (Mjadala), wasikilizaji waliweza kupata ufahamu kuhusu masuala ibuka. Wengi wa wasikilizaji wa Sulwe, 97% (N=68) kati ya 70 waliohusishwa katika utafiti huu walihoji kwamba, kipindi hicho kiliwafaa sana kwa vile kilijadilia masuala ibuka yaliyoathiri jamii. Mfano wa masuala hayo ni changamoto zilizokumba wakuzaji wa miwa katika kaunti ya Bungoma ambao huuzwa miwa yao katika kiwanda cha kusaga sukari cha Nzoia. Hali hiyo iliakisi mtazamo wa Prah (2005), anaposema kwamba lugha za kiasili huwafikia watu wa mashambani kwa haraka zaidi na moja kwa moja.

Ingawa redio zingine zinazotumia lugha za Kiswahili na Kiingereza zilikuwa na mijadala kuhusu masuala ibuka, ziliigemea zaidi yale ya taifa kwa jumla. Ilibainika kwamba, vituo vya redio vya Sulwe na West FM viliegemea zaidi masuala yaliyoathiri jamii za Waluyia na hususan yale ya kaunti ya Bungoma na Trans Nzoia. Hali hiyo iliakisi ripoti ya Halmashauri ya Vyombo vya Habari nchini Kenya (MCK, 2012), kwamba, sababu kuu ya kusikilizwa zaidi kwa vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili ni, asilimia kubwa ya habari, (36%) kuwa habari za mashinani na kieneo.

Matumizi ya Kibukusu katika redio za FM yaliweza pia kuhifadhi tamaduni za Wabukusu. Uhifadhi huu ulitokana na matumizi ya lugha zenyewe, misemo na methali zilizofafanuliwa pamoja na miiko iliyosisitizwa katika baadhi ya vipindi vilivyopeperushwa mathalan “Lusimo lwe endalo” na “Lumasaba”. Aidha, ilibainika

kwamba utamaduni kama wa upashaji tohara kitamaduni ulihifadhiwa kupitia kwa vipindi kama vile “Lumasaba” na “Embalu yefwe.” Kupitia kwa vipindi hivi, wasikilizaji walifahamishwa kuhusu kudumisha tamaduni za Wabukusu na umuhimu wa udumishaji wa utamaduni huo.

Vilevile, utafiti ulibaini kwamba redio za Sulwe na West FM ziliboresha hali za uchumi wa wasikilizaji kwa kuwapa habari zilizowawezesha kufanya uamuzi wa busara kiuchumi. Wasikilizaji wa vituo hivi vya redio waliweza kuboresha hali zao za uchumi kupitia kwa vipindi kama vile “Bukusi ne bukulani.” Kupitia kwa kipindi hicho, wasikilizaji waliotaka kuuza vitu, waliweza kulinganisha bei za bidhaa hizo katika masoko mbalimbali kabla kupeleka bidhaa hizo sokoni. Ufahamu huu uliwasaidia wasiendeleo kupunjwa na walaghai ilivyokuwa ikitendeka kabla kuja kwa vituo hivi vinavyotumia Kibukusu. Wengi wa wasikilizaji; 78% (N=109) kati ya 140 waliohojiwa walisema kwamba matangazo ya biashara hususan kupitia kwa “Bukusi ne bukulani,” yaliwafaa sana. Kwa hivyo, wenyeji wanapata uwezo wa kujiinua kiuchumi kutokana na wao kupewa nafasi kuyaelewa masuala ya soko vizuri zaidi. Hilo liliwezekana kutokana na lugha inayotumiwa katika vituo hivyo kuwawezesha kuelewa masuala yanayohusiana na maendeleo vizuri zaidi kama alivyogundua Miguda-Atyang (2002).

Wakati uo huo, matumizi ya Kibukusu katika redio za FM yaliwezesha wasikilizaji kupata habari kuhusu siasa. Miongoni mwa siasa zilizoangaziwa ni zile za kaunti ya Bungoma. Siasa za kaunti hiyo zilizungumziwa kwa kina hususan kupitia kwa redio ya Sulwe FM. Vilevile, siasa za kaunti za Kakamega, Vihiga na Busia (uliokuwa mkoa wa magharibi, kabla ugatuzi) ziliweza kuangaziwa. Kwa mfano, wanasiasa mbalimbali wa kaunti ya Bungoma waliweza kualikwa katika mojawapo ya vituo hivyo vya redio za FM zilizotumia Kibukusu na kujadili kwa kina kuhusu siasa za

kaunti ya Bungoma na hasa zilizohusu jamii ya Waluyia. Wanasiasa vilevile waliweza kuwafikia wapigaji kura kwa urahisi zaidi kutokana na vituo hivi kutumia Kibukusu. Kwa kutumia vituo hivi, wanasiasa hao waliweza kuwafikia wananchi walioko mashinani kutokana na matumizi ya Kibukusu. Hili lilidhihirika kupitia kwa himizo lililotolewa na baadhi ya wanasiasa hao. Waliwashauri wakaazi wa Bungoma kusikiliza redio za West na Sulwe FM katika hafla mbalimbali.

Wakati uo huo, ilibainika kwamba wasikilizaji waliweza kuchangia sana katika mijadala ya kisiasa kwa njia huru, kwa ama kutoa maoni au kwa kuuliza maswali katika mijadala hiyo. Kwa mujibu wa wasikilizaji wa vituo hivyo, hawakuwa na tatizo lolote la kutoa michango yao katika mijadala. Hawakuwa na tatizo kuchangia mijadala kwa vile lugha iliyotumika ilikuwa lugha yao ya kwanza waliokuwa na umilisi. Kwa hivyo, wasikilizaji waliweza kushiriki kikamilifu katika mijadala hiyo. Kushiriki huko kikamilifu kuliakisi maoni ya Muthwii (2002), aliyehoji kwamba, vituo vya redio zinazotumia lugha za kiasili vimeongeza nafasi kwa wakaazi wa mshambani kujieleza na kutatua matatizo yao kutokana na umilisi zaidi katika lugha hizo.

Kwa hivyo, matumizi ya Kibukusu katika redio za FM yalijitokeza kama rasilimali kwa wasikilizaji kwa vile, ingawa lugha kama Kiswahili iliweza vilevile kutumika kuangazia masuala ya siasa, Kibukusu kilipotumika, masuala hayo ya siasa yalieleweka wazi zaidi kwa wasikilizaji. Aidha, redio zilizotumia Kiswahili ziliegemea zaidi siasa za nchi nzima huku muda uliotengewa siasa za kaunti ukiwa mfupi. Kwa hivyo, wasikilizaji walichangamkia zaidi matumizi ya Kibukusu kuangazia masuala hayo.

Kibukusu kilijitokeza vilevile kama rasilimali katika uangazaji wa masuala ya afya kwa wasikilizaji kwa kuwafahamisha kuhusu jinsi ya kuboresha afya zao. Urasilimali huu ulijitokeza kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, wasikilizaji walifahamishwa kuhusu dalili za magonjwa mbalimbali na kushauriwa watafute matibabu kwa wakati ufaao. Wakati uo huo, lugha hii iliwasaidia wasikilizaji kwa kuwashauri kuhusu pahali pa kutafuta matibabu mbalimbali. Hizo ni habari ambazo hazingeweza kuwasilishwa vyema kupitia kwa ama Kiswahili au Kiingereza. Kwa mujibu wa 57% (N=80) kati ya wasikilizaji 140 walioshiriki katika utafiti huu, usikilizaji wa vipindi vya afya hususan vilivyohusu dalili za magonjwa mbalimbali uliwawezesha kupata habari ambazo walizitumia kuboresha afya zao.

Vipindi vingi vilivyoangazia masuala ya afya vilijikita katika shughuli za afya kwenye kaunti ya Bungoma. Kutokana na hali hiyo, vipindi hivi viliweza kuangazia masuala hayo kwa uketo huku 93%, (N=130) kati ya wasikilizaji 140 walioshiriki katika utafiti huu wakisema kwamba matumizi ya Kibukusu kuangazia masuala ya afya yalikuwa na mvuto mkubwa. Walisema kwamba mvuto huo ulitokana na lugha iliyotumika. Lugha ya matumizi iliwawezesha kufahamu zaidi yaliyozungumziwa. Maoni ya wasikilizaji hao yanaafikiana na ugunduzi wa Kamau (2011), kwamba, vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili ni “rafiki” wa wasikilizaji atoaye habari wanazotumia kufikia maamuzi kuhusu masuala mbalimbali.

Wasikilizaji wa vituo hivyo vilevile walihoji, matumizi ya Kibukusu kuangazia masuala ya afya yalikuwa bora zaidi kuliko lugha zingine. Mtazamo huo wa wasikilizaji uliakisi maoni ya Castle (2014), anapohoji kwamba, lugha za kiasili zinapotumika, wasikilizaji wengi huweza kuupokea na kuelewa ujumbe kwa njia rahisi. Hata hivyo ilibainika kwamba wataalamu wengi wa afya waliotumika walikuwa ni wale wa tiba za kiasili. Kutokana na idhibati iliyotolewa na wasikilizaji,

watangazaji, wataalamu pamoja na dondoo zilizosikilizwa katika vipindi mbalimbali, Kibukusu kilijitokeza kama rasilimali kwa wazungumzaji wake. Urasilimali huu ulitokea katika vipindi vilivyokuwa vya jamii, uchumi, siasa na afya.

6.3 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu unatoa mchango wa kitaaluma kwa njia mbalimbali. Kwanza, matokeo ya utafiti huu yanatoa picha halisi ya mchango wa lugha za kiasili katika redio za FM nchini Kenya kwa maendeleo ya jamii husika. Hili linatokana na ithibati zinazotokana na utafiti huu zinazodhihirisha kwamba lugha za kiasili katika redio za FM ni rasilimali inayowawezesha wazungumzaji wake kufikia maamuzi faafu kuhusiana na masuala mbalimbali yanayowahusu.

Aidha, matokeo ya uchunguzi huu yatakuwa mchango kwa tafiti ambazo zimefanywa kuhusu matumizi ya lugha za Kiafrika katika vyombo vya habari. Hususan, matokeo haya yatatoa mchango katika tafiti za matumizi ya lugha za kiasili katika redio za FM.

Utafiti huu vilevile utakuwa wa manufaa kwa wapangaji lugha kitaifa na katika viwango vya kaunti. Katika viwango vya kitaifa, matokeo ya utafiti huu yatawezesha wapangaji lugha katika kiwango hicho kufikia maamuzi bora zaidi ya majukumu yanayofaa kupewa lugha za kiasili ikizingatiwa kwamba lugha hizo ni za thamani kubwa kwa wazungumzaji.

Katika viwango vya kaunti, matokeo ya utafiti huu yatawezesha wapangaji lugha katika viwango hivyo kuibuka na mikakati madhubuti ya kupanua matumizi ya lugha hizo hasa katika vyombo vya habari. Wakati uo huo, matokeo ya utafiti huu yatawezesha serikali za kaunti kukeza katika lugha za kiasili maadamu zinatekeleza majukumu muhimu katika mawasiliano yanayowahusu wakaazi wa kaunti hizo.

Hatimaye, utafiti huu utatoa mchango kwa ukuzaji na uhifadhi wa lugha za Kiafrika. Hili litawezekana iwapo lugha za kiasili zitafundishwa katika vyuo vikuu kwa lengo la kubadilisha mitazamo hasi kuhusiana na lugha hizo. Wakati uo huo, makuzi ya lugha hizo yataweza kufikiwa kupitia kwa tafiti zinazoweza kutekelezwa na taasisi za utafiti pamoja na vyuo mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba kuna udhibiti katika uundaji wa istilahi.

6.4 Mapendekezo ya Utafiti

Mapendekezo yanayowasilishwa hapa yanatokana na matokeo ya utafiti huu na yanalenga kuchangia katika kuimarisha lugha za kiasili kama rasilimali kwa wazungumzaji. Mapendekezo hayo ni:

Sheria za vyombo vya habari nchini Kenya zinafaa kuhusisha kipengele kinachopendekeza kwamba kila kituo cha redio kinachotumia lugha za kiasili kihakikishe kinatenga muda fulani kwa kipindi kinachofundisha umuhimu wa amani. Kwa kufanya hivyo, mitazamo hasi kuhusiana na matumizi ya lugha za kiasili itaweza kubadilika.

Vilevile, serikali ya kitaifa inapaswa ipunguze ushuru wa uchapishaji wa machapisho ya lugha za kiasili ili kuzipa motisha kampuni za uchapishaji kuchapisha vitabu kama vile makamusi ya lugha za kiasili.

Aidha, ufundishaji wa lugha za kiasili unapaswa ufufuliwe tena kama njia mojawapo ya kuzidumisha. Lugha hizi zinapokuzwa na kueleweka na watu wengi wa makabila mbalimbali, itakuwa vigumu kwa wazungumzaji wa lugha hizo kuzitumia visivyo kwa vile watajua kwamba zinaeleweka na hata wale wasio wazaliwa wake.

Serikali za kaunti zinapaswa zianzishe taasisi za kutafitia lugha za kiasili zilizoko katika kaunti husika ili zishughulikie tafiti katika hizo lugha. Taasisi hizo zinaweza kupewa majukumu ya uuandaji wa istilahi sanifu za kutumika katika matumizi ya kila siku ya lugha hizo. Taasisi hizo zinaweza vilevile zikapewa jukumu la kudhibiti istilahi zinazotumika katika lugha hizo za kiasili. Taasisi hizi zinafaa zifanye kazi na vyyo vikuu ama vilivyoko katika kaunti husika au vilivyoko karibu pamoja na wazee kutoka jamii husika walio na umilisi katika lugha hizo za kiasili. Kwa kufanya hivyo uibukaji wa istilahi kiholela utadhibitiwa.

Licha ya hayo, serikali za kaunti zinaweza vilevile kuimarisha lugha hizi za kiasili kwa kutoa matangazo na mipango yake kwa wakaazi kwa kutumia vituo vya redio vinavyotangaza kwa lugha za kiasili. Kwa kufanya hivyo, wazungumzaji wa lugha za kiasili wataona umuhimu wa lugha za kiasili.

Vilevile, serikali za kaunti zinaweza zikaanzisha sera za lugha katika viwango vya kaunti. Sera hizo zinafaa zisaidie kuimarisha lugha nyingi na uhifadhi wa lugha za kiasili, unaotambuliwa na Katiba ya Kenya ya 2010 (ROK, 2010).

Vyyo vikuu vinaweza pia vikachangia katika uimarishaji wa lugha za kiasili kwa kufundisha baadhi ya lugha za kiasili. Kwa kufanya hivyo, hali hiyo itaweza kubadilisha mitazamo hasi kuhusiana na matumizi ya lugha za kiasili. Hatimaye, Wakenya wanaweza kuanza kuzitazama lugha za kiasili kichanya.

Navyo vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili vinaweza kuboresha thamani ya vipindi vya masuala ya afya kwa kuwahusisha matatibu wa kisasa. Wataalam hawa wanaweza kuhusishwa katika vipindi vyao vinavyohusu masuala ya afya kusudi kuimarisha zaidi imani ya wasikilizaji katika yanayowasilishwa upande wa afya.

6.5 Mapendekezo kuhusu Tafiti za Baadaye

Utafiti huu ulilenga kuchunguza lugha za kiasili zinavyojitokeza kama rasilimali kwa wanaozizungumza. Utafiti uliteua vituo viwili vya redio; kile kilichotumia lugha ya kiasili pekee na kilichotumia ya kiasili na ya Kiswahili. Zifuatazo ni tafiti zaidi zinazoweza kufanywa:

1. Utafiti wa kulinganisha utendakazi wa vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili pekee na vile vinavyotumia lugha za kiasili pamoja na Kiswahili.
2. Utafiti linganishi kuhusu umaarufu kati ya vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili pekee na vile vinavyotumia lugha za kiasili na Kiswahili.
3. Tafiti kuhusu uzingatiaji wa madili ya uanahabari miongoni mwa redio za FM zinazotumia lugha za kiasili.
4. Kutafitia mchango wa vituo vya redio zinazotumia lugha za kiasili katika ubunifu wa istilahi mpya ambazo zimekubalika na kutumika.
5. Pana haja vilevile ya tafiti zaidi kufanyiwa nyanja zingine kama vile elimu na dini ambazo hazikutafitiwa na utafiti huu.

MAREJELEO

- Ary, D. na wenzake. (1972). *Introduction to Research in Education*. New York: Holtrine and Winston. Inc.
- Berg, B. L. (2004). *Qualitative Research Methods (5th ed)*. Boston: Pearson Education.
- Buliba, F. A. (2002). Lugha, Utamaduni na Jamii, Katika Maendeleo Kitaifa na Kimataifa. Katika Shitemi, N. L. , Noordin, M., Opijah, A. na Mukuria, D (wh). *Kiswahili A Tool For Development, the Multidisciplinary Approach*, uk 52-59. Eldoret: Moi University Press.
- Calhoun, C. Light, D. & Keller, S. (1995). *Understanding Sociology*. New York: Glencoe/McGraw-Hill.
- Castle, P. (2014). The Waves That Change? Agricultural Advice Via Radio in Local Languages: Benefits and Gaps. At *Basel University's Centre for African Studies*, Petersgraben 11, 4051 Basel, Switzerland.
- Chabata, E. (2001). Monolingual Lexicography and Linguistics Variation in Shona. Katika Mdee na Mwansoko (wh), *Makala ya Kongamano la Kimataifa, Kiswahili 2000*, uk 266-278. Dar es Salaam: TUKI.
- Crowley, T. (2007). *Field Linguistics, A Beginner's Guide*. New York: Oxford University Press.
- Dik, S.C. (1981). *Basic Principals of Functional Grammar in Syntax and Semantics, Volume 13*. New York: Academic Press.
- Evariste, N. (2001). Uhusiano Kati ya Ulughamoja na Maendeleo. Katika Mdee na Mwansoko (wh), *Makala ya Kongamano la Kimataifa, Kiswahili 2000*, uk 95-108. Dar es Salaam: TUKI.
- First Bungoma County Integrated Development Plan 2013- 2017. Bungoma: DenKev Enterprises and Company Limited.
- Fraenkel, J. and Wallen, N. (1993). *How to Design and Evaluate Research in Education Second Edition*. New York: Mc Graw-Hill Inc.
- Gachathi, P.J. (1976). *Report of The National Committee on Educational Objectives and Policies*. Nairobi: Government Printers.
- Gathigi, G. W. (2009). "Radio Listening Habits Among Rural Audiences: an Ethnographic Study of Kieni West Division in Central Kenya." Tasnifu ya Uzamifu, the Sripps College of Communication of Ohio University.
- Gina, W. (2001). *The Post Graduate Research Handbook*. London: Palgrave Study Guides.
- Githethwa, N. (2008). *The Way Forward for Community Radios in Kenya*. Proceedings of The National Seminar held in Nairobi on 25-26th June 2008. Nairobi: Econews Africa.

- Halliday, M.A.K. (1994). *Functional Grammar, 2nd Edition*. London: Arnold.
- Halliday, M.A.K. and Matthiessen, C. (2004). *An Introduction to Functional Grammar 3rd Edition*. London: Arnold.
- Iraki, F. K. (2010). Culture and Development: Lessons Learnt From The Post-Election Violence in Kenya. *The Journal of Language, Technology and Entrepreneurship in Africa*, 2. 1: 261-276.
- Kachale, E. C. (2008). Accessibility of ICT to Speakers of Indigenous African Languages. *Katika Open Space*, Vol 2, Issue 3, uk 88-94. Johannesburg: OSISA.
- Kamau, M. M. (2011). *Vernacular Radio and Democracy in Kenya: A Historical Reconstruction of Audiences' Usage of Kass and Inooro Radio Stations in Uasin-Gishu District*. Tasnifu ya Uzamifu. Eldoret: Chuo Kikuu cha Moi.
- Kamunge, M. J. (1988). *Report of The Presidential Working Party on Education and Manpower Training for The Next Decade and Beyond*. Nairobi: Government Printers.
- Kanana, F. E. (2013). Examining African Languages as Tools for National Development: The Case of Kiswahili. *Katika The Journal of Pan African Studies*, uk 41-68. Vol. 6, no. 6, November 2013.
- Khamisi, A. M. (2008). Filosofia ya Kukuza Lugha. *Katika Kiango (mh). Ukuzaji wa Istilahi za Kiswahili*, uk 1-9. Dar es Salaam: TUKI.
- KNBS. (2013). *Exploring Kenyans Inequality, Pulling Apart or Pulling Together?* Nairobi: Kenya National Bureau of Statistics.
- Koehn, D. K. (1999). *Totally Integrated Quality Education and Training (TQET). Report of The Commission of Education into The Education System of Kenya*. Nairobi: Government Printers.
- Kombo, D. K. and Tromp, L.A. (2006). *Proposal and Thesis Writing, An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.
- Kothari, C. R. (2004). *Research Methodolgy, Methods and Techniques*. Second Edition. New Delhi: Wiley Eastern Limited.
- Kumar, R., (2011). *Research Methodology: Astep by Step Guide for Beginners*. London: Sage Publications Ltd.
- Luoch, O. T. and Ogutu, E. (2002). The Use of Mother Tongue and Tribalism a Misconceived Association. *Katika: Owino, R. F (mh). SPEAKING AFRICAN, African Language for Education and Development*, uk 89-98. Cape Town: CASAS.
- Makunja, G. S. (1995). Sarufi na Msamiati wa Kiswahili." *Katika: Vyombo Vya Habari. Katika Mlacha (mh), Kiswahili na Vyombo vya Habari*. Dar es Salaam: TUKI.
- Marshall, C. and Rossman, G. B. (2011). *Designing Qualitative Research (5th ed)*. Los Angeles: Sage Publications Ltd.

- Mbeke, P.O. and Mshindi, T. (2008). *Kenya Media Sector Analysis Report*. Canadian International Development Agency-Kenya.
- McCombs, M. and Shaw, D. (1993). The evolution of Agenda-Setting Research: Twenty-Five Years in The Market Place of Ideas. *Journal of Communication*, 43, 58-67.
- Mdee, J. S. (1999). Matumizi ya Istilahi katika Kiswahili na Jinsi Yanavyoathiri Mawasiliano. Katika Tumbo-Masabo na Mdee (wh). *Mulika nambari*. 25, uk 37-48. Dar es Salaam: TUKI.
- Media Council of Kenya. (2012). Performance of Vernacular Radio Stations in Kenya, *September/ October 2011 Monitoring Report. Media*. Kenya. Government Press. Nairobi.
- Merriam, S. B. (1988). *Case Study Research in Education: A Qualitative Approach*. San Francisco: Jossey-Bass.
- Michieka, M.M. (2011). Language in Education and the role of Applied Linguistics in Kenya. *Journal of Language, Technology and Entrepreneurship in Africa Vol. 3 No. 1*.
- Miguda-Attyang, J. (2002). Language, Communication and Poverty Allevation. Katika: Owino, R. F (mh). *SPEAKING AFRICAN, African Language for Education and Development*, uk 293-300. CapeTown: CASAS.
- Mlacha, S. A. K. (1995). Vyombo Vya Habari na Usambazaji wa Fasihi. Katika: Mlacha (mh) *Kiswahili Vyombo Vya Habari*. Dar es Salaam. TUKI.
- Mohochi, E. S. (2006). Kiswahili na Vyombo Vya Habari Nchini Kenya: Makosa Matumizi ya Lugha. Katika Massamba (mh) *KISWAHILI Juzuu*. 69, uk 52-62. Dar es Salaam: TUKI.
- _____ (2007). Kiswahili, Usambazaji wa Habari na Uhamishaji wa Umma kwa Ajili ya Maendeleo. Katika: Senkoro, F.E.M.K (mh). *Lugha na Fasihi ya Kiswahili, Afrika Mashariki*, uk 114-128. Dar es Salaam: CHAKAMA.
- Morse, J. (1994) *Critical Issues in Qualitative Research Methods*. Thousand Oaks, CA: Sage.
- Moto, F. (2002). African Languages and Crisis of Identity, The Case of Malawi. Katika Owino, R. F (mh). *SPEAKING AFRICAN, African Language for Education and Development*, uk 33-44. Cape Town: CASAS.
- Msanjila, Y.P. (2002). Dhima ya Lugha ya Kiswahili katika Karne ya Ishirini na Moja. Katika: Kihore (mh). *KISWAHILI Juzuu* 65, uk 16-23. Dar es Salaam. TUKI (1997).
- Muaka, L. (2011). "Language Perceptions And Identity Among Kenyan Speakers uk 217-230." Katika: Bokamba na Wenzake (wh). *Proceedings of the 40th Annual Conference on African Linguistics*.

- Mudhune, S. E. (2002). African Languages in The Manufacturing Industry. The Case of Kenya. Katika: Owino, R. F (mh). *SPEAKING AFRICAN, African Language for Education and Develoment*, uk 301-30. Cape Town: CASAS.
- Mugambi, P. M. (2007). Kutumia Utofauti wa Lugha ili Kuleta Maendeleo ya Kitaifa & Maeneo. Katika Senkoro, F.E.M.K (mh). *Lugha na Fasihi ya Kiswahili, Afrika Mashariki*, uk 45-53. Dar es Salaam: CHAKAMA.
- Mugenda, O. M. and Mugenda, A. G. (2003). *Research Methods, Qualitative & Quantitive Approaches*. Nairobi: ACTS Press.
- Mukoma, N. (2014, November 22). Time To Save African Languages from Extinction. *Standard on Saturday*, uk 26 – 27.
- Muluka, B. (2010, March 22). Take or Leave, The Key to Ethnic Unity Lies in FM Stations. *The Standard*, uk 15.
- Musau, P. M. (2002). The Development of African Languages for Modern Discourse, The Case of Kiswahili. Katika Owino, R. F (mh). *SPEAKING AFRICAN, African Language For Education and Develoment*, uk 253-265. CapeTown: CASAS.
- Mutahi, K. (2002). Kiswahili as A Tool of Development in Kenya. Katika Shitemi, N. L. , Noordin, M., Opijah, A. na Mukuria, D (wh). *Kiswahili A Tool For Development, the Multidisciplinary Approach*, uk 8-13. Eldoret: Moi University Press.
- Muthwii, J. M. (2002). Status Language Planning in Multilingual States in Africa. Katika Owino, R. F (mh). *SPEAKING AFRICAN, African Languag for Education and Develoment*, uk 77-87. Cape Town: CASAS.
- Mwita,B. M. (2002). Rural Development in Kenya: Is Kiswahili The Language of Hope or Despair? Katika Shitemi, N. L. , Noordin, M., Opijah, A. na Mukuria, D (wh). *Kiswahili A Tool For Development, the Multidisciplinary Approach*, uk 124-132. Eldoret: Moi University Press.
- Nachmias, C. F. and Nachmias, D. (1996). *Research Methods in the Social Sciences (5th ed)*. London: St Martin's Press.
- Ndii, D. (2010). Decentralization in Kenya Background Note.
- Ngugi, M. P. (2013). The New Constitution and Teaching of African Languages: What is The Way Forward for Kenya. *International Journal of Arts and Commerce Vol 1. No. 3*.
- Nyika, A. (2015). Use of Mother Tongue at Universities in a Global Context. *South African Journal of Science Vol. 111 No. ½ January/ February*.
- O'leary, Z. (2004). *The Essential Guide to doing Research*. New Delhi: Vistaar Publications.
- Ochieng, P. (2014, February 23). Why We Should Invest Heavily in All Three Languages. *The Sunday Nation uk 13*.

- Ogechi, N.O. and Bosire, E.O. (2010). *Identity And The New Communication Technologies; Evidence from Kenya*. (Haijachapishwa).
- Okombo, O. (2014, April 12). Languages Hold The Key to Kenya's Economy. *The Saturday Nation* uk 21.
- _____ (2014, February 1). Teach Children their Mother Tongue. *The Saturday Nation*, uk 25
- Okoth, E. (2015). *Emergence and Growth of Vernacular radio in Kenya. A Case Study of Radio Having a Positive Economic Impact*. Reuters Institute for The Study of Journalism. University of Oxford.
- Ominde, S. H. (1964). *Kenya Education Commission Report*. Republic of Kenya. Nairobi: Government Printers.
- Ongarora, D. O. (2002). African Languages in Development Prospects & Encumbrances. Katika Owino, R. F (mh). *SPEAKING AFRICAN, African Language for Education and Develoment*, uk 65-75. CapeTown: CASAS.
- Onyebadi, U. (2008). *Towards an Examination and Expansion of The Agenda Setting Theory: Did The Media Matter in Kenya's Presidential Election, 2007?* Tasnifu ya Uzamifu. University of Missouri.
- Orao, J. (2009). Kenyan Indigenous Languages And Mass Media: Challenges And Opportunities. *Stellenbosch Papers in Linguistics PLUS*. Vol.38.2009, 77-86.
- Orodho, A. J. and Kombo, D. K. (2002). *Research Methods*. Nairobi: Kenyatta University, Institute of Open learning.
- Oso, W.Y and Onen, D. (2005). *A General Guide To Writing Research Proposal And Report, A Handbook for Beginning Researchers*. Kisumu: Option Printers and Publishers.
- Patton, M. Q. (1990). *Qualitative Evaluation and Research Methods* (2nd ed.). Newbury Park, CA: Sage.
- Peil, M. (1995). *Social Science Research Methods, A Handbook for Africa* (Second Revised Edition). Nairobi: East African Educational Publishers.
- Prah, K. K. (2002). Researching African Languages For Scientific & Technological Development. The CASAS Experience. Katika: Owino, R. F (mh). *SPEAKING AFRICAN, African Language for Education and Develoment*, uk 9-16. Cape Town: CASAS.
- _____ (2005). *Speaking African on The Radio*, A CASAS Study in Cooperation With The UNESCO Communication Development Division. Cape Town: Centre for Advanced Studies of African Society (CASAS).
- _____ (2008). African Languages In a Globalising World, uk 19-23. *Open Space, Vol 2, Issue 3*. Johannesburg: OSISA.

- Quane, A and Glanz, C. (2010). Why and How Africa Should Invest in African Languages and Multilingual Education, An Evidence and Practice Based Policy Advocacy Brief. UNESCO Institute For Life Long Learning.
- Roberts, M. J. (2009). Conflict Analysis of the 2007 Post-election Violence in Kenya
- ROK (2010). *The Constitution of Kenya, 2010*. Nairobi: The Government Printer.
- Ryanga, C. W. (2002). Indigenous Languages & National Identity, The Kenyan Experience. Katika Owino, R. F (mh). *SPEAKING AFRICAN, African Language For Education and Develoment*, uk 55-63. Cape Town: CASAS.
- Sankoff, D. (2001). Statistics in Sociolinguistics.(Mestchrie, R). *Consise Encyclopedia of Sociolinguistics, Elsevier B.V, uk 828-834*. University of Cape Town: South Africa.
- Seidu, A., Andani, A. and Abdul-Malik, A. (2011). The Role of Community Radio in Livelihood Improvement: The Case of Simli Radio. Field Actions Science Reports Vol. 5 .
- Shitemi, N. L. (2002). Languages as a Tool for Development: Issues to Ponder. Katika Shitemi, N. L. , Noordin, M., Opijah, A. na Mukuria, D (wh). *Kiswahili A Tool For Development, the Multidisciplinary Approach*, uk 14-20. Eldoret: Moi University Press.
- _____. (2010). *Lugha, Mawasiliano na Maendeleo Mashambani*. (Haijachapishwa).
- Simala, I. K. (2002). Empowering Indegenous African Languages for Sustainable Development. Katika Owino, R. F (mh). *SPEAKING AFRICAN, African Language for Education and Develoment*, uk 45-53. Cape Town: CASAS.
- Singh, K. (2007). *Quantitative Social Research*. New Delhi: Sage Publications India Pvt Ltd.
- Singleton, R. A. (1993). *Approaches to Social Research*. NewYork: Oxford University Press.
- Somekh, B and Lewin, C. (2005). *Research Methods in the Social Sciences*. New Delhi: Vistaar Publications.
- Thatiah, J. (2014. November, 1). Teach Children their Mother Tongue. *The Saturday Nation*, uk 14.
- The Kriegler Report on Post Election Violence in Kenya, 2008*.
- Wabwire, J. (2013). The Role of Community Radio in Development of the Rural Poor. New Media and Mass. *The International Institute for Science, Technology and Education (IISTE) Journal* Vol.10, 2013, uk 40 – 46.
- Wanjiku, R. (2009). *Kenya Communications Amendment Act (2009) Progressive or Retrogressive?* Nairobi: Association for Progressive Communications (APC).

- Were, W. (2014). *A Traditional Ritual Ceremony As Edurama: A Case Study Of Imbalu Ritual Among The Bukusu Of Western Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu. Nairobi. Chuo Kikuu cha. Kenyatta.
- Wolff, E. H. (2002). The Heart of The African Languages, Question in Education. Katika Owino, R. F (mh). *SPEAKING AFRICAN, African Language for Education and Develoment*, uk 129-148. CapeTown: CASAS.
- Wolff, E. H. (2006). The Language Factor in Discourse on Development And Education. Katika Kembo-Surre na Ogechi (wh), *Language Planning For Development in Africa*, uk 1-22. Eldoret: Moi University Press.
- Yates, S.J. (2004). *Doing Social Science Research*. London: Sage Publication Ltd.

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO I: Hojaji kwa Wasikilizaji

Nambari ya mhojiwa.....

Hujambo,

Ninafanya utafiti kuhusu lugha za kiasili kama rasilimali ya jamii kupitia redio za FM: uchunguzi wa kaunti ya Bungoma. Ni matarajio yangu kwamba utafiti huu utasaidia kutoa mapendekezo jinsi ya kuboresha matumizi ya lugha za kiasili kupitia redio za FM. Wewe ni kati ya wasikilizaji walioteuliwa kushiriki katika utafiti huu. Kwa hivyo unaombwa ujaze hojaji kwa njia sahihi iwezekanavyo kisha uirudishe. Ninaahidi kwamba habari zote utakazotoa zitahifadhiwa kwa siri wakati wa utafiti na baada ya utafiti huu. Ninashukuru kwa kujitolea kwako kuwezesha utafiti huu ukamilike.

Maagizo

Tunakuomba uweke mviringo (circle) kwa jibu utakaloteua

a) Habari za kimsingi

1. Jinsia yako
 - a) Mwanamume
 - b) Mwanamke
2. Umri wako
 - a. Miaka 15 – 20
 - b. Miaka 21 – 30
 - c. Miaka 31 – 40
 - d. Miaka 41 – 50
 - e. Miaka 51 – 60

- f. Zaidi ya miaka 60
- 3. Kiwango chako cha elimu
 - a. Sijasoma
 - b. Shule ya msingi
 - c. Shule ya Sekondari
 - d. Elimu ya juu
- 4. Kazi unayofanya.
 - a. Sifanyi kazi yoyote
 - b. Mkulima
 - c. Mfanyi biashara
 - d. Mwalimu
 - e. Tabibu (Medic)
 - f. Kama si kati ya hizo zilizoorodheshwa, itaje.....

b) Lugha zizozungumzwa na usikilizaji redio

- 5. Wewe huzungumza lugha gani?
 - a. Kiteso
 - b. Kibukusu
 - c. Kitachoni
 - d. Kiwanga
 - e. Kisabaoti
 - f. Kama si kati ya hizo zilizoorodheshwa, basi ni gani?.....
- 6. Wewe husikiliza redio kwa muda gani kwa siku?
 - a. Sisikilizi kabisa
 - b. Saa moja
 - c. Saa mbili

- d. Saa tatu
 - e. Zaidi ya saa tatu
 - f. Siku nzima
7. Je, wewe husikiliza redio za FM za lugha za kiasili?
- a. Ndiyo
 - b. Hapana
8. Iwapo wewe husikiliza, huzisikiliza redio hizo wakati gani?
- a. Asubuhi kabla kwenda kazi
 - b. Mchana
 - c. Jioni
 - d. Usiku
9. Iwapo wewe husikiliza redio za FM zinazotumia lugha za Kiasili, ni redio gani ambazo wewe husikiliza?
- a. West FM
 - b. Sulwe FM
 - c. Redio Mambo
 - d. Mulembe FM
 - e. Zote zilizo rodheshwa
10. Toa sababu za wewe kuteua kituo cha redio kinachotumia lugha ya Kiasili unachosikiliza
- i).....
 - ii).....
11. Wewe husikiliza vipindi gani vya redio?
- a. Vya habari tu
 - b. Vya masuala ya afya tu

- c. Vya masuala ya siasa tu
- d. Vya masuala ya uchumi tu
- e. Vya masuala ya jamii
- f. Vipindi vyote.

12. Unapenda kusikiliza zaidi vipindi gani kati ya vilivyoorodheshwa hapo juu?

.....

.....

.....

i) Je unafurahia uwasilishaji wa vipindi hivyo?

- a. Ndiyo kidogo
- b. Ndiyo
- c. Ndiyo kabisa
- d. Sina uhakika

ii) Toa sababu

c) Maoni kuhusu manufaa ya vipindi.

13. Je, vipindi unavyosikiliza hukufaidi kwa njia gani?

- a. Havinifaidi sana
- b. Hunifaidi kidogo
- c. Havinifaidi kabisa
- d. Havinifaidi
- e. Sina uhakika

14. (i). Ni kipindi/vipindi gani vinavyowasilishwa kwa lugha za kiasili ambavyo hukufaidi zaidi?.....

.....

.....

15. Taja baadhi ya manufaa unayopata kutokana na usikilizaji wa vipindi ulivyotaja katika swali la 14 hapo juu.

i).....

ii).....

iii).....

iv).....

v).....

16. Je, ni manufaa gani unayopata kutokana na matumizi ya Kibukusu katika uwasilishaji wa vipindi ambayo hungepata laiti Kiswahili au lugha ingine ingetumika?

i).....

ii).....

iii).....

iv).....

d) Changamoto za matumizi ya lugha za kiasili katika redio

17. (i) Kwa maoni yako, ni changamoto gani zinazokumba matumizi ya lugha za kiasili kupitia kwa redio za FM?

i).....

ii).....

iii).....

iv).....

(ii). Je, serikali inafanya jitihada tosha kukuza lugha za kiasili kupitia redio za FM?

a. Ndio

b. Hapana

c. Sina uhakika

(iii). Toa sababu za jawabu ulilotoa hapo juu.....

.....

18. Kwa maoni yako, yepi yafaa kufanywa ili kuimarisha matumizi ya lugha za kiasili kupitia redio za FM?

i.

ii.

iii.

KIAMBATISHO II: Hojaji kwa Watangazaji

Hujambo,

Ninafanya utafiti kuhusu lugha za kiasili kama rasilimali ya jamii kupitia redio za FM; uchunguzi wa kaunti ya Bungoma. Ni matarajio yangu kwamba utafiti huu utasaidia kutoa mapendekezo jinsi ya kuboresha matumizi ya lugha za kiasili kupitia redio za FM. Wewe ni kati ya wanahabari walioteuliwa kushiriki katika utafiti huu. Kwa hivyo, unaombwa ujaze hojaji kwa njia sahihi iwezekanavyo kisha uirudishe. Ninaahidi kwamba habari zote utakazotoa zitahifadhiwa kwa siri wakati wa utafiti na baada ya utafiti huu. Ninashukuru kwa kujitolea kwako kuwezesha utafiti huu ukamilike.

Maagizo

Tunaomba uweke mviringo (circle) kwa jibu utakaloteua

a.Habari kuhusu kituo cha redio na lugha za matumizi

1. Kituo chako cha redio ni kipi?.....
2. Kituo chenu cha redio hutumia lugha zipi?.....
.....
3. Lugha za kiasili katika kituo chenu cha redio hutumika kwa saa ngapi?.....
.....
4. Je, huwa unahusika na matangazo ya lugha gani?
 - a). Kiswahili
 - b). Kibukusu
 - c). Kisabaot.
 - d). Kiteso.

b. Habari kuhusu vipindi vinavyowasilishwa kwa lugha za kiasili

5. Ni vipindi vya aina gani hufanywa na kituo chenu cha redio kwa kutumia lugha za kiasili?

- a. Vya masuala ya jamii.
- b. Vya masuala ya uchumi.
- c. Vya masualaya siasa.
- d. Vya masualaya afya.
- e. Vya masuala yote yaliyoorodheshwa.

6. Kila mojawapo ya masuala hayo hutengewa muda gani?.....

.....

7. Ni vikundi gani vya wasikilizaji mnavyolenga katika matangazo yenu mnapotumia lughazakiasili?

- a) Watoto.
- b) Vijana.
- c) Watu wa umri wa kati (wastani).
- d) Wazee.
- e) Watu wa umri wote.

c. Habari kuhusu lugha za kiasili kuwa rasilimali

8. i). Kwa maoni yako, je matumizi ya lugha za kiasili kwa redio ni rasilimali kwa wazungumzaji wake?

- a) Ndio
- b) Hapana.
- c) Sina uhakika.
- d) Fafanua jawabu lako

9. Ni masuala gani ambayo hayangewafikia wazungumzaji wa Kibukusu iwapo

Kiswahili kingetumika kwa nafasi yake?

.....

10. Baadhi ya watu wanaamini kwamba vituo vya redio vinavyotumia lugha za kisili

ni vya muhimu sana kwa wazungumzaji lugha hizo. Wegine husema, vituo hivyo vinafaa kuangaziazaidi lugha kuu zinazoeleweka na watu wengi. Je, msimamo wako ni upi kuhusiana na mitazamo hii miwili?

.....

d. Jinsi ya kuimarisha lugha za kiasili kupitia redio za FM

11. Kwa maoni yako, ni mchango gani mkubwa unaotolewa na lugha za kiasili kupitia kituo chenu cha redio?.....

.....

12. Kwa maoni yako, kituo chenu cha redio kinachotumia lugha za kiasili kina umuhimu gani kikilinganishwa na vyombo vingine, kuimarisha lugha za kiasili?.....

13. Ni mbinu gani zaidi zinazoweza kutumika kuimarisha lugha za kiasili kupitia redio za FM?.....

e). Changamoto za matumizi ya lugha za kiasili katika redio za FM

14. Ni changamoto gani zinazokumba kituo chenu cha redio, lugha za kiasili zinapotumika?.....

.....

.....

15. Je, changamoto hizi zinaweza kutatuliwa vipi?.....

.....
.....

16. Kwa maoni yako, ni kwa kiwango kipi kuna udhibiti katika sekta ya utangazaji unaofanywa na serikali?.....

.....
.....
.....

KIAMBATISHO III: Mwongozo wa Usaili kwa Mhariri

1. Masuala gani huangaziwa katika vipindi vifuatavyo?
 - d. Jamii
 - e. Afya
 - f. Uchumi
 - g. Siasa
2. Maadamu Kibukusu kinatumika katika masuala hayo, je, kimehitimu kuwa lugha ya kisasa? Tetea hoja yako.
3. Wewe kama mhariri, huhakikisha vipi kwamba wasikilizaji wanafaidika kutokana na vipindi vya jamii, afya, uchumi na siasa?
4. Je, kwa maoni yako, lugha za kiasili zina uwezo wa kuangazia masuala ya jamii, afya, uchumi na siasa kikamilifu? Tetea jawabu lako.
5. a). Je, lugha za kiasili zinapotumika katika redio za kiasili, ni rasilimali kwa jamii husika?
 b). Ikiwa ndio, toa sababu.
6. Ni masuala gani ambayo hayangewafikia wakaazi wa kaunti ya Bungoma kama Kibukusu kisingetumika?
7. Je, kuteuliwa kwa Kiswahili kama Lingua franca ya Afrika Mashariki kumeathiri vipi matumizi mapana ya lugha za kiasili?
8. Ni, mikakati gani ambayo mmeweka kuongeza idadi ya wasikilizaji wa lugha za kiasili mnazotumia katika kituo chenu cha redio?
9. Ni mikakati gani ambayo mmeweka kuhakikisha kwamba mawasiliano baina yenu na wasikilizaji wenu hayaathiriki kutokana na wasikilizaji wenu kukosa umilisi katika lugha mnayotumia?

10. Je, matumizi ya Kibukusu kupitia redio yenu ya FM yametokana na msukumo wa wingi wa wazungumzaji au urasilimali wake kwa wazungumzaji?
11. Matumizi kimakusudi ya Kibukusu katika redio yenu yameathiri vipi mwelekeo wa matumizi ya lugha za kiasili katika kaunti ya Bungoma?
12. Je, changamoto zipi hujitokeza lugha za kiasili zinapotumika katika redio za FM kuangazia masuala ya jamii, afya, uchumi na siasa?
13. Pendekeza suluhisho kwa changamoto hizi.

KIAMBATISHO IV: Mwongozo wa Usaili kwa Mtangazaji

1. Je, wewe huhusika katika utangazaji wa kipindi/vipindi vinavyohusu masuala gani?
2. Kwa maoni yako, usikilizaji wa vipindi vyenu vinavyowasilishwa kwa Kibukusu ni asilimia gani?
3. Je, kwa maoni yako, matumizi ya Kibukusu katika kituo chenu cha redio yana wafuasi wengi?
4. Je, kuna upigaji wa simu wakati wa uwasilishaji vipindi kutoka kwa wasikilizaji wenu?
5. Iwapo upo, ni kwa kiwango kipi?
6. Ni mbinu gani mnayotumia kuwezesha jamii inayosikiza kituo chenu iielewe jamii yao na mazingira yao kwa upana na undani?
7. Kituo chenu huhakikisha na kushiriki katika maamuzi na majadiliano kuhusu masuala tofauti yanayoathiri maisha yao kiviipi kwa kutumia Kibukusu?
8. Je, kwa maoni yako, Kibukusu ni rasilimali kwa wazungumzaji, kinapotumika katika redio za FM? Tetea hoja yako.
9. Orodhesha baadhi ya changamoto za matumizi ya Kibukusu kuangazia masuala ya jamii, siasa, afya na uchumi.
10. Je, changamoto hizi zinaweza kutatuliwa vipi?

KIAMBATISHO V: Mwongozo wa Usaili kwa Magalacha

1. Wewe ni mtaaalamu katika masuala gani?
2. Je, umesomea kazi yako?
3. Iwapo umeisomea, ni hadi kiwango gani?
4. Mnapowasilisha vipindi kuhusu taaluma yako, huwa mnatumia lugha gani?
5. Changamoto gani mnazokumbana nazo mnapotumia lugha hiyo kuangazia masuala ya taaluma yako?
6. Pendekeza njia zinazoweza kutumika kutatua changamoto hizo.
7. a). Kwa maoni yako, lugha za kiasili zinaweza kuwa rasilimali kwa wazungumzaji wake?
b). Tetea jawabu lako.

KIAMBATISHO VI: Baadhi ya Data Iliyochanganuliwa

1. Ninyosia papa we babana, Nekesa we Kibichori, Wafula we Sanandiki nende Joseck we Khuchwele. Burume, ambabolela endi bache mumikunda khuraka khubela efula yolile asi.
2. Ningila mumilimo nende ambano: Maraka, Wanyonyi nende Wafula boosi bafundi be Chinju be Enakalira. Embabolela endi bachape ekasi ne kamani.
3. Endotia bakosi abano nende chipepapak: Wekesa Nyongesa, Simiyu Barasa nende Dorcas Nakhumicha.
4. Sipindi sya Lotia bakosi syachenjile liba le omusakhulu wase. Anyuma ao abele omusakhulu wase salotanga mapema ta. Ne lundi abele alotanga namelile kabisa. Lelo omusakhulu wase oli omufundi we chinju, echa mapema mala nakulilekho babana sisindu khukhwama anje khurekelesia Sulwe.
5. Ese mbuka busa sikila babandu balala hasa wanasiasa ne babeyanga amilukha kye kamasika! Onyola omundu kenyokha amasika ali, ese enga MCA namwe enga Omubunge we lubeka luno, nakhekombile khusubisia namulekhwa nende bafubi endi, endema nenabo. Omwana wa marehemu wamalile kamasomo ke endererwa oyo ndamubukula emuwe kimilimo kusudi ayete babasie. Mwanasiasa chana alekha khukhola enga ne kalaka. Oba oli namulekhwa namwe omwana wa marehemu amulondakho khumukhebusia endakano chana, ne mwanasiasa oyo abarafwilila ne khubatimania. Ese mbuka busa!
6. Kumwima enga kuno kuli kwe embelekeu saana. Onyola omundu akobola engo ne anyola omukhaye wewe karere kumunwa khu kundi. Enga ne amureba ali sina sibi, ne omukhaye oyo aloma ali ese mayi masala wase mungo omuno kakhayile. Omundu oyuno enga ne aulila aro ne acha khu mawe ne khukhwanja khumurafwilila ali ewe mayi lekhana nende enju yase kabisa, oli khowenya khufuna enju yase ne wilemo namwe? Ese embuka saana enbelekeu ye lukano oluno!
7. Bodaboda be chimbeka cha Mukuyuni bamema babana bakhana be bikuli balekhe khukhola busale ne babana bano ne khubawa bisombo. Bodaboda



benabo bakhola bibima bibii byenebo khu bana chirika che babana babwe!
Balekhekimima kimibii kyenekyo enga ta khuile kamasina kabwe khu babami
mala babatile.

8. Bamenywa be Embakalo, Naitiri besindukhile lifwa la mwalimuniye berire silo sye likoloba mala ne bara kumubili kwewe khumwanda kumubofu kucha Naitiri. Balikhebekicha babemelesi be bulindi nalimo omwimelesi we bapolisi mbo batile khangu babandu baberile mwalimu oyoo enga ta bacha khukhwimurukula kukhwenya babemelesi abo bauyiswe.
9. Engokho etwaya khu soko ye Kimilili luno elikhekula chisilingi chimia saba, sisonga chimia chirano ne chinywinywi chisilingi chimia chibili. Chikhafu nacho, chiunwa chakhakulanga khusilingi chielefu salasini, chieyi chielefu ishirinanane, che kamabele chielefu salasini na tano ne chimosoti chielefu ishirina nane.
10. Bukusi ne bukulani sinjetanga khumanya ebei ye bibiayo hata nakhakosa khuchakhusoko esiku endala. Sinjetanga khumanya bibiayo khebikendela mu silingichinga ne ekhanyola hasara ta. Nono nenja khukula sisoyayo khumulimi, endamo chisendi nicho endi nende bung'ali endi chilakobola. Anyuma aoo, khwabahatisyanga busa mala alala khunyola hasara embofu kakila abele onyala wakula sisoyayo khumulimi khusendi chingali oli ocha khusoko ne onyola ombo bibiayo bili asi sana.
11. Chiredio chefwe chino che Lubukusu ne chikhecha ta napanga siibi! Bachurusi abele bamenya khukhubeya alubeka lwe ebeyi ye bibiayo. Lelo naona kakila ndekeresyanga kachilila khu chisoko, emanya bukusi bwe bibiayo ne khacha khukula namwe khukusya ta.
12. Kamatangasio ke ekampuni ya Syngenta kanjetile lukali po. Esese abele bhiukhaa khebimalila kamaindi. Lakini enga nenaulila kamalesi kamaya ka Actelic gold khubirira West FM, nacha nakakula mala kanjeta lukali. Kamalile bhiukha mumaindi kase. Andi kamakunia kase salasini ke kamaindi kosi bufu busa.
13. Efwe balimi be Nzoia sekhekhubona bukhala bwe khuraka kimiba ta ne sikilaekampuni selakhurunganga ta enyuma we khurema kimiba! Nzoia

seyakhurungile kamapesa kefwe khu miesi sita ta. Sisyuma sye Nzoia esino syakhulerere kumtambo saana ne khubela efwe khweyikina kimiba kyong'ene. Bona babana benyekhana khucha ebikuli mala sebakhurungile ta. Khokhusaba wanasiasa befwe bengilile akari khubona mbo khwarungilwe chisendi chefwe chili Nzoia.

14. Serikali yefwe ye ekaunti ye Ebungoma eli kherumikhila chisendi chefwe bubu. Badala ye khuchirumikhila khurusyayo bumanani, khebonaka busa chisendi chenyecho! Chiredio chefwe enchino che Lubukusu cha khuyetile khura abuwanga bikholwa bye buhalukha bibikholeka mukaunti ye Ebungoma.
15. Chisilingi emia na ishirini cha Kenya chichenjebwe khudola endala ya Amerika, esilingi endala ya Kenya khu chisilingi salasini na tano che Ebuganda ne esilingi endala ya Kenya khu silingi ishirini na tano cha Tanzania.
16. Khunyolanga kamakeni ka siasa kakekholekhanga mukaunti ya Bungoma khubirira khu miinda kya Sulwe nende West FM.” Anyuma awo abele sonyola kamakeni kenako esiku eng'ene ta, ne aandi hata sekhwanyolanga kamakeni kenako khubirira kimiinda kikyabao ta. Nono chiredio echino chakhuyetile khumanya kasiyasa chichikholekha mkaunti mapema.

KIAMBATISHO VII: Idhini ya Kufanya Utafiti

PAGE 2	PAGE 3
<p>THIS IS TO CERTIFY THAT: Prof./Dr./Mr./Mrs./Miss/Institution David Misiko Wasike of (Address) Moi University P.O.Box 3900-30100, Eldoret</p>	<p>Research Permit No. NCST/RCD/14/012/378 Date of issue 18th April 2012 Fee received KSH.2,000</p>
<p>has been permitted to conduct research in</p>	
<p>Location District Bungoma County</p>	
<p>on the topic: Matumizi ya lugha za kiasili kuangazia masuala ya kiafya, kiuchumi na kisiasa: Uchunguzi wa Sulwe na West FM.</p>	<p>Applicant's Signature</p> 
<p>for a period ending: 31st April, 2013.</p>	<p>Secretary National Council for Science & Technology</p> 